**31 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 31 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David Mbunge wa Same Magharibi, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Priscus Tarimo.

Na. 488

### Upungufu wa Walimu Maeneo Yenye Mazingira Magumu – Same

**MHE. PRISCUS J. TARIMO K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani na Shule za Mwembe – Mbaga, Same na Chome – Suji ambazo hazina walimu kutokana na mazingira magumu ya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiajiri walimu kila mwaka na kuwapangia vituo vya kazi kulingana na mahitaji ambapo maeneo yenye mazingira magumu hupewa kipaumbele. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Same ilipangiwa walimu 364 wakiwemo walimu 249 wa shule za msingi na walimu 115 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali inatarajia kuajiri watumishi wa kada za walimu na afya 12,000 ambapo baadhi yao watapangiwa katika maeneo yenye

upungufu mkubwa zaidi zikiwemo Shule za Tarafa za Mwembe – Mbaga, Same na Chome – Suji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo hayo kila wanapopangia walimu wapya baada ya muda mfupi huwa wanahama na ni kwa sababu ya hayo mazingira magumu kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuajiri walimu wenye vigezo ambao ni wenyeji wa maeneo yale kama hizi Tarafa za Mwembe – Mbaga, Chome- Suji ambao wana vigezo ili kuondoa tatizo hilo ikiwa ni sambamba na kuwajengea nyumba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali ina mpango gani wa kuongeza walimu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum haswa kwenye shule hizi, kama shule ya *Moshi Technical* pale Moshi Mjini, Mwereni pamoja na Msandaka Palu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Priscus Tarimo na nimhakikishie tu kwamba katika utaratibu wa ajira za kada mbalimbali wakiwemo walimu, jambo la kwanza tunaona ni muhimu sana kuwa na sura ya Kitaifa badala ya kuwa na watu wanaotoka eneo hilo wakaajiriwa kuwa walimu katika eneo hilo peke yake na hii ni katika kudumisha Utaifa wetu. Watu wanatoka Iringa wanafanya kazi Kilimanjaro, wanatoka Mwanza wanafanya kazi Kigoma inajenga Utaifa pia inaleta ufanisi kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Spika, mpango ambao umewekwa na Serikali katika maeneo ambayo ni ya mbali au magumu kwa watumishi

kuishi na kufanya kazi maeneo hayo. Tulishaelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kuwa na mpango maalum wa *retention scheme* kwa ajili ya watumishi, waalimu, watumishi wa Sekta ya Afya na watumishi wengine ambapo kupitia mapato ya ndani wanatenga motisha kwa ajili ya kuwapa walimu kama motisha *allowance*. Pia wahakikishe kwamba wanajenga nyumba kwa ajili ya walimu au watumishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitumie nafasi hii kuwakumbusha Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kutekeleza mpango wa *retention scheme* ambao ulitolewa na Serikali ili maeneo hayo magumu watumishi waendelee kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuhusiana na walimu katika maeneo ya shule zenye mahitaji maalum. Serikali imeendelea kufanya hivyo na katika vibali vyote vya ajira, moja ya kipaumbele huwa ni walimu ambao wanapelekwa kufundisha shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya hivyo hata kwa ajira ya zinazokuja ili tuweze kuondoa *gap* ya watumishi katika maeneo hayo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kuuliza katika Mkoa wa Simiyu tuna shule 28 za sekondari na msingi zilizojengwa hivi karibuni lakini kila shule unakuta ina walimu wawili au watatu. Je, lini Serikali italeta walimu wa kutosha katika Mkoa wetu wa Simiyu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Simiyu ni miongoni mwa mikoa iliyoainishwa kwamba ina upungufu mkubwa zaidi wa watumishi. Tumekuwa tukipeleka

watumishi zaidi na ajira zinazofuata tutatoa kipaumbele kwa Mkoa wa Simiyu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka Mbunge wa Lupa swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe.

Na. 489

**Uhitaji wa Watumishi wa Kada ya Afya na Elimu – Chunya**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE K.n.y. MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka watumishi wa Kada ya Afya na Elimu katika Wilaya ya Chunya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE )** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wa kada za elimu na afya kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. Kati ya mwaka 2020/2021 na 2022/2023, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ilipokea jumla ya watumishi 397 wakiwemo wa afya 84 na elimu 313 ambapo walimu wa shule za msingi walikuwa walimu 244 na shule za sekondari walikuwa 69.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 22,112 wakiwemo wa afya 10,112 na elimu 12,000 ambao watapangiwa vituo vya kazi katika maeneo yenye upungufu mkubwa ikiwemo Wilaya ya Chunya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza tuishukuru Serikali kwa juhudi kubwa inayofanya kuajiri watumishi hasa wa kada ya afya na walimu.

Mheshimiwa Spika, shule nyingi za pembezoni katika Wilaya ya Chunya kwenye kata za Lualaje, Ifumbo, Mafyeko na Kambi Katoto zimekosa walimu pamoja na watumishi wa afya. Je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi wa kuhakikisha inafanya msawazisho ili walimu walioko mijini na walioko kule wafanane?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni lini Serikali itaandaa mpango maalum wa kufanya sensa ya kuhakikisha tunakuwa na takwimu za walimu na watumishi wa afya walio mijini na walio vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsate sana. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ally Jumbe, Mbunge wa Kyela kwa kazi nzuri na kubwa anayowafanyia wananchi wa Jimbo la Kyela. Nianze kwa kumpa uhakika kwamba, kwanza tunatambua kuna baadhi ya shule zilizoko pembezoni mwa miji au halmashauri zina upungufu mkubwa sana wa watumishi zikiwemo hizo za maeneo ya Kambi Katoto, Mafyeko na maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja.

Mheshimiwa Spika, tayari tumeshaweka mpango wa kuhakikisha maeneo yale ambayo yana upungufu mkubwa zaidi wa watumishi wanapelekwa na ndiyo maana kwenye mfumo wa ajira wa sasa, ni mfumo kwanza wa kieletroniki pia kila anayeomba ajira analazimika kuomba kwenye maeneo ambayo yameainishwa na ule mfumo *automatically* unaweka nafasi nyingi zaidi kwenye shule, halmashauri au mikoa ambayo ina upungufu mkubwa zaidi wa watumishi. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo tutalifanyia kazi ili tupunguze *gap* la watumishi katika shule hizo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusiana na kufanya sensa ya walimu walioko mijini na vijijini. Tayari tulishafanya hivyo miaka miwili iliyopita na tunafahamu uwiano wa walimu vijijini na watumishi wa afya vijijini na mijini. Mpango uliopo sasa kwanza ni kuhakikisha kwamba kipaumbele cha ajira kinakwenda kwenye halmashauri za vijijini zaidi. Pili, tunazuia uhamisho kutoka vijijini kwenda mijini

kwenye majiji, manispaa ili kuhakikisha kwamba tuna-*balance* uwepo wa watumishi katika vijiji na katika miji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji Mbunge wa Mwera sasa aulize swali lake.

Na. 490

**Changamoto za Muungano Zilizopatiwa Ufumbuzi**

**MHE. ZAHOR MAHAMMED HAJI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itautaarifu Umma kuhusu changamoto za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi ili Wanasiasa wasipotoshe Wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor swali lako ni namba 490.

**MHE. ZAHOR MAHAMMED HAJI:** Ahsante.

**SPIKA:** Inabidi useme wewe ndio Mheshimiwa Waziri ajibu.

**MHE. ZAHOR MAHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba Serikali inipatie jawabu langu la swali namba 490.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea na programu za kutoa elimu kwa Umma kupitia hotuba za Viongozi Wakuu, makongamano, maonesho maalum, utayarishaji wa vipindi vya televisheni, redio, magazeti, uandishi na uchapishaji wa vitabu ikiwemo kitabu cha hoja zote zilizopatiwa ufumbuzi kwa lengo la kutoa taarifa kuhusu changamoto

zilizopatiwa ufumbuzi. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2024/2025 Ofisi imepanga kuongeza nguvu katika kutoa elimu kwa kutumia ipasavyo mitandao ya kijamii, vikao na makundi maalum, ziara za kimafunzo na makongamano.

Aidha, hoja zilizopatiwa ufumbuzi zimewekwa kwenye tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo ni www.vpo.go.tz

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji swali la nyongeza.

**MHE. ZOHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaishukuru Serikali pamoja na majibu mazuri, bado inaonekana *public* haielewi vizuri mambo haya ambayo Serikali inasema yamepatiwa ufumbuzi. Je, Serikali kwa kuanzia kwetu sisi Wabunge iko tayari kutuletea maandiko hayo hasa ya machapisho ili na sisi tuwe sehemu ya hao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je Serikali iko tayari kuendelea na mkakati huu kwa sababu bado inaonekana taaluma inayotolewa na Serikali ni tofauti inayotolewa na wenzetu kule ambao wanapotosha jamii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Zohor kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi sana katika kuieleza jamii juu ya suala zima la umuhimu wa Muungano pia tumejitahidi sana kuieleza jamii juu ya changamoto ambazo zimekuwa zikijitokeza kwenye Muungano huu kupitia njia tofauti kama tulivyoeleza katika suala la msingi. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tupo tayari kuongeza juhudi ama jitihada ili wananchi waweze kupata zaidi elimu ya Muungano na waweze kunufaika na waendelee kuutunza Muungano huu kupitia njia tofauti kama tulivyozieleza.

Mheshimiwa Spika, hata ukitazama Muungano huu, changamoto tulizotokanazo na tulizonazo sasa ni tofauti maana sasa zimebakia changamoto nne ambazo muda wowote tunakwenda kuzimaliza.

Mheshimiwa Spika, tupo tayari kuwapatia Waheshimiwa Wabunge, hivyo vitabu ambavyo tumevieleza pamoja na machapisho. Nataka nitoe maelekezo hapa kupitia Mkurugenzi wa Muungano na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Muungano katika Ofisi ya Makamu wa Rais wahakikishe kwamba Waheshimiwa Wabunge ndani ya wiki inayofuata ndani ya vishikwambi na maeneo mengine iwe tayari wameshapata machapisho hayo na vitabu hivyo ili waweze kunufaika na kujua changamoto zilizotatuliwa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima Mbunge wa Kawe sasa aulize swali lake.

Na. 491

**Kudhibiti Mito Inayopanuka - Kawe**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa dharura wa kudhibiti Mito inayopanuka na kuhatarisha maisha na mali za wananchi katika Jimbo la Kawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Katika kukabiliana na changamoto za kudhibiti mito kupanuka hususan kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Serikali imechukua hatua ya dharura kwa kuandaa Mwongozo wa Usafishaji Mchanga, tope na taka ngumu kwenye mito na mabonde katika Mkoa wa Dar es Salaam 2021 ukiwa na lengo la kuelekeza aina ya mfumo wa usafishaji wa mito kwa kuchimba

mchanga, tope na taka ngumu zinazohitaji kuondolewa ili kudhibiti mtiririko wa maji katika mito na mabonde.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwongozo huu unatoa maelekezo ya hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na wadau wa kuhifadhi na utunzaji wa mazingira katika kuhakikisha mazingira ya mito yanalindwa na kuhifadhiwa na kutumika katika njia sahihi ya uchimbaji mchanga ikiwa ni pamoja na kudhibiti uchimbaji wa michanga na ujenzi wa makazi ndani ya meta 60 kutoka kwenye kingo za mito.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Serikali za Mitaa kote nchini kusimamia kikamilifu Sheria ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ili kuzuia shughuli za kibinadamu kama vile uchimbaji wa mchanga na kuendelea kuelimisha jamii juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira ili kupunguza athari zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri sina haja ya swali la nyongeza kwa sababu swali langu la msingi halijajibiwa. Nimeuliza kuhusu mpango wa dharura kuhusu kupanuka kwa mito kwenye Jimbo la Kawe lakini Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu Dar es Salaam. Kwa hiyo sitakuwa na swali la nyongeza na kama itakupendeza ningeomba swali langu lijibiwe tena baadaye.

**SPIKA:** Nilikuwa najaribu kulitazama jibu hapa ili nijue maombi yako niyajibu kwa namna gani lakini ngoja nitalitazama halafu nitakujibu baadaye. Sasa Mheshimiwa Aida Khenani ulisimama kwa ajili ya swali la nyongeza lakini mwenye swali amekataa majibu. Kwa hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri nitatoa mwongozo baadaye ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 492

**Kukamilisha Miradi ya Umeme Vitongoji na Vijiji Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha miradi ya Umeme katika Vitongoji na Vijiji ambavyo havijafikiwa na miradi hiyo Wilayani Karatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa niaba ya Wizara ya Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Karatu ina jumla vijiji 57 ambapo vijiji vyote vimeshapatiwa umeme. Aidha, Jimbo hilo lina vitongoji 265 na kati ya hivyo, 125 vina umeme na 140 havina umeme. Kazi ya kusambaza umeme katika vitongoji ambavyo havina umeme inaendelea ambapo Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji 10 kupitia mradi wa ujazilizi 2B na vitongoji 15 kupitia Mradi wa Vitongoji 15 kwa kila Jimbo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, hivyo, vitongoji 115 ndivyo vilivyosalia ambapo kazi ya kuvipelekea umeme itaendelea kuratibiwa na Wakala Nishati Vijijini kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, vitongoji 115 vilivyosalia ni vingi kwa idadi na wananchi wanahitaji umeme, je, ni lini kwa uhakika wananchi hao watapelekewa huduma hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mkandarasi aliyepewa kazi ya ujazilishi bado anatusuasua kutekeleza mradi huo, nini kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vitongoji 115 kwa sasa *REA* inakamilisha hatua za mwisho za kumpata mkadarasi, ni imani yetu ni kwamba ndani ya wiki moja ijayo mkandarasi huyu atakuwa amesaini mkataba. Aidha, kazi hiyo inatarajiwa kuanza katikati ya mwezi ujao.

Mheshimiwa Spika, kwa lile swali lake lingine, ninaielekeza *REA* wamsimamie kwa ukaribu mkandarasi yule aweze kutimiza wajibu wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Jimbo la Lushoto lina vitongoji vingi sana ambavyo havijapatiwa umeme hasa Kitongoji cha Mgambo, Mzizima na Kindoi, je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vitongoji hivyo umeme?

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge watatu mlisimama, lakini Mheshimiwa Dunstan Kitandula amesimama kwa niaba ya Wizara nyingine. Kwa hiyo, ulizeni maswali yenu halafu yeye ataondoka nayo atakwenda kuikabidhi Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anatropia, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L THEONEST:** Mheshimiwa Spika, wakati *line* kuu za umeme zikipita, hupita kwenye vijiji na kijiji au kitongoji husika wanajikuta hawapatiwi umeme. *Line* kuu imepita katika Kata za

Kimuli, Kamuli na maeneo mengine, nataka nijue ni mkakati gani wa kuhakikisha ambapo *line* kuu inapita vijiji husika na wakazi husika wawe wanapatiwa umeme badala ya kuona nguzo tu wakati wao hawana umeme?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Nyamang'uta kuna Vitongoji vya Sengera na Nyamiri ambavyo vimezungukwa na umeme na vingine havijapata umeme kwa muda mrefu, ni lini vitongoji hivi vitapata umeme?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali matatu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, wewe yachukue umpelekee Mheshimiwa Waziri wa Nishati, halafu Waheshimiwa Wabunge watajibiwa atakapokuja Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

Na. 493

**Kurejesha Utaratibu wa *Recognition of Prior Learning***

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itarejesha utaratibu wa *Recognition of Prior Learning?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeandaa Mwongozo wa Kutathmini na Kutambua Maarifa yaliyopatikana Nje ya Mfumo

Rasmi *(Recognition of Prior Learning)*. Mwongozo unaweka utaratibu wa utambuzi na urasimishaji wa maarifa yaliyopatikana nje ya mfumo wa shule katika fani mbalimbali za amali kwa lengo la kuwawezesha walengwa kushiriki kikamilifu katika ulimwengu wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023 mfumo wa kutambua na kurasimisha ujuzi na stadi zinazopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo umepewa kipaumbele. Serikali itatekeleza afua za kuimarisha utaratibu wa utambuzi na urasimishaji wa maarifa, ujuzi na stadi zinazopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo. Aidha, elimu nje ya mfumo rasmi itatambuliwa na watakaopitia mfumo huo watakuwa na fursa ya kujiunga na mfumo rasmi wa elimu kulingana na vigezo vitakavyowekwa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme tu kwamba sina swali la nyongeza, isipokuwa tu ninatoa shukrani kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nilipoingia tu Bungeni hapa kwa mara ya kwanza haya ndiyo yaliyokuwa mapambano yangu, ili watu wenye ujuzi nje ya shule waweze kupatiwa nafasi ya kusoma. Mimi ni tunda la watu ambao wamepata nafasi hiyo, na sasa hivi ninafanya *Masters* ya *Mass Communication* kwa kutumia kipaji peke yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na timu yote ya Wizara ya Elimu. Kazi hii sasa imekamilika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 494

**Kigezo cha Mtihani wa Kuandika Kabla ya Kujiunga na *VETA***

**MHE. ROSE C. TWEVE** aliuliza: -

Je, kigezo cha mtihani wa kuandika kabla ya kujiunga na Vyuo vya Ufundi *(VETA)* ni cha lazima kwa wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* inatoa mafunzo ya ufundi stadi kwa nadharia kwa 30% na vitendo kwa 70%.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa stadi za kuandika, kusoma na kuhesabu katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi *(VETA)* hutoa mitihani ya majaribio *(aptitude test)* wa kujiunga kwenye vyuo vyake. Hii ni kwa sababu kuna umuhimu wa kubaini endapo wanaotaka kujiunga na vyuo vya *VETA* wanamudu stadi za KKK ikiwa ni kigezo cha kujiunga na vyuo vya ufundi stadi na pia kwa ajili ya muendelezo wa kielimu kwa hapo baadae pindi mwanafunzi akihitaji kujiendeleza zaidi. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana kabisa kwamba kwenye *issue* ya ufundi vitendo ni muhimu zaidi kuliko nadharia. Kwa Juni, 2023 tu zaidi ya watoto 37% ya zaidi ya wanafunzi 18,000 walishindwa kujiunga na *VETA*. Sasa kama *focus* ni vitendo hauoni sasa ni muhimu kwa wizara yake kupitia vigezo ili *qualification* iwe zaidi kwenye vitendo zaidi ya nadharia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Tweve, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba kwa hivi sasa vigezo tunavyotumia ni hivi vya kuweka mtihani huu wa kuandika ili kupima zile stadi za KKK.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu ni kwamba tuna maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi pamoja na umaskini na namna pekee ya kuondoa huu ujinga ni pamoja na kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ametoa hili wazo hapa, naomba tuuchukue ushauri wake ili twende tukaufanyie tathmini na kuangalia namna bora ya kufanya hii mitihani, aidha kwa kuandika au kwa hiyo namna ambayo yeye amependekeza, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca haukusimama mwanzo, lakini nakupa nafasi. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua ni kwa nini Wizara imebadilisha vigezo vya wanafunzi wanaojiunga kwenye vyuo vya kati vya afya ambavyo vimesababisha kukosa wanafunzi wengi, na kwamba kwa vile vyuo kukosa wanafunzi itasababisha upungufu wa wauguzi katika zahanati na vituo vya afya vingi vilivyojengwa nchini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha madaraja au zile *credits* za zamani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nijibu swali dogo la Mheshimiwa Jesca kuhusiana na suala la kubadilisha vigezo hasa kwa wale wanaojiunga na kada hizi za afya.

Mheshimiwa Spika, suala la vigezo vya kujiunga na shule siyo *static,* ni kitu ambacho kinatakiwa kibadilike kulingana na mwenendo wa elimu yetu jinsi ulivyo, lakini kwa vile ametoa ushauri hapa tuweze kwenda kuangalia upya, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba tutakwenda kufanya mapitio ya hivyo vigezo ili tuweze kuangalia changamoto iko wapi. Ninajua kuna kigezo kimoja cha kwamba ni lazima mtu afaulu hesabu ndicho ambacho kimewaangusha wengi, lakini hivyo nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, ushauri wake tumeupokea na tutakwenda kuufanyia kazi na baadaye tutakuja na majibu sahihi, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 495

**Kuimarisha Upatikanaji Mtandao wa Simu – Tabora Mjini**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuimarisha upatikanaji wa mtandao wa simu katika kata 29 za Tabora Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imejenga minara ya mawasiliano ya simu saba katika Jimbo la Tabora Mjini. Minara hiyo ilijengwa na Vodacom na Halotel katika Kata za Itetemia, Kabila, Kalunde, Ndevelwa, Tumbi na Uyui kupitia awamu mbalimbali za miradi iliyotekelezwa kati ya Agosti, 2017 na Januari, 2020.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigitali Kata za Ifucha na Kiloleni zitajengewa minara na kampuni ya Honora (Tigo). Kwa upande wa Kata ya Kakola *UCSAF* imeingia mkataba na *TTCL* kwa ajili ya kujenga mnara katika kata hiyo. Utekelezaji wa mradi huu ni miezi 24 kuanzia tarehe 13 Mei, 2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa miradi inayoendelea, Serikali kupitia *UCSAF* itafanya tathmini ya hali ya mawasiliano katika Jimbo la Tabora Mjini ili kubaini maeneo yenye uhitaji wa kufikishiwa mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Tabora Mjini lenye kata 29 bado kuna kata ambazo zina matatizo sana ya mawasiliano katika baadhi ya maeneo, kwa mfano, ukienda Kata ya Ndevelwa kuna maeneo ambayo huwezi kabisa kupata mawasiliano. Ukienda Kata ya Ikomwa na hata hiyo Kata ya Itetemya, tena karibu na mjini kabisa, kuna maeneo kama yale ya Kipalapala pale ambapo kuna *mission* bado kuna shida ya mtandao na maeneo mengine.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha yale maeneo yote ya Tabora Mjini ambayo hayafikiwi na mawasiliano yatafikiwa na hayo mawasiliano? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kata ya Kiloleni ambayo iko kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri iko *center* kabisa ya Mji wa Tabora kwa maana ipo mjini pale pale. Sasa pengine niwashauri

tu, nilikuwa na ombi, kwa kuwa pale Kiloleni hakuna shida kabisa ya mawasiliano ni mjini kabisa, kwa nini huo mtambo ambao mtaupeleka pale katika Kata ya Kiloleni ambayo iko mjini kabisa msipeleke maeneo ambayo bado kuna shida ya mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, tayari kuna jitihada zinafanyika na tutazisimamia kuhakikisha mawasiliano yanaimarika katika maeneo haya ya Jimbo la Tabora Mjini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuhamisha mtambo kutoka Kiloleni kwenda eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali tuko tayari kushauriana naye na baada ya hapa tuonane ili tuweze kuona namna njema ya kufanya katika hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Tabora Kaskazini, kata mbili ambazo ni Kata ya Igulungu, Kijiji cha Mbeya ambako kuna zahanati hakuna kabisa mawasiliano, lakini pia Kata ya Ibiri hakuna mawasiliano; je, ni lini Serikali itajenga minara katika kata hizo mbili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Almas Maige, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kata hizi mbili jana tuliongea na Mheshimiwa Maige na tayari watendaji wanashughulikia. Katika mwaka ujao wa fedha tutafanya baadhi ya maeneo ili kuhakikisha mawasiliano yanakaa vizuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi. Mheshimiwa Vita Kawawa swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali ilipeleka Kampuni ya *TTCL* kupitia *UCSAF* kwenda kujenga minara miwili katika Kijiji cha Mtelawamwahi na Kijiji cha Mdwema, lakini tangu walipokwenda mpaka leo hawajurudi kujenga hiyo minara; je, Serikali inaweza kuhimiza Kampuni ya *TTCL* kujenga hiyo minara ya Mdwema na Mtelwamwahi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa kuwa katika vijiji hivi tutafutailia kwa karibu na ikiwezekana tutakwenda kufanya ziara ili kuona ni kwa nini minara hii haijajengwa na lengo ni kuona wananchi wanapata mawasiliano ya uhakika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 496

## Ujenzi wa Majosho na Malambo – Same Mashariki

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majosho na malambo katika Kata za Bendera, Kalemawe na Maore katika Jimbo la Same Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa majosho na malambo nchini ili kudhibiti magonjwa yanayoenezwa na wadudu na kuongeza upatakanaji wa maji kwa ajili ya mifugo. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara inaendelea na ujenzi wa majosho 246 kwa gharama ya shilingi bilioni 5.6 na kusambaza dawa za ruzuku za kuogesha mifugo lita 56,000 nchi nzima. Pia ujenzi wa malambo na visima virefu kwa ajili ya maji ya mifugo unaendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa majosho na malambo yakiwemo ya Jimbo la Same Mashariki kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Hivyo natoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Same kuainisha maeneo yanayofaa kwa ujenzi wa malambo katika kata hizo, kufanya usanifu na kuwasilisha gharama zake Wizarani ili yaweze kujumuishwa katika mpango wa bajeti ya Wizara wa mwaka 2025/2026 kadiri ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kutoa wito kwa wafugaji na wadau wengine hapa nchini kuungana na Serikali kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji ili kusaidia kupunguza changamoto ya maji kwa mifugo hapa nchini, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Maore, Kijiji cha Muheza, Kitongoji cha Nandululu tembo wameingia na kubomoa miundombinu ya maji, hivyo wafugaji hupata shida sana kwa ajili ya mifugo kupata maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kujenga miundombinu hiyo ya maji ili kutatua tatizo hili?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kuongozana na mimi kwenda kuona hali halisi ilivyo katika eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ninatambua kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Mbunge Zuena Bushiri katika kufuatilia masuala ya mifugo hususani katika Mkoa wake wa Kilimanjaro. Nimwondoe shaka, jambo lake nimezungumza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na amenithibitishia kwamba jambo hilo wanaliweka katika mpango wa kuhakikisha linajengwa kwa dharura kupitia visima ambavyo Bunge lako Tukufu lilipitisha katika Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliyopitishwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kuongozana, nimthibitishie tu kwamba nimzengumza na Mheshimiwa Mnyeti pamoja na Mheshimiwa Ulega wamesema watakuwa tayari watakaporudi, wapange tu muda gani wafike katika hayo maeneo ambayo umeanisha yana changamoto, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, nimekuona umesimama, lakini Waziri hatoweza kutoa majibu kwa sababu anafanya kwa niaba. Kwa hiyo, muulize atampelekea Waziri halafu Waziri atakutumia majibu.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itajenga majosho na malambo katika Kata za Kandawale na Miguruwe kama ilivyoahidi katika siku zilizopita?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe chukua hilo swali nenda nalo na utamkabidhi Waziri anayehusika ili aweze kumpa majibu Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nimepokea, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Vijijini sasa aulize swali lake na swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu.

Mheshimiwa Naibu Waziri wewe chukua hilo swali nenda nalo utamkabidhi Waziri anayehusika ili aweze kumpa majibu Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nimepokea, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake na swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu.

Na. 497

**_NIDA_ na _RITA_ Kuwa na Ofisi Kila Halmashauri**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA K.n.y. MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuwa na Ofisi ya *NIDA* na *RITA* katika kila halmashauri nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuwa na Ofisi za *NIDA* katika kila halmashauri nchini. Katika kutambua umuhimu huo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* ina jumla ya majengo na Ofisi za Usajili 16 kati ya hizo 13 ni Ofisi za Usajili za Wilaya. Serikali katika kutambua uhitaji wa ofisi za usajili, katika mwaka wa fedha 2024/2025 *NIDA* imetenga jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 5.2 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa majengo 35 yakiwemo ofisi 31 ya ofisi za usajili katika halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali ina mpango wa kuziunganisha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA)* ili kuwa na taasisi moja itakayoshughurika na matukio muhimu maishani. Zoezi hilo linatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2024, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali imetenga 5,235,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi 31 la usajili.

Swali langu nataka kufahamu, je, Serikali mtakuwa tayari kuiweka Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha katika awamu ya kwanza ya kujenga ofisi hizo za usajili katika hizi shilingi 5,235,000,000?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kutokana na usaumbufu wanaoupata wananchi kila wapatapo huduma kuhitajika kitambulisho chake, ni kwa nini sasa Serikali isiweke kitambulisho kimoja kikatoa huduma zaidi ya moja? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mwakamo, mawili kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa mwenye swali alikuwa ni Mheshimiwa Mwakamo, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ameuliza kwa niaba. Kwa hiyo, yale mawili ya nyongeza anajibiwa aliyeuliza Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika ujenzi wa ofisi hizi za vitambulisho tulikuwa tuna awamu mbili; awamu ya kwanza imeshakamilika, awamu ya pili ndio hii tunakwenda kutumia fedha hizi shilingi bilioni 5.2 kwa ajili kuanza. Kulikuwa kuna mikao baadhi ya wilaya zimeshapata na kuna mikoa baadhi ya wilaya hazijapata, kwa mfano katika Mkoa wa Dar es Salaam ilikuwa Kinondoni na baadhi ya wilaya nyingine, lakini Zanzibar katika Mkoa wa Kusini Wilaya ya Kati tayari Wilaya ya Kusini bado.

Mheshimiwa Spika, katika awamu hii fedha hizi tutakwenda kujenga vituo kwenye mikoa yote Tanzania lakini zaidi tutahakikisha katika Mkoa wa Pwani, Kibaha na Bagamoyo tunakwenda kuipa kipaumbele, hiyo tuko tayari na tumeridhia hilo.

Mheshimiwa Spika, hili lingine tumelichukua, tunakwenda kulifanyia kazi ingawa Serikali inatambua changamoto hii, lakini kikubwa zaidi kama tulivyosema katika jibu la msingi tumeanza sasa kwenda kuiunganisha *RITA* na *NIDA* angalau sasa tuanze kupunguza changamoto zile za mrundikano wa vitambulisho vingi na kwa baadhi wananchi kupata usumbufu katika upatikanaji wa huduma, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, sasa aulize swali lake.

Na. 498

**Kauli ya Serikali Kutozuia Maiti kwa Sababu ya Deni la Matibabu**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, ni kweli kauli ya Serikali kwa hospitali kutozuia maiti kwa sababu ya deni la matibabu ni ya kisiasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA,** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilishatoa maelekezo kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini kupitia Waraka Na. 1 wa mwaka 2021 wa kutozuia maiti na kuweka utaratibu wa kulipia gharama za matibabu na madeni ya miili.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Waganga Wakuu wa Mikoa, Waganga Wakuu wa Wilaya pamoja na Waganga Wafawidhi wa Hospitali kwa ngazi zote nchini kuzingatia maelekezo ya mwongozo huu na kuhakikisha wananchi wanapata huduma pasipo kuwepo kwa vikwazo vinavyochelewesha marehemu kuzikwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, swali la nyongeza.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri aliyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado hata kwenye mikoa yetu na wilaya mbalimbali bado watu wanazuiwa maiti zao na sisi kama wawakilishi wa wananchi huwa tunapigiwa simu kuhusiana na hili suala la kuzuia maiti.

Kwa hiyo, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu yake aliyosema kwamba sasa hivi wametoa mwongozo naomba hao watu wazingatie mwongozo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ili watu hawa ambao wanapoteza wapendwa wao badala ya kuanza kuzuiwa kwamba wasichukue watu wao, je, kwa nini sasa Serikali isiweze kuimarisha Bima ya Afya ili hawa watu wakapewa mwili wao kwa sababu wanakuwa wamepata matatizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kweli ni Mbunge ambaye amekuwa akishirikiana na Wizara ya Afya kwa masuala mbalimbali yanayohusu afya kwenye wilaya yake ambayo anaisimamia.

Mheshimiwa Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge tutakachokifanya nitumie tena hii fursa kuwambia Waganga Wafawidhi, Waganga Wakuu wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Wilaya zetu na wataalamu wote wa afya wahakikishe huu mwongozo wanaufuata, lakini niwaombe Wakurugenzi wanaohusika na Idara ya Tiba kwenye Wizara yetu kuanzia leo waanze kushuka chini na kuanza kufanya *declamation* ya waraka huu ili watu wengi na wataalamu wengi wajue kwamba kuna huu waraka ili waweze kuuzingatia.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ilikuwa ni Bima ya Afya, hili la Bima ya Afya ninyi wenyewe mmeshatusaidia tumepitisha Muswada wa Bima ya Afya kwa wote nikuombe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wenzangu tutakapoanza tuhamasishe kwa pamoja wananchi kwa sababu ndilo kweli suluhisho la kumaliza tatizo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, pamoja na Serikali kuendelea kutoa kauli kuhusiana na kutozuiliwa kwa

maiti kwenye vituo vya afya na hospitali mbalimbali nchini, lakini hii imekuwa ni changamoto kubwa maeneo mengi na hii inaonekana kauli ya Mawaziri na Serikali haizingatiwi.

Sasa nataka kujua mpango wa Serikali ni upi kutoa kauli yenye ukali zaidi ili kauli zao ziweze kutekelezeka huko kwenye maeneo ya hospitalini na vituo vya afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi naamini nimtoe tu wasiwasi Mbunge kauli za Serikali zinasikilizwa ila mtu akishafariki hospitalini haikufanyi *automatically* kwamba hutakiwi kulipia, ila kuna *process* za kuzingatia ili kuhakikisha kweli huyu ni yule asiyeweza kulipia au huyu ni wa kupewa utaratibu maalum kuhakikisha anamaliza hili deni, lakini tukubaliane hakuna kanisa wala msikiti uliouaga shetani, shetani bado yupo anatusumbua na kuna baadhi ya watendaji ambao si wasikivu tutaendelea kupambana nao pamoja na ninyi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi ambao hata kulipia huduma za matibabu wanakuwa hawana, lakini mgonjwa anapofariki wamekuwa hawana uwezo kabisa kwa mfano wiki iliyopita tu kuna maiti ilitoka Muhimbili watu walikuwa wanashindwa kujichangisha mpaka maiti ikachelewa kupelekwa kuzikwa. Ni kwa nini sasa hawa wasifutiwe tu maana yake waliambiwa kwamba watakapozika waende wakalipe zile gharama wanakuwa wanapata usongo wa mawazo mpaka hata afya ya akili inakuwa inawazidi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge, lakini niendelee kusisitiza kuna utaratibu, moja; mwananchi anapotoka na anajua kwamba hawezi kulipa matibabu kwenye eneo husika washirikiane na

Mwenyekiti wa Kijiji husika pamoja na Mtendaji Kata ili anapokwenda hospitali awe tayari hata kama akiwa hospitali hizo *process* ziendelee ili awe na barua yake kutoka Ofisi ya Kata ambayo inamthibitisha kwamba hana uwezo wa kulipa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ninyi wote hapa ni mashahidi, hata wakati mwingine japo siyo utaratibu ambao ningependa kwa sababu wengi hawawezi kutufikia, lakini ninyi Wabunge ni mashahidi mkileta kwetu matatizo ambayo kuna wananchi ambao wameshindwa kulipia tumekuwa tukihakikisha yanatatuliwa, lakini ili kutokulazimisha wakati wote Wabunge msumbuliwe hebu tuendelee kuwaelimisha wananchi kwamba kuna watendaji wetu wa kata wakipatikana barua basi mwananchi huyo *automatically* anasaidiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru, aaanh, kuna Mbunge mwingine. Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 499

**Madhara kwa Mtoto Anayezaliwa Bila Kulia au Kuchelewa Kulia**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, ni madhara gani humpata mtoto anapozaliwa na kuchelewa kulia au kutolia kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, madhara yanayoweza kumpata mtoto anapozaliwa na kuchelewa kulia ni kuathirika kwa ubongo ambapo hupelekea:-

(i) Kupata utindio wa ubongo;

(ii) Kuchelewa kwa hatua za makuzi na maendeleo ya mtoto kama vile kuchelewa kukaa, kutembea na kuongea; na

(iii) Kutochangamana na wenzake au kutokucheza na wenzake na kadhalika, madhara ni mengi.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa kila mjamzito kuanza kliniki mapema mara tu anapogundulika kuwa na ujauzito sambamba na kuhakikisha wanajifungulia katika vituo vya kutolea huduma ili ikiwa kuna tatizo la uzazi pingamizi watoa huduma waweze kuwasaidia mapema kabla mtoto hajaathirika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ni kwa nini Serikali haitoi elimu na elimu ikawa endelevu kwa wanawake wanapokuwa wajawazito na pale wanapojifungua ili wapate uelewa kuhusu madhira haya uliyoyataja yanayotokana na watoto kutolia wanapozaliwa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; watoto wanaoathiriwa na jambo hili huwa wanatibiwa kwa gharama kubwa na kwa muda mrefu, je, ni kwa nini Serikali sasa haioni haja ya kupunguza au kuweka ruzuku katika dawa wanazotumia watoto ili waweze kutibiwa kwa gharama nafuu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kweli amekuwa akifuatilia kwa karibu sana masuala haya hasa kwenye Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, moja kwanza nimtoe wasiwasi, kwa sababu ukiona Serikali imeboresha miundombinu unaweza ukaona

jinsi teknolojia imepelekwa mpaka kule chini, miundombinu imeboreshwa na hiyo matokeo yake ndio maana *WHO* walitegemea kwamba Tanzania ishushe vifo vya akina mama toka vifo 556 mpaka 225 ifikapo mwaka 2025, lakini kwa kazi kubwa iliyofanyika maana yake toka mwaka jana hata kabla ya muda ulitegemewa vimeshuka mpaka vikafika 104. Maana yake kuna juhudi kubwa sana ya kuhamasisha, lakini kufanya kwa vitendo kuhakikisha zile huduma zinafika chini na akinamama wengi wana-*enroll clinic* ndio maana vifo vimepungua.

Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba tutaendelea kufanya hiyo juhudi na kuongeza nguvu kwenye eneo hilo la elimu, lakini pia Wabunge tushirikiane kwenye mikutano yenu kuhamasisha.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, wanapopata matatizo umemsikia Waziri wa Afya alipokuwa anafanya *presentation* ya bajeti yake hapa, moja ya maeneo ya kipaumbele katika yale maeneo kumi mojawapo ni eneo la utengamao tiba utengamao tunataka sasa hivi kuwekeza nguvu nyingi katika eneo hilo na kuwatambua hawa watoto mapema na kama ikiwezekana kuwapeleka kwenye vituo maalum vya mazoezi na mambo mengine ambavyo wataweza kufanya shughuli zao kama kawaida.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake wa Makundi Maalum, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 500

**Kuthibiti Vitendo vya Udhalilishaji Watoto Nchini**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali isiweke kwenye mpango wa maendeleo wa kila mwaka kipaumbele cha kudhibiti vitendo vya udhalilishaji watoto nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake wa Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imejumuisha masuala yote ya ukatili na udhalilishaji wa watoto katika Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ambapo tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi wa kwanza inaonesha jumla ya shilingi bilioni 30.5 zimetumika katika utekelezaji wa afua za kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na huku Serikali ikiwa imetumia shilingi bilioni 25 na wadau wa maendeleo wametumia shilingi bilioni 5.5 za fedha hizo. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha za utekelezaji wa Mpango Kazi wa Pili wa MTAKUWWA ikiwa ni jitihada za kuendelea kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hapa nchini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nitumie fursa hii kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo inajitahidi kutenga bajeti kwa ajili ya kulinda watoto wetu, lakini hata hivyo vitendo hivi vinazidi kwenda kwa kasi hasa ukatili wa watoto wadogo kwa ubakaji na ulawiti ni jambo baya sana.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, swali langu la kwanza; je, mpango kazi wa kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa awamu ya pili mmekadiria kuweka kiasi gani cha bajeti?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; pamoja na jitihada za Serikali kushirikiana na wadau mbalimbali wa Serikali ikiwemo Polisi,

Mahakama na wengine, je, Serikali haioni umuhimu kushirikiana na wadau muhimu sana katika Taifa hili ambao ni viongozi wa dini ambao wana majumba ya ibada katika maeneo yote tunayoishi kufanya nao makongamano kwa sababu wao ndio wadau wakubwa wanaokataza mabaya na kuamrisha mema? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Najma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga fedha 983,778,118,850 kwa ajili ya mpango wa pili wa MTAKUWWA ili kupingana na vitendo hivi vya kuatili ikishirikiana na Wizara za Kisekta pamoja na fedha za wadau.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, viongozi wa dini ni wadau na Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa MTAKUWWA ili kuendeleza kufanya makongamano na kuhamasisha majukwaa mbalimbali ili kupinga janga hili la ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa, kumekuwa na matukio ya kupiga picha za watu ambao wamepata athari za ukatili pamoja na udhalilishaji, nini kauli ya Serikali kuhusiana na kadhia hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq kuwa ni kweli kumekuwa na masuala ya kupiga picha kwa waathirika wa vitendo vya ukatili, Serikali inatoa kauli kali kwa wale wote ambao wanapiga picha vitendo vya ukatili na kuvirusha katika ma-*group* ya *whatsApp* au mitandao ya

kijamii, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao kwa sababu sheria, taratibu na miongozo ipo yote kwa ajili ya kuhakikisha mtu analindwa na kupata haki zake katika ukatili wa kijinsia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abbas Tarimba, swali la nyongeza.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, ningependa nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, ni nini kauli ya Serikali katika ku-*fast track* uchunguzi wa mashauri ya masuala kama ya ulawiti na mengineyo yanapowafika watoto na kisha kupelekwa mahakamani ili mashauri hayo yaamuliwe kwa uharaka zaidi kuliko kucheleweshwa?

**SPIKA:** Nawaza kama hili ni la kwako au ni la Mambo ya Ndani ya Nchi? Hilo linaenda Mambo ya Ndani wao ndio wanaofanya uchunguzi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Wizara ya Mambo ya Ndani watamjibu kwa maandishi Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na pia, majibu upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mbarawa, mbona unahama nikiwa nimesimama sasa? Haya ahsante sana.

Wakati wa swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kawe, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Swali Na. 491, Mheshimiwa Naibu Waziri alisoma majibu ya msingi hapa. Mheshimiwa Mbunge alipopewa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza akasema hana swali kwa sababu, jibu lililotolewa halijajibu swali alilokuwa ameliuliza. *(Kicheko)*

Sasa nilikuwa napitia hapa swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge na jibu ambalo Serikali imelileta kama jibu la msingi, Mheshimiwa Mbunge aliuliza, "Je, kuna mpango gani wa dharura wa kudhibiti mito inayopanuka na kuhatarisha maisha na mali za wananchi katika Jimbo la Kawe?" Kwa namna swali lilivyoulizwa ni kwamba, ni jambo ambalo linaendelea, maana amesema mito inayopanuka.

Sasa majibu ya upande wa Serikali kwanza hayajataja Kawe, Jimbo la Kawe ama mito iliyoko Kawe haijatajwa, lakini pia, jibu linaeleza kwa ujumla Dar es Salaam wamefanya nini. Sasa kwa sababu, hata katika hili jibu hakuna jambo la dharura linalotajwa kuhusu Dar es Salaam. Sasa inaniwia ugumu kidogo kusema kwamba, Mheshimiwa Mbunge swali lake limejibiwa kwa sababu, Kawe haijatajwa popote, lakini pia, majibu hayaashirii kwamba, ni mpango wa dharura.

Kilichoelezwa hapa ni mpango ambao upo, ambao umetolewa tangu mwaka 2021 na Mheshimiwa Mbunge anauliza kinachoweza kufanyika sasa. Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Mbunge halijajibiwa, lijibiwe upya.

Waheshimiwa Wabunge, Wabunge mbalimbali hapa wameuliza maswali ya nyongeza na nikasema Serikali itawapa majibu kwa maana ya kwamba, Wizara zinazohusika ambazo majibu yao yamejibiwa hapa kwa niaba, ili majibu yale yatimize masharti ya Kanuni zetu ya kujibiwa kikamilifu ni lazima yajibiwe na mtu ambaye anazo hizo taarifa. Sasa wale Wabunge ambao nilisema kwamba, watajibiwa na Mawaziri wanaohusika, yale maswali yao Mheshimiwa Waziri wa Nchi, yajibiwe kwa maandishi; Waheshimiwa Wabunge wajibiwe maswali yao yale kwa maandishi.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa la wageni tuliokuwanao Bungeni asubuhi hii:-

Tutaanza na wageni wangu ambao wanatoka *Compassion International Tanzania;* yupo Ndg. Marry Agrey Lema ambaye ni Mkurugenzi Mkuu. Yupo Ndg. Zalote Leolang'a Kaki Lukumai

ambaye ni Meneja Mwandamizi wa Ushirikiano, Ndg. Marry John Kasanga, Meneja Mwandamizi Usaidizi wa *Programme,* yupo Ndg. Makene Elias Mfwele, Meneja Mwandamizi Usaidizi wa *Programme* na Ndg. Israel Macha, Meneja Mwandamizi wa Watu na Washirika wa Kimkakati wa utamaduni. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni wa Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii na tutaanza na Dkt. Hassan Abas, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara, karibu sana. Yupo Generali Mstaafu George Marwa Waitara, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA),* karibu sana. Tunae Ndg. Generali Mstaafu Venance Salvatory Mabeyo, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (*NCAA)*. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Meja Generali Mstaafu Hamis Semfuko, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA),* karibu sana. Vilevile Balozi Dkt. Ramadhan Dau, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB),* karibu sana. Tunaye Dkt. Oswald Masebo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Makumbusho ya Taifa *(NMT)*. Yupo Ndg. Imani Kajula, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri, Chuo cha Taifa cha Utalii. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia, yupo Ndg. Mussa Juma Kuji, Kamishna wa Uhifadhi Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA),* karibu sana. Tunaye Ndg. Mabula Misungwi Nyanda, Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (*TAWA)*. Vilevile Dkt. Elirehema Doriye, Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA)*. Yupo *Prof*. Dos Santos Silayo, ambaye ni Kamishna wa Uhifadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzani *(TFS)*. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Dkt. Noel Lwoga, Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa *(NMT)*. Tunaye Ndg. Ephraim Mafuru, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* na pia, yupo Ndg. Maria Kigalu, Mkurugenzi wa Kituo cha Usawa wa Jinsia na Uchumi Jumuishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine ambao ni wageni wenu; msitembee nikiwa nimesimama.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Wageni 15 wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hawa ni watendaji wa *Venny Construction and Real Estate Company Limited*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, kuna wageni 10 wa Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi ambaye ni Naibu Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, hawa ni waanzilishi wa Shirika la Mwanamke Salama Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. Mgeni wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka, ambaye ni mfanyakazi wa *Fast Link* Safari *and Tours* kutoka Kyerwa, Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Pia, kuna mgeni wa Mheshimiwa Festo Sanga, ambaye ni mdogo wake kutoka Manyoni. Wageni wawili wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, ambao ni ndugu zake kutoka Musoma. Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Anthony Mwantona, ambao ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Rungwe na wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Riziki Lulida, ambao ni wanachama wa Shirika lisilo la Kiserikali la *Media Climate Conversation*. Wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Issa Mtemvu, ambao ni Walimu wa Shule ya Msingi King'ongo kutoka Jimbo la Kibamba, Jijini Dar es Salaam. Wageni 22 wa Mheshimiwa Anastazia Wambura, hawa ni wanafunzi kutoka Chuo cha Udaktari cha *Saint* Francis, Ifakara, Morogoro na wengine ni wageni 57 wa Mheshimiwa Hamisi Taletale, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 75 na walimu nane wa Chama cha Skauti Tanzania kutoka *Kings Modern Primary*.

Waheshimiwa Wabunge mnazungumza hapo, Mheshimiwa na mwenzio.

Wengine ni wanafunzi 75 na walimu nane wa Chama cha Skauti Tanzania kutoka *Kings Modern Primary and Secondary School* na *Mount Fort Primary School* Yombo za Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 70 na walimu watano kutoka Shule ya Wasichana ya kiislamu Kilimanyaro *(Kilimanjaro Islamic Secondary School)* ya Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni nane kutoka Kikundi cha Watu Binafsi Wanaotoka Ujerumani ambao ni wakazi wa Tanzania wanaoishi Zanzibar, Morogoro na Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili; tangazo la kwanza linatoka kwangu. Nawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Shally Josepha Raymond amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake wa *SADC-PF*.

Haya, akiwa amesimama ngoja niwasomee, "Amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake wa *SADC-PF* katika kikao cha jukwaa hilo kilichofanyika tarehe 16 Mei, 2024. Wadhifa huu ni wa kipindi cha miaka miwili, kuanzia mwaka 2024 hadi 2026."

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nampongeza sana Mheshimiwa Shally Josepha Raymond kwa heshima hii ambayo ameliletea Bunge letu, lakini pia, ameiletea nchi yetu na tunamtakia kila la heri katika majukumu yake hayo ambayo ameaminiwa na Wabunge wenzake kwenye Jukwaa hili la *SADC*. Kila la heri Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine ni, kesho Saa Nne asubuhi, Ukumbi wa Msekwa, kutakuwa na semina, kwa ajili ya Wabunge wote itakayohusu Matumizi ya Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana kwenye semina hii ambayo itatolewa na Wizara ya Fedha.

Baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba yetu.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, Muongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 54 ambayo inaagiza Shughuli za Bunge zisimame, ili jambo la dharura liweze kujadiliwa. Hivi ninavyoongea ziko habari zinasambaa mtandaoni za idadi ya watu 36 wa Jimbo la Buchosa ambao wameliwa na mamba**.** Hili ni tukio la kusikitisha. Tunao yatima wengi sasa huko jimboni kwetu; kwa idhini yako kama utaniruhusu naomba nitoe maelezo kidogo halafu niwaombe Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tuweze kujadili namna bora ya kuishauri Wizara ya Maliasili na Utalii, ili kuweza kuokoa maisha ya watu hawa. Kwa dhini yako naomba niendelee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo kanuni zinataka ueleze kwa dakika chache. Sasa nikijiridhisha kwamba ni jambo la dharura nitakupa nafasi utoe hoja yako.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, nitaanza na maelezo mafupi ya kwamba, Tarehe 14, Mwezi wa Nne, mama mmoja anaitwa Rose Tibenderana aliwaacha watoto wake wawili akaenda ziwani kuchota maji, ili awapikie watoto wake uji, hakurudi, akaliwa na mamba na kuwaacha watoto wawili yatima. Hivi ninavyoongea jumla ya watu 36, na majina yao ninayo hapa naweza nikakutajia wote kwa idhini yako, wameshaliwa na mamba ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, juzi tulikutana kwenye Semina ya Maliasili na Utalii juu ya wanyama wakali wanavyoshambulia watu, lakini mamba hakutajwa. Sasa ni kweli kabisa mamba analindwa na Sheria za Kimataifa. Upo mkataba unaitwa *CITES;* Mkataba wa *CITES* unawalinda mamba, lakini haki ya kuishi ya binadamu

inalindwa na Sheria na yako Maazimio ya Kimataifa ambayo yanahakikisha kwamba, haki ya kuishi ya binadamu ni lazima ilindwe na Sheria. Kwa hiyo, binadamu ni lazima aishi kwanza kabla mamba hajaishi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachokiona naanza kuhisi kama, mamba anaweza akaanza kuwa na thamani kuliko binadamu wa Buchosa. Kwa misingi hiyo ninaomba sana tutafute namna yoyote ya kujadili, kama Wabunge, ili tuweze kuishauri Wizara ya Maliasili na Utalii tutafanya nini, ili tuweze kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri ametujengea vizimba kule kwetu, lakini vizimba peke yake havitoshi. Tutafute namna ya kujadiliana hapa tutoe maelekezo kwa Wizara tuweze kuokoa maisha ya watu wetu. Nasubiri maelekezo.

**SPIKA:** Hawa watu 36 wamekufa katika kipindi gani?

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, watu 36 wamekufa ndani ya miaka mitatu.

**SPIKA:** Miaka?

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, mitatu.

**SPIKA:** Miaka mitatu.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, lakini wengi zaidi wamekufa hivi karibuni.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Eric Shigongo, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 54, akieleza maelezo ambayo kwa kutumia Kanuni ya 54, kama Mbunge, anaruhusiwa kuomba kuahirisha Shughuli za Bunge, ili kujadili jambo la dharura. Yeye katika maelezo yake anaona kwamba, jambo hili ni la dharura kwa sababu, kuna mwananchi ambaye amefariki Mwezi Aprili, ameeleza hapo. Ametaja idadi ya watu ambao wamefariki kwa kuliwa na mamba.

Waheshimiwa mnaozungumza huko nyuma tusikilizane.

Ameeleza hapa kwamba, watu 36 wamefariki kwa ujumla, lakini hii idadi ni katika kipindi cha miaka mitatu. Sasa Bunge linajali maisha hata ya mtu mmoja, siyo hoja ya idadi ya watu waliofariki. Hata kama angekuwa amefariki mtu mmoja ni kazi yetu, kama Bunge, kuishauri Serikali juu ya hatua wanazoweza kuchukua kuzuia huyo mtu mmoja kufa katika mazingira hayo.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo Kanuni ya 55 inaweka masharti ya jambo gani linaweza kujadiliwa kama jambo la dharura. Sasa mnaweza kuwa mmemsikia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hao watu wamefariki katika kipindi cha miaka mitatu na huyu ambae amefariki hivi karibuni amefariki mwezi wa nne.

Sasa siyo kwa maana ya kutokujali maisha kwa sababu, ni Mwezi wa Nne, hapana, lakini ni kwamba, jambo linaloweza kuletwa kwa dharura kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 55 ambayo inaweka masharti jambo hili linakuwa limepungua kwenye kuwa la dharura, lakini kwa sababu tunajali maisha hata ya mtu mmoja. Serikali ipo hapa ndani, leo na Jumatatu tutakuwa tukimsikiliza Mheshimiwa Waziri hapa, nafikiri Mheshimiwa Mbunge atapata nafasi ya kusema sasa yale ya wananchi halafu tutasikia Serikali inafanya nini katika jambo hili ambalo watu wamepata madhara makubwa ya kuacha yatima, kama alivyosema, lakini wengine hata kama hawakuacha yatima hoja ni kwamba, kuna uhai wa mtu ambao umepotea katika mazingira ambayo tungeweza kuzuia.

Kwa hiyo, katika kipindi hiki cha siku mbili tuendelee kuishauri Serikali hatua za ziada ambazo wanaweza kuchukua, ili hao wananchi wa Buchosa wasiendelee kupata madhara haya. Hatutaweza kulijadili kama jambo la dharura, lakini Serikali imesikia hoja hii ya Mbunge wa Buchosa na changamoto ambazo wananchi wake wanapitia. Kama iko namna ya kufanya tofauti na hivi ambavyo wanafanya sasa, basi zishauriwe kipindi hiki ambacho tutakuwa tukijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namuita Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Waziri wa Maliasili na Utalii, aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo imepitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida pamoja na miradi ya maendeleo ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu hali ya amani, upendo na utulivu pamoja na kuendelea kuwajalia afya njema viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wote, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na viongozi wengine mbalimbali wa Serikali na Wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha Hotuba yangu ya Bajeti ya Wizara ninayoiongoza ikiwa ni bajeti yangu ya kwanza tangu nipewe dhamana ya kuongoza na kusimamia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, ninaomba kutumia fursa hii adhimu kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kusimamia Wizara ya Maliasili na Utalii. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, nitaendelea kutekeleza wajibu wangu na kufanya kazi kwa uaminifu, ufanisi na uadilifu mkubwa ili kutimiza matarajio yake katika kuimarisha uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya Watanzania na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu madarakani. Nampongeza kwa kuendelea kusimamia misingi ya Taifa letu na kuyahakikishia mataifa mbalimbali kwamba Tanzania ni mahali salama pa kutembelea na kwamba ni nchi yenye fursa za uhakika za uwekezaji katika sekta ya maliasili na utalii. Fursa hizo zimejielekeza katika kuleta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Sote ni mashahidi wa jinsi uongozi wake unavyogusa Watanzania katika kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele sekta hii kwa kufanya uwekezaji mkubwa ambao umekuwa na matokeo chanya katika kuimarisha uhifadhi, kuongeza watalii na mapato hivyo kuleta manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi yetu. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, napenda kutaja mafanikio matatu makubwa yaliyotokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya maliasili na utalii chini ya uongozi wake mahiri kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka kwa idadi ya watalii ambapo idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa 96% kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi watalii 1,808,205 kwa mwaka 2023. Aidha, idadi ya watalii wa ndani waliotembelea vivutio vya utalii imeongezeka kwa 152% kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,985,707 kwa mwaka 2023. Kwa hakika hii ni rekodi kubwa sana ambayo haijawahi kufikiwa katika nchi yetu; *(Makofi)*

(ii) Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii ambapo mapato yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.3 kwa mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.4 kwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la 161% kwa watalii wa kimataifa. Aidha, mapato yatokanayo na utalii wa ndani yameongezeka kutoka shilingi bilioni 46.3 kwa mwaka 2021 hadi shilingi bilioni 175.3 kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la 279%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali uliongezeka kutoka shilingi 397,428,671,968 kwa mwaka 2020/2021 hadi shilingi 680,150,218,337 kwa mwaka 2022/2023. Vilevile, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kuanzia Julai 2023, hadi kufikia Aprili 2024, Wizara ya Maliasili na Utalii imekusanya jumla ya shilingi 750,992,839,479.75, sawa na 97.12% ya lengo la makusanyo kwa mwaka huu wa fedha. Makusanyo haya pia ni rekodi ya juu ya mapato kuwahi kuwekwa katika sekta hizi nchini. *(Makofi)*

(iii) Kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori kumeiwezesha Tanzania kuendelea kuongoza barani Afrika kwa kuwa na simba wapatao 17,000; nyati 225,000; na chui 24,000. Sambamba na hilo, takwimu zinaonesha kwamba faru wameongezeka kutoka 163 kwa mwaka 2021 hadi 252 kwa Aprili, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi jinsi uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unavyogusa Wananchi wa Tanzania kwa kuwaletea maendeleo kwa kiasi kikubwa; anavyoongoza nchi kwa ujasiri na kwa umahiri akizingatia falsafa yake ya maridhiano, mabadiliko, ustahimilivu na kujenga upya kwa kuzingatia utawala

bora na kuchochea maendeleo kiuchumi na kijamii pamoja na kuifanya nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla tuendelee kumuunga mkono Rais wetu ili aweze kutimiza maono yake ya Tanzania kuwa kinara wa utalii na uhifadhi duniani na kuwanufaisha Watanzania wote. Kwa hakika chanda chema huvikwa pete, Mheshimiwa Rais anastahili na anastahili zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini na ufuatiliaji anaoufanya katika kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kwa namna ambavyo anaendelea kuwa mstari wa mbele katika kutoa miongozo mbalimbali ya kuhakikisha maliasili zetu zinahifadhiwa na kulindwa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake thabiti na kuendelea kusimamia masuala yanayoimarisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020/2025 na maelekezo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais pamoja na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimshukuru kwa kuendelea kutuongoza vyema na kuweka dira katika utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi na uendelezaji utalii Nchini. Wahenga wanasema; "Ajipigaye hawezi kulia", Mheshimiwa Waziri Mkuu, unachapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Doto Biteko, Mbunge, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake.

Aidha, namshukuru kwa miongozo na maelekezo mbalimbali ya kuimarisha maendeleo ya Taifa letu na kuendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nikupongeze kwa dhati wewe binafsi; Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu kwa umahiri wa hali ya juu. Aidha, nitumie fursa hii kukupongeza kwa kuteuliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge ya Kitaifa Duniani (*IPU*) na kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka barani Afrika kupata kushika nafasi hiyo. Kwa hakika, umekuwa mfano wa kiongozi bora kutokana na uadilifu na weledi ulionao katika kutekeleza majukumu yako Kitaifa na Kimataifa kwa maendeleo ya nchi yetu na kwa dunia kwa ujumla. Wanasema wewe ni mwanamke na nusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoendelea kukusaidia kuongoza Shughuli za Bunge kwa ufanisi, weledi na pia kwa kutumia uzoefu mkubwa. Hakika Mheshimiwa Zungu naye pia ni johari yenye thamani kwa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza kwa ufanisi mijadala ndani ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa ushauri na maoni wanayotoa katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa ujumla wake. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu mbalimbali yanayochochea maendeleo ya Taifa letu. Aidha, niwapongeze Mawaziri wote kwa kufanikisha kupitisha bajeti za Wizara zao na niwashukuru kwa namna wanavyoshirikiana na sekta ya maliasili na

utalii katika utekelezaji wa majukumu yake kwa manufaa ya Watanzania wote. Kwa hakika nyinyi ni jeshi lisiloshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wahenga wanasema; "Usiache mbachao kwa msala upitao", kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge, Mwenyekiti wetu; Mheshimiwa Najma Giga, Mbunge na Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango, ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha sambamba na maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kushirikiana kwa karibu na Kamati hii kwa manufaa na maslahi mapana ya Taifa letu katika kuendelea kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Vilevile, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa miongozo, ushauri na mapendekezo yao katika kuhakikisha uhifadhi na usimamizi endelevu wa maliasili na malikale pamoja na uendelezaji wa utalii nchini. Niwahakikishie kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii itafanya kazi kupitia ushauri wote na mapendekezo mbalimbali ambayo mnayatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu na watendaji wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano, ubunifu, usimamizi na utekelezaji wa mikakati ya Wizara ya kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mbunge na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa kunisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu na Kamishna wa Polisi, Benedict Wakulyamba, Naibu Katibu Mkuu, kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza shughuli za kila siku za Wizara. Vilevile, nawashukuru wakurugenzi wa idara, wakuu wa vitengo, wenyeviti wa bodi, wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara na

watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao na juhudi wanazofanya kuhakikisha tunafanikisha malengo ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naliahidi Bunge lako Tukufu kwamba kwa ari na kasi tuliyonayo tutahakikisha rasilimali za maliasili zinanufaisha taifa letu kwa ujumla na kuhakikisha utalii unaendelea kukua zaidi na kuwa na mchango mkubwa zaidi katika uchumi na Pato la Taifa na ajira.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzishukuru Wizara mbalimbali tunazoshirikiana nazo ikiwemo: Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Madini; Wizara ya Maji; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; na Wizara nyingine zote. Vilevile, wadau wetu wa uhifadhi na utalii, Halmashauri za Wilaya na Mikoa kupitia kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya;

Sekta binafsi, wadau wa maendeleo, asasi zisizo za Kiserikali na wananchi wote, kwa namna ambavyo wanaendelea kushirikiana na Wizara yetu katika kuimarisha uhifadhi na utalii na kuendelea kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu kiuchumi, kijamii na kiekolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii inatambua mchango wao muhimu na itaendelea kushirikiana nao kwa karibu ili kuhakikisha uhifadhi na utalii unaendelea kustawi nchini. Mmedhihirisha msemo wa; "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuishukuru kwa dhati familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpenzi, Balozi Mbelwa Kairuki pamoja na watoto wetu Precious Kemilembe, Esther Kokubelwa na Hubert Mwesigwa kwa kunivumilia ninapokua mbali nao, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa

na Mheshimiwa Rais ya kusimamia sekta hii muhimu ya maliasili na utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kumpoteza kiongozi wetu mpendwa, Hayati Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nitoe pole tena kwa kuondokewa na Hayati Edward Lowassa aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hakika tutaendelea kuwakumbuka na kuwaenzi kwa michango yao na mambo makubwa waliyofanya katika sekta ya maliasili na utalii na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, kwa kuwapoteza Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani – Zanzibar; na Mheshimiwa Francis Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nipende kutambua mchango mkubwa kutoka kwa askari na Maafisa wa Jeshi la Uhifadhi wanaofanya kazi kubwa ya kuhakikisha maliasili zetu za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale zinahifadhiwa na kulindwa na kuendelea kupambana wakiwa kazini katika hifadhi mbalimbali zilizopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wapo vijana wetu wazalendo, ambao katika kutimiza wajibu wao kwa taifa, wakiwa hifadhini, wakilinda rasilimali za nchi, walijeruhiwa na wengine kupoteza maisha. Mashujaa wanne waliopoteza maisha ni John Munisi; Julius Katambi; Alphonce Olomi; na Samwel Nassari na waliojeruhiwa ni askari 22. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii ilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu, kushambuliwa na majangili wanaovamia maeneo ya hifadhi pamoja na ajali za vyombo vya usafiri. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliojeruhiwa na azipumzishe roho za marehemu wapendwa wetu mahali pema peponi, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, napenda kutoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki wa wale wote waliopoteza wapendwa wao kwa kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na wale wote ambao walijeruhiwa au mali zao kuharibiwa na wanyamapori katika maeneo mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaendelea kuweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha usalama wa wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu unaimarishwa na kuzingatiwa. Vilevile, kuelimisha na kushirikisha wananchi na wadau wa uhifadhi kuhusu mambo muhimu ya Sheria za Uhifadhi na ushirikishwaji katika mikakati ya Serikali ya kukabiliana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kufanya tanbihi kwa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takribani 307,800 ambazo ni sawa na 32.5% ya eneo lote la nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo haya yanajumuisha hifadhi za taifa 21, eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mapori ya akiba 29, mapori tengefu 23, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (*WMAs*) 38, ambapo tunayasimamia maeneo matatu ya ardhioevu chini ya Mkataba wa *Ramsar*. Hifadhi za

misitu ya asili 464, hifadhi za misitu ya mazingira asilia 23, mashamba ya miti ya Serikali 24, hifadhi za nyuki 14, maeneo ya malikale 142 na makumbusho za taifa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki, fukwe na urithi wa utamaduni yana mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi, urithi wa utamaduni na ukuaji wa uchumi kitaifa na kimataifa. Sekta ya Maliasili inachangia asilimia 21.5 katika Pato la Taifa ambapo asilimia 17.2 ni utalii, asilimia 4.3 ni misitu na nyuki.

Mheshimiwa Spika, pia, sekta hii inachangia asilimia 30.9 ya mapato ya fedha za kigeni ambapo asilimia 25 yanatokana na utalii, asilimia 5.9 misitu na nyuki na inaajiri takriban watu milioni 3.6 wenye ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, maeneo ya hifadhi pia ni vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe hai wengine. Aidha, sehemu kubwa ya wakazi wa Tanzania katika maeneo ya vijiji hutegemea rasilimali hizo kwa ajili ya kujikimu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 773.3. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 572.9 zinakusanywa na Wizara kupitia taasisi za *TANAPA*, Ngorongoro pamoja na *TAWA* na kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia *TRA*. Shilingi bilioni 200.4 zinakusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya mapato kutoka Idara, Mifuko na baadhi ya taasisi zake kupitia mfumo wetu wa *MNRT Portal*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2024, Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 750.9 sawa na asilimia 97.1 ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 599.6 zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya Taasisi za *TANAPA*, Ngorongoro na *TAWA*. Aidha, Shilingi bilioni 151.4 zimekusanywa na wizara kutokana na vyanzo vya idara na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa kutumia shilingi bilioni 654.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 486.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 168.2 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2024, Wizara na taasisi zake ilipokea shilingi bilioni 588.5 sawa na asilimia 89.9 ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 444.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 143.9 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 99.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 44.3 ni fedha za nje. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi bilioni 169.6 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 274.9 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafanikio ya sekta ya maliasili na utalii kwa mwaka huu wa fedha, kama nilivyoeleza awali, Serikali imefanya jitihada mbalimbali katika kuhakikisha usimamizi thabiti wa maeneo ya hifadhi za maliasili na malikale na kuendeleza utalii nchini. Kupitia jitihada hizo, Wizara ya Maliasili na Utalii imepata mafanikio mbalimbali kama ilivyoainishwa katika ukurasa wa 18 – 137 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kutaja mafanikio mengine muhimu yaliyopatikana katika mwaka huu wa fedha wa 2023/2024 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ongezeko la idadi ya watalii wa kimataifa, katika kutekeleza programu maalum ya *Tanzania-the Royal Tour* iliyoasisiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikakati mingine ya wizara na wadau, watalii wa kimataifa wameendelea kumiminika nchini ambapo idadi yao imeongezeka kwa asilimia 24.3 kutoka watalii milioni 1.4 kwa mwaka 2022 hadi watalii milioni 1.8 mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko hilo, Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi zilizovunja rekodi ya idadi ya juu zaidi ya watalii kuwahi kufikiwa kabla ya janga la UVIKO-19 kupitia kundi la *Best performing destinations January to December 2023* la Shirika la

Utalii Duniani *UN Tourism*. Tanzania imeshika nafasi ya 12 duniani na nafasi ya pili Barani Afrika kwa ongezeko la watalii ikilinganishwa na vipindi kama hivyo kwa mwaka 2019 na mwaka 2023. Rekodi hizo zimetajwa katika *World Tourism Barometer* ya Shirika la Utalii Duniani ya Januari 2024.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, taarifa ya Machi, 2024 imeonesha Tanzania imeshika nafasi ya tano duniani na nchi ya kwanza Barani Afrika, kwa ongezeko la watalii ikilinganishwa na mwaka 2019 kabla ya UVIKO-19. Kwa hakika haya ni mafanikio makubwa na sote kwa pamoja tunastahili kuvikwa mashada ya pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ongezeko la mapato yatokanayo na utalii, mapato ya jumla yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 2.5 kwa mwaka 2022 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.4 kwa Mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 36. Ongezeko hilo kwa upande wa mapato, limewezesha Tanzania kuingia katika nchi 10 bora ikiwa ni ya tatu kwa upande wa Afrika na ya tisa duniani ambazo mapato yake ya utalii yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 28 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, kwa upande wa *World Tourism Barometer* ya Machi 2024, kwa kipindi cha Januari – Machi mwaka huu 2024, Tanzania imefanikiwa kuongeza idadi ya mapato kwa asilimia 62 ikiwa ni ya 4 duniani ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha robo ya kwanza kwa mwaka 2019. Ongezeko hilo limeiwezesha Tanzania kwa upande wa mapato yatokanayo na utalii, kuwa nchi ya kwanza Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii, Wizara pia imefanikiwa kuanza utekelezaji wa uwekezaji mahiri kwenye maeneo ya wanyamapori ambapo jumla ya dola za Marekani milioni 2.7 sawa na shilingi bilioni 7.1 zimepatikana ikiwa ni ada ya vitalu zilizokusanywa tangu kusainiwa kwa mkataba tarehe 3 Januari, mwaka huu. Kwa mujibu wa mkataba katika kipindi cha miaka 20, Wizara inategemea

kuongeza mapato dola za Marekani milioni 312 sawa na dola za Marekani milioni 115.5 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu kwa upande wa Tanzania kuendelea kutangazwa kimkakati kupitia filamu na matukio, tumeendelea kutangaza utalii Kimataifa kwa kuendelea kusambaza duniani filamu ya *Tanzania - the Royal Tour* lakini pia kupitia filamu mpya ya *Amazing* Tanzania ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar wameshiriki kama wahusika wakuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, msanii mahiri wa filamu wa Nchini China Bw. Jin Dong ameshiriki kuitangaza Tanzania kupitia filamu hiyo. Filamu hiyo ya *Amazing Tanzania* imelenga kuitangaza katika Ukanda wa Asia, hususan soko la China linalozalisha zaidi ya watalii milioni 80 Kimataifa. Hatua hiyo inaenda sambamba na utekelezaji wa Programu ya *Tanzania - the Royal Tour* katika kukuza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzinduzi wa filamu hiyo ya *Amazing Tanzania*, ulifanyika tarehe 15 Mei, 2024 Jijini Beijing – China, sambamba na Maadhimisho ya Miaka 60 ya Kidiplomasia kati ya Tanzania na China. Lakini pia *Amazing Tanzania* itazinduliwa pia Tanzania hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania pia imeongoza katika ubunifu kwa kutangaza utalii kupitia uandaaji wa matukio maalum kwa kushirikiana na wadau ikiwemo *Epic Tanzania Tour* iliyofanyika Disemba, 2023, katika Hifadhi yetu ya Taifa ya Serengeti. Tukio hilo lilihusisha watalii na wawekezaji takriban 80 wakiongozwa na mchezaji Veterani wa Tennis Bw. John McEnroe. Pia nchi yetu iliweza kutangazwa kupitia *tour* hiyo kimataifa katika vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo jarida maarufu la *World Tennis Magazine*, tovuti ya *Forbes* na gazeti la *The Times* la Uingereza ambayo ni mojawapo ya masoko makubwa ya utalii wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nne, kufuatia utekelezaji madhubuti wa Kanuni za Matumizi ya Uvunaji wa Wanyamapori na masharti ya

Mkataba wa *CITES – Tanzania*, imefanikiwa kuingia katika kundi la kwanza la nchi wanachama zenye Sheria zinazotekeleza Mkataba wa *CITES* kikamilifu. Hatua hii itaiwezesha Tanzania kufanya biashara ya uwindaji wa kitalii na mataifa ambayo yameweka masharti ya kupokea nyara kutoka kwenye nchi ambazo sheria zake ziko katika kundi la kwanza.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na kutatua migogoro ya mipaka ambapo Wizara imeweza kushirikiana na wananchi na kufanikiwa kumaliza migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji katika mapori ya akiba Swagaswaga, Mkungunero, Wamimbiki, Igombe, Liparamba, Mpanga Kipengere, *Selous*, Hifadhi ya Taifa Serengeti na vijiji 112 vinavyozunguka Hifadhi za Misitu 32.

Mheshimiwa Spika, sita tumeweza kuimarisha shughuli za upandaji miti ambapo Tanzania ili kuweza kuendelea kuwa Tanzania ya kijani, kama Wizara tumeweza kuzalisha jumla ya tani 17.9 za mbegu za miti ya spishi mbalimbali. Wizara tumeweza pia kukuza miche milioni 34.1 ambayo tumeipanda katika mashamba yote 24 ya Serikali na mingine tumeigawa kwa wananchi, taaasisi na mashirika kwa ajili ya kupandwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Mkutano Mkuu wa 48 wa Shirikisho la Wafugaji Nyuki Duniani uliofanyika tarehe 4 – 8 Septemba, mwaka jana katika Jiji la Santiago Chile, Tanzania ilishinda na kuidhinishwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 50 wa Shirikisho la *APIMONDIA*. Sambamba na mkutano huo, shirikisho litakuwa likisheherekea *Jubilee* ya Miaka 50 tangu kuanza kwa mikutano yake. Mkutano huo utakaofanyika Tanzania mwaka 2027, unatarajiwa kuhudhuriwa na washiriki takribani 6,000 kutoka mataifa zaidi ya 130 duniani.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kupitia mkutano huo, tutaweza kupata faida mbalimbali zikiwemo kuhamasisha na kuimarisha matumizi ya teknolojia za ufugaji nyuki na kuongeza thamani ya mazao ya nyuki, kuimarisha mtandao wa masoko ya mazao ya nyuki ndani na nje ya nchi na kuongeza kiwango cha mazao

kitakachouzwa nje ya nchi, pia kuhamasisha ufugaji nyuki kibiashara na kuongeza ajira hasa kwa vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa shughuli za ufugaji nyuki na biashara ya mazao ya asali, Wizara pia tumefanikiwa kuboresha shughuli za ufugaji nyuki na biashara ya asali kwa masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kutoa mafunzo ya usimamizi wa manzuki pamoja na kuimarisha ufuatiliaji wa shughuli za uzalishaji na utunzaji wa taarifa za manzuki kwa kutumia mfumo wa *honey traceability*.

Mheshimiwa Spika, aidha Wizara imefanikiwa kukusanya na kupeleka sampuli 70 za asali kutoka katika Wilaya 34 kwenye maabara ya kimataifa Ujerumani ili kupima ubora wake. Matokeo yanaonesha asilimia 96 ya sampuli hizo zilizopelekwa zimekidhi viwango vya ubora wa kimataifa na hivyo kutoa fursa kwa asali ya Tanzania kuendelea kuuzwa katika masoko mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kufunguka kwa utalii wa malikale Kusini mwa Tanzania, Wizara tumeendelea kuhakikisha kwamba maeneo ya malikale yanaendelea kukidhi vigezo vya kimataifa na kuvutia watalii. Vilevile tumeweza kupandisha hadhi eneo la Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, lenye hadhi ya urithi wa dunia kuwa miongoni mwa maeneo yenye mahusiano ya kisayansi kati ya binadamu na mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadhi hiyo imetolewa na *UNESCO* mwezi Julai, 2023 na kuongeza idadi ya maeneo yenye sifa hiyo nchini kutoka matano hadi sita. Mafanikio hayo yamechochea shughuli za utalii wa malikale kwa kuongeza idadi ya watalii wa Kimataifa katika eneo la Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, hususan kupitia utalii wa meli.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utatuzi wa migogoro inayotokana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, pamoja na kwamba tumepata mafanikio mbalimbali katika eneo hilo, Wizara imekuwa ikikabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu ambapo pamoja na mambo mengine, tumeandaa mkakati wa kifaita wa

kusimamia utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanayamapori wa mwaka 2020 – 2024.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mkakati huo, wizara imejenga mabwawa 32 katika mapori ya akiba na hifadhi mbalimbali za Taifa. Mabwawa haya yamesaidia kupunguza matukio ya wanyamapori hususan kipindi cha kiangazi ambapo wanyamapori hutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na chakula. Nafahamu eneo hili linavyogusa Waheshimiwa Wabunge wengi na nawahakikishia kwamba Wizara hatulali kukabiliana nalo na kazi zaidi zifuatazo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2023, wizara ilijenga vituo 16 na kufanya jumla ya vituo kufika 154 vikijumuisha Ofisi za Kanda. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha, tunaendelea na ukamilishaji wa vituo 6 na ujenzi wa vituo 10 katika Wilaya 10 katika hatua mbalimbali za awali. Sambamba na hilo, Wizara tumeweka vituo vya muda vya askari *(ranger stations)* katika maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu ili kudhibiti matukio ya wanyamapori kwa haraka katika Wilaya 40 ambazo zina changamoto zaidi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vituo hivi ni endelevu kwa maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, tumeongeza idadi ya askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kutoka 139 waliokuwepo mwaka 2022/2023 hadi 437 kwa mwaka huu wa fedha. Tumeongeza Askari Wanyamapori wa Vijiji *(VGS)* kutoka 95 hadi 184. Lakini pia tunawashirikisha *VGS* katika doria za mwitikio wa haraka ambao umeweza kudhibiti matukio 6,401 ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya 73.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika jitihada za kuokoa maisha ya watu na mali zao wakati wa kudhibiti matukio tajwa niliyoyaeleza, jumla ya wanyamapori wakali na waharibifu 113 walivunwa wakiwemo nyati 18, tembo 23, viboko 28, mamba 21, simba 3, fisi 9, chui mmoja pamoja na nyani 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi tumekuwa tukitumia helikopta kuwaondoa wanyamapori hususan tembo katika maeneo ya makazi na katika mashamba ya wananchi. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Mei 2024, takriban tembo 451 waliondolewa kwenye maeneo ya wananchi katika Wilaya 4 na kurejeshwa katika maeneo ya hifadhi. Matumizi ya helikopta yamesaidia sana hivyo ka kutambua hilo, Wizara tumepanga kununua helikopta 2 mpya ili kuongeza juhudi hizi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara ilihamisha simba 10 waliokuwa wanahatarisha maisha ya wananchi katika eneo la Vilima Vitatu Wilaya ya Babati. Kati ya hao, simba 3 walirudishwa katika Hifadhi ya Taifa Tarangire na simba 7 tuliwapeleka katika Pori letu la Akiba Rungwa. Kwa upande mwingine, chui mmoja alihamishwa kutoka Kijiji cha Robanda kwenda katika Dar es Salaam *Zoo* ili kuimarisha usalama wa wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia tunaendelea kutumia teknolojia ya kufuatilia mienendo ya wanyamapori wakiwemo tembo kwa kuwafunga mikanda maalum ya mawasiliano *(GPS-Satellite Collars)* ili kupata taarifa za moja kwa moja na kuwadhibiti kabla ya kusababisha madhara kwa binadamu. Hadi Mei mwaka huu, jumla ya tembo 35 kwa mwaka huu wa fedha, yumeweza kufunga viongozi wa makundi wa tembo mikanda maalumu ya mawasiliano katika mifumo ikolojia 8.

Mheshimiwa Spika, mikanda hii ya *GPS-Satellite Collars*, imekuwa ikionesha mahali walipo ili kuwafuatilia na kuwadhibiti kabla ya madhara kutokea ambapo tumeweza kupitia kufunga mikanda hii kuzuia matukio 318.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla katika kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu, jumla ya shilingi bilioni 45.14 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa helikopta mbili, uchimbaji wa mabwawa 30 katika Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba na Ujenzi wa vizimba 50 katika maeneo yenye changamoto kubwa ya mamba na viboko katika Halmashauri za Wilaya 18. Aidha, Wizara itaendelea kutumia teknolojia katika

kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kununua ndege zisizo na rubani au *drones* 16 na mikanda maalum ya mawasiliano *GPS Satellite Collars* 100 kwa ajili ya kufuatilia mienendo ya wanyamapori hao na haswa tembo.

Mheshimiwa Spika, mikanda hiyo itafungwa kwa tembo viongozi katika maeneo ya Kusini, Kaskazini na Kanda ya Ziwa. Vilevile, tutanunua na kusambaza vifaa vya kudhibiti tembo yakiwemo mabomu baridi 35,000. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi Tanzania tumeboresha kilipuzi au bomu baridi ili kudhibiti tembo wanapoingia katika maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, bomu hilo lilizinduliwa rasmi tarehe 13 Mei, mwaka huu. Baada ya uzinduzi huo tarehe 22 Mei mwaka huu Wizara yetu ilikabidhiwa rasmi mabomu baridi 4,000 katika Makao Makuu ya Shirika la Mzinga-Morogoro ili kuanza kutumika katika Halmashauri 20 zilizo katika mifumo ikolojia mitano. Aidha, mafunzo ya jinsi ya kutumia mabomu hayo baridi yameshatolewa kwa maafisa 433 wakiwemo Askari wa Wanyamapori wa Vijiji, Maafisa Wanyamapori wa Wilaya na Askari wa Jeshi la Uhifadhi na kupewa jumla ya mabomu baridi 1,450 mpaka sasa kwa ajili ya kuingia uwandani. Zoezi hili hivi sasa litaendelea pia katika maeneo mengine yenye changamato ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha huu tunao malizia Wizara imeongeza idadi wa Askari wa Uhifadhi kwa kuajiri jumla ya Askari 488 na kuwapanga kwenye vituo mbalimbali kwa ajili ya shughuli za uhifadhi. Ikiwemo kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Wizara imeweka utaratibu maalum wa wananchi kutoa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kupitia namba maalum za kupiga simu bila malipo ambapo katika miaka hii miwili ya fedha tumepokea taarifa za matukio 1,082 na tuliweza kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi tunaendelea kuzijengea uwezo jamii zetu ili waweze

kudhibiti wanyamapori, wakali na waharibifu kwa kutoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2023/2024 jumla ya askari wanyamapori wa vijiji au *(VGS)* 882 wamepatiwa mafunzo maalum juu ya uhifadhi na mbinu za kujikinga na wanyamapori hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tumeweza kutoa elimu katika mikutano ya wananchi 1,646 ili kuhamasisha katika vijiji 740 kwenye Wilaya 85 na tuliweza kuwafikia wananchi 576,918. Mafunzo hayo yatasaidia kuongeza nguvu na ufanisi katika kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu na tunaamini itapunguza madhara yatokanayo na wanyamapori hao.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine tutaongeza ajira za Askari wa Uhifadhi 850 ili kuimarisha uhifadhi na doria za kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Pia, tutaendelea na ujenzi wa vituo 10 vya askari katika Wilaya za Mbarali, Kalambo, Kilwa, Bariadi, Manyoni, Kilosa, Rufiji, Morogoro Vijijini, Babati pamoja na Monduli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kutekeleza Mpango wa Miaka mitano wa Taifa wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori ili kuimarisha ustawi wa wanyamapori na kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. Hadi kufikia Aprili mwaka huu, uongoaji wa shoroba nane kati ya 20 za kipaumbele upo katika hatua mbalimbali na shoroba moja ipo katika hatua ya kuidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada nyingine za kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara tumeendelea kuboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori kwa kudhibiti ueneaji wa mimea vamizi katika maeneo ya Hifadhi za Taifa lakini pia katika eneo la Hifadhi la Ngorongoro. Hatua hii imeimarisha upatikanaji wa malisho ya wanyamapori na kuwafanya kutumia muda mwingi zaidi ndani ya Hifadhi badala ya kutoka nje kutafuta malisho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi bilioni 2.4 zimelipwa kwa wananchi 10,552 waliopata

madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya 48. Aidha, Wizara tumefanya mapitio ya Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011 kwa kuongeza viwango vya malipo kwa asilimia 50 kwa matukio ya majeraha ya muda, uharibifu wa mazao na vifo vya mifugo lakini pia tumeongeza kwa asilimia 100 kwa majeraha ya kudumu na vifo. Maelezo ya kina yanapatikana katika Hotuba yangu kuanzia ukurasa wa 19 hadi ukurasa wa 28. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya Ngorongoro imeendelea kuhamasisha wananchi wanaoishi ndani ya eneo la Ngorongoro kuhama kwa hiyari kwenda katika maeneo yaliyotengwa na Serikali ikiwemo Msomera, Saunyi pamoja na Kitwai na maeneo mengine ambayo wananchi wanayachagua. Hadi kufikia Aprili mwaka huu Serikali ilikwishatoa shilingi bilioni 286.6 ili kuwezesha zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa tayari nyumba 1,000 zimeshakamilika Msomera lakini vilevile tunakamilisha ujenzi wa nyumba zingine 1,500 Msomera.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Ngorongoro itaendelea pia kusimamia zoezi hili la wananchi wanaohama kwa uhiyari kwa kuendelea kutoa programu ya utoaji wa elimu, kuhamasisha wananchi kuhama kwa hiyari lakini pia kuandikisha na kuthaminisha maendelezo katika vijiji 25 vya eneo la Ngorongoro. Pia, tutaendelea kulipa stahiki ya fidia na motisha kwa wananchi wanaojiandikisha kuhama katika eneo la Hifadhi kwa hiyari.

Mheshimiwa Spika, pia, tutaendelea kukamilisha nyumba 2,500 za Msomera, Kitwai na Saunyi ili wananchi watakaohama kwa hiyari waweze kuelekea katika maeneo hayo na tutatoa chakula kwa miezi 18 kwa kaya zote zitakazokuwa zilihama kwa hiyari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka ujao wa fedha tutaendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi kupitia matangazo katika ligi na mashindano ya michezo yenye wafuatiliaji wengi zaidi duniani.

Tutatumia watu mashuhuri na wenye ushawishi, Mabalozi wa hiari wa utalii, vyombo vya habari vya Kimataifa vyenye ushawishi pamoja na mitandao ya kimataifa ya utalii kama vile *TripAdvisor* na *Expedia Group,* vyombo vya habari kama *CNN* na vingine. Aidha, tutaendelea kushiriki katika maonyesho na matukio ya utalii na kutangaza utalii kupitia Mashirika ya Ndege ya Kimataifa ikiwemo *Qatar Airways, Emirates,* pamoja na *Turkish Airlines* ambapo kwa sasa tunakamilisha makubaliano nao na kupitia pia mikutano ya habari. Pia, tunaendelea kukamilisha taratibu za kujitangaza kupitia ligi za michezo Duniani za Marekani na Uingireza na kupitia matukio makubwa ya burudani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea pia kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki ikiwemo kupandisha hadhi Hifadhi za Misitu, kuwa Hifadhi za Misitu Mazingira Asilia. Tutaandaa mipango ya usimamizi wa misitu, tutaendeleza doria za ki-intelijensia katika Hifadhi zetu za misitu na nyuki. Pia, tutaweka mifumo maalum ya mawasiliano katika misitu ya hifadhi zetu za asili na mashamba ya miti ili kuweza kubaini moto na kutoa elimu ya uhifadhi na kupambana na kuzuia matukio ya moto lakini pia tutaanza utekelezaji wa programu yetu ya miaka 10 ya nyuki kwa ajili ya vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutatangaza pia maeneo 11 kuwa Urithi wa Taifa, tutahuisha taarifa za maeneo 21 yaliyotangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa katika Mikoa ya Dodoma, Singida na Lindi. Pia, tutaandaa miongozo na taratibu za kutwaa na kuhamisha umiliki wa rasilimali za malikale kutoka kwa wamiliki kwenda kwa wadau ili kuendeleza shughuli za uhifadhi na kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera yetu ya mambo ya kale na kujenga Makumbusho ya Marais hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mazingira ya biashara ya utalii nchini yanaimarika kuendana na matokeo chanya ya Filamu ya *Tanzania the Royal Tour* tumekuwa tukifanya vikao na wadau wa sekta mbalimbali na kupata maoni yao na kuyafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kufanya juhudi za makusudi kimageuzi na kufanya maboresho kama ifuatavyo: -

(i) Tumeendelea kutekeleza maelekezo yaliyoainishwa katika Mpango wa Kitaifa wa Kuboresha Mazingira ya Biashara katika Utalii, Maliasili na Misitu;

(ii) Tumechukua juhudi mahususi za kuboresha Kanuni na Sheria ikiwemo Kanuni za Tozo za Utalii za Mwaka 2015 na maboresho yake ya Mwaka 2017 na Kanuni za Usajili na Ulipaji wa Leseni za Wakala wa Biashara za utalii za Mwaka 2015 na maboresho yake ya Mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, maeneo mahususi yatakayoboreshwa na utekelezaji wake utaanza Julai, 2024 na mengine kuanzia Desemba, 2024 kama itakavyoainishwa baadaye katika kanuni ni pamoja na kuhuisha muda wa kulipa Ada ya Leseni ya Biashara za utalii na kuwa katika kipindi cha miezi 12 kuanzia siku ya mwisho ambayo wakala wa biashara za utalii amelipia leseni yake badala ya utaratibu wa sasa ambapo hata kama mtu amekata leseni Novemba zote zinafikia ukomo Desemba, kupunguza Ada ya Leseni ya Biashara za utalii kwa wakala wa kupandisha watalii mlimani *(mountain climbing)*, kufuta tozo kwa waongoza watalii wenye leseni hai kila wanapoingia hifadhini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hapa tutafuta Tozo hiyo ya *park entry fees* kwa waongoza utalii au *tour guides*. Wadau wa utalii, kulipa Ada ya Leseni ya Biashara za utalii kwa kutumia shilingi za Tanzania badala ya Dola za Kimarekani na kuongeza muda wa Leseni ya Biashara za utalii kwa Waongoza watalii ambapo kwa sasa leseni yao itadumu kwa kipindi cha miaka mitatu badala ya mwaka mmoja wa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua umuhimu wa Sekta ya Maliasili na Utalii katika kuchangia Pato la Taifa. Hivyo, pamoja na maboresho haya, maboresho mengine yanayohusu kodi mbalimbali katika Sekta zetu ikiwemo masuala ya uwindaji, masuala ya misitu, utalii na nyuki yataainishwa kwenye Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali itakapowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Niwahakikishie wadau wa Utalii, Misitu na Malikale na Maliasili tuko nao pamoja milele na daima hatutawaacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 968.8 kwenye Idara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha Wizara inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 348.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 250.9 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 97.2 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Mishahara shilingi bilioni 125.4 na Matumizi Mengineyo shilingi bilioni 125.5. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha shilingi bilioni 18.1 fedha za ndani na shilingi bilioni 79.2 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 250.9 zinajumuisha shilingi bilioni 30.7 kwa ajili ya Wizara na shilingi bilioni 220.2 kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, shilingi bilioni 8.5 ni Mishahara na shilingi bilioni 22.2 ni Matumizi Mengineyo. Fedha za taasisi zinajumuisha shilingi bilioni 116.9 za Mishahara na shilingi 103.3 za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 348,125,419,000 kwa matumizi ya Fungu 69 la Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025. Kati ya fedha hizo, shilingi 250,884,083,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 97,241,336,000 ni za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha shilingi 125,366,391,000 za Mishahara na shilingi 125,517,692,000 za Matumizi Mengineyo. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha shilingi 18,074,661,000 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, napenda tena kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa mara nyingine tena kwa namna ambavyo ameendelea kutoa dira na maelekezo ili kuimarisha zaidi Sekta yetu ya Maliasili na Utalii na kuwezesha kufikia malengo yetu. Natumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaoutoa katika kuliongoza Bunge letu. Pia, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao

mbalimbali inayolenga kuiboresha zaidi Sekta yetu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu nitumie nafasi hii tena kipekee kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa hakika Naibu Waziri wangu amekuwa msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu wakati wote, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kusimamia vyema utekelezaji wa kazi mbalimbali za Wizara. Niwashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara, Wenyeviti wa Bodi zetu zote chini ya Taasisi, Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinipatia wakati wote na juhudi wanazozifanya kuhakikisha kwamba tunatimiza ifuatavyo majukumu. Nawaomba waendelee na juhudi hizo ili tuweze kutimiza malengo tuliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, nipende pia kuzishukuru nchi rafiki, Jumuiya za Kikanda, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali na Wadau wengine wakiwemo Sekta Binafsi kwa ushirikiano wao katika kukuza na kuendeleza Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii ili kuchochea maendeleo ya jamii na uchumi wa nchi kwa ujumla. Nawashukuru sana Serikali ya Canada, China, Umoja wa Falme za Kiarabu, Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, Ujerumani, Uswizi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende pia kuchukua nafasi hii kuyashukuru na kuyatambua Mashirika na Taasisi za Kimataifa ikiwemo *AfDB, AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, RTI, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNTourism, IORA, USAID, Honey Guard Foundation, CIFOR, ICRAF, INBAR, GATSBY, FOREST-FARM FACILITY, SIX RIVERS, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF* na *WWF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wadau wetu wa ndani wa Maliasili na Utalii wakiwemo *TCT, TATO, HAT, TAHOA, TLTO, TTGA, KGA, NTSGS, IGS, TGS, KTGA, NGTF, KPA, TPO, TACTO, TAOA, TAWTO, TWEA, CWMAC, TABEDO, TAF, TTGAU, API-SUPPORT, HEAT, SHIVIMITA, Nature Tanzania* na wadau wote wanaoshiriki kikamilifu katika uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji na utangazaji ikiwemo ofisi zetu za Ubalozi nje ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho niwashukuru pia viongozi wote wa dini na kimila kwa namna ambavyo wamekuwa wakihakikisha rasilimali zetu zikiwemo wanyamapori, misitu na malikale zinaendelea kulindwa na kuhifadhiwa kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vijavyo. Wamekuwa mstari wa mbele kupiga vita shughuli zinazoharibu mazingira ikiwemo ukataji miti hovyo, uchomaji wa mikaa kiholela na kufanya shughuli za kilimo ndani ya Hifadhi kinyume na sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine natambua mchango mkubwa unaotolewa na wenzetu wa Vyuo Vikuu, Vyo vya Kati, Shule za Sekondari na Msingi kwa namna ambavyo wamejikita katika utunzaji wa rasilimali misitu na nyuki kwa kuanzisha vitalu vya miti na miradi ya ufugaji nyuki katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, natambua mchango wa Taasisi za Tafiti kwa namna zinavyoshirikiana na Wizara kutafuta majawabu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta yetu. Kipekee niwashukuru sana Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Taasisi za Hima Sheria na Vyombo vya Habari kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu. Niwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika Uhifadhi wa Maliasili, Malikale na Uendelezaji Utalii.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili kuweza kutimiza majukumu yake kikamilifu. Tunatambua michango inayotolewa na wadau hawa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Niwashukuru sekta zote tulizoshirikiana nazo katika kutekeleza majumu yetu, lakini pia wananchi kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha nipende kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kushiriki katika uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji wa utalii. Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: https://www.maliasili.go.tz

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo imepitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**2. Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kuendelea kuijalia Nchi yetu hali ya amani, upendo na utulivu pamoja na kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wanaoongoza Wizara mbalimbali, Manaibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge, Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali na Viongozi wengine wa Serikali na Wananchi kwa ujumla. Vilevile, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na

kuwasilisha Hotuba yangu ya Bajeti ya Wizara ninayoiongoza ikiwa ni bajeti ya kwanza tangu nipewe dhamana ya kuongoza na kusimamia Wizara hii.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutumia fursa hii adhimu kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kusimamia Wizara ya Maliasili na Utalii. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, nitaendelea kutekeleza wajibu wangu na kufanya kazi kwa uaminifu, ufanisi na uadilifu mkubwa ili kutimiza matarajio yake katika kuimarisha uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya Watanzania na Taifa kwa ujumla.

4. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima ninaomba nitumie fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka 3 madarakani. Aidha, nimpongeze kwa kuendelea kusimamia misingi ya Taifa letu na kuyahakikishia mataifa mbalimbali kuwa Tanzania ni mahali salama pa kutembelea na kuwa ni Nchi yenye fursa za uhakika za uwekezaji katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Fursa hizo zimejielekeza katika kuleta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Sote ni mashahidi wa jinsi uongozi wake unavyogusa Watanzania katika kuwaletea maendeleo.

5. **Mheshimiwa Spika**, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta hii kwa kufanya uwekezaji mkubwa ambao umekuwa na matokeo chanya yenye mchango mkubwa katika kuimarisha uhifadhi, kuongeza watalii na mapato hivyo kuleta manufaa makubwa kwa uchumi wa Nchi yetu. Pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana napenda kutaja mafanikio 3 makubwa kutokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wake mahiri kama ifuatavyo:-

**(i)** **Kuongezeka kwa idadi ya watalii** ambapo idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa asilimia 96 kutoka watalii 922,692

Mwaka 2021 hadi watalii 1,808,205 Mwaka 2023. Aidha, idadi ya Watalii wa Ndani waliotembelea vivutio vya utalii imeongezeka kwa asilimia 152 kutoka watalii 788,933 Mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,985,707 Mwaka 2023.

**(ii)** **Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii** ambapo mapato yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 1.3 Mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.4 Mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 161 kwa watalii wa kimataifa. Pia, mapato yatokanayo na utalii wa ndani yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 46.3 Mwaka 2021 hadi Shilingi bilioni 175.3 Mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 279. Aidha, **ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali** uliongezeka kutoka Shilingi 397,428,671,968 Mwaka 2020/2021 hadi Shilingi 680,150,218,337 Mwaka 2022/2023. Vilevile, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kuanzia Julai 2023, hadi kufikia Aprili 2024, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 750,992,839,479.75** sawa na **asilimia 97.12** ya lengo la makusanyo.

**(iii)** **Kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori** kumeiwezesha Tanzania kuendelea kuongoza barani Afrika kwa kuwa na simba wapatao 17,000; nyati 225,000; na chui 24,000. Sambamba na hilo, takwimu zinaonesha kuwa faru wameongezeka kutoka 163 Mwaka 2021 hadi 252 Aprili, 2024.

**6.** **Mheshimiwa Spika,** sote ni mashahidi kwa jinsi uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unavyogusa wananchi wa Tanzania kwa kuwaletea maendeleo kwa kiasi kikubwa, anavyoongoza Nchi kwa ujasiri, umahiri akizingatia adhima yake ya maridhiano, mabadiliko, ustahimilivu na kujenga upya kwa kuzingatia utawala bora na kuchochea maendeleo kiuchumi na kijamii pamoja na kuifanya Nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote tuendelee kumuunga mkono Rais wetu ili kutimiza maono yake ya Tanzania kuwa kinara wa utalii na uhifadhi duniani na kuwanufaisha Watanzania wote.

**7. Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini na ufuatiliaji anaoufanya katika kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kutoa miongozo mbalimbali ya kuhakikisha maliasili zetu zinahifadhiwa na kulindwa.

**8. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake thabiti na kuendelea kusimamia masuala yanayoimarisha Muungano wetu.

**9. Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani amekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 – 2025 na maelekezo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais pamoja na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimshukuru kwa kuendelea kutuongoza vyema na kuweka dira katika utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi na uendelezaji utalii Nchini.

**10. Mheshimiwa Spika,** nampongeza pia, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumsaidia Waziri Mkuu kutekeleza majukumu yake. Aidha, namshukuru kwa miongozo na maelekezo mbalimbali ya kuimarisha maendeleo ya Taifa letu na kuendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025.

**11. Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze kwa dhati wewe binafsi, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu kwa umahiri wa hali ya juu. Aidha, nitumie fursa hii kukupongeza kwa kuteuliwa kuwa Rais wa 31 wa Muungano wa Mabunge ya Kitaifa Duniani (IPU) na mwanamke wa kwanza kutoka barani Afrika kushika nafasi hiyo.

Kwa hakika, umekuwa mfano wa kiongozi bora kutokana na uadilifu na weledi ulionao katika kutekeleza majukumu yako kitaifa na kimataifa kwa maendeleo ya Nchi yetu na dunia kwa ujumla.

**12. Mheshimiwa Spika,** nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kukusaidia kuongoza shughuli za Bunge kwa ufanisi, weledi na uzoefu mkubwa.

**13. Mheshimiwa Spika,** pia niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuongoza kwa ufanisi mijadala ndani ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa ushauri na maoni wanayotoa katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa ujumla wake.

**14. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Manaibu Waziri kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu mbalimbali yanayochochea maendeleo ya Taifa letu. Aidha, niwapongeze kwa kufanikisha kupitisha bajeti za Wizara zao na niwashukuru kwa namna wanavyoshirikiana na Sekta ya Maliasili na Utalii katika utekelezaji wa majukumu yake kwa manufaa ya Watanzania wote.

**15. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.) Mwenyekiti; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wa Kamati kwa michango, ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka huu wa Fedha sambamba na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka ujao wa Fedha. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kushirikiana kwa karibu na Kamati hii kwa manufaa na maslahi mapana ya Taifa letu katika kuendelea kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Vilevile, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa miongozo, ushauri na mapendekezo yao katika kuhakikisha

uhifadhi na usimamizi endelevu wa maliasili na malikale pamoja na uendelezaji wa utalii Nchini. Niwahakikishie kuwa Wizara itafanyia kazi ushauri na mapendekezo mbalimbali yanayotolewa.

**16. Mheshimiwa Spika,** sina budi kuwashukuru kwa dhati Viongozi wenzangu na Watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano, ubunifu, usimamizi na utekelezaji wa mikakati ya Wizara ya kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula (Mb.), Naibu Waziri kwa kunisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Dkt. Hassan Abbas, Katibu Mkuu; na Kamishna wa Polisi, Benedict Wakulyamba, Naibu Katibu Mkuu kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli za kila siku za Wizara.

Vilevile, nawashukuru Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro – NCAA, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCTA na Shirika la Makumbusho ya Taifa – NMT na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao na juhudi wanazofanya kufanikisha malengo ya Wizara. Ninaliahidi Bunge lako Tukufu kuwa kwa ari na kasi tuliyonayo tutahakikisha rasilimali za maliasili zinanufaisha Taifa letu kwa ujumla na kuhakikisha utalii unaendelea kukua zaidi na kuwa na mchango mkubwa zaidi katika uchumi, Pato la Taifa na Ajira.

**17. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuzishukuru Wizara mbalimbali tunazoshirikiana nazo zikiwemo: Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na

Mazingira, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wizara ya Madini, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Wadau wetu wa uhifadhi na utalii, Halmashauri za Wilaya na Mikoa, Sekta binafsi, wadau wa maendeleo na Asasi zisizo za Kiserikali, NGO's na wananchi wote kwa kuendelea kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuimarisha uhifadhi na utalii na kuendelea kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Nchi yetu kiuchumi, kijamii na kiikolojia. Wizara ya Maliasili na Utalii inatambua mchango wao muhimu na itaendelea kushirikiana nao kwa karibu ili kuhakikisha uhifadhi na utalii unaendelea kustawi Nchini.

**18. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuishukuru kwa dhati familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpenzi, Balozi Mbelwa Kairuki pamoja na watoto wetu Precious Kemilembe, Esther Kokubelwa na Hubert Mwesigwa kwa kunivumilia ninapokua mbali nao, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ya kusimamia sekta hii muhimu ya Maliasili na Utalii.

**19. Mheshimiwa Spika,** ninaomba nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kumpoteza Kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nitoe pole tena kwa kuondokewa na Hayati Edward Ngoyai Lowassa aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika tutaendelea kuwakumbuka na kuwaenzi kwa michango yao na mambo makubwa waliyofanya katika Sekta ya Maliasili na Utalii na Taifa kwa ujumla.

**20. Mheshimiwa Spika,** nitumie pia nafasi hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa na wananchi kwa

kuwapoteza Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani – Zanzibar; na Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**21. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kutambua mchango mkubwa kutoka kwa Askari na Maafisa wa Jeshi la Uhifadhi wanaofanya kazi kubwa ya kuhakikisha maliasili zetu za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale zinahifadhiwa na kulindwa na kuendelea kupambana wakiwa kazini katika hifadhi mbalimbali zilizopo Nchini. Katika Mwaka huu wa Fedha wapo vijana wetu wazalendo, ambao katika kutimiza wajibu wao kwa Taifa wakiwa hifadhini wakilinda rasilimali za Nchi walijeruhiwa na wengine kupoteza maisha. Mashujaa 4 waliopoteza maisha ni John Eugen Munisi; Julius Katambi; Alphonce Olomi; na Samwel Edward Nassari na waliojeruhiwa ni Askari 22. Hali hii ilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu, kushambuliwa na majangili wanaovamia maeneo ya hifadhi pamoja na ajali za vyombo vya usafiri.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliojeruhiwa na azipumzishe roho za marehemu wapendwa wetu mahali pema peponi, Amina.

**22. Mheshimiwa Spika,** pia, ninatoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki wa wale wote waliopoteza wapendwa wao kwa kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na wale wote ambao walijeruhiwa au mali zao kuharibiwa na wanyamapori hao katika maeneo mbalimbali hapa Nchini. Nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kuweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha usalama wa wananchi dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu unaimarishwa na kuzingatiwa. Vilevile, kuelimisha na kushirikisha wananchi na wadau wa uhifadhi mambo muhimu kuhusu Sheria za Uhifadhi na ushirikishwaji katika mikakati ya Serikali ya kukabiliana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

**23.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

**24. Mheshimiwa Spika**, kulingana na Muundo wa Wizara ya Maliasili na Utalii ulioidhinishwa Januari 2022, jukumu kuu la Wizara ni kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili za wanyamapori, misitu, nyuki, malikale na kuendeleza utalii. Majukumu mengine ni pamoja na:-

(i) Kuandaa na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo mbalimbali inayolenga uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki, malikale na maendeleo ya utalii;

(ii) Kusimamia ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu kwa kufanya doria ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu;

(iii) Kujenga uwezo wa Sekta ya Maliasili na Utalii ili iweze kusimamia rasilimali za maliasili na malikale, kuendeleza utalii, kufanya tafiti na kutoa mafunzo kupitia vyuo vilivyo chini ya Wizara;

(iv) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili, utalii na malikale;

(v) Kushirikisha wadau mbalimbali katika utunzaji na uhifadhi wa maliasili na malikale kwa kutoa elimu na huduma za ugani; na

(vi) Kukuza na kuendeleza mazao ya utalii, kuimarisha utangazaji na kuboresha huduma za utalii kwa lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**25. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takriban 307,800 sawa na asilimia 32.5 ya eneo lote la Nchi. Maeneo haya yanajumuisha Hifadhi za Taifa 21, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 38 ambapo kati ya hizo 22 zimeidhinishwa na 16 ziko kwenye hatua mbalimbali za kuidhinishwa, maeneo 3 ya Ardhioevu chini ya Mkataba wa Ramsar, Hifadhi za Misitu ya Asili 464, Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 23, Mashamba ya Miti ya Serikali 24, Hifadhi za Nyuki 14, Maeneo ya Malikale 142 na Makumbusho za Taifa 7.

**26. Mheshimiwa Spika,** maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki, fukwe na urithi wa utamaduni yana mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi, urithi wa utamaduni na ukuaji wa uchumi kitaifa na kimataifa. Sekta ya Maliasili na Utalii inachangia asilimia 21.5 katika Pato la Taifa ambapo asilimia 17.2 ni utalii, asilimia 4.3 ni misitu na nyuki. Vilevile, Sekta hii inachangia asilimia 30.9 ya mapato ya fedha za kigeni ambapo asilimia 25 yanatokana na utalii, asilimia 5.9 misitu na nyuki; na kuajiri watu takriban milioni 3.6 wenye ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa Mwaka. Kwa upande mwingine, maeneo ya hifadhi pia ni vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe hai wengine. Aidha, sehemu kubwa ya wakazi wa Tanzania katika maeneo ya vijijini hutegemea rasilimali hizo kwa ajili ya kujikimu.

**27. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 - 2025, Sera na Sheria mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), Mikataba ya Kikanda na Kimataifa na maelekezo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

**28. Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 3.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**29. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 773,268,687,704.92.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 572,905,619,470.92** zinakusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia TRA; na **Shilingi 200,363,068,234** zinakusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya mapato kutoka Idara, Mfuko wa NFA na Taasisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCTA na Shirika la Makumbusho ya Taifa - NMT kupitia mfumo wa MNRT Portal.

**30. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Aprili 2024, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 750,992,839,479.75** sawa na **asilimia 97.12** ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 599,605,179,102.43** zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA. Aidha, **Shilingi 151,387,660,377.32** zimekusanywa na Wizara kutokana na Idara, Mifuko na Taasisi zake kupitia mfumo wa MNRT Portal.

### 3.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**31. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya**Shilingi 654,668,208,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 486,501,449,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya

Kawaida na **Shilingi 168,166,759,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**32. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili 2024, Wizara na taasisi zake ilipokea jumla ya **Shilingi 588,527,337,033.19** sawa na asilimia **89.9** ya fedha iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 444,586,950,250.95** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 143,940,386,782.24** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **Shilingi 169,594,347,552.16** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 274,992,602,698.79** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

### 3.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

#### 3.3.1 Sekta ya Wanyamapori

**33. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya tafiti za wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Sekta hii inasimamia Hifadhi za Taifa 21, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, maeneo 3 ya ardhioevu na bustani 5 za wanyamapori za Serikali. Aidha, Sekta hii inasimamia shughuli za uhifadhi katika maeneo 38 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori, mashamba 4 ya ufugaji wa wanyamapori, bustani 32 za wanyamapori, maeneo 26 ya mazalia ya wanyamapori pamoja na ranchi 5 za sekta binafsi.

**34. Mheshimiwa *Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya sekta ya wanyamapori hufanywa na Idara ya Wanyamapori, Shirika la Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Aidha, utekelezaji wa jukumu hili unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya Mwaka 2007 na kusimamiwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura ya 283; Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura ya 284; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania Sura

ya 260; na Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Sura ya 209.

### 3.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

**35. Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la migongano baina ya binadamu na wanyamapori katika maeneo mbalimbali Nchini. Migongano hiyo imekuwa ikiathiri pato la kaya, uchumi wa Nchi na kuleta taharuki pale wanyamapori wanapoingia katika maeneo ya wananchi. Tafiti zimeonesha visababishi vikuu vya migongano ni ukosefu na kutokuzingatiwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi, kuzibwa kwa mapito ya wanyamapori, kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu karibu na maeneo yaliyohifadhiwa na maeneo ya mtawanyiko, uingizaji wa mifugo kwenye maeneo yaliyohifadhiwa, mabadiliko ya tabia nchi na ongezeko la mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa. Katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara inatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori wa Mwaka 2020 – 2024.

**36. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Mkakati huo, Wizara kupitia TAWA na TANAPA imejenga mabwawa 32 katika Pori la Akiba Kizigo 10 (Wilaya ya Manyoni); Pori la Akiba Mkungunero 1 (Wilaya ya Kondoa); Hifadhi ya Taifa Ruaha 20 (Wilaya za Mbarali, Chunya na Iringa Vijijini); na Hifadhi ya Taifa Mkomazi 1 (Wilaya ya Same). Mabwawa haya yamesaidia kupunguza matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu hususan kipindi cha kiangazi ambapo wanyamapori hutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na chakula.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha shughuli za uhifadhi ikiwemo udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu Wizara ina jumla ya vituo 154 vinavyojumuisha Ofisi za Kanda. Kati ya hivyo, vituo 16 vimejengwa Mwaka 2022/2023 katika Wilaya za Meatu, Itilima, Busega, Lindi, Rufiji, Liwale, Tunduru, Nachingwea, Mwanga, Songwe, Iringa Vijijini, Nzega, Mvomero, Chamwino, Mpwapwa na Kondoa. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara kupitia Taasisi zake za TANAPA na NCAA imeendelea na

ukamilishaji wa vituo 6 katika Wilaya za Korogwe, Same, Serengeti, Bunda Vijijini, Namtumbo na Ruangwa.

Ujenzi wa vituo 10 katika Wilaya za Mbarali, Kalambo, Kilwa, Bariadi, Manyoni, Kilosa, Rufiji, Morogoro Vijijini, Babati na Monduli upo katika hatua za awali. Aidha, Wizara kupitia TAWA imekuwa ikiweka vituo vya muda vya askari (ranger stations) kwenye maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa ajili ya kudhibiti matukio ya wanyamapori kwa haraka katika Wilaya 40 zikiwemo Manyoni, Morogoro Vijijini, Chalinze, Meatu, Bariadi, Buchosa, Tunduru, Liwale, Mbarali, Korogwe, Handeni, Simanjiro na Babati ambazo zina changamoto zaidi. Ujenzi wa vituo hivi ni endelevu kwa maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu.

**38. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara kupitia taasisi zake imeongeza idadi ya askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kutoka 139 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi 437 Mwaka wa Fedha 2023/2024; na kuongeza askari wanyamapori wa Vijiji (Village Game Scout - VGS) kutoka 95 hadi 184. Ushirikishwaji wa VGS katika doria za mwitikio wa haraka zimewezesha kudhibiti matukio 6,401 ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya 73. Aidha, katika jitihada za kuokoa maisha ya watu na mali zao wakati wa kudhibiti matukio tajwa, jumla ya wanyamapori wakali na waharibifu 113 walivunwa wakiwemo nyati 18, tembo 23, viboko 28, mamba 21, simba 3, fisi 9, chui 1 na nyani 10.

**39. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi imekuwa ikitumia helikopta kuwaondoa wanyamapori hususan tembo katika maeneo ya makazi na mashamba ya wananchi kwa kutumia helikopta. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Mei 2024, takriban tembo 451 waliondolewa kwenye maeneo ya wananchi kwa kutumia helikopta katika Wilaya za Same 200, Bunda 90, Mvomero 100, Mbarali 61 na kurejeshwa katika maeneo ya hifadhi.

Aidha, tembo 3 viongozi wa makundi yaliyoondolewa Mvomero (1) na Mbarali (2) wamefungwa mikanda maalum ya mawasiliano ili kufuatilia mienendo yao.




Waziri wa Maliasili na Utalii (kushoto) akishiriki zoezi la kuwaondoa tembo kwenye maeneo ya wananchi Wilaya ya Mbarali na kuwarejesha katika maeneo ya hifadhi.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara kupitia Taasisi zake (TAWA, TANAPA na TAWIRI) ilihamisha simba 10 waliokuwa wanahatarisha maisha ya wananchi katika eneo la Vilima Vitatu katika Wilaya ya Babati. Kati ya hao, simba 3 walirudishwa ndani ya Hifadhi ya Taifa Tarangire na simba 7 walipelekwa Pori la Akiba Rungwa. Kwa upande mwingine, chui 1 alihamishwa kutoka Kijiji cha Robanda kwenda Dar es Salaam Zoo ili kuimarisha usalama wa wananchi katika maeneo yao.

**41. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori - TAWIRI imeendelea kutumia teknolojia ya kufuatilia mienendo ya wanyamapori wakiwemo tembo kwa kuwafunga Mikanda Maalum ya Mawasiliano (GPS-Satellite Collars) ili kupata taarifa za moja kwa moja na kuwadhibiti kabla ya kusababisha madhara kwa binadamu. Hadi kufikia Mei 2024, jumla ya tembo 35 viongozi wa makundi wamefungwa mikanda Maalumu ya Mawasiliano katika Mifumo Ikolojia ya Tarangire-Manyara, Serengeti - Mara, NyerereSelous-Mikumi, Mkomazi, Katavi-Rukwa-Lukwati, Mahale-Katavi, Burigi Chato-Moyowosi-Kigosi na Ruaha-Rungwa. Mikanda hii huonesha mahali walipo kwa ajili ya kuwafuatilia na kuwadhibiti kabla ya madhara kutokea ambapo jumla ya matukio 318 yaliweza kuzuiliwa.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Dkt. Eblate Ernest Mjingo akimfunga tembo kiongozi wa kundi mkanda wa mawasiliano (GPS Satellite Collars) ili kufuatilia mienendo ya tembo katika Mfumo Ikolojia wa Serengeti.

**42. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara kwa kushirikiana na JWTZ imeboresha kilipuzi (bomu baridi) kwa ajili ya kudhibiti tembo wanapoingia kwenye maeneo ya wananchi. Aidha, bomu hilo lilizinduliwa rasmi tarehe 13 Mei, 2024 na baada ya uzinduzi tarehe 22 Mei 2024 Wizara ilikabidhiwa rasmi mabomu baridi 4,000 katika Makao Makuu ya Shirika la Mzinga-Morogoro kwa ajili ya kuanza kutumika kwenye Halmashauri 20 zilizo katika mifumo ikolojia 5 Nchini. Halmashauri za Wilaya hizo ni pamoja na Nachingwea, Liwale, Manispaa ya Lindi (Mchinga), Mtama, Ruangwa, Tunduru, Namtumbo, Karatu, Same, Mwanga, Mvomero, Mkinga, Korogwe, Meatu, Busega, Itilima, Bariadi, Bunda Mjini, Bunda Vijijini na Karagwe. Zoezi hili litaendelea katika maeneo mengine yenye changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu.

**43. Mheshimiwa Spika,** hadi tarehe 24 Mei, 2024 jumla ya maafisa 433 wakiwemo Askari wa Wanyamapori wa Vijiji, Maafisa Wanyamapori wa Wilaya na Askari wa Jeshi la Uhifadhi kutoka Kanda ya Kusini, Kanda ya Mashariki, Kanda ya Magharibi na Kanda ya Kaskazini wameshapata mafunzo ya matumizi ya Mabomu Baridi. Aidha, jumla ya Mabomu Baridi 1,450 yamegawiwa kwa watumishi hao kwa ajili ya kuingia uwandani na kuanza kuondoa tembo kwenye makazi ya wananchi.




Picha ya kwanza kushoto Waziri wa Maliasili na Utalii akikabidhiwa mojawapo ya bomu baridi na Luteni Jenerali Mstaafu Samwel Ndomba na picha ya pili kulia ni baadhi ya Wabunge wanaotoka kwenye majimbo yenye changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu wakifurahia tukio hilo.

**44. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imeongeza idadi ya askari wa uhifadhi kwa kuajiri jumla ya askari **488** (TANAPA **217** TAWA **108** TFS **92** na NCAA **71**) na kuwapanga kwenye vituo mbalimbali kwa ajili ya shughuli za uhifadhi ikiwemo kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Wizara imeongeza vitendea kazi ikiwemo magari 12 na pikipiki 10 kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hiyo.

**45. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara imeweka utaratibu maalum wa wananchi kutoa taarifa za matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kupitia namba maalum za kupiga simu bila malipo. Utaratibu huo umewekwa katika Kanda za kiutendaji za Taasisi za Uhifadhi TAWA 8, TANAPA 4, NCAA 1 na Wizarani 1 ili kuwezesha wananchi kutoa taarifa na kupata msaada wa haraka. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2023/2024, jumla ya taarifa za matukio 1,082 zilipokelewa na kufanyiwa kazi.

**46. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi inaendelea kuzijengea uwezo jamii kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji. Katika kipindi cha Mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 jumla ya Askari Wanyamapori wa Vijiji 882

wamepatiwa mafunzo maalum juu ya uhifadhi na mbinu za kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu.

Aidha, elimu hiyo pia imetolewa katika mikutano 1,646 ya uhamasishaji iliyofanyika katika Vijiji 740 katika Wilaya 85 na kufanikiwa kuwafikia wananchi 576,918. Mafunzo hayo yatasaidia kuongeza nguvu na ufanisi katika udhibiti wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu na hivyo kupunguza madhara yatokanayo na wanyamapori hao.

**47. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022 – 2026 ili kuimarisha ustawi wa wanyamapori na kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori. Utekelezaji wa Mpango huo, unahusisha Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira; Wizara za Kilimo; Wizara ya Maji; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Uchukuzi; Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Hadi kufikia Aprili 2024, zoezi la uongoaji wa shoroba 8 ambazo ni: Udzungwa – Nyerere, Katavi – Mahale, Ruaha – Katavi, Rungwa – Ruaha, Tarangire – Manyara (Kwakuchinja), Ngorongoro – Manyara (Upper Kitete) na Lake Manyara – Ngorongoro (Yaeda Chini) kati ya 20 za kipaumbele lipo katika hatua mbalimbali. Aidha, shoroba 1 ya Udzungwa – Nyerere ipo katika hatua ya kuidhinishwa.

**48. Mheshimiwa Spika,** kutokana na baadhi ya Vijiji vinavyopakana na maeneo yaliyohifadhiwa kutokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Wizara kupitia TANAPA imewezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 74 vinavyopakana na Hifadhi za Taifa za Serengeti 37, Ziwa Manyara 25 na Tarangire 12. Utekelezaji wa mipango hii utasaidia kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu Wizara imeendelea kuboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori kwa kudhibiti ueneaji wa mimea vamizi katika eneo lenye hekta

2,909.89 katika Hifadhi za Taifa Burigi-Chato, Katavi, Mikumi, Ruaha, Kisiwa cha Rubondo, Kisiwa cha Saanane, Serengeti na Mto Ugalla; na hekta 866.68 katika Eneo la Hifadhi la Ngorongoro. Hatua hii imeimarisha upatikanaji wa malisho ya wanyamapori na kuwafanya kutumia muda mwingi ndani ya Hifadhi badala ya kutoka nje kutafuta malisho.

**50. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Mei, 2024, jumla ya Shilingi **2,400,258,500** zimelipwa kwa wananchi 10,552 waliopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya 48. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za Mwaka 2011 kwa kuongeza viwango vya malipo kwa asilimia 50 kwa matukio ya majeraha ya muda, uharibifu wa mazao na vifo vya mifugo na asilimia 100 kwa majeraha ya kudumu na vifo.

**51. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi, ulinzi, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, kwa kuandaa na kuzindua Mkakati wa Kutekeleza Sera ya Taifa ya Wanyamapori wa Mwaka 2023-2033. Mkakati huo unatoa dira na mwelekeo wa Serikali katika kusimamia rasilimali za wanyamapori ili kuhakikisha kuwa Sekta ndogo ya wanyamapori inaendelea kuleta manufaa ya kiuchumi kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

**52. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Wizara imeandaa Mpango wa Usimamizi wa Tembo wa Mwaka 2023-2033 kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi wa tembo; Mpango wa Utekelezaji wa Kutafuta Fedha wa Mwaka 2023-2033 kwa ajili ya kutekeleza Mkakati wa Kuzuia Ujangili wa Mwaka 2023-2033; na Mkakati wa Kusimamia Maeneo ya Hifadhi za Jamii – WMAs wa Mwaka 2023-2033.

**53. Mheshimiwa Spika,** Tanzania imefanikiwa kuingia katika Kundi la Kwanza (Category I) la Nchi wanachama zenye Sheria zinazotekeleza Mkataba wa CITES kikamilifu. Hatua hii itaiwezesha Tanzania kufanya biashara ya uwindaji wa kitalii na mataifa ambayo yameweka masharti ya kupokea nyara kutoka kwenye Nchi ambazo Sheria zake ziko katika Kundi la Kwanza.

### 3.3.1.2 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

**54. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kusimamia Hifadhi za Taifa kwa kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa maliasili. Hadi kufikia Aprili 2024, Shirika limefanya doria 47,847 ambapo jumla ya watuhumiwa 3,323 wa makosa mbalimbali ya ujangili walikamatwa wakiwa na silaha aina mbalimbali. Aidha, mitego 3,103 aina ya nyaya inayotumika kutega wanyamapori katika hifadhi iliteguliwa. Juhudi hizi zimewezesha kupungua kwa matukio ya ujangili yakiwemo ya tembo kutoka tembo 4 Mwaka 2022 hadi tembo 2 kwa Aprili 2024. Vilevile, Shirika limeendelea kutumia teknolojia za kisasa katika kuimarisha usimamizi na ulinzi wa wanyamapori ikiwemo matumizi ya visukuma mawimbi, doria za kutumia ndege na kuweka alama za masikio kwa faru. Aidha, katika juhudi za kupunguza ujangili kwa kushirikiana na wananchi, Shirika limeanzisha vikundi 17 vya ulinzi shirikishi katika Hifadhi za Taifa Ruaha 4, Nyerere 3, Mkomazi 3, Mto Ugalla 2, Ibanda-Kyerwa 2 na Kilimanjaro 3.

**55. Mheshimiwa Spika,** Shirika limetatua changamoto ya mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa Serengeti na Vijiji 7 vya Wilaya ya Serengeti. Vijiji hivyo ni pamoja na Bisarara, Nyamburi, Bonchugu, Mbalibali, Machochwe, Nyamakendo na Merenga. Aidha, Shirika limeendelea kuimarisha mipaka ya hifadhi kwa kuweka jumla ya vigingi 216: Hifadhi ya Taifa Serengeti 184 kwenye eneo linalopakana na Vijiji vya Kegonga, Nyandage, Kenyamosabi, Masanga, Karakatonga, Gibaso na Nyabirongo katika Wilaya ya Tarime; na Hifadhi ya Taifa Tarangire 32 kwenye eneo linalopakana na Vijiji vya Gijedabong na Kimotorok. Aidha, Shirika limefanya uhakiki wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa upande unaopakana na Mikoa ya Ruvuma, Pwani, Morogoro na Lindi. Vilevile, Shirika limekamilisha kazi ya uthamini wa eneo la Ghuba ya Speke lenye ukubwa wa kilomita za mraba 138 ili kuliunganisha na Hifadhi ya Taifa Serengeti.

**56. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuimarisha uhifadhi na kuboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori, Shirika limeng'oa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,216.15 katika Hifadhi za Taifa Burigi-Chato 162, Katavi 308,

Mikumi 110.05, Ruaha 324, Kisiwa cha Rubondo 80, Kisiwa cha Saanane 17, Serengeti 178 na Mto Ugalla 37.1. Aidha, jumla ya hekta 521,250 zilichomwa kwa mioto ya awali (prescribed burning) kwa utaratibu wa moto mpango (fire management plan) kwa lengo la kuimarisha nyanda za malisho katika Hifadhi za Taifa za Kitulo, Ziwa Manyara, Milima ya Mahale, Mikumi, Nyerere, Kisiwa cha Rubondo, Saadani, Tarangire na Milima ya Udzungwa. Vilevile, Shirika limedhibiti matukio 76 ya moto katika maeneo ya Hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Mikumi, Katavi, Mkomazi, Serengeti, Milima ya Udzungwa na Tarangire. Pamoja na juhudi hizi, Shirika limeendelea kutoa elimu kwa jamii zinazozunguka hifadhi za Taifa kwa kufanya Mikutano 841 yenye jumla ya Washiriki 76,289 katika Vijiji 718 kwenye Wilaya 31 ikiwemo namna ya kudhibiti moto, uhifadhi na utunzaji mazingira. Aidha, jumla ya kilomita 412.6 za makinga moto zililimwa katika Hifadhi za Taifa 5: Arusha (40.1), Gombe (8), Mkomazi (263), Burigi-Chato (6) na Tarangire (95.5) ili kudhibiti kuenea kwa moto.

**57. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Shirika limeendelea na jitihada za kuvutia wawekezaji katika huduma za malazi ambapo wawekezaji 27 wamepatikana na wanaendelea na ujenzi. Aidha, jumla ya huduma za malazi (loji 4, kambi za kudumu 23) zenye vitanda 1,148 zinajengwa katika Hifadhi za Taifa 5: Serengeti 780, Ruaha 170, Tarangire 100, Saadani 50 na Mikumi 48. Sambamba na hilo, Shirika linaendelea na ujenzi wa nyumba 3 za kulala wageni za gharama nafuu zenye jumla ya vitanda 178 katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Mikumi na Ruaha; hosteli katika Hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Saadani na Nyerere; pamoja na vituo 3 vya kutolea taarifa katika Hifadhi za Taifa Serengeti, Ruaha na Mikumi.

**58. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza idadi ya watalii na mapato, Shirika limeibua na kuendeleza mazao mbalimbali ya utalii. Mazao yaliyoibuliwa ni pamoja na utalii wa michezo ikiwemo Tennis kwa kutumia uwanja wa kuhamishika (tennis mobile court) na kuendelea kwa ujenzi wa awamu ya kwanza ya uwanja wa mchezo wa Golf unaotarajiwa kukamilika Disemba, 2024 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Vilevile, ujenzi wa daraja la

juu linalounganisha vilima na miti (Canopy walkway) katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Udzungwa unaendelea.

**59. Mheshimiwa Spika**, kufuatia jitihada mbalimbali za Wizara zilizofanyika, Shirika limevutia watalii ambapo hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya Watalii 1,598,608 walitembelea hifadhi za Taifa sawa na ongezeko la asilimia 11.4 ikilinganishwa na Watalii 1,435,069 waliotembelea katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2022/2023. Vilevile, Shirika limekusanya mapato ya Shilingi 353,441,080,170.15 sawa na ongezeko la asilimia 21.58 ikilinganishwa na mapato ya Shilingi 290,698,543,140.17 zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**60. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Shirika limeimarisha na kuendeleza miundombinu ya utalii kwa kufungua barabara mpya zenye urefu wa kilometa 694.5 katika Hifadhi ya Taifa Nyerere; ujenzi wa vituo 8 vya askari katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Mto Ugalla, Burigi-Chato, Ruaha, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe; na nyumba 29 za watumishi katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Ruaha, Mkomazi, Mto Ugalla, Gombe na Tarangire. Aidha, barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 3,631 zimekarabatiwa katika Hifadhi za Taifa Arusha, Ziwa Manyara, Katavi, Kilimanjaro, Tarangire, Ruaha, Saadani, Burigi-Chato, Mikumi, Rumanyika-Karagwe, Serengeti na Mkomazi; na njia za kupandia milima zenye urefu wa kilomita 157 zimekarabatiwa. Vilevile, Shirika limefanya ukarabati wa viwanja 12 vya ndege katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Serengeti, Katavi, Tarangire na Mkomazi. Ujenzi wa viwanja vya ndege 4 katika Hifadhi za Taifa Ruaha 2, Mikumi 1 na Nyerere 1 unaendelea.

**61. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuboresha huduma kwa watalii na watumishi. Shirika limejenga mfumo wa usambazaji maji safi kwa watumishi katika Hifadhi ya Taifa Ruaha; malango mapya 4 katika Hifadhi za Taifa Nyerere 1, Mikumi 2 na IbandaKyerwa 1 na ujenzi wa Ofisi ya Utawala Kanda ya Kusini. Vilevile, Shirika liko katika hatua ya ukamilishaji wa ujenzi wa malango 8 katika Hifadhi za Taifa Tarangire (lango la Mamire); Ibanda-Kyerwa (lango la

Kifurusa); Nyerere (lango la Msolwa na Likuyu); Mikumi (lango la Kikwaraza na Doma) pamoja na Serengeti (lango la Kleins na Machochwe). Shirika limeendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji maduhuli katika malango yote ya hifadhi za Taifa ikiwemo uwekaji wa mifumo ya malango janja (smart gates) 6 katika Hifadhi za Taifa Serengeti 3, Ziwa Manyara 1 na Tarangire 2.

**62. Mheshimiwa Spika,** Shirika katika kukuza utalii, limeendelea kushiriki na kushirikiana na wadau wa utalii katika kuandaa maonesho na matukio mbalimbali ikiwemo ushiriki wa Ruaha Great Marathon pamoja na matukio mbalimbali ya kimichezo yaliyoratibiwa na Wizara. Kwa upande mwingine, Hifadhi ya Taifa Serengeti imeendelea kupokea tuzo za Africa's Leading National Park inayotolewa na World Travel Awards mara 5 mfululizo kuanzia Mwaka 2019, 2020, 2021, 2022 na 2023; Best Nature Destination World 2023 inayotolewa na Trip Advisor; Tuzo ya Ubora wa Kimataifa inayotolewa na European Society for Quality Research (ESQR) mara 4 mfululizo kuanzia Mwaka 2020 (Gold category), 2021 (Platinum category), 2022 (Diamond category) na mara nyingine tena 2023 (Diamond category); na tuzo ya Top Attractions kwa Afrika 2023 iliyotolewa na Trip Advisor kwa Hifadhi za Taifa Serengeti na Tarangire.

**63. Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Shirika linaendelea kutekeleza miradi 108 ya ujirani mwema katika sekta za elimu, afya, usalama, maji na barabara yenye thamani ya jumla ya Shilingi bilioni 40.7 ambapo Shilingi bilioni 36.5 kupitia ufadhili wa mradi wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) na Shilingi bilioni 4.2 kupitia fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya miradi hiyo, miradi 75 imekamilika, miradi 10 iko katika hatua za ukamilishaji na miradi 23 ipo katika hatua ya awali ya utekelezaji. Aidha, miradi iliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa vyumba 44 vya madarasa na ofisi 16 za walimu katika Wilaya za Serengeti, Ngorongoro, Bariadi, na Bunda; mabweni 4 ya wasichana katika shule za sekondari na msingi zilizopo Wilaya za Mpanda, Same, Mwanga na Serengeti; na nyumba 15 zenye uwezo wa kukaa familia 30 za walimu katika Wilaya za Serengeti 9 na Ngorongoro 6. Aidha, Shirika limewezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Vijiji

74 vinavyopakana na hifadhi za Taifa Serengeti 37, Ziwa Manyara 25 na Tarangire 12.

**64. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Shirika limewezesha Vikundi 166 vya kiuchumi vya jamii katika Wilaya za Chamwino 9, Iringa 25, Kilolo 9, Kilombero 56, Kilosa 15, Mvomero 10, Morogoro 26, Meatu 3, Itilima 9 na Busega 4. Aidha, jumla ya Shilingi bilioni 3.22 zimetolewa kwa vikundi husika kwa lengo la kuvisaidia kuimarika kiuchumi ili kuweza kujiendesha na kupunguza utegemezi wa rasilimali za wanyamapori na misitu. Vilevile, vikundi 16 vya Wilaya za Itilima 9, Meatu 3 na Busega 4 vilipatiwa jumla ya mizinga ya nyuki 300 pamoja na vifaa vingine vikiwemo mavazi ya kinga 60, vifaa vya ukaguzi (bee smoker-75, honey filter-15 na tool hives-60), vifaa vya uchakataji mazao (bee pressing machine-15) pamoja na ndoo 300 za kutunzia asali.





Makabidhiano ya mizinga 25 ya kufugia nyuki kwa kikundi cha "Hapa Kazi" Wilaya ya Bunda na mizinga ya nyuki 200 kwa vikundi 3 vya Wilaya ya Kigoma.

**65. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mahusiano kati ya Hifadhi na wananchi, Shirika lilishiriki kikamilifu katika shughuli za uokoaji wa maafa yaliyotokana na maporomoko ya udongo huko Hanang. Shirika lilitoa vifaa vya uokozi ikiwemo mitambo (Grader na Excavator) na vikosi 3 vyenye Askari 27. Aidha, Shirika kupitia Msajili wa Hazina liliwasilisha mchango wa Shilingi 10,000,000 ili kusaidia waathirika.

**66. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za uhifadhi na utalii, Shirika limeendelea kuandaa na kuhuisha

mipango ya ujumla ya usimamizi na uendelezaji (General Management Plans) wa Hifadhi za Taifa. Katika kipindi cha Julai hadi Aprili, 2024 Shirika limekamilisha mapitio ya mipango ya ujumla ya usimamizi na uendelezaji wa Hifadhi za Taifa za Ruaha na Nyerere. Aidha, mapitio ya mpango wa usimamizi na uendelezaji wa Hifadhi ya Taifa Mkomazi upo katika hatua za ukamilishaji.

### 3.3.1.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania –TAWA

**67. Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti ujangili na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa, Mamlaka imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori kwa kufanya doria mbalimbali na kutumia vikosi vya mwitikio wa haraka. Hadi kufikia Aprili 2024, doria 11,593 sawa na asilimia 80 ya lengo la doria 14,487 zimefanyika. Kupitia doria hizo, jumla ya mifugo 41,294, watuhumiwa 2,304, bunduki 91 na risasi 276 zimekamatwa pamoja na kutegua mitego 2,056 ya nyaya za kutegea wanyamapori.
Kufuatia kuimarika kwa ulinzi katika maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka, idadi ya vifo vya tembo wanaouawa kwa ujangili imepungua kutoka tembo 6 kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi tembo 3 Aprili 2024. Vilevile, Mamlaka imekarabati kilomita 764.5 za barabara za doria katika Mapori ya Akiba Kizigo na Selous na ujenzi wa chumba maalum cha ufuatiliaji wa faru katika Pori la Akiba Maswa. Katika hatua nyingine, Mamlaka imenunua pikipiki 10 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi pamoja na kuwapatia mafunzo ya kijeshi ya ukakamavu na utayari askari wa wanyamapori 458.

**68. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kutatua migogoro ya mipaka katika maeneo ya hifadhi, Mamlaka imeweka alama za mipaka ambapo hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya vigingi 726 vimesimikwa katika Mapori ya Akiba ya Igombe 117, Liparamba 60, Mpanga Kipengere 160 na Kilombero 389. Aidha, migogoro ya mipaka kati ya Vijiji na Mapori ya Akiba Swagaswaga, Mkungunero, Wamimbiki, Igombe, Liparamba, Mpanga Kipengere na Selous imemalizika. Kwa upande mwingine, Mamlaka imelipa fidia jumla ya Shilingi 348,149,727.35 kwa kaya 93 kati ya Shilingi 511,567,707.34 za kulipa kaya 145 kutoka katika

Kitongoji cha Ndaja (Kijiji cha Keikei) na Vitongoji vya Kagera na Msumbiji (Kijiji cha Kisondoko) kwa ajili ya kuhama kutoka Pori la Akiba Mkungunero. Vilevile, Serikali imememega eneo lenye ukubwa wa ekari 103,544.48 kutoka katika Mapori ya Akiba Swagaswaga 8,890.26, Mkungunero 12,466, Wamimbiki 17,752.41, Mpanga Kipengere 51,007.51, Liparamba 8,154.3 na Uwanda 5,274 na kurejesha kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo, makazi na ufugaji.

**69. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha miundombinu ya ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, Mamlaka imejenga kituo 1 cha askari katika Pori la Akiba Swagaswaga; vivuko 15 (Pori la Akiba Lukwati 8 na Bustani ya Wanyamapori Ruhila 7); maghala 4 ya silaha (Igombe, Lukwika Lumesule, Mpanga Kipengere na Lwafi); karakana 2; daraja lenye urefu wa mita 20 katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere; lango la watalii na makasha (Cage) 3 za wanyamapori (simba, chui na mamba) katika Pori la Akiba Pande. Katika hatua nyingine, Mamlaka imekamilisha uandaaji wa Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa Pori la Akiba Moyowosi. Aidha, uandaaji wa Mpango wa Jumla wa Usimamizi wa Mapori ya Akiba Maswa, Ugalla na Kilombero unaendelea kwa kushirikisha wadau.

**70. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeendelea kushiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji katika maeneo yake. Miongoni mwa Maonesho hayo ni pamoja na;- Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2023), Dallas Safari Club International - USA na maonesho ya ndani ya Nchi. Kufuatia juhudi hizo, idadi ya watalii wa picha waliotembelea maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka imeongezeka kutoka watalii 139,749 Aprili 2023 hadi kufikia 157,725 Aprili, 2024. Aidha, Mamlaka imeshiriki katika kikao cha 77 cha Kamati Kuu ya Mkutano wa 19 wa Nchi wanachama wa CITES ambao unatoa fursa ya kujadili uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori.

**71. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeendelea kukusanya mapato yatokanayo na shughuli za utalii ambapo hadi kufikia

Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 57,647,139,960.28 sawa na asilimia 73.54 ya lengo la Mwaka zimekusanywa. Aidha, katika kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii, Mamlaka imesaini mikataba 6 ya Uwekezaji Mahiri kwenye Maeneo ya Wanyamapori (Special Wildlife Investment Concession Areas - SWICA) katika vitalu vya Ikorongo, Grumeti, Maswa Mbono, Maswa Kimani, Maswa North, Mkungunero na Selous-LL1. Hatua hiyo imewezesha Mamlaka kukusanya jumla ya Dola za Marekani 2,773,000 sawa na Shilingi bilioni 7.1 ikiwa ni ada ya vitalu tangu kusainiwa kwa mikataba tarehe 03 Januari, 2024. Uwekezaji huu unatarajiwa kuongeza mapato kufikia Dola za Marekani milioni 312 kwa mujibu wa mkataba katika kipindi cha miaka 20 ya uwekezaji sawa na wastani wa Dola za Marekani milioni 15.5 kwa Mwaka.

**72. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine Mamlaka iligawa vitalu kwa njia ya mnada wa kielektroniki ambapo jumla ya vitalu 3 vya daraja la II (1) na la III (2) viliuzwa kwa thamani ya Dola za Marekani 163,000 ikilinganishwa na Dola za Marekani 66,000 ambazo zingekusanywa kwa kugawa vitalu hivyo kwa njia ya utawala (administrative allocation). Mauzo kwa njia ya mnada wa kielektroniki yanawezesha soko kuamua thamani ya vitalu vya uwindaji wa kitalii hivyo kuongeza mapato na uwazi katika ugawaji wa vitalu.

**73. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha mahusiano kati ya hifadhi na jamii na kuhakikisha wananchi wananufaika na uhifadhi, Serikali imeendelea kurejesha stahili kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori 13 Halmashauri za Wilaya 29 na Vijiji 71 ambapo jumla ya Shilingi 7,349,380,416.73 zilitolewa. Aidha, TAWA imechangia Shilingi 110,991,120 kwa ajili ya miradi ya maendeleo iliyoibuliwa na wananchi. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na ununuzi wa madawati 160 katika Wilaya ya Bunda 100 na Morogoro 60; mchango wa ununuzi wa mashine 2 za Kusaga Mkoa wa Mara; kuchangia ujenzi wa zahanati 1 na darasa 1 Wilaya ya Bunda; na ujenzi wa zahanati ya Bungu Wilaya ya Korogwe. Vilevile, Mamlaka ilitoa mkono wa pole wa jumla ya Shilingi 10,000,000 kwa waathirika wa mafuriko katika Wilaya ya Hanang na ununuzi wa vyakula na magodoro kwa waathirika wa

mafuriko katika Wilaya ya Rufiji ikiwa ni sehemu ya kugusa jamii zinazopata madhila.

**74. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeendelea kuimarisha mahusiano na wananchi kwa kutoa vibali vya ufugaji nyuki na uvuvi endelevu katika mapori ya akiba kwa kutoa jumla ya vibali 33,682 vya kufanya shughuli za uvuvi na ufugaji nyuki katika Mapori ya Akiba ya Ugalla 198, Uwanda 11,593, Moyowosi 1,213, Inyonga 64, Rukwa 17,716 na Kilombero 2,898 ambapo jumla ya wavuvi 8,046 na wafugaji nyuki 2,472 walipewa vibali. Kupitia vibali hivyo, Mamlaka imekusanya mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 1.49. Mathalan, katika Pori la Akiba la Uwanda pekee wananchi wamekuwa wakinufaika kwa kuvua wastani wa tani 10 za samaki kwa siku hivyo kuongeza ajira na kipato wakati wa msimu wa uvuvi.

**75. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa ofisi 4 katika Mapori ya Akiba Msanjesi, Moyowosi, Lukwika Lumesule na Igombe, nyumba 7 za watumishi katika Mapori ya Akiba Rukwa 2, Ugalla 2, Igombe 2 na Selous 1, kuchimba visima 7 na kuweka mtandao wa maji katika Mapori ya Akiba Lukwika Lumesule 1, Kijereshi 2 na Maswa 4. Aidha, Mamlaka imewezesha watumishi 297 kuhudhuria mafunzo. Kati ya hao, watumishi 48 ni mafunzo ya muda mrefu na watumishi 249 mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

### 3.3.1.4 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro – NCAA

**76. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, Mamlaka imeendelea kufanya doria 251 zilizowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 339 wa makosa mbalimbali, mifugo 16,683, silaha 1 - riffle, magazine 4, meno ya tembo 28 na vipande 67 pamoja na kutegua mitego 23 ya nyaya za kutegea wanyamapori. Katika hatua nyingine, Mamlaka imesafisha mipaka yenye jumla ya kilomita 116 na kuweka vigingi 26 kwa ajili ya kuepusha migogoro ya mipaka na matukio ya moto holela.

**77. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha nyanda za malisho, Mamlaka imefyeka na kung'oa mimea vamizi (Invasive Plant Species) katika eneo lenye ukubwa wa hekta 866.68 pamoja na kuchoma moto eneo lenye ukubwa wa hekta 2,156 kwa utaratibu wa moto mpango (prescribed burning) ndani ya Kasoko ya Ngorongoro (Ngorongoro Crater) na eneo la Ndutu. Vilevile, Mamlaka imetoa elimu ya namna ya kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, mimea vamizi na mabadiliko ya tabianchi kwa kufanya mikutano 25 katika Kata 5 za Wilaya ya Karatu (Daa, Qurus, Mbulumbulu, Rhotia na Ganako) na Vijiji 9 (Arash, Ololosokwan, Soitsambu, Oloipiri, Olorien, Maaloni, Piyaya, Malambo na Makao) vinavyopakana na Hifadhi ambapo jumla ya wananchi 3,160 walifikiwa.

**78. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kurejesha uoto wa asili kwa maeneo yaliyoharibika kutokana na mabadiliko ya tabia Nchi kwa kugawa miche ya miti kwa wananchi waliopo katika Wilaya 3 (Karatu, Monduli na Meatu) zinazozunguka Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Zoezi hili limechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza kasi ya wananchi kuvamia eneo la hifadhi kwa ajili ya kujipatia kuni. Katika Mwaka huu wa Fedha, Mamlaka imezalisha miche ya miti 107,512 na kugawa jumla ya miche 28,654 kwa wadau mbalimbali (watu binafsi 69 na Taasisi 28). Miche hiyo iligawiwa katika maeneo ya Wilaya za Karatu 1,000, Monduli 2,000 na Same 3,100 pamoja na Shule 22,554. Sambamba na hilo, Mamlaka imepanda jumla ya miche 365 katika maeneo ya ofisi za Makao Makuu Kamyn.

**79. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imeendelea kuhamasisha wananchi wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kuhama kwa hiari kwenda katika maeneo yaliyotengwa na Serikali ambayo ni Msomera-Handeni, Saunyi-Kilindi, Kitwai-Simanjiro na maeneo mengine ambayo wananchi wanayoyachagua. Aidha, hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya Shilingi 286,681,137,369 zimetolewa na Serikali ili kuwezesha utekelezaji wa zoezi hilo. Katika awamu ya pili ya utekelezaji, jumla ya nyumba 1,000 kati ya nyumba 5,000 (Msomera - 2,500; Saunyi - 1,000; na Kitwai - 1,500) zinazotarajiwa kujengwa zimekamilika. Vilevile,

nyumba 1,500 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi katika Kijiji cha Msomera (hatua ya bati - nyumba 600, hatua ya Lenta - 260 na hatua ya usawa wa madirisha - 640). Sambamba na hilo, jumla ya kaya 822 zenye watu 5,354 na mifugo 21,136 zimehama kwa hiari. Kwa ujumla, tangu kuanza kwa zoezi hili mwezi Julai 2022, jumla ya Kaya zilizohama kwa hiari ni 1,373 zenye watu 8,364 na mifugo 36,457.

**80. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha usalama na kuboresha maisha ya wananchi wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Serikali kupitia Mamlaka imeendelea kutoa fidia na motisha kwa wenyeji wanaohama kwa hiari ndani ya hifadhi. Motisha na fidia zinazotolewa ni pamoja na nyumba yenye vyumba 3 na sebule; kiwanja na hati miliki ya ardhi yenye ukubwa wa ekari 2.5; shamba na hati miliki ya ardhi yenye ukubwa wa ekari 5; fidia ya maendelezo yaliyofanyika ndani ya Hifadhi; usafiri wa watu na mali zao hadi katika maeneo yaliyotengwa; na Shilingi milioni 10 kwa kila Mkuu wa Kaya. Sambamba na hilo, Serikali inatoa chakula kwa kipindi cha miezi 18 kwa kaya zote zilizohamia Msomera kwa awamu ya kwanza na ya pili ya zoezi hili. Mathalan, katika kipindi cha utekelezaji hadi kufikia Aprili 2024, Mamlaka imenunua jumla ya tani 520 za mahindi ambapo tani 392 zilitolewa kwa kaya zilizohamia Kijiji cha Msomera awamu ya kwanza na ya pili.

**81. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine Mamlaka imeendelea na jukumu la kuendeleza jamii ya wenyeji waishio ndani ya Hifadhi kwa kutoa huduma za kijamii. Katika kutekeleza jukumu hili, Mamlaka imetoa ufadhili kwa wanafunzi 2,224 katika ngazi ya Shule za Sekondari wanafunzi 1,797; Vyuo vya kati wanafunzi 338; na Vyuo Vikuu wanafunzi 89. Hadi kufikia Aprili 2024, Mamlaka imelipa jumla ya Shilingi 1,402,913,600 kugharamia ada, nauli na matumizi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Vilevile, Mamlaka imewezesha utoaji wa huduma za afya kwa wenyeji katika Zahanati ya Ngorongoro.

**82. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro imeboresha miundombinu ya utalii ndani ya Hifadhi, kwa kukarabati mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita

320 unaojumuisha barabara kuu ya Loduare hadi Golini; View Point hadi Nayobi; na mtandao wa barabara za Ndutu, Kasoko ya Ngorongoro. Aidha, Mamlaka imekarabati viwanja vidogo vya ndege 2 vya Ndutu na Ngorongoro. Kwa upande mwingine, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa barabara ya Endulen hadi Ndutu yenye urefu wa kilomita 20 kwa kiwango cha changarawe. Vilevile, Mamlaka imesambaza maji katika maeneo ya Ndutu, Laitoli na kufanya ukarabati wa vyoo 7 katika maeneo ya Olduvai, Seneto ya Juu, Seneto ya Chini, Lerai Picnic Site, Nyati Public Campsite, Viewpoint, na Loduare. Pamoja na hayo, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa mradi wa maji katika vyoo vya Ngoitoktok.

**83. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya utalii imeendelea kuimarika ikilinganishwa na kipindi ambacho Nchi nyingi zilikumbwa na janga la mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024 Mamlaka imepokea jumla ya Watalii 780,281 sawa na ongezeko la asilimia 22.1 ikilinganishwa na watalii 639,540 waliotembelea katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2019/2020 kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19. Vilevile, Mamlaka imekusanya mapato ya Shilingi 188,519,361,412 sawa na ongezeko la asilimia 52.66 ikilinganishwa na mapato ya Shilingi 123,490,469,339 zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kushinda tuzo mbili za kimataifa kama kivutio bora cha utalii barani Afrika (2023 Best of the Best Travellers' Choice na Africa's Leading Tourist Destination 2023).

**84. Mheshimiwa Spika,** katika kuvutia wawekezaji, Mamlaka imekamilisha kuandaa Mkakati wa Muda Mfupi wa Kuongeza Idadi ya Vitanda Ndani ya Hifadhi. Mkakati huo umebainisha jumla ya maeneo 16 yanayofaa kwa uwekezaji wa kambi za utalii za muda mfupi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya huduma za malazi ambazo zitaongeza vitanda 850. Hadi kufikia Aprili 2024, maeneo 5 yameshapata wawekezaji na wapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Sambamba na hilo, Mamlaka imepata wawekezaji 2 kwa ajili ya kuwekeza katika kambi za kudumu za muda mrefu ambapo uwekezaji huu utaongeza vitanda 150 ndani ya Hifadhi.

**85. Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Mamlaka imeendelea kuwajengea uwezo watumishi 275 kwa kuwawezesha kupata mafunzo ya muda mfupi 240 na mafunzo ya muda mrefu 35. Aidha, watumishi wapya 80 wamehudhuria mafunzo ya kijeshi katika kituo cha Mlele. Vilevile, Mamlaka inaendelea na ujenzi wa ofisi za Makao Makuu katika eneo la Kamny Wilayani Karatu ambapo ujenzi umefikia asilimia 71.5.

**3.3.1.5 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI**

**86. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ina jukumu la kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori Nchini kwa lengo la kuishauri Serikali na wadau namna bora ya uhifadhi na utalii endelevu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Taasisi imefanya miradi ya utafiti 29, ambapo tafiti hizo zilijikita katika kutatua changamoto za uhifadhi zikiwemo; mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori, matumizi ya teknolojia katika uhifadhi, afya ya mifumo ikolojia, nyuki na mazao yake, mahusiano ya viumbe na ikolojia zao, uhifadhi wa bioanuai na urejeshwaji wa baadhi ya wanyamapori katika mifumo ikolojia. Aidha, Taasisi iliratibu na kusimamia miradi ya utafiti 93 ya watafiti wa ndani na nje ya Nchi waliosajiliwa. Matokeo ya tafiti hizi yanalenga kutatua changamoto za uhifadhi na kuendeleza utalii ili kukuza pato la Taifa.

**87. Mheshimiwa Spika,** TAWIRI pia imefanya sensa moja ya wanyamapori katika mfumo ikolojia wa Katavi-Rukwa-Lukwati kwa lengo la kupata idadi na mtawanyiko wa wanyamapori aina ya Kanivora wakubwa (simba, fisi, chui, na mbwa mwitu). Uchakataji wa takwimu zilizopatikana unaendelea ili kutoa taarifa kamili, hata hivyo matokeo ya awali yameonesha uwepo na mtawanyiko mzuri wa wanyamapori hawa katika mfumo ikolojia huu kinyume na taarifa zilizokuwepo hapo awali. Aidha, matokeo haya yanadhihirisha uwepo wa wanyamapori hawa kwa idadi ya kuridhisha kama ilivyobainishwa na sensa zilizotangulia ambazo zilionesha kuwa Tanzania pamoja na kuwa na idadi inayoridhisha ya spishi mbalimbali za wanyamapori, inaongoza barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya nyati 225,000, simba 17,000 na chui 24,000.

**88. Mheshimiwa Spika,** TAWIRI imefanya tathmini katika maeneo 2 (Msolwa - Hifadhi ya Taifa Nyerere na Usangu - Hifadhi ya Taifa Ruaha) yaliyobadilishiwa matumizi kutoka vitalu vya uwindaji na kuwa sehemu ya Hifadhi za Taifa kwa lengo la kutambua maeneo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji wa utalii wa picha. Matokeo yameonesha uwepo wa spishi mbalimbali na mtawanyiko mzuri wa wanyamapori ambapo eneo la Msolwa spishi 16 za wanyamapori zilionekana wakiwemo nyati, tembo, viboko, pundamilia na swala pala. Aidha, upande wa Usangu spishi 21 za wanyamapori zilionekana, zikijumuisha kongoni, nyamera, swala pala, kuro, palahala, korongo, tembo, pofu na nyati. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa maeneo haya yanafaa kwa uwekezaji wa utalii wa picha na TANAPA wameshaanza kuweka miundombinu na kuyatangaza kwa wawekezaji.

**89. Mheshimiwa Spika,** TAWIRI imeendelea kutumia teknolojia kutatua changamoto inayotokana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. Pamoja na kutumia helikopta kurejesha makundi ya tembo hifadhini kutoka kwenye makazi ya wananchi, TAWIRI pia imefunga jumla ya mikanda 25 yenye mawasiliano (GPS Satellite Collars) kwa makundi 16 ya tembo, makundi 4 ya simba, kundi 1 la mbwa mwitu, na mamba 4 ili kufuatilia mienendo yao katika Mifumo Ikolojia Selous-Nyerere-Mikumi, Moyowosi-Malagarasi-Kigosi na Katavi-Rukwa-Lukwati. Aidha, TAWIRI imetoa mafunzo ya mbinu rafiki za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo kwa wakufunzi 1,626 kwa lengo la wao kusambaza elimu hiyo kwa wananchi wengine katika Halmashauri za Wilaya 28 zikiwemo; Meatu 8, Bariadi 7, Itilima 7, Busega 227, Monduli 68, Babati 66, Mwanga 193, Same 117, Ruangwa 23, Liwale 30, Lindi (Mchinga) 20, Mtama 20, Tunduru 20, Namtumbo 20, Bunda 41, Mbarali 31, Chamwino 59, Nachingwea 64, Iringa 47, Wanging'ombe 20, Kilolo 21, Itigi 31, Kalambo 44, Nkasi 12, Kaliua 36, Mlele 13, Urambo 13 na Handeni 368.

**90. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha afya za wanyamapori, TAWIRI imeendelea kufanya chunguzi za magonjwa ya wanyamapori katika Mifumo ikolojia mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa hakuna milipuko ya magonjwa na pale

inapotokea inadhibitiwa mara moja kabla haijasababisha madhara kwa uhifadhi na utalii. Hata hivyo kwa kipindi hiki hakuna tishio la magonjwa ya wanyamapori lililojitokeza.

**91. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti mimea vamizi kwenye maeneo yaliyohifadhiwa, TAWIRI imeendelea kuboresha ubunifu wa namna ya kutumia mimea vamizi kama malighafi ya kutengeneza nishati jadidifu. Ubunifu huu unalenga kupunguza mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, kuboresha nyanda za malisho, na hapo baadae, teknolojia hii inaweza kutumika kupunguza utegemezi wa jamii katika nishati inayotokana na miti. Utafiti huu unaendelea katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

**92. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kufanya tafiti TAWIRI ina jukumu la kusambaza matokeo ya tafiti hizo kwa watumiaji. Kutekeleza jukumu hilo, TAWIRI iliandaa Kongamano la 14 la Kimataifa la Kisayansi lililohudhuriwa na washiriki 650 kutoka Nchi 22 ambapo mada 132 ziliwasilishwa. Mada kuu ya kongamano hilo ilikuwa ni kuimarisha mahusiano baina ya Jamii na Wanyamapori kwa ajili ya Uhifadhi Endelevu wa Bioanuai na Uchumi wa Jamii (Human Wildlife Coe-existence for Biodiversity Conservation and Socio-Economic Development).

**93. Mheshimiwa Spika**, TAWIRI ina jumla ya watumishi 129, ambapo watumishi 37 sawa na asilimia 29 ni wanawake. Aidha, Taasisi imeendelea kutoa stahiki kwa watumishi wake ambapo watumishi 9 walipandishwa vyeo, 9 wapo kwenye masomo ya muda mrefu (shahada ya uzamivu 4, shahada ya uzamili 4, shahada ya kwanza 1), 70 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na pia semina kwa ajili ya kujikinga na VVU-UKIMWI, magonjwa yasiyoambukiza na afya ya akili zimetolewa kwa watumishi wote.

### 3.3.1.6 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori MWEKA – CAWM

**94. Mheshimiwa Spika**, Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani katika nyanja za usimamizi wa wanyamapori na utalii. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,067 sawa na asilimia 106 ya lengo la wanafunzi 1,000 ambapo

wanafunzi 368 (34.5%) ni wanawake. Chuo kimetoa mafunzo katika ngazi za Cheti cha msingi cha ufundi, Cheti cha Ufundi, Stashahada ya kawaida, Shahada ya kwanza na Shahada ya uzamili. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 224 (watanzania 156 na wasio watanzania 68). Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na Uongozaji wa Watalii wa Mlima, Usimamizi wa RaNchi, Mashamba na Bustani za Wanyamapori, Ukamataji na Uhamishaji wa Nyoka, na Ikolojia ya kitropiki na uhifadhi wa Wanyamapori. Washiriki kutoka nje ya Tanzania walitoka katika vyuo vikuu vya Manchester Metropolitan (Uingereza), New York - Oswego na Brigham Young (Marekani).

**95. Mheshimiwa Spika,** ili kwenda na wakati na kutoa mafunzo yanayoweza kujibu changamoto zinazotokana na mabadiliko ya kiikolojia, kiuchumi, kijamii na kisera yanayotokea Nchini na duniani kote, Chuo kimepitia mitaala yake 12 na kuandaa mitaala 10. Kufuatia mapitio na kuandaliwa kwa mitaala mipya, kwa sasa Chuo kinatoa shahada 3 za uzamili (Masters programmes); stashahada 3 za uzamili (Postgraduate Diploma); shahada 2 za awali (Bachelor degrees); Stashahada 2 za juu (Higher Diploma); stashahada 4 za kawaida (Ordinary Diploma); kozi 4 za Cheti cha ufundi (Technician Certificate) na kozi 4 za Cheti cha Awali cha Ufundi (Basic Technician Certificate).

**96. Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha utoaji wa mafunzo na kujibu changamoto zinazokabili Sekta za Wanyamapori na Utalii, Chuo kimeendelea kufanya tafiti mbalimbali katika maeneo kadhaa Nchini. Matokeo ya tafiti hizi yamewasilishwa katika makongamano ya kitaifa na kuchapishwa katika majarida mbalimbali ya kimataifa. Moja ya miradi ya utafiti inayoendelea ni "Mradi wa kukuza Utafiti na Ubunifu wa Ushirikishwaji wa Jamii katika Uhifadhi na Usimamizi wa Taka (Strengthening Research and Innovation in Natural Resources Management and Waste Management – RiNaWa)" unaotekelezwa katika Nchi 4 za SADC (Tanzania, Zambia, Msumbiji na Malawi). Pamoja na kuja na suluhu dhidi ya tatizo la taka katika mazingira, Mradi huu utasaidia kuandaliwa kwa mitaala ya Uhifadhi wa Mazingira na Usimamizi wa Taka (Environmental and waste Management) na

Ushirikishwaji wa Jamii katika Uhifadhi (CommunityBased Conservation).

**97. Mheshimiwa Spika**, Chuo kimetoa huduma za ushauri na ugani kwa jamii pamoja na kushiriki katika shughuli za kitaifa na uhifadhi ikiwemo kupambana na janga la maporomoko lililoikumba Wilaya ya Hanang, kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira katika Wilaya za Pangani na Moshi, kusaidia udhibiti wa matukio ya moto katika hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA) na kusaidia kung'oa mimea vamizi katika Hifadhi ya Taifa ya Arusha na Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Aidha, wanataaluma na wanafunzi wa Chuo wameshiriki katika zoezi la tathmini za bioanuai na maliasili katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na Hifadhi mpya ya Wanyamapori Makuyuni, iliyoko Monduli.

**98. Mheshimiwa Spika,** ili kuweka mazingira rafiki yanayotakiwa kwa watumishi na wanafunzi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi, Chuo kimeendelea kuboresha miundo mbinu yake kwa kufanya ukarabati wa nyumba 3 za watumishi na kuendelea na ujenzi wa jengo la kutolea mafunzo la ghorofa 2 ambalo limefikia asilimia 98. Jengo hili linatarajiwa kukamilika Juni 2024, na kuanza kutumika katika muhula wa masomo unaoanza Oktoba 2024. Litakapokamilika, jengo hili litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 kwa wakati mmoja.

**99. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha MWEKA kimefanya maadhimisho ya Miaka 60 na Mahafali ya 59 tangu kilipoanzishwa Juni 1963. Mgeni Rasmi katika kilele cha Maadhimisho haya yaliyofanyika tarehe 25 Novemba 2023, alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.). Chuo kilianza kutoa mafunzo kikiwa na jumla ya wanafunzi 25 kutoka Nchi za Malawi, Kenya, Uganda, Cameroon na Tanzania. Hadi kufikia Mwaka wa masomo 2022/2023 Chuo kimeweza kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa takriban wanafunzi 11,000 kutoka Nchi 28 za Bara la Afrika na 26 nje ya Afrika katika ngazi za Cheti, Stashahada na Shahada. Kupitia wahitimu wake, Chuo cha MWEKA kimekuwa na mchango mkubwa kwenye nyanja ya usimamizi wa wanyamapori na utalii ndani na nje ya Tanzania.

**100. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha MWEKA kimeendelea kuwawezesha wafanyakazi kupata mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi kwa kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya watumishi 89 wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na wengine 20 wamewezeshwa kufanya mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya Nchi kwa ngazi za Stashahada 1, Shahada ya Kwanza 1, Shahada za Uzamili 7 na Shahada za Uzamivu 11. Aidha, Chuo kimewezesha na kusimamia mafunzo ya kimkakati kwa watumishi wake yaliyohusu Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma, Kupambana na Changamoto za Afya ya Akili, Kupambana na Rushwa, kuzuia Ukimwi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

### 3.3.1.7 Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi – PWTI

**101. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi ina jukumu la kutoa mafunzo ya Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji Watalii kwa elimu kiwango cha Cheti cha awali na Cheti kwa kada za uaskari wa wanyamapori na uongozaji utalii. Mchakato wa kuanza kutoa mafunzo kwa kiwango cha Stashahada umekamilika na inatarajiwa kuanza kutolewa kuanzia Mwaka wa masomo 2024/2025. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Taasisi imedahili wanafunzi 646 wa kozi za muda mrefu, na 108 wa kozi fupi ambao waliongezewa ujuzi katika kupunguza migogoro kati ya wanyamapori na binadamu. Vilevile, Taasisi imeshirikiana na TANAPA kuendesha mafunzo ya waajiriwa wapya 220 katika kambi ya mafunzo kwa vitendo Fort Ikoma, Serengeti. Katika kujengea uwezo watumishi wa Taasisi, jumla ya watumishi 4 wanafadhiliwa katika kiwango cha Shahada ya Uzamivu 2, Shahada ya Uzamili 1 na Stashahada 1. Aidha, katika kuboresha mazingira ya masomo kwa Mwaka 2023/2024, Chuo kimeboresha miundombinu ya mabweni ikiwepo mfumo wa umeme na mfumo wa majisafi na majitaka.

### 3.3.1.8 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga – CBCTC

**102. Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu – Sekamaganga kina jukumu la kuzijengea uwezo jamii zinazoishi jirani na maeneo yenye wanyamapori ili ziweze kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kituo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 628 kwa kozi za muda mrefu na mfupi ambapo wanaume ni 502 na wanawake ni 126. Idadi hiyo inajumuisha wanafunzi wa kozi za muda mrefu za Utalii na uongozaji watalii 159. Kati ya hao, wanaume ni 101 na wanawake ni 58. Wanafunzi wa kozi za muda mfupi ni 469. Aidha, kozi za muda mfupi zilihusisha VGS 364 (wanaume 311 na wanawake 53); waongoza watalii 27 (wanaume 15 na wanawake 12); mafunzo rejelezi kwa askari wa TAWA 28 (wanaume 25 na wanawake 3); na mafunzo maalum ya mwitikio wa haraka kwenye matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu (Rapid Response Team) kwa askari 50 (wanaume 48 na wanawake 2) kutoka Jeshi la Uhifadhi wa wanyamapori na Misitu pamoja na VGS. Vilevile, hadi kufikia Aprili 2024, Kituo kimekusanya mapato yenye jumla ya Shilingi 1,068,507,400 kutokana na ada za mafunzo.

**103. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, kituo kimeboresha miundombinu ya mafunzo kwa kuanza ujenzi wa madarasa 2 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 na bweni 1 lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64. Vilevile, kituo kimenunua vitanda 60 (Double deckers) na madawati 200.

**104. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi kwa watumishi, Kituo kiliwezesha watumishi 2 kuanza mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao, mmoja alipata ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili katika usimamizi wa Utalii wa Kimataifa (Masters of Science and International Tourism Management) Nchini Indonesia na mwingine anasoma Stashahada (Diploma) ya uhifadhi wanyamapori katika Chuo cha Wanyamapori MWEKA.

### 3.3.1.9 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF

**105. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umewezesha utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Operesheni za kuzuia ujangili zilizowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 45, vipande 51 vya meno ya tembo, magamba 114 ya kakakuona, kobe hai 11 na nyara zingine. Vilevile, jumla ya silaha 13: AK 47 (1), Rifle (8), Shotgun (3) na Gobore (1) na risasi 65 za AK 47 zilikamatwa.

**106. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Mfuko umewezesha utatuzi wa migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa; mchakato wa upandishaji hadhi maeneo ya hifadhi; usimamizi wa maeneo 38 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kwa jamii (WMAs); utoaji elimu ya uhifadhi kwa wananchi; uratibu wa uhifadhi wa faru Nchini; na utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia katika Sekta ya Wanyamapori.

### 3.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

**107. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Aidha, utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta hizi unasimamiwa na Sheria ya Misitu, Sura ya 323, Sheria ya Ufugaji Nyuki, Sura ya 224 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Sura ya 277. Vilevile, uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki unaratibiwa na Idara ya Misitu na Nyuki. Aidha, usimamizi wa rasilimali hizo uko chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi (FITI), Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki – Tabora (BTI) na Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF). Kwa upande mwingine, Serikali za Mitaa (Vijiji na Halmashauri) zina jukumu la kuhifadhi na kusimamia rasilimali hizo katika maeneo yao.

**108. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina uoto wa misitu kwenye eneo la jumla ya hekta milioni 48.1 ambapo asilimia 93 ni misitu ya miombo na asilimia 7 ni misitu iliyofunga. Usimamizi wa misitu Nchini umegawanyika katika mamlaka mbalimbali ikiwemo misitu iliyo chini ya usimamizi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa (Vijiji na Halmashauri) na Sekta Binafsi. Hifadhi za Misitu ya Serikali kuu kwa sasa zipo 464 (hifadhi za misitu ya asili 417 ikijumuisha hifadhi za mikoko; misitu ya hifadhi ya mazingira asilia 23; na mashamba ya miti ya kupandwa 24). Kwa upande mwingine, Serikali za Mitaa zinasimamia jumla ya misitu 158 yenye hekta milioni 3.1 sawa na asilimia 6.5; misitu iliyo katika ardhi za Vijiji ni hekta milioni 21.9 sawa na asilimia 45.7; watu binafsi hekta milioni 3.5 sawa na asilimia 7.3; na ardhi ya jumla yenye hekta milioni 2.9 sawa na asilimia 6. Aidha, TFS inasimamia hifadhi za nyuki 14 zenye hekta 36,640.43 na mashamba ya nyuki 3. Vilevile, Serikali za Vijiji zinasimamia hifadhi za nyuki 18 zenye ukubwa wa hekta 39,345 na sekta binafsi inasimamia hifadhi ya nyuki 1 yenye hekta 454. Hifadhi za nyuki ni maeneo mahsusi kwa ufugaji nyuki, tafiti na uhifadhi kwa ujumla.

### 3.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

**109. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha mazingira ya kibiashara na kuvutia uwekezaji katika sekta ya misitu na nyuki, Wizara imefanya maboresho ya tozo mbalimbali zikiwemo: tozo za ufugaji nyuki kibiashara ndani ya hifadhi za nyuki za Serikali Kuu; tozo ya ukaguzi na usafirishaji wa mazao ya nyuki nje ya Nchi; tozo ya matumizi ya makundi ya nyuki kwa ajili ya uchavushaji na kuandaa miongozo ya kuratibu biashara ya mazao na huduma za misitu na nyuki. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni ya Tozo za Mazao ya Nyuki Tangazo la Serikali Na. 760 ya tarehe 27 Oktoba, 2023; Kanuni ya Matumizi Endelevu ya Mazao ya Misitu Tangazo la Serikali Na. 615 ya tarehe 25 Agosti, 2023. Vilevile, Wizara imeandaa Mkakati na Mpango kazi wa Kitaifa wa Kuendeleza zao la Mianzi wa Mwaka 2023; Mkakati wa Pili wa Kitaifa wa Kilimo Misitu wa Mwaka 2024; Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Usimamizi katika Hifadhi za Misitu ya Asili wa Mwaka 2023; Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji na Utunzaji wa Kitalu

cha Miche ya Miti wa Mwaka 2024; na Mwongozo wa Kitaifa wa Upandaji na Utunzaji wa Miti wa Mwaka 2024.

**110. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imeimarisha ushirikishwaji wa wadau katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki, kwa kuratibu vikao 2 vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki - NABAC, vikao 2 vya wadau wa misitu kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), kikao 1 cha wafanyabiashara na wasafirishaji wa mazao ya misitu pamoja na kikao 1 cha Kamati ya Uendeshaji ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa (Engineered Wood Products - EWP).

**111. Mheshimiwa Spika,** Wizara imetoa elimu kwa jamii kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Hatua hiyo imewezesha kuanzisha hifadhi 4 za misitu ya Vijiji vya Ndongosi, Muhukulullilahi, Liweta na Litowa Wilaya ya Songea kwa Tangazo la Serikali Na. 670/2023 zenye jumla ya hekta 14,676.31; kutoa Tangazo la Amri ya kuanzisha eneo la Msitu wa Hifadhi wa Kigosi kuwa Hifadhi ya Msitu wa Taifa wa Kigosi kwa Tangazo la Serikali Na. 345 la tarehe 03 Mei, 2024 wenye ukubwa wa hekta 923,904.

**112. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kunufaika kupitia rasilimali za misitu, Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki unaojulikana kwa jina la "Achia Shoka Tundika Mzinga". Mpango huu una lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki na ajira. Aidha, Mpango huu utatekelezwa Nchi nzima kwa kipindi cha Miaka 10 kuanzia Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**113. Mheshimiwa Spika,** Tanzania kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Jukwaa la Kuendeleza Ufugaji Nyuki Tanzania (TABEDO) ni Mwanachama wa Shirikisho la Wafugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA). Shirikisho hilo lilianzishwa kwa lengo la kuwaunganisha wafugaji nyuki duniani ili waweze kufanya shughuli za ufugaji nyuki kwa ufanisi zaidi. Aidha, kupitia Mkutano Mkuu wa 48 wa Shirikisho la Wafugaji Nyuki Duniani uliofanyika kuanzia tarehe 4 hadi 8 Septemba, 2023 katika Jiji la Santiago

Nchini Chile, Tanzania ilishinda na kuidhinishwa kuwa Mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa 50 wa Shirikisho hilo (50th APIMONDIA Congress) utakaofanyika tarehe 20 hadi 25 Septemba, 2027 Jijini Arusha. Sambamba na Mkutano huo, Shirikisho litakuwa likisheherekea Jubilee ya Miaka 50 tangu kuanza kwa mikutano yake.

**114. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ilipata ushindi huu mara baada ya kupata kura 68 dhidi ya Jumuiya ya Falme za Kiarabu (UAE) ambao walipata kura 35. Mkutano wa 50 wa Apimondia unatarajiwa kuhudhuriwa na washiriki takribani 6,000 kutoka mataifa zaidi ya 130 duniani. Aidha, kupitia Mkutano huo faida mbalimbali zinatarajiwa kupatikana zikiwemo: kuhamasisha na kuimarisha matumizi ya teknolojia mbalimbali za ufugaji nyuki na kuongeza thamani ya mazao ya nyuki; kuimarisha mtandao wa masoko ya mazao ya nyuki ndani na nje ya Nchi na hivyo kuongeza kiwango cha mazao kitakachouzwa nje ya Nchi; kuhamasisha ufugaji nyuki kibiashara hivyo kuongeza ajira hasa kwa vijana na wanawake; kujenga uwezo kwa vyuo na taasisi zinazofanya utafiti wa ufugaji nyuki; kuendelea kuimarisha shughuli za utalii hasa utalii wa nyuki (Api-tourism) kwa kushawishi washiriki wa Mkutano kutembelea vivutio vyetu vilivyopo Nchini. Katika kuhakikisha jambo hili linafanyika kwa mafanikio makubwa, Wizara ya Maliasili na Utalii imeunda Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi inayojumuisha wataalam wa Serikali na Sekta binafsi. Kwa upande mwingine, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Honey Junction Ltd inaandaa maonesho ya Asali (Tanzania Honey Show) yatakayofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 18 hadi 21 Juni, 2024. Hatua hii ni sehemu ya utayari wa Tanzania kuwa Mwenyeji wa Apimondia. Nitumie nafasi hii kuhamasisha Watanzania kuchangamkia fursa ya uwepo wa Mkutano huu mkubwa kwa maendeleo ya Nchi yetu.

**115. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara ya Maliasili na Utalii imeshiriki Mkutano wa 28 wa Dunia wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu tarehe 30 Novemba hadi 12 Disemba, 2023 kwa lengo la kujenga mahusiano na wadau wa kimataifa na kutangaza fursa za uwekezaji katika biashara ya kaboni pamoja na nafasi ya kutumia

miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabiachi kupitia mifuko ya kimataifa na wahisani wa maendeleo. Aidha, ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo pamoja na mambo mengine alipata fursa ya kutangaza na kuvutia wawekezaji katika sekta za misitu hasa kwenye eneo la biashara ya kaboni.

**116. Mheshimiwa Spika,** vilevile, Wizara ya Maliasili na Utalii imeshiriki Kongamano la Kimataifa la Usimamizi wa Ikolojia ya Misitu ya Miombo lililofanyika Jijini Washington DC, Marekani kuanzia tarehe 16 hadi 18 Aprili, 2024. Kongamano hilo lilikuwa ni utekelezaji wa Azimio la Maputo la Mwaka 2022 ambapo Wakuu wa Nchi 11 za ukanda wa SADC waliazimia kuweka misingi ya Nchi hizo kushirikiana katika usimamizi wa misitu hiyo kwa ajili ya ustawi wa jamii, uhifadhi wa bioanuai na ustahimilivu wa hali ya hewa.

**117. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imeratibu maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Upandaji Miti Kitaifa yaliyofanyika Wilaya ya Same Mkoa wa Kilimanjaro kuanzia tarehe 18 hadi 21 Machi 2024 ambapo waoneshaji 47 kutoka katika Mikoa mbalimbali walishiriki. Vilevile, Wizara imeratibu maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika kitaifa Jijini Dodoma kuanzia tarehe 17 hadi 20 Mei, 2024 ambapo waoneshaji 90 kutoka katika Mikoa mbalimbali walishiriki. Mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho hayo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, katika maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani Mwongozo wa Kitaifa wa Uandaaji na Utunzaji wa Kitalu cha Miche ya Miti wa Mwaka 2024; na Mwongozo wa Kitaifa wa Upandaji na Utunzaji wa Miti wa Mwaka 2024 ilizinduliwa. Kupitia maadhimisho hayo, wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali, Sekta binafsi na wananchi waliotembelea maonesho walinufaika kwa kupata elimu kuhusu utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki; elimu ya matumizi ya bidhaa mbalimbali zitokanazo na mazao ya misitu na nyuki; teknolojia zinazotumika kwenye uchakataji wa mazao ya misitu na nyuki; na taratibu za kufanya biashara ya mazao ya

misitu na nyuki. Kwa upande mwingine, washiriki walipata fursa ya kuuza bidhaa mbalimbali pamoja na kukuza mitandao ya kibiashara.

**118. Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu, usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki upo chini ya Mamlaka mbalimbali ikiwemo: Serikali Kuu, Serikali za Mitaa (Halmashauri na Vijiji) na Sekta binafsi. Mathalan, Halmashauri zinamiliki na kusimamia jumla ya misitu 158 yenye hekta milioni 3.1; na Serikali za Vijiji zinasimamia maeneo ya misitu yenye hekta milioni 21.9 sawa na asilimia 45.7 ya eneo lote la misitu lililoko Nchini. Hata hivyo, katika kipindi cha hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la matukio ya uvamizi wa maeneo hayo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu hali inayosababisha uoto wa asili wa maeneo hayo kupungua. Kwa kuzingatia kuwa, Mamlaka hizo zina jukumu la kuhifadhi na kulinda misitu hiyo, nitoe rai kwa Mamlaka husika kuhakikisha kuwa zinatenga rasilimali za kutosha kwa ajili ya ulinzi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali hizo.

### 3.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

**119. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umepewa jukumu la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki zilizo chini ya Serikali Kuu. Aidha, Wakala unatekeleza majukumu yote ya kiutendaji yaliyokuwa yanatekelezwa na Idara ya Misitu na Nyuki isipokuwa mambo yanayohusu utungaji wa Sera, Sheria na Programu za Sekta ya Misitu na Nyuki. Majukumu hayo ni pamoja na: Kuanzisha na kusimamia Misitu ya hifadhi na Hifadhi za Nyuki za Serikali kuu; Kuanzisha na kusimamia mashamba ya miti na manzuki ya Serikali kuu; Kusimamia rasilimali za misitu na nyuki katika ardhi ya jumla (General Land); Kusimamia utekelezaji wa Sheria za Misitu na Ufugaji Nyuki; Kukusanya Maduhuli yatokanayo na mazao ya misitu; Kutoa huduma za ugani katika maeneo ya Wakala; Kufanya biashara ya mazao na huduma za Misitu na Ufugaji Nyuki; na Kufanya tathmini kuhusu utekelezaji wa kazi za Wakala.

**120. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wakala umeimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za misitu kwa

kuandaa Mipango ya Usimamizi ya Misitu 30 yenye ukubwa wa hekta 995,313 na kufanya doria 1,198. Aidha, Wakala umeanza kutumia teknolojia za kisasa ikiwemo ndege nyuki (drone) kwa lengo la kupata taarifa za matukio mbalimbali katika hifadhi za misitu. Kupitia doria hizo, jumla ya watuhumiwa 1,223 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Aidha, doria ziliwezesha kukamatwa na kutaifishwa kwa magunia 21,596 ya mkaa uliovunwa bila kufuata utaratibu, mbao 24,036 zenye mita za ujazo 1,498, kuni zenye mita za ujazo 90 na magogo 1,256 yenye mita za ujazo 415, mifugo 12,694, pikipiki 1,514, magari 149 na vyombo vya majini (marine vessels) 7 vilikamatwa ambapo taratibu za kisheria zinaendelea.

**121. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha alama za mipaka zinaonekana na kupunguza migogoro ya mipaka na wananchi, Wakala umeimarisha mipaka ya misitu 68 kwa kuweka vigingi 1,365 na mabango 161; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,023; na kuchimba mitaro 20 inayoonesha uelekeo wa mpaka. Aidha, Wakala umejenga barabara zenye urefu wa kilomita 46.1, kalavati 4, madaraja 6, kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 964 na madaraja 10.

**122. Mheshimiwa Spika,** Wakala umekabiliana na majanga ya moto kwenye hifadhi za misitu kwa kusafisha njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 1,628, kuajiri na kutoa mafunzo kwa vikosi vya kupambana na moto 15 vyenye watu 375, kusimamia minara ya kuonea moto 21; na kutoa mafunzo ya njia za kuepuka majanga ya moto na mbinu za kukabiliana na moto kwa wananchi 13,793 kutoka Vijiji 229 vinavyozunguka mashamba 5 ya miti ya Sao Hill, Wino, Korogwe, Silayo na Rondo na baadhi ya Vijiji vya Wilaya za Serengeti na Songea. Vilevile, Wakala unatumia teknolojia ya kisasa kwa kuimarisha matumizi ya mitambo ya kuzima moto na mfumo wa satellite wa kubaini matukio ya moto pori mapema katika maeneo yaliyohifadhiwa na maeneo yaliyo nje ya hifadhi. Hatua hii imewezesha kukabiliana na majanga ya moto kwa haraka kabla ya kuenea na kusababisha madhara makubwa. Aidha, jumla ya matukio ya moto 344,278 yalibainishwa na kuzimwa ambapo matukio 160,062 yalitokea

katika maeneo yaliyohifadhiwa na matukio 184,216 nje ya maeneo yaliyohifadhiwa.

**123. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora za miti na kufanikisha Kampeni ya Tanzania ya Kijani, Wakala umezalisha jumla ya tani 17.9 za mbegu za miti ya spishi mbalimbali na kukuza miche 34,126,916 ya aina mbalimbali ambayo imepandwa katika mashamba 24 ya Serikali na miche 11,577,802 imegawiwa kwa watu binafsi, Taasisi na Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi kwa ajili ya kupandwa katika maeneo yao. Hadi Aprili, 2024 Wakala umepanda miti katika hekta 7,322 na kurudishia miti iliyokufa kwenye hekta 2,038. Aidha, Wakala umeendeleza mashamba ya miti kwa kupalilia hekta 22,330, kupogolea hekta 7,331 na kupunguzia miti kwenye hekta 2,190. Sambamba na hilo, Wakala umeendelea kuhifadhi maeneo ya mikoko kwa kupanda miche 223,777 kwenye eneo la hekta 79.3 katika maeneo ya mwambao wa bahari yaliyopo Kibiti, Tanga, Temeke, Kilwa, Lindi na Bagamoyo.




Shughuli za Upandaji Miti na Uhifadhi katika Shamba la Miti SaoHill, Iringa

**124. Mheshimiwa Spika,** kufuatia juhudi mbalimbali za kuendeleza utalii ikolojia sambamba na kutumia fursa zinazotokana na Programu ya Tanzania - the Royal Tour, Wakala umeendeleza vivutio vya utalii ikolojia na kupandisha hadhi misitu 3 yenye ukubwa wa hekta 25,224 kuwa Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia. Misitu hiyo ni pamoja na Uvinza - Kigoma; Matogoro Mashariki - Ruvuma; na Vilima vya Hassama - Manyara. Vilevile, Wakala umeimarisha miundombinu ya utalii katika hifadhi za misitu kwa kutengeneza kilomita 73 na kukarabati kilomita 355

za njia za kutembea kwa miguu kwa watalii na kilomita 964 za barabara za msituni.

**125. Mheshimiwa Spika,** Wakala umetumia njia mbalimbali kutangaza vivutio vya utalii ikolojia, urithi wa utamaduni pamoja na uhifadhi wa rasilimali za misitu kwa kuzalisha na kurusha picha jongefu zenye makala 12 na jumbe fupi 69, vipindi 28 vya redio na 49 vya televisheni, kushiriki katika matamasha 19 ya ndani na nje ya Nchi na kusambaza machapisho zaidi ya 12,000. Aidha, matukio na matamasha ya kutangaza utalii ikolojia yameendelea kufanyika kwa kushirikiana na wadau yakiwemo Rombo Marathon, Bata Msituni, Meru Forest Trail Run, Mkeka na Khanga, Sao Hill Rally na "Twenzetu Tukacharu Rau". Juhudi hizi zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya utalii ikolojia kutoka 205,429 Aprili 2023 hadi 211,764 Aprili 2024 sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Hadi kufikia Aprili 2024, mapato yanayotokana na shughuli mbalimbali katika maeneo ya vivutio vya utalii ikolojia yameongezeka na kufikia Shilingi 1,689,095,459 sawa na ongezeko la asilimia 29.4 ikilinganishwa na Shilingi 1,192,524,070 zilizokusanywa kipindi kama hicho Mwaka 2023.

**126. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wakala umejenga malango 5 katika hifadhi za mazingira asilia za Matogoro, Mlima Hanang, Amani, Nilo na Pugu Kazimzumbwi; ofisi 1 katika Hifadhi ya Ziwa Duluti na vyoo 7 katika Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia Amani, Vikindu, kituo cha Malikale cha Kolo; na kukarabati hosteli 1 katika hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia Amani. Vilevile, kambi za kitalii 12 na minara 2 ya kutazamia vivutio imekarabatiwa katika Mashamba ya miti Meru, Rubare, West Kilimanjaro, Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia za Mlima Hanang, Minziro, Kilombero, Kalambo, Mlima Rungwe na Uzungwa Scarp. Pia, benchi 8, meza 3 zimetengenezwa katika Shamba la Miti West Kilimanjaro. Sambamba na hilo, Wakala umeimarisha miundombinu ya vituo vya Michoro ya Miambani Kolo – Kondoa na Magofu ya Tongoni – Tanga kwa kukarabati kilomita 5 za njia za kutembea kwa miguu, ujenzi wa banda 1 la kupumzika watalii, mageti 3 na mabango 8. Uboreshwaji wa miundombinu hiyo umechangia kuleta hamasa

kwa wananchi kutembelea maeneo ya vivutio vya utalii katika hifadhi hizo.

**127. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wakala umefanikiwa kuanza utekelezaji wa mradi wenye thamani ya Shilingi bilioni 14.8 wenye lengo la kuimarisha ustahimilivu wa bioanuai katika baadhi ya hifadhi za misitu ya mazingira asilia dhidi ya athari ya mabadiliko ya tabianchi unaotekelezwa katika hifadhi 9 ambazo ni Nou, Mlima Hanang, Pugu Kazimzumbwi, Uzigua, Hassama Hill, Pindiro, Rondo, Mwambesi na Essimingor. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia na utasaidia utunzaji wa rasilimali za misitu; kuboresha miundombinu ya utalii na maisha ya jamii inayoishi karibu na hifadhi; na kufungua fursa za uwekezaji kwenye maeneo ya hifadhi za misitu.

**128. Mheshimiwa Spika,** Wakala umeimarisha shughuli za ufugaji nyuki kwa kusimamia manzuki 185 na mashamba 3 ya Nyuki ya Kipembawe (Chunya), Mwambao (Handeni na Kilindi) Nawima (Kalambo) na Kati (Manyoni, Chemba na Kondoa) ambapo kilo 12,869 za asali na kilo 666 za nta zenye thamani ya Shilingi 154,428,000 na 9,990,000 mtawalia zimezalishwa. Aidha, Wakala unasimamia na kufanya ufuatiliaji wa shughuli za uzalishaji na utunzaji wa taarifa za manzuki kwa kutumia mfumo wa Honey Traceability. Mfumo huu unatumika kusajili wafanyabiashara wa mazao ya nyuki na kutoa vibali vya kusafirisha mazao hayo ndani na nje ya Nchi. Aidha, mfumo wa Honey Traceability unatumika kutunza takwimu za wafanyabiashara wa mazao ya nyuki ili kutoa taarifa muhimu kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya Nchi pamoja na kuonesha uhalisia wa chanzo cha mazao hayo. Natoa rai kwa wadau wa ufugaji nyuki kujisajili kwenye mfumo huo ili kuongeza tija katika shughuli za ufugaji nyuki Nchini.

Shughuli za ufugaji nyuki zikiendelea katika Shamba la Nyuki - Wilayani Manyoni, Mkoa wa Singida

**129. Mheshimiwa Spika,** Wakala umekusanya sampuli 70 za asali kutoka katika Wilaya 34 na kuzipeleka kwenye maabara ya kimataifa iliyopo Nchini Ujerumani kwa lengo la kupima ubora wake. Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 96 ya sampuli hizo zimekidhi viwango vya ubora wa kimataifa na hivyo kutoa fursa kwa asali ya Tanzania kuendelea kuuzwa katika masoko mbalimbali duniani yaliyopo Nchi za Ujerumani, Ubelgiji, Uholanzi, Ufaransa, Uingereza, Marekani, Saudi Arabia, Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu, Lebanon, Poland, Kenya, Rwanda, Comoro, Botswana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Aidha, masoko makubwa ya nta ni pamoja na Japan, Marekani, Ujerumani na Poland. Vilevile, Wakala umekamilisha ujenzi na ununuzi wa mitambo ya kiwanda kipya cha kuchakata mazao ya nyuki katika Wilaya ya Nzega. Pia, mizinga ya nyuki 916 imezalishwa kupitia viwanda vya Wakala vilivyopo Wilaya za Kondoa na Mufindi. Katika kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za ufugaji nyuki, Wakala umetoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa vikundi 103 vya ufugaji nyuki vyenye wanachama 1,135 katika kanda 7 za usimamizi wa misitu za TFS.

**130. Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi, elimu ya uhifadhi imetolewa kupitia vipindi 25 vya televisheni vinavyorushwa kupitia TBC Taifa katika kipindi cha **Misitu ni Uhai**. Aidha, jumla ya nakala 3,000 za miongozo ya Sekta za Misitu na Ufugaji Nyuki imesambazwa. Vilevile, kupitia mikutano, wananchi zaidi ya 5,000 wa Vijiji 145 katika Wilaya za

Dumila, Mkuranga, Kyerwa, Nyamagana, Chato, Maswa, Rorya, Bunda, Misungwi, Ukerewe, Misenyi, Busega, Butiama, Kibondo, Kasulu, Mwanga, Muheza, Handeni, Njombe, Nyasa, Songea, Namtumbo, Serengeti, Muleba, Hanang, Mbulu, Lushoto, Pangani, Same, Makete, Ludewa, Kalambo, Kilolo, Nkasi na Kishapu walijengewa uwezo kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa misitu. Michango ya maendeleo kwa jamii yenye thamani ya Shilingi 4,826,026,845 ilitolewa ikijumuisha miche 10,644,242 yenye thamani ya Shilingi 4,402,572,374; mizinga ya nyuki 1,040 yenye thamani ya Shilingi 156,000,000 na mchango wa vifaa na fedha wenye thamani ya Shilingi 267,454,471 kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika vijiji vinavyopakana na misitu ya hifadhi.

**131. Mheshimiwa Spika,** katika upande mwingine, Wakala umetatua migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Hifadhi katika Vijiji 112 vinavyozunguka hifadhi za misitu 32. Aidha, jumla ya eneo la hifadhi lenye ukubwa wa hekta 88,618 limemegwa na kuwapatia wananchi. Zoezi hili limekwenda sambamba na uhakiki na upimaji upya wa kilomita 161, kusafisha kilomita 880, kusimika vigingi 1,360 na kuweka mabango 139 katika maeneo ya hifadhi. Jitihada hizi zimepunguza kwa asilimia 96 migogoro iliyobainishwa katika hifadhi za misitu inayosimamiwa na Wakala kutoka jumla ya migogoro 438 iliyotolewa maamuzi na Baraza la Mawaziri Mwaka 2020 na kubakia na migogoro 15 ambayo utatuzi wake upo katika hatua mbalimbali.

**132. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wakala umeimarisha na kuendeleza mikakati ya kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kujenga weledi na ukakamavu wa maafisa na askari wa Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu kwa kutoa mafunzo ya utayari kwa watumishi 133 wakiwemo askari na maafisa wapya 99 walioajiriwa. Watumishi 455 walipata mafunzo ya muda mfupi na 95 mafunzo ya muda mrefu katika nyanja mbalimbali zikiwemo utumiaji sahihi wa mifumo ya kitaifa ya usimamizi wa rasilimaliwatu ili kuboresha utendaji kazi.

**133. Mheshimiwa Spika,** Wakala umeboresha mazingira ya kazi kwa kuendelea na ujenzi wa majengo 32 ikiwemo ofisi 8, nyumba

4 za watumishi, vituo 18 vya askari, zahanati 1 na lango 1 la utalii. Aidha, Wakala umekamilisha ujenzi wa maghala 8 ya silaha na kuboresha mfumo fungamanishi wa TEHAMA wenye vipengele (modules) 14 ili kuendana na mabadiliko na utoaji huduma kwa wadau. Kutokana na juhudi hizo, usimamizi wa rasilimaliwatu umeimarika na kuwezesha Wakala kupata tuzo ya kuwa mshindi wa kwanza katika Usimamizi Bora wa Rasilimaliwatu kwa Mwaka 2023 miongoni mwa Wakala za Serikali Nchini.

### 3.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

**134. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) ina jukumu la kufanya na kuratibu tafiti za misitu na ufugaji nyuki na kutoa ushauri wa kitaalam katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imefanya jumla ya tafiti 17 zikiwemo tafiti 5 za kimkakati. Tafiti za kimkakati zilizofanyika ni pamoja na tathmini ya rasilimali za misitu kwa ajili ya kuongeza tija katika viwanda vya mazao ya misitu Nchini. Tathmini hii imefanyika katika Mikoa ya Kanda za Magharibi, Kati, Nyanda za Juu Kusini na Ziwa ambapo imebainika kuwepo kwa viwanda takriban 940 vya msingi (viwanda vinavyopokea malighafi moja kwa moja kutoka msituni) vyenye mahitaji ya malighafi za mita za ujazo 7,473,826. Aidha, tathmini imebaini kuwa malighafi zinazopatikana kwa sasa ni mita za ujazo 3,772,239 sawa na asilimia 50 ya mahitaji. Vilevile, tathmini imebaini uwepo wa takriban hekta 266,457.98 zilizopandwa miti kwa ajili ya kutoa malighafi kwenye viwanda vya misitu vilivyopo Nchini. Upungufu wa malighafi uliopo unaonesha kuwa uwekezaji kwenye viwanda vya misitu ni mkubwa kuliko kasi ya upandaji miti. Hivyo, nitoe rai kwa wananchi kuchangamkia fursa hii iliyopo kwa kuanzisha mashamba ya miti katika maeneo yao.

**135. Mheshimiwa Spika**, TAFORI pia imefanya tathmini ya idadi ya miti, hali ya masoko na mchango wa miti jamii ya Mkurungu (Pterocarpus tinctorius), Msandali (Osyris lanceolate), na Msekeseke (Swartzia madagascariensis) ambayo ina mahitaji makubwa sokoni. Tathmini hii imefanyika katika Mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Songwe, Lindi, Ruvuma, Dodoma, Manyara,

Arusha, Tanga na Iringa. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa miti hii inapatikana katika maeneo husika na hupatikana kwa viwango tofauti kati ya jamii moja na nyingine katika misitu iliyohifadhiwa. Mahitaji ya miti jamii ya Mkurungu kwenye soko la kimataifa kwa Mwaka ni takriban mita za ujazo 188,440 ambapo Tanzania inachangia asilimia 7.4 sawa na mita za ujazo 13,883. Kwa kutambua umuhimu wa aina hii ya miti, Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa inaendelea kuhifadhiwa na kuimarisha upatikanaji wake kwa miaka mingi ijayo. Miongoni mwa mikakati iliyopo ni pamoja na kukusanya mbegu za miti hiyo na kuanzisha vitalu vya miche kimkakati kwa jamii hiyo ya miti na miti mingine ya asili katika vituo vya Morogoro, Babati, Mlele na Rondo.

**136. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa changamoto zilizopo kwenye sekta ya ufugaji nyuki hasa zile zinazohusu uzalishaji wa asali zinapata ufumbuzi, TAFORI inaendelea na utafiti wa Miaka 3 utakaokamilika Mwaka 2025 unaohusu maeneo yanayofaa kwa ufugaji nyuki katika kanda mbalimbali za kilimo-ikolojia; aina ya mizinga inayofaa kwenye kila kanda ya kilimo-ikolojia; na uwezo wa Nchi wa kuzalisha asali pamoja na sifa za asali zinazozalishwa. Vilevile, utafiti unaangalia athari za spishi za mimea vamizi kwenye ufugaji wa nyuki; pamoja na kuandaa kalenda ya ufugaji nyuki kwa kila kanda ya kilimoikolojia. Utafiti huu umeanza kufanyika katika wilaya za Kongwa, Chamwino, Manyoni, Sikonge, Kasulu, Mlele, Bukombe, Butiama, Itilima, Morogoro, Kibiti, Handeni, Pangani, Mtama, Tunduru, Mufindi, Njombe, Chunya, Siha, Same na Simanjiro. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa maeneo yanayofaa kwa ufugaji nyuki yametawaliwa na uoto wa Miombo, Migunga, Afromontane (uoto wa mlimani), Mikoko pamoja na uoto wa vichaka vya Itigi. Utafiti huu umesaidia kubaini maeneo yenye uwezo wa kutoa asali yenye sifa za kipekee.

**137. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa takwimu za misitu na ufugaji nyuki zinahifadhiwa na kupatikana kwa wakati, TAFORI imeboresha mfumo wa kieletroniki wa kuhifadhi na kutoa taarifa za misitu na nyuki kwa kuanzisha moduli inayotoa nafasi kwa wadau kuwasilisha taarifa za tafiti na miradi wanayotekeleza

inayohusu Sekta za Misitu na Nyuki ambapo kwa sasa wadau wameanza kuitikia wito wa kuwasilisha takwimu. Aidha, Taasisi ya TAFORI inaendelea na zoezi la kuhamasisha wadau kujiunga kwenye mfumo huu. Kwa upande mwingine, TAFORI imekamilisha ukusanyaji wa taarifa za mazao na huduma mbalimbali za misitu na nyuki kwa ajili ya kufanya tathmini ya mchango wa sekta ya misitu kwenye Pato la Taifa (GDP) kwa kutumia "Green Accounting''.

### 3.3.2.4 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - Tabora – (BTI)

**138. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - Tabora (BTI) kina jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada (Technician Certificate) na Stashahada (Ordinary Diploma) ya Ufugaji Nyuki, mafunzo ya muda mfupi, Ushauri juu ya masuala ya Ufugaji Nyuki na Utafiti. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Chuo kilidahili wanafunzi 394 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ambapo wanafunzi 206 ni wanaume na 188 ni wanawake. Aidha, Chuo cha BTI kiliendesha mafunzo ya muda mfupi kwa vikundi 14 vilivyohusisha washiriki 216. Katika kipindi hicho, Chuo kilikamilisha zoezi la kupitia mitaala ambayo imeanza kutumika mwezi Novemba, 2023.

**139. Mheshimiwa Spika**, katika kuongeza mapato ya ndani, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki – Tabora (BTI) kimetengeneza mizinga ya nyuki 630 kwa wateja mbalimbali ambapo jumla ya Shilingi 56,700,000 imekusanywa. Aidha, Chuo kilishiriki wiki ya utumishi wa umma ambapo pamoja na shughuli nyingine zilizofanyika kilikuwa na banda la kutoa elimu na ushauri kwa wananchi juu ya masuala mbalimbali katika mnyorororo wa ufugaji nyuki. Jumla ya wadau 306 walitembelea banda hilo na kupata elimu. Katika kuboresha miundombinu, Chuo kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) kimeanza ujenzi wa kumbi 2 za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kila moja. Vilevile, Chuo kupitia mradi wa BEVAC kimeanza ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 350 kwa wakati mmoja.

### 3.3.2.5 Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI

**140. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI kina jukumu la kutoa mafunzo na ujuzi katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Chuo kimedahili wanafunzi 358 wanawake 167 na wanaume 191. Vilevile, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya matumizi endelevu ya mazao ya misitu na nishati mbadala kwa wanavijiji 50 wa Wilaya 4 za Mkoa wa Morogoro (Mvomero, Wilaya ya Morogoro, Ulanga na Malinyi). Pamoja na mafunzo ya upangaji madaraja ya mbao (Timber Grading) kwa Maafisa Misitu 11 kutoka Wilaya ya Liwale.

**141. Mheshimiwa Spika,** Chuo kupitia Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) kimeweza kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na kujenga uwezo kwa watumishi. Aidha, Chuo kimepata watumishi wapya 6 kwa ajili ya kuongeza ufanisi na kimepokea gari 1 aina ya land cruiser kwa ajili ya kuwezesha shughuli za mafunzo. Vilevile, Chuo kimekarabati karakana ya mbao na mashine za kuchakata magogo kwa lengo la kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

### 3.3.2.6 Chuo Cha Misitu, Olmotonyi - FTI

**142. Mheshimiwa Spika;** Chuo cha Misitu - Olmotonyi – FTI kina jukumu la kutoa mafunzo ya misitu na uhifadhi wa mazingira kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada na mafunzo ya muda mfupi ya misitu na uhifadhi wa mazingira. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Chuo cha Misitu - Olmotonyi kimedahili na kutoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada ya misitu kwa wanafunzi 840. Kati ya hao wanafunzi 470 ni wanaume na wanafunzi 370 ni wanawake. Katika kuimarisha ufanisi wa kazi, Chuo kimewezesha watumishi 3 kupata mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika fani ya misitu na usimamizi wa maliasili, Mtumishi 1 alipata mafunzo ya shahada ya kwanza ya misitu na Mtumishi 1 mafunzo ya uzamivu. Pia, kuwawezesha watumishi 5 kupata mafunzo mahsusi ya muda mfupi ya mbinu ya kufundisha kwa njia za masafa na huduma ya ofisi. Vilevile, Chuo kimewezesha

watumishi kupata mafunzo ya kutumia mfumo wa Nest, PEPMIS, SARIS na MUSE na kushiriki katika michezo mbalimbali.

**143. Mheshimiwa Spika,** katika kuwahudumia wadau, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya upimaji wa misitu kidijitali kwa maafisa misitu 10 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na mafunzo ya kutumia na kufanya matengenezo ya mashine ya kuangusha miti (chainsaw) kwa wafanyakazi 8 wa kampuni ya Geita Gold Mine. Pia, Chuo kimetoa elimu ya uhifadhi na upandaji miti kwa wanafunzi 1,850 katika shule 8 za Kata ya Olmotonyi, Kaloleni, Mateves na Kisongo zilizopo Wilaya ya Arumeru na Jiji la Arusha. Vilevile, Chuo kimetoa ushauri wa kitaalam kwa Taasisi za TANAPA na TAWA kuhusu aina na kiasi cha miti iliyopo katika baadhi ya hifadhi.

**144. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza chachu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira, Chuo kiliotesha miche ya miti 42,000 na kupanda miche ya miti 40,000 katika shamba la Chuo na miche ya miti 500 iligawiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na miche 1,500 iligawiwa kwa shule 8 katika Kata za Olmotonyi, Kaloleni, Mateves na Kisongo pamoja na wananchi wanaozunguka Chuo. Aidha, Chuo kimetoa huduma ya afya kwa wanafunzi 500 na wananchi 150 katika Kijiji cha Olmotonyi na Sambasha kupitia Zahanati ya Chuo.

**145. Mheshimiwa Spika,** Chuo kimeimarisha mafunzo na huduma za ugani kwa kuingia makubaliano (MOU) na taasisi 2 zisizo za Kiserikali za Dorcas na Hope Beares kwa ajili ya kujengeana uwezo wa kuandika miradi, kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu na mazingira, kuwezesha wananchi kutumia rasilimali za misitu kiuendelevu na kukuza uchumi. Aidha, Chuo kimefanya marejeo ya mitaala 5 ya mafunzo ya misitu na upimaji wa rasilimali za misitu ngazi ya Astashahada na Stashahada na kuboresha miundombinu ya mafunzo kwa kukarabati mabweni 3 na kununua vitendea kazi mbalimbali vya mafunzo.

### 3.3.2.7 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

**146. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mfuko ulitoa ruzuku kwa miradi 112 inayoendelea yenye thamani ya Shilingi 1,273,944,799 na miradi mipya 119 yenye thamani ya Shilingi 1,649,312,300 ya uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni, uanzishwaji wa mashamba ya miti na kuboresha uhifadhi kupitia ufugaji nyuki, utengenezaji na matumizi ya nishati mbadala inayotekelezwa katika Wilaya 102 za Mikoa 26. Ruzuku imetolewa kwa watu binafsi; vikundi vya kijamii vikiwemo vikundi vya vijana na wanawake; mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs); Asasi za kiraia (CSOs); Taasisi za dini (FBOs); Taasisi za mafunzo na Taasisi za utafiti; na Taasisi za Serikali zikiwemo shule za msingi na sekondari, Idara, Mashirika na Wakala wa Serikali, na Mamlaka mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, Mfuko ulifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi 201 iliyopatiwa ruzuku kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa ufanisi.

**147. Mheshimiwa Spika**, Mfuko umewezesha TAFORI kufanya na kuratibu tafiti 6 za kimkakati pamoja na kuwezesha uandaaji Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki unaojulikana kama "Achia Shoka, Tundika Mzinga".

Aidha, Mfuko ulitoa ufadhili wa masomo katika Shahada ya Uzamili na Uzamivu kwa watumishi 2 kutoka TAFORI na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) katika fani ambazo hazina wataalam katika Sekta ya misitu ambazo ni magonjwa ya mimea (Plant Pathology) na uzalishaji wa mimea kwa kutumia teknolojia za kisasa (Tree Breeding). Vilevile, Mfuko ulitoa tuzo kwa wanafunzi 21 waliofanya vizuri katika mafunzo ya nadharia na vitendo na Shahada ya Misitu kwa Vyuo vya FTI, FITI, BTI na SUA. Halikadhalika, Mfuko ulitoa tuzo ya ufadhili kwa wanafunzi 9 waliofaulu vizuri katika ngazi ya Astashahada wanaofadhiliwa kusoma Stashahada ya Misitu (FTI 3); ufugaji nyuki (BTI 3); na viwanda vya misitu (FITI 3). Sambamba na hilo, Mfuko ulinunua magari 2 kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu na

nyuki na ukusanyaji wa maduhuli. Kwa upande mwingine, Mfuko umepata hadhi ya kuwa Taasisi baada ya Muundo wake kupitishwa na kuidhinishwa Aprili, 2024. Kupitia Muundo huo mpya, Mfuko utaongeza ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake.

**148. Mheshimiwa Spika**, Mfuko uliwezesha pia vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki – NABAC; Kamati ya Uendeshaji ya Mazao ya Misitu yaliyohandisiwa – EWP; na Kikundi kazi cha Misitu kilichopo chini ya Baraza la Taifa la Biashara - TNBC. Aidha, Mfuko uliwezesha mafunzo ya kujenga uwezo wa kuandaa maandiko kwa ajili ya kuomba fedha za tozo ya upandaji miti kwa Maafisa Misitu wa Mikoa 26 na wawakilishi kutoka TFS Makao Makuu na Kanda, pamoja na kuwezesha maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Upandaji Miti Kitaifa yaliyofanyika Wilayani Same, Mkoani Kilimanjaro. Vilevile, uliwezesha Wizara kushiriki katika Mkutano wa Wafugaji Nyuki Duniani (Apimondia) uliofanyika Nchini Chile na Mkutano wa 28 wa Dunia wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu. Kwa upande mwingine, Mfuko uliandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 13 wa Shirikisho la Mifuko ya Uhifadhi Barani Afrika (CAFE`) uliofanyika Jijini Arusha na kuhudhuriwa na washiriki 47 kutoka Nchi 17 za Afrika na Nchi 3 za Latini Amerika.


### 3.3.3 Sekta ya Utalii

**149. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii ndani na nje ya Nchi. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999, Sheria ya Utalii, Sura ya 65 na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364. Kulingana na Muundo, jukumu hilo linatekelezwa kupitia Idara ya Utalii inayosimamia maendeleo ya utalii, udhibiti wa ubora na huduma; Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) iliyokasimiwa dhamana ya kutangaza na kuhamasisha utalii ndani na nje ya Nchi; na Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) wenye jukumu la kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani ya utalii na ukarimu.


### 3.3.3.1 Idara ya Utalii

**150. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kukuza utalii ikiwa ni pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma, miundombinu ya utalii na utangazaji wa vivutio vya utalii kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo Programu Maalum ya Tanzania-the Royal Tour. Kufuatia utekelezaji wa mikakati hiyo, idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa asilimia 20 kutoka watalii 1,527,230 Mwaka 2019 hadi watalii 1,808,205 Mwaka 2023. Aidha, idadi ya watalii imeongezeka kutoka 351,755 kwa kipindi cha Januari hadi Machi, 2019 hadi kufikia watalii 520,324 kwa kipindi kama hicho kwa Mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 48 la watalii waliowahi kufikiwa kwa robo ya kwanza baada ya UVIKO-19 Mwaka 2019. Kwa upande mwingine, mapato yatokanayo na shughuli za utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 Mwaka 2019 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.4 Mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 31 kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania.

**151. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, World Tourism Barometer ya Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) Januari 2024, imeitambua Tanzania kuwa miongoni mwa Nchi ambazo zimevunja rekodi ya idadi ya juu zaidi ya watalii wa kimataifa (Best performing destinations January to December 2023) kuwahi kufikiwa kabla ya janga la UVIKO-19 Mwaka 2019. Aidha, Tanzania imeshika nafasi ya 12 duniani kwa ongezeko la watalii ikitanguliwa na Uturuki, Qatar, Saudi Arabia, Albania, El Salvador, Colombia, Andorra, Ethiopia, Curacao, Jamhuri ya Dominican na Visiwa vya US Virgin. Vilevile, Tanzania ni Nchi ya 2 Barani Afrika kwa ongezeko la watalii ikilinganishwa na vipindi kama hivyo vya mwaka 2019 na 2023 kama inavyoonekana katika kielelezo hapa chini.




**152. Mheshimiwa *Spika,*** Ongezeko la watalii limeiwezesha Tanzania kwa Mwaka 2023 kuingia katika Nchi 10 bora zenye mapato zaidi yatokanayo na shughuli za utalii ikiwa ni Nchi ya 3 barani Afrika baada ya Morocco na Mauritius. Aidha, Tanzania imekuwa Nchi ya 9 duniani ikitanguliwa na Serbia, Pakistan, Uturuki, Romania, Ureno, Mauritius, Morocco na Latvia ambazo mapato yake ya Sekta ya Utalii yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 28 ikilinganishwa na rekodi za Mwaka 2019 kabla ya janga la UVIKO-19 kama inavyoonekana katika kielelezo hapa chini.




**153. Mheshimiwa *Spika,*** katika hatua nyingine, Tanzania imefanikiwa kurekodi idadi ya juu zaidi ya watalii wa kimataifa iliyofikia asilimia 53 katika kipindi cha Januari hadi Machi 2024 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa Mwaka 2019 kabla ya UVIKO-19. Ongezeko hilo limeitambua Tanzania kama Nchi ya 5 Duniani ikitanguliwa na Qatar, Albania, Saudi Arabia na El Salvador na ya kwanza Barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya watalii. Aidha, kwa upande wa mapato yatokanayo na utalii, Tanzania imeendelea kufanya vyema na kushika nafasi ya 4 Duniani ikitanguliwa na Serbia, Uturuki na Pakistan kwa ongezeko la asilimia 62 ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha robo ya kwanza kabla ya UVIKO-19 Mwaka 2019. Taarifa hizi ni kwa mujibu wa World Tourism Barometer ya Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) Mei, 2024.

**154. Mheshimiwa *Spika,*** halikadhalika, kwa mujibu wa World Tourism Barometer ya Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) ya Machi 2024, Tanzania imefanikiwa kuongeza idadi ya mapato kwa asilimia 62 ikishika nafasi ya nne duniani baada ya Serbia, Uturuki na Pakistan ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha robo ya kwanza kabla ya UVIKO-19 Mwaka 2019. Ongezeko hilo limeiwezesha Tanzania kuwa Nchi ya Kwanza Afrika.

**155. Mheshimiwa Spika,** sambamba na mafanikio hayo, Mlima Kilimanjaro umetambuliwa na Kampuni ya Usafiri ya Uingereza iitwayo Explore Worldwide kama alama ya asili zinazokumbukwa Duniani yaani The World's Most Unforgettable Natural Landmarks, baada ya kupata alama zaidi kati ya maeneo 150 yaliyofanyiwa tafiti na kampuni hiyo. Aidha, wadau wa Sekta ya Utalii walishinda tuzo za World Travel Awards katika vipengele mbalimbali ikiwemo: Kisiwa cha Thanda kilichopo Shungumbili Mafia kushinda tuzo ya World Leading Exclusive Private Island kwa Mwaka 2023; Zara Tours kupata tuzo ya Africa's Leading Tour Operator 2023 kwa mara ya pili mfululizo; na Twiga Tours kushinda tuzo ya Africa's Responsible Tourism Award 2023. Vilevile, zao la utalii wa puto Nchini limeng'ara Kimataifa ambapo Kampuni ya Serengeti Balloon Safaris ilipata Certificate of Excellence kutoka TripAdvisor. Kwa ujumla, tuzo hizo zimeendelea kuitangaza Tanzania na kuimarisha utambulisho wake katika soko la utalii Kimataifa.

**156. Mheshimiwa Spika,** utangazaji utalii Kimataifa umeendelea kufanyika kwa kuendelea kusambaza filamu ya Tanzania - the Royal Tour na kupitia filamu mpya ya Amazing Tanzania ambapo **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** wameshiriki kama wahusika wakuu. Aidha, msanii mahiri wa filamu wa Nchini China Bw. Jin Dong ameshiriki pia kuitangaza Tanzania kupitia filamu hiyo. Filamu hiyo imelenga kuitangaza Tanzania katika ukanda wa Asia, hususan soko la China linalozalisha zaidi ya watalii milioni 80 wa Kimataifa, hatua inayoenda sambamba na utekelezaji wa malengo ya Programu ya Tanzania - the Royal Tour katika kukuza utalii. Uzinduzi wa filamu hiyo ulifanyika tarehe 15 Mei, 2024 Jijini Beijing, China sambamba na Maadhimisho ya Miaka 60 ya Kidiplomasia kati ya Tanzania na China katika Sekta za Utalii na Utamaduni. Tukio hilo lilihudhuriwa na washiriki mbalimbali wakiwemo Wakala Wakubwa wa Biashara za Utalii. Aidha, filamu ya Amazing Tanzania itatafsiriwa kwa lugha mbalimbali zinazotumika Bara la Asia na kurushwa katika vyombo vya habari Nchini China na kutangazwa kwa njia za kidijitali ikiwemo mitandao ya kijamii.






Uzinduzi wa filamu ya Amazing Tanzania uliofanyika tarehe 15 Mei, 2024 Jijini Beijing, China sambamba na Maadhimisho ya Miaka 60 ya Kidiplomasia kati ya Tanzania na China katika Sekta za Utalii na Utamaduni.

**157. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kutangaza utalii, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Sekta Binafsi iliandaa Tukio la Epic Tanzania Tour lililofanyika Disemba, 2023 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Tukio hilo lilihusisha watalii na wawekezaji takriban 80 wakiongozwa na mchezaji Veterani wa Tennis namba moja duniani Bw. John McEnroe. Aidha, kupitia Epic Tanzania Tour Nchi yetu ilitangazwa Kimataifa katika vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo jarida maarufu la World Tennis, tovuti za Forbes na gazeti la The Times la Uingereza.




Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati (kushoto) akimpongeza mcheza tennis mashuhuri duniani, John McEnroe mara baada ya kumkabidhi Kombe katika mashindano ya mchezo maalum wa tennis yaliyofanyika Hifadhi ya Taifa Serengeti.

**158. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano na matukio ya utalii Kimataifa ikiwemo: Mkutano wa WTTC Global Summit uliofanyika Novemba, 2023 Jijini Kigali, Rwanda; Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani Septemba, 2023 Jijini Riyadh, Saudi Arabia; Mkutano Mkuu wa 25 wa UN - Tourism uliofanyika Oktoba, 2023 Jijini Samarkand, Uzbekistan na Mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Utalii Kanda ya Afrika uliofanyika Agosti, 2023 Nchini Mauritius ambapo Tanzania ilichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na Mjumbe wa Kamati Tendaji ya Shirika hilo. Ushiriki wa Tanzania katika matukio hayo ya Kimataifa ulilenga kuwa sehemu ya maamuzi katika chombo hicho muhimu cha utalii Duniani, kufahamu fursa zilizopo katika utalii wa Kimataifa, kuitangaza Tanzania na vivutio vyake, kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Utalii, kubadilishana uzoefu katika kukuza Sekta ya Utalii na kuongeza wigo wa fursa za mafunzo mbalimbali kwa wadau wa utalii.




Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akihutubia na kufuatilia matukio katika Mkutano wa WTTC Global Summit uliofanyika Novemba, 2023 Jijini Kigali, Rwanda.

**159. Mheshimiwa Spika,** kufuatia ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (World Travel and Tourism Council - WTTC), Wizara ya Maliasili na Utalii imefanikiwa kujiunga na Baraza hilo. Hatua hii itaiwezesha Tanzania kuvutia mikutano ya Kimataifa inayoratibiwa na Baraza hilo na kupata taarifa za utalii wa Kimataifa zikiwemo uendelezaji na utangazaji utalii; masoko na mazao mapya ya utalii na kuvutia uwekezaji wa huduma za utalii. Vilevile, Bodi ya Utalii Tanzania ipo katika hatua

za mwisho za kukamilisha taratibu za kuwa Mwanachama wa Shirika la Mikutano Duniani (International Congress & Convention Association – ICCA) kwa ajili ya kuongeza fursa za uenyeji wa mikutano na matukio ya Kimataifa.

**160. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa Sheria ya Utalii, Sura ya 65 kwa kuzikagua Wakala wa Biashara za Utalii 387 na 1,576 za Waongoza Watalii. Kaguzi hizo zilifanyika katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Songwe, Dodoma pamoja na malango ya kuingilia wageni ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi za Taifa za Ziwa Manyara, Mikumi, Tarangire na Ruaha. Hatua hiyo ililenga kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayosimamia biashara za utalii Nchini, na kutambua Wakala wapya wa biashara za utalii ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na Ada ya Leseni za Biashara za Utalii Nchini.

**161. Spika,** uhakiki wa Wakala wa biashara za utalii umefanyika katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Songwe na Dodoma ambapo jumla ya huduma za malazi 378 zilihakikiwa na kutambuliwa kuwa na sifa ya kukusanya Tozo ya Kitanda Siku (Bed Night Levy). Aidha, hatua hiyo imeongeza idadi ya huduma za malazi zenye sifa ya kukusanya Tozo ya Kitanda Siku katika Mikoa tajwa kutoka 2,699 Mwaka 2021 hadi kufikia 3,077 Mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 14. Aidha, kupitia zoezi hilo, watoa huduma za malazi walipata fursa za kupokea ushauri wa kitalaam kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za malazi ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya soko la utalii wa ndani na Kimataifa.

**162. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kukutana na kushirikiana na wadau mbalimbali kupitia vikao vya ushirikiano kwa lengo la kupokea maoni ya kuimarisha na kukuza Sekta ya Utalii Nchini. Hatua hiyo imehusisha matukio mbalimbali, ikiwemo Kikao cha Kamati ya Ushauri wa Kitaalam kilichofanyika Julai, 2023 Jijini Dodoma; Kikao cha Kikundi Kazi cha Kongani ya Sekta ya Utalii chini ya Jukwaa la Baraza la Biashara la Taifa kilichofanyika Disemba, 2023 Jijini Arusha; Mkutano wa wadau wa

utalii kwa ajili ya kutoa maoni kuhusu Rasimu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999 uliofanyika Disemba, 2023 Jijini Arusha; pamoja na Kikao cha Wizara na Wadau wa Utalii kilichofanyika Aprili, 2024 Jijini Arusha. Jitihada hizo zimekuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo kujenga uelewa wa pamoja wa masuala yanayohusu usimamizi wa Sekta ya Utalii; kutatua changamoto zinazoikabili Sekta; na kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa utalii kutoka Sekta ya Umma na Binafsi.

**163. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuendeleza na kupanua wigo wa mazao ya utalii Nchini, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau imetekeleza zoezi la kubaini vivutio vya utalii ambapo jumla ya vivutio vya utalii 58 vyenye sifa za kuendelezwa vimebainishwa vikihusisha Mkoa wa Rukwa vivutio 15 na Mkoa wa Morogoro vivutio 43. Vivutio vilivyobainishwa katika Mkoa wa Morogoro ni pamoja na Safu za Milima ya Uluguru, Milima ya Kanga, Michoro ya Miambani ya Ukaguru Petroglifi na Pango la Tambiko Msitu wa Kimboza. Kwa upande wa Mkoa wa Rukwa ni pamoja na Maporomoko ya Maji (Sali, Hululu, Kifuka, Choma), Mapango ya Bokela na Mwanaluvele, Maporomoko ya Maji (Kalambo na Ntembwa), Kanisa la Kale Kipili na Eneo la Utamaduni la Milanzi. Sambamba na hatua hiyo, vivutio 17 vimebainishwa katika Mkoa wa Songwe kwa lengo la kuviendeleza na kuvitangaza. Vivutio hivyo ni pamoja na Maporomoko ya Maji ya Mto Momba (Mpona), Safu za Milima ya Ufipa, eneo la Kimondo cha Ivuna, Fukwe za Ziwa Rukwa, Bwawa la Chumvi la Itambula, Madaraja ya Kale ya Kamba ya Kiteputepu, Majengo ya Makanisa katika maeneo ya Mkulwe na Ngome ya Malkia na Vituo vya Utamaduni vya Kabila la Wanyamwanga.

**164. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kukuza zao la utalii wa mikutano na matukio Nchini. Juhudi hizo zinahusisha mafanikio ya kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa kama vile: Mkutano wa Jukwaa la Chakula Barani Afrika - AGRF Summit uliofanyika Septemba, 2023; Mkutano wa 24 wa Kamisheni ya Misitu na Wanyamapori Afrika uliofanyika Oktoba, 2023; Global

Youth Climate Summit uliofanyika Oktoba, 2023; 2024 Eastern Africa Regional Early Childhood Conference on Early Childhood uliofanyika Machi, 2024; na WomenLift Health Global Conference 2024 uliofanyika Aprili, 2024. Aidha, kupitia uendelezaji wa zao hilo la kimkakati Tanzania imefanikiwa kuwa mwenyeji wa mikutano na matukio makubwa ya Kimataifa ikiwemo Kongamano la 109 la Esperanto Duniani litakalofanyika Agosti, 2024 Jijini Arusha likihusisha zaidi ya washiriki 1,000.

**165. Mheshimiwa Spika,** katika kutangaza na kuendeleza zao la utalii wa meli, Wizara imeendelea kushirikiana na wakala wa utalii ambao ni pamoja na Takims Holidays, Savannah Tours Ltd, Akom Destination Management na Abercrombie & Kent (A&K) wenye mtandao mkubwa katika soko la utalii wa meli Kimataifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 safari za meli 10 za kitalii zimefanyika ambazo zimeleta jumla ya watalii 1,310. Meli hizo ni kutoka kampuni ya Hedridren Sky iliyofanya ziara mara 2 ikiwa na watalii 204, Le Champlain iliyofanya ziara mara 4 ikiwa na watalii 482, Le Bougainville iliyofanya ziara mara 2 ikiwa na watalii 279, The World iliyofanya ziara mara 1 ikiwa na watalii 115 pamoja na Silver Cloud iliyofanya ziara mara moja ikiwa na watalii 230. Watalii hao walitoka katika Nchi za Marekani, Ufaransa, Canada, Italia, Ubelgiji, Australia, Austria, Uingereza, Ujerumani, Poland, Urusi, China, Uhispania, Denmark, Equador, Korea ya Kusini, Luxembourg, Ureno, Singapore, Uswizi, Ufini, Norway, Afrika ya Kusini na Visiwa vya Bahama. Ujio wa meli hizo umekuwa na manufaa katika kuongeza idadi ya watalii wa Kimataifa na mapato. Kwa upande mwingine, Wizara imeendeleza juhudi za kutanua wigo wa mazao ya utalii Nchini ikihusisha utalii wa michezo (sports tourism), utalii wa tiba (medical tourism), utalii wa nyuki (api-tourism), utalii wa vyakula (gastronomy) na halal tourism.

**166. Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kuendeleza zao la utalii wa fukwe Nchini, Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa Mkakati wa Uendelezaji Utalii wa Fukwe Katika Ukanda wa Pwani (Sustainable Coastal Tourism Development Strategy) wa kipindi cha Mwaka 2024 – 2034. Aidha, Wizara inaendelea na maandalizi ya Mwongozo wa Pamoja wa Uendelezaji wa Sekta

ya Utalii utakaotoa fursa za moja kwa moja kwa wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu katika kuendeleza na kukuza Sekta ya Utalii Nchini. Mwongozo huo utajikita katika kutambua, kubainisha, kuboresha na kutangaza vivutio vya utalii.

### 3.3.3.2 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB

**167. Mheshimiwa *Spika,*** Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Bodi ya Utalii Tanzania imeendelea kuratibu ushiriki wa Nchi katika kuhamasisha na kutangaza utalii kwenye masoko mbalimbali Duniani. Utangazaji huo umefanyika kupitia maonesho 20 ya utalii ya Kimataifa katika Nchi ambazo ni masoko ya utalii ya msingi na kimkakati. Maonesho hayo ni pamoja na: WTM – London (Uingereza), ITB Berlin (Ujerumani), World Travel Latin America – WTML (Brazil), Meetings Africa na WTM Africa (Afrika Kusini), East African Regional Tourism Expo – EARTE (Kenya), IFTM – Top Resa (Ufaransa), IMEX (Ujerumani), KOFTA (Korea Kusini), My Tanzania Roadshow katika Nchi za Ulaya, Japan Tourism Expo (Japan), International Tourism & Travel Show – ITTS (Canada), China Outbound Travel and Tourism Market (China), FITUR (Hispania), OTM – India (India), Dallas Safari Club International (Marekani) na Global Geoparks Network Conference (Morocco).

**168. Mheshimiwa *Spika,*** ushiriki wa Wizara katika maonesho hayo ya kimataifa pia ulihusisha taasisi zingine ikiwemo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA), na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS). Wadau kutoka Sekta Binafsi hususan wakala wa biashara za utalii, watoa huduma za malazi, na kampuni za ndege nao walishiriki pamoja na Wizara katika Maonesho hayo kwa lengo la kuongeza tija ya ushiriki wetu.

**169. Mheshimiwa Spika,** maonesho hayo ambayo yalihusisha Sekta Binafsi yametoa mchango muhimu katika kuvitangaza vivutio vya utalii Kimataifa, kuvutia uwekezaji katika utalii, pamoja na kuongeza idadi ya watalii na mapato. Juhudi hizo zimewezesha kuandaliwa kwa misafara ya utangazaji utalii yaani Roadshows katika Nchi 6 ambazo ni Uswisi, Italia, Ufaransa,

Ujerumani, Brazili na China. Aidha, kupitia ushiriki huo, Tanzania imeweza kufikia masoko mapya, kuanzisha uhusiano wa kibiashara na kutafuta fursa za masoko mchanganyiko kwa muktadha wa kupunguza utegemezi katika masoko ya msingi ya utalii.

**170. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Bodi ya Utalii iliandaa Onesho la Saba la Swahili International Tourism Expo - S!TE 2023 lililofanyika tarehe 6 hadi 8 Oktoba, 2023 Jijini Dar es Salaam. Onesho hilo lilihusisha waoneshaji 99 na wanunuzi 72 wa Kimataifa ikilinganishwa na waoneshaji 77 na wanunuzi 43 wa Mwaka 2022. Kupitia onesho hilo, Wakala wa Utalii 63 na Waandishi wa Habari 9 kutoka Nchi za Uingereza, Marekani, Australia, Bangladesh, Canada, China, Jamhuri ya Czech, Finland, Indonesia, India, Japan, Kenya, Uholanzi, Nigeria, Oman, Pakistan, Poland, Qatar, Romania, Urusi, Rwanda, Afrika Kusini na Uhispania walipata fursa ya kushiriki semina za utalii na mikutano ya kibiashara (speed networking and B2B sessions). Vilevile, Onesho hilo lilihusisha Bodi za Utalii kutoka Nchi rafiki za Afrika ikiwemo Malawi na Uganda.

**171. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii iliratibu kwa mara ya kwanza Kongamano la Uwekezaji Utalii Tanzania (Tanzania Tourism Investment Forum) kwa lengo la kutangaza fursa mbalimbali za uwekezaji wa huduma za utalii na miundombinu ikiwemo malazi, biashara za utalii na uendelezaji wa mazao ya utalii. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki zaidi ya 150 wakijumuisha Viongozi wa Serikali; Mabalozi wanaowakilisha Nchi mbalimbali ikiwemo China, Indonesia, Saudi Arabia, Oman, Rwanda, Msumbiji; Wawekezaji; na wadau waliopo katika mnyororo wa thamani wa Sekta ya Utalii.

**172. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza ubunifu wa utangazaji utalii, Bodi ya Utalii Tanzania iliratibu ziara za kimkakati za mafunzo ya utalii (FAM - Trips) 9 zenye jumla ya washiriki 91 kutoka Nchi za Afrika Kusini, Kenya, Nigeria, Australia, Qatar, Canada, Urusi, Ujerumani, Romania, Indonesia, Uhispania, Uholanzi, Jamhuri ya Czech, India, Indonesia, Pakistan, Bangladesh, Poland, Uingereza na Oman. Ziara hizo zilihusisha

Waandishi wa Habari na Wakala wa Safari za utalii kutoka Nchi mbalimbali akiwemo Mwandishi Ojeer Thandiwae kutoka Gazeti maarufu The Times la Uingereza. Aidha, washiriki hao walipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Urithi wa Dunia wa Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, Pugu hills, Matema Beach, Lake Ngosi, Kalambo Falls, Hifadhi za Taifa (Mikumi, Serengeti, Udzungwa, Mkomazi, Nyerere, Ruaha), Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Zanzibar. Ziara hizo zimeendelea kuleta tija kwa Nchi katika masuala ya utangazaji utalii. Mathalan, kuwezesha Waandishi wa Vyombo vya Habari na Wakala wa Safari za Utalii kupata uzoefu wa vifurushi vya utalii vinavyofungamanisha mazao na vivutio vilivyopo Nchini kwa dhumuni la kuhamasisha watalii kutoka Nchi zao kuja kutembelea Tanzania.

**173. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania imeanzisha ushirikiano na kampuni kubwa za utalii Duniani kwa lengo la kuimarisha utangazaji utalii. Utekelezaji huo ni pamoja na kusaini Makubaliano ya Awali ya Ushirikiano (Letter of intent) na Kampuni ya Expedia Group ya Marekani yenye ushawishi mkubwa katika masuala ya utangazaji wa vivutio, uuzaji wa vifurushi vya mazao ya utalii na huduma mbalimbali zinazotumiwa na watalii katika soko la Kimataifa. Mathalan, Expedia Group ina mtandao unaowafikia watu takriban milioni 450 Duniani kwa mwezi na umeunganishwa na mifumo mingine kama vile Trivago, Travel Velocity, na Booking.com inayotumiwa na idadi kubwa ya watalii katika Nchi zaidi ya 70 katika masoko ya Ulaya na Amerika.

**174. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania inaendelea na mazungumzo na kampuni za kimataifa kwa lengo la kushirikiana katika kutangaza vivutio vya utalii zikiwemo TUI Group ya Ujerumani; Google ya Marekani; Chimelong na Omni Horizon Group za China. Aidha, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) imeanzisha ushirikiano na Chama cha Wakala wa Utalii Marekani kijulikanacho kwa jina la United States Tour Operator Association (USTOA) kwa lengo la kutangaza utalii katika soko hilo la utalii ikiwa ni Nchi inayoongoza kwa kuleta watalii Tanzania. Sambamba na hilo, TTB imesaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano na kampuni ya Extreme Rally ya Uingereza kwa lengo

la kushirikiana katika kufanikisha michezo ya mbio za magari ili zifanyike Tanzania.

**175. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania ilitumia fursa ya Shindano la Kimataifa la Urembo na Utanashati kutangaza vivutio vyetu vya utalii kwa watu wenye usikivu hafifu (Miss and Mister Deaf International) lililofanyika Nchini Novemba, 2023 likihusisha washiriki 157 kutoka Nchi za Marekani, Ufaransa, Ujerumani, Romania, Macedonia, Mexico, Australia, India, Thailand, Pakistan, Morocco na Afrika Kusini. Aidha, washiriki 135 walipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya Taifa Mikumi. Tukio hilo la Kimataifa lilifuatiliwa na watu mbalimbali Duniani zikiwemo Nchi walizotoka washiriki. Vilevile, TTB iliratibu tukio la kuweka Rekodi ya Dunia ya Guinness World Records ya kupiga Kinubi kileleni mwa Mlima Kilimanjaro ambao ni Mlima mrefu zaidi Barani Afrika, iliyowekwa na Mpiga Kinubi maarufu Bi. Siobhan Brady kutoka Ireland. Tukio hilo lilitangazwa katika tovuti na mitandao ya Guinness World Records yenye wafuasi zaidi ya milioni 10.2 Duniani hivyo, kuchagiza utangazaji wa Mlima Kilimanjaro katika masoko mbalimbali na kuvutia watalii kutembelea Nchini.




Mpiga Kinubi maarufu Bi. Siobhan Brady kutoka Ireland aliyeweka Rekodi ya Dunia ya Guinness World Records ya kupiga Kinubi kileleni mwa Mlima Kilimanjaro

**176. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania ilishirikiana na wadau wa Sekta Binafsi kuratibu safari 5 za treni ya kifahari Duniani ijulikanayo kama Rovos Rail, inayotumia teknolojia ya zamani ya injini ya mvuke. Safari hizo zilianzia Jijini Capetown, Afrika Kusini hadi Dar es Salaam, kupitia mtandao wa reli

ulioounganishwa na TAZARA zikiwa na jumla ya watalii 255. Aidha, wageni hao walitembelea vivutio vya utalii vikijumuisha Makumbusho ya Taifa, Hifadhi za Taifa Nyerere, Mikumi, Serengeti na maeneo ya Bagamoyo na Zanzibar.

**177. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania imeendelea kushirikiana na Ofisi za Balozi za Tanzania katika Nchi mbalimbali kutangaza utalii. Hatua hii imeenda sanjari na utoaji wa semina kuhusu utangazaji utalii kwa Waheshimiwa Mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika Nchi 9 zikiwemo Austria, Ufaransa, Oman, Namibia, Brazil, Uingereza, Ethiopia, Uholanzi na Indonesia. Kupitia semina hiyo, viongozi hao walijengewa uelewa kuhusu rajamu ya Tanzania, Unforgettable! inayotambulisha Nchi kiutalii pamoja na kuwakabidhi vitendea kazi ikiwemo msimbopapo (QR Codes) wenye kutoa taarifa za utalii na vivutio kidijitali.

**178. Mheshimiwa Spika,** katika kuyafikia masoko ya msingi na kimkakati na kujenga imani ya watalii katika masoko hayo, Bodi ya Utalii Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Nchini Uingereza imeajiri Afisa wa Dawati la Utalii, ambapo kwa kuzingatia uzoefu wake anashughulikia masoko ya utalii ya Uingereza na Ireland. Vilevile, semina maalum kuhusu vivutio na mazao ya utalii zilitolewa kwa Maafisa Uhamiaji na Wanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi - NDC ambacho ni Chuo chenye wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali. Halikadhalika, Bodi ya Utalii Tanzania imesambaza msimbopapo (QR Code) wenye dodoso la Tathmini ya Ubora wa Huduma za utalii Nchini katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Kilimanjaro na Abeid Amani Karume ili kupata mrejesho wa huduma mbalimbali za utalii Nchini kwa lengo la kuziboresha. Hadi sasa jumla ya madodoso 218 yamefanyiwa upembuzi ambapo asilimia 93 ya watalii waliojaza madodoso hayo wameonesha kuridhishwa na huduma za utalii zitolewazo hapa Nchini.

**179. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, shughuli za utangazaji zimeendelea kufanyika kupitia Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali (Destination Digital Marketing Command Centre -

DDMCC). Hatua hiyo imewezesha kusambaza taarifa zinazohusu vivutio kwa watalii watarajiwa na wadau waliopo sehemu mbalimbali Duniani. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2024 idadi ya wafuatiliaji (followers) wa taarifa za utalii wa Tanzania walifikia 851,761 zenye maoni zaidi ya 48,413 katika mitandao ya kijamii inayosimamiwa na Bodi. Kwa upande mwingine, Bodi ya Utalii iliandaa maudhui 48 yaliyotumika kutangaza kidijitali vivutio na mazao ya utalii, hususan katika Kanda ya Utalii Kusini. Vilevile, iliandaa matangazo ya utalii yaliyooneshwa mubashara wakati wa michuano ya ligi ya Mabingwa Afrika (CAF Championship League) na Kombe la Mapinduzi (Mapinduzi Cup – Zanzibar).

**180. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile Wakala wa Safari za Utalii na Vyombo vya Habari kutangaza utalii wa ndani kupitia Kampeni za uhamasishaji ikiwemo Likizo Time. Kupitia kampeni hiyo ya Likizo Time jumla ya watalii wa ndani 2,146 walitembelea vivutio vya utalii Nchini. Vilevile, Bodi imeendelea kuratibu na kushiriki matukio ya ndani yenye mwitikio mkubwa wa Wananchi kama vile Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), Nanenane, Utalii Karibu Kusini, Kizimkazi Festival, Mafia Festival, Z-Summit (Zanzibar), Kijereshi Festival, Tamasha la Kumbukizi ya Vita ya Majimaji na Utalii wa Utamaduni, Tamasha la Majimaji Nandete, East African Trade Fair – Mwanza, Mpalano Festival, Tulia Traditional Dances Festival, Azimio la Arusha Festival, Same Utalii Festival, NBC Marathon, Tanga Tourism and Business Expo, Chato Utalii Festival na tukio maalum la kupanda Mlima Lolmalasin katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha utalii wa ndani wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani.

### 3.3.3.3 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

**181. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala Na. 30 ya Mwaka 1997, na kina dhamana ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani za utalii na ukarimu. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Chuo kimetoa mafunzo ya umahiri (Competence Based Education and Training - CBET) kwa jumla

ya wanafunzi 1,493 ambapo wanafunzi 250 kati ya hao wanawake walikuwa 77 na wanaume 173 walifanya programu maalum ya Uanagenzi na 1,243 kati ya hao wanawake 599 na wanaume 644 wanafanya mafunzo kwa ngazi ya Astashada na Stashahada.

**182. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii pia kimeendelea kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa huduma za utalii. Mafunzo hayo yametolewa kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari wa vyeo mbalimbali wa Jeshi la Polisi Tanzania 8,250; Watumishi 74 wa Shirika la Reli wanaotarajiwa kuhudumia wasafiri katika treni ya kisasa ya umeme ya SGR, Watumishi 19 kutoka Wakala wa Huduma za Ndege za Serikali, Wadau 51 kutoka Wilaya ya Pangani, Vijana 420 kupitia Tamasha la Chato Utalii Festival kutoka Geita na waratibu matukio 110 kutoka Taasisi mbalimbali. Utoaji wa mafunzo hayo umekuwa na manufaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga uwezo wa wadau wa utalii kutoa huduma bora kwa wageni.

**183. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kiliandaa Kongamano la 3 la Kitaaluma la Chuo (Convocation Day) lililofanyika Disemba 2023 na kuhudhuriwa na washiriki 412. Aidha, Chuo kinaendelea na ushirikiano na Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam (Dar es Salaam Marine Institute - DMI) katika utoaji wa mafunzo ya mapishi ya kwenye meli (Ship Cooks) ili la kuongeza wigo kwa vijana wa Kitanzania kupata fursa za ajira katika meli za kitalii zinazosafirisha watalii Duniani. Aidha, Chuo cha Taifa cha Utalii kimetoa mafunzo kwa Mabaharia 19 katika fani ya mapishi ya kwenye meli.

**184. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kimeendelea kushirikiana na Taasisi ya China (Confucius Institute - CI UDSM) katika utoaji wa mafunzo ya Lugha ya Kichina kwa wanafunzi na wadau wengine. Jumla ya Wanafunzi 235 wanaendelea na mafunzo ya lugha hiyo kwa Mwaka wa Masomo 2023/2024. Kwa upande mwingine, Chuo kimesaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano na Jeshi la Polisi, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Chuo cha VETA Chato kwa lengo la kuendelea kuimarisha utoaji wa

huduma za ukarimu na utalii kwa wageni mbalimbali wanaotembelea Nchini. Aidha, katika kuboresha miundombinu ya utoaji wa mafunzo, Chuo kimeendelea na ujenzi wa Jengo la Taaluma lenye uwezo wa kutoa mafunzo kwa Wanafunzi zaidi ya 1,200 Jijini Arusha.

**185. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kina jumla ya Watumishi 117 waliopo katika ajira ya masharti ya kudumu na Watumishi 55 wa mikataba ya muda mfupi na kujitolea. Aidha, mwezi Novemba, 2022 Chuo kilifanikiwa kuidhinishiwa Muundo Mpya wa Taasisi (Organizational Structure) pamoja na Miundo ya Maendeleo ya Utumishi na Mishahara (Schemes of Service and Salary Structure) ambayo utekelezaji wake umekamilika kwa Watumishi kubadilishiwa vyeo na mishahara. Vilevile, jumla ya nafasi 15 kati ya 18 sawa na asilimia 79 za Uongozi zimejazwa na zilizobaki taratibu za kuzijaza zinaendelea katika Mamlaka husika. Kwa upande mwingine, Mpango wa Mafunzo umeendelea kutekelezwa ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Watumishi 44 wamepata mafunzo ambapo Watumishi 14 wamepata mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 30 ya muda mfupi.

**186. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kiliandaa Tamasha la Vyakula vya Asili (Local Food Festival) lililofanyika tarehe 29 Septemba, 2023 Jijini Dar es Salaam kwa dhumuni la kutangaza na kuibua mapishi ya vyakula vya asili ya Tanzania. Hatua hiyo inaenda sambamba na malengo ya UN-Tourism katika kukuza zao la utalii wa vyakula (Gastronomy Tourism) duniani. Aidha, Chuo kilishiriki Onesho la 8 la Kimataifa la Hospitality Expo tarehe 06 hadi 08 Novemba, 2023 Jijini Doha, Qatar na Kongamano la 5 la Africa Youth in Tourism Innovation Summit and Challenge Julai, 2023 ambapo kupitia maonesho haya watalaam wa Chuo walipata nafasi ya kubadilishana kubadilishana uzoefu na washiriki kutoka Nchi mbalimbali.

**187. Mheshimiwa Spika,** katika juhudi za kutanua wigo wa kutangaza na kutambulisha kazi za kitaaluma zinazotekelezwa na Chuo Kimataifa, mfumo wa kidijitali wa kukusanya na kuhifadhi machapisho (Institutional Repository System - IR)

umeanzishwa. Mfumo huo unawezesha watalaam kutoka Nchi mbalimbali kuchapisha maandiko na tafiti katika fani za utalii na ukarimu. Aidha, Mafanikio hayo ni mojawapo ya hatua za kimkakati katika kuvutia watalam zaidi kushirikiana na Chuo katika masuala ya kitaaluma na utafiti.

### 3.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale

**188. Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi, kutafiti na kuendeleza rasilimali za malikale. Utekelezaji wa jukumu hilo unazingatia Sera ya Malikale ya Mwaka 2008, Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281. Sekta hii inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale, Shirika la Makumbusho ya Taifa na Mfuko wa Mambo ya Kale.

#### 3.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

**189. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa maeneo ya Malikale yanalindwa kisheria na kuendelezwa kiutalii, Wizara imetangaza maeneo 11 ya malikale katika Gazeti la Serikali kupitia matangazo Namba 163 na Namba 166 ya tarehe 15 Machi, 2024 kuwa Urithi wa Taifa. Maeneo hayo yanahusiana na maendeleo ya jamii kabla ya ujio wa wakoloni, harakati za Tanganyika kupinga Ukoloni, harakati za Waasisi wa Taifa kupigania Uhuru wa Tanganyika; na mchango wa Tanzania katika kupigania ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika. Hatua hii imechangia ongezeko la maeneo ya Urithi wa Taifa kutoka 131 hadi 142.

**190. Mheshimiwa Spika,** maeneo yaliyotangazwa ni Gofu la Kale la Afya – Tabora; Minara 3 ya Kumbukumbu ya Kudai Uhuru wa Tanganyika; Jengo la Redio Tanzania Dar es Salaam - Idhaa ya Nje; Kituo cha Kumbukizi ya “Mtwa” Mkwawa Kalenga; Jengo la Kale lililotumika wakati wa Utawala wa Kijerumani na Handaki lililotumika na Jamiii ya Wachaga kujificha wakati wa Vita vya wenyewe kwa wenyewe (Mireshe) katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka; Nyumba ya Kumbukizi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere-Magomeni; Mapango ya Nang’oma

na Namaingo yaliyotumiwa na wenyeji kujificha na kupanga mikakati wakati wa Vita vya Majimaji na Mnara wa kumbukumbu wa mashujaa wa Vita ya Majimaji katika eneo la Nandete. Maeneo mengine ni iliyokuwa Kambi ya wapigania Uhuru wa Nchi ya Msumbiji kwa sasa Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga na Kambi ya Wapigania Uhuru wa Nchi za Kusini mwa Afrika katika eneo la Kongwa. Utangazaji wa maeneo hayo utaimarisha uhifadhi wake kisheria na kutumika kama zao jipya la utalii wa malikale.

**191. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wadau wengine imefanya tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo 27 ya malikale ya Urithi wa Taifa katika Mikoa ya Tanga (19), Tabora (3) na Pwani (5). Tathmini hiyo imelenga kuhuisha orodha ya maeneo ya Urithi wa Taifa na kuandaa Mpango wa kuyaboresha yaliyo katika hali mbaya na kuyakabidhi kwa wadau wenye uwezo na nia ya kuyatumia kwa maendeleo endelevu. Aidha, Wizara imebaini maeneo mapya 69 ya malikale yanayokidhi vigezo vya kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa katika Mikoa ya Morogoro 8, Rukwa 8, Songwe 6, Mbeya 9, Katavi 3, Dodoma 7, Kagera 7, Tabora 4, na Tanga 17. Taratibu za kuyatangaza kuwa urithi wa Taifa zinaendelea kufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333.

**192. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imeratibu na kufanya vikao 6 na semina 1 kwa lengo la kutatua migogoro ya uhifadhi na kujenga uelewa juu ya matumizi endelevu ya malikale. Vikao vilivyofanyika ni baina ya Wizara ya Maliasili na Utalii na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Kanisa Katoliki Jimbo la Mwanza na Wazee wa Mila na Desturi wa eneo la Kageye katika Wilaya ya Magu, Mwanza; Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kinondoni na Jamii zinazoishi karibu na Kituo cha Malikale Kunduchi, Dar es Salaam; Wakazi wanaoishi jirani na Eneo la Malikale Engaruka, Arusha na Amboni -Tanga; na kikao baina ya Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani kuhusu mgogoro wa Eneo la Malikale Chole, Mafia. Taarifa na majadiliano katika vikao hivyo yataisadia Serikali kutatua migogoro iliyopo katika maeneo hayo. Aidha, kikao

kimoja cha wadau 70 wa Malikale kimefanyika Wilayani Bagamoyo kwa lengo la kushirikisha wadau kuhakiki taarifa za uwepo wa rasilimalikale 298 zikijumuisha majengo ya kihistoria 148, makaburi 131, visima vya kale 4, minara 2 pamoja na maeneo 13 ya wazi yenye taarifa za kihistoria.

**193. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa maeneo ya malikale yanaendelea kukidhi vigezo vya Kimataifa, Wizara imeendelea kusimamia Miongozo, Sera na Taratibu za uhifadhi wa maeneo ya malikale likiwemo eneo la Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, lenye Hadhi ya Urithi wa Dunia ambapo Julai, 2023 lilipata hadhi ya UNESCO kwa kuingizwa katika Orodha za Watu na Hifadhi Hai (Man and Biosphere Reserve) inayojumuisha maeneo 748 yaliyomo katika Nchi 134 Duniani. Hatua hii imeongeza idadi ya maeneo ya Watu na Hifadhi Hai Nchini kutoka 5 hadi 6. Mafanikio hayo, yamechochea shughuli za utalii wa malikale kwa kuongeza idadi ya watalii wa Kimataifa katika eneo hilo, hususan kupitia utalii wa meli.

**194. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Mpango wa Urejeshwaji wa Malikale na Masalia ya Miili ya Binadamu iliyochukuliwa wakati wa Ukoloni. Katika kuhakikisha kuwa Mpango huo unatekelezwa ipasavyo, Kamati za Kitaifa zimeundwa kwa ajili ya kuratibu suala hilo. Kamati zilizoundwa ni Kamati ya Wataalam, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kamati ya Majadiliano. Katika hatua za awali, Serikali imeandaa utaratibu wa urejeshwaji wa masalia yaliyopo Nchini Ujerumani. Hatua hii ni utekelezaji wa makubaliano baina ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Frank-Walter Steinmeier, Rais wa Shirikisho la Ujerumani kuhusu kufanya majadiliano ya kurejesha au kunufaika na malikale zilizochukuliwa wakati wa ukoloni. Utekelezaji wa suala hili utafanikisha kurudisha Nchini mabaki ya miili ya binadamu na malikale zilizochukuliwa.

**195. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uhifadhi wa maeneo yaliyopo katika Orodha ya Urithi wa Dunia, Wizara imeshiriki Mkutano wa 45 wa Kamati ya Urithi wa Dunia uliofanyika Riyadh,

Saudi Arabia ambapo hali ya uhifadhi wa maeneo ya Hifadhi ya Serengeti, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Pori la Akiba Selous, Mji Mkongwe wa Zanzibar, Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ilijadiliwa. Aidha, Wizara ilishiriki Mkutano wa 23 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa UNESCO wa Mwaka 1972 uliofanyika Paris Ufaransa ambapo Ajenda mahsusi ya Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi kuhusu kulinda maeneo ya Urithi wa Dunia yanayoathirika na mabadiliko hayo, ilijadiliwa. Matokeo ya ushiriki wa Tanzania katika mikutano hiyo ni pamoja na Tanzania kufanikiwa kuishawishi Kamati ya Urithi wa Dunia (WHC) kuondoa maamuzi yake ya kuuweka Mji Mkongwe wa Zanzibar kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia uliopo hatarini kutoweka na kuweka utaratibu mzuri wa kufanya ufuatiliaji (Reactive Monitoring Mission) wa shughuli zinazotekelezwa katika maeneo ya Urithi wa Dunia yaliyojadiliwa katika Mkutano huo.

### 3.3.4.2 Shirika la Makumbusho ya Taifa – NMT

**196. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Makumbusho ya Taifa lina jukumu la kukusanya, kuhifadhi, kutafiti na kutoa elimu kwa umma kuhusu mikusanyo ya kisayansi na kiutamaduni yenye hadhi ya urithi wa Taifa. Aidha, Shirika linasimamia na kuendeleza vituo 7 vya Makumbusho ya Taifa na maeneo 96 ya Malikale yaliyopo sehemu mbalimbali Tanzania Bara.

**197. Mheshimiwa Spika,** Shirika limekamilisha ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi na utalii kwa kujenga vituo 2 vya taarifa na kumbukumbu. Vituo hivyo ni Mbuamaji - Dar es Salaam kitakachowekwa katika makumbusho ndogo na maonesho ya kudumu ili kutafsiri Historia ya miji ya kale ya Pwani ya Afrika Mashariki. Pia, Kituo cha Mikumbi - Lindi kitawekwa makumbusho ndogo na maonesho ya kudumu ili kutafsiri Historia ya Mkoa wa Lindi na Ukombozi Kusini mwa Bara la Afrika. Aidha, Kituo cha Tendaguru - Lindi kitakachotafsiri sayansi na historia ya mjusi mkubwa (Dinosaria) kipo katika hatua za ukamilishaji kwa kuweka sakafu, madirisha na kupaka rangi. Hatua hii, itafungua maeneo hayo kwa shughuli za utalii pamoja na kuimarisha uhifadhi. Aidha, Shirika limejenga jengo jipya lenye uwezo wa kuhifadhi magari 14 yenye historia ya Tanzania katika Kituo cha

Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni - Dar es Salaam. Magari hayo yatahifadhiwa kitaalam na kuandaliwa Onesho la kudumu la kidijitali litakalovutia watalii.

**198. Mheshimiwa Spika,** Shirika limefanya tathmini na kukarabati majenzi ya kale 6 pamoja na kuendesha programu ya ufasili wa majenzi hayo yaliyopo eneo la Kua katika Wilaya ya Mafia. Lengo ni kuboresha eneo hilo kwa ajili ya utalii pamoja na kutoa mafunzo ya uhifadhi kwa jamii zinazozunguka hifadhi hiyo. Aidha, ukarabati wa nyumba za asili 4 za jamii ya Wangoni umefanyika katika Makumbusho ya Majimaji - Songea. Pia, nyumba 3 za asili za jamii za Wakinga, Wamakua na Wamwera zimekarabatiwa katika Kijiji cha Makumbusho. Vilevile, ujenzi wa nyumba 1 ya asili ya jamii ya Wasambaa umefanyika katika Kijiji cha Makumbusho na kufanya jumla ya nyumba za asili kuwa 31.

**199. Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha watalii wa ndani na nje ya Nchi kutembelea Makumbusho, Shirika limeandaa maonesho 12 ya muda, likiwemo Onesho la Kimataifa la Historia ya Tanzania na India; Onesho linalojumuisha kazi za Ufundi na Sanaa za kitanzania na Nchi za Ghuba; Onesho la Michezo kwa Klabu ya Simba; Onesho la Miamba na Uchoraji; Onesho la Kujenga Uelewa wa kazi na sanaa zinazofanywa na wenye ulemavu wa ngozi (Albino) katika Uhifadhi na Utalii wa Malikale; na Onesho la Historia ya Miji ya Kale ya Swahili baina ya Oman na Tanzania. Aidha, uandaaji na uwekaji wa maonesho hayo umefanikisha kujenga uzalendo kwa wananchi; kutambua manufaa yatokanayo na shughuli za uhifadhi wa Malikale Nchini pamoja na kuleta watalii takriban 4,500; Hivyo, kuwezesha idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya Makumbusho na Malikale kuwa 226,135 katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024.

**200. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Shirika limeongeza ubunifu katika kuandaa maonesho kwa kutumia TEHAMA. Hatua hiyo imehusisha Kituo cha Kumbukizi ya Vita vya Majimaji - Songea na Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni - Dar es Salaam ambapo wageni wanaweza kuona maudhui ya maonesho mbalimbali kwa njia za kidijitali kupitia teknolojia ya Interractive Touch Kiosk na Augmented Reality. Maonesho

yanayofanyika kwa njia hiyo ni pamoja na Historia ya Vita vya Majimaji, Mchango wa Wanawake katika kupigania Uhuru wa Tanganyika na Uhifadhi wa Mila na Desturi za jamii ya Wamakonde.

**201. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeratibu na kufanya tafiti 5 ambazo ni Alama na Aina za Ulaji wa Nyama ili kutambua mtindo wa utafutaji chakula na aina ya mazingira waliyokuwa wanaishi binadamu wa kale. Utafiti huo ulifanyika katika Bonde la Laetoli kupitia Masalia ya mifupa kwa miaka milioni 2 iliyopita; Utafiti katika Usimamizi na Tafsiri ya Urithi wa Afrika; Utafiti kwa ajili ya Ujenzi wa Onesho la Historia ya Tanzania na Ujerumani uliofanyika katika Mikoa ya Lindi, Tabora, Ruvuma, Dodoma, Kilimanjaro na Iringa; Utafiti kwa ajili ya Makumbusho zijazo uliofanyika katika Wilaya za Tunduru, Mbinga, Songea, Madaba na Namtumbo; na Utafiti wa Wageni wa Kimataifa wanaotembelea Makumbusho ya Taifa kwa ajili ya kupata taarifa na takwimu zitakazosaidia kuboresha Mkakati wa Makumbusho wa kuvutia watalii.

**202. Mheshimiwa Spika,** Shirika limetoa machapisho 5 ambayo ni chapisho la ufukuzi na utambuzi wa masalia ya binadamu (Forensic exhumation and human remains identification); chapisho la changamoto za Masoko ya Makumbusho na Malikale Nchini; chapisho la biashara haramu ya Malikale Nchini Tanzania: 'Ripoti ya Uchunguzi'; chapisho la utafiti wa Soko la kimataifa kwa Makumbusho za Taifa Tanzania; na chapisho la matokeo ya uwepo wa mitazamo mingi juu ya malikale zinazoakisi biashara ya kale ya utumwa katika uhifadhi wa Mji Mkongwe wa Mikindani. Machapisho haya yatawezesha kuongeza wigo wa utafiti katika maeneo ya Malikale na kukuza soko la utalii wa Malikale.

**203. Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha wadau kuhifadhi historia na kuzitumia kuongeza fursa za ajira, Shirika limetoa ushauri kwa taasisi 5 na jamii 2 kuanzisha makumbusho binafsi. Taasisi hizo ni Hospitali ya Taifa ya Muhimbili iliyohamasishwa kuhifadhi historia ya afya na tiba Nchini; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzisha Makumbusho ya Chuo Kikuu; Shirika la Reli

Tanzania kuanzisha Makumbusho ya Historia ya Usafiri wa Reli; Wakala wa Ndege za Serikali kwa ajili ya uhifadhi wa ndege aina ya Foker iliyotumika wakati wa harakati za kupigania Ukombozi wa Bara la Afrika; na Taasisi binafsi ya Registered Trustees of Liberty Care Centres kuanzisha makumbusho inayotembea (mobile exhibition). Vilevile, jamii za Wamatengo kutoka Wilaya ya Mbinga, Ruvuma na Familia ya Mwami Theresa Ntare wa Kigoma zimehamasishwa kuanzisha Makumbusho kwa ajili ya kuhifadhi, kuendeleza, na kutangaza historia zao. Hatua hiyo itaongeza idadi ya makumbusho Nchini ambazo zitapelekea ongezeko la watalii wa ndani na nje ya Nchi katika maeneo ya vivutio vya malikale na makumbusho.

**204. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, jamii 4 za Wanyambo, Wamasai, Wandamba na Wanyakyusa zimekutana chini ya uratibu wa Makumbusho ya Taifa ambapo zimekubaliana kuendelea kuenzi na kutunza mila na desturi kupitia ujenzi wa nyumba za asili na kuandaa matamasha kama sehemu ya Utalii wa Utamaduni katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam. Halikadhalika, warsha za kitafiti 3 zimefanyika kwa jamii ili kujenga uelewa wa uhifadhi na matumizi endelevu ya malikale. Warsha hizo zilijumuisha machifu wapatao 43 kutoka jamii mbalimbali za kitanzania kwa lengo la kupata taarifa za mikusanyo ya mila inayohifadhiwa Ujerumani. Vilevile, semina 2 zimefanyika ili kutoa elimu ya uhifadhi kwa wakazi 35 wa Mji Mkongwe wa Mikindani, na semina 3 kwa wakazi 80 wa Vijiji vya Chole, Juani na Jibondo katika Wilaya ya Mafia.

**205. Mheshimiwa Spika,** katika nyanja za kimataifa, Shirika limeshiriki warsha 4, makongamano 2 na programu 2 za uhifadhi wa malikale, utafiti na uendelezaji wa urithi wa utamaduni. Warsha zilizofanyika ni pamoja na warsha ya kuhifadhi kumbukumbu za maeneo ya Malikale yaliyo katika hatari ya kutoweka iliyofanyika Nchini Kenya; warsha ya kulinda urithi wa Afrika iliyofanyika Nchini Marekani; warsha ya kuandaa Onesho la historia ya Tanzania na Ujerumani iliyofanyika Nchini Ujerumani; na warsha kuhusu mwelekeo wa makumbusho zijazo iliyofanyika Nchini India. Aidha, Shirika limeshiriki kongamano la Viongozi na Wataalam wa Malikale kujadili mradi wa pamoja

katika uhifadhi lililofanyika Nchini Canada; kongamano la wazi kuhusu urithi wa Afrika lililofanyika Nchini Uingereza; programu ya uhifadhi katika Makumbusho ya Metropolitan iliyofanyika Nchini Marekani na programu ya Utafiti katika nyaraka iliyofanyika Nchini Afrika Kusini.

**206. Mheshimiwa Spika,** katika kutoa elimu kwa umma na kusimamia matumizi endelevu ya malikale, Shirika limeratibu matamasha 5 ya kumbukumbu na utamaduni ambayo ni Tamasha la Majimaji, Tamasha la Wachaga, Tamasha la Wandamba, Tamasha la Hekaya za Wanyakyusa na Tamasha la kuenzi desturi ya Kimakonde. Pia, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa Shirika limeshiriki kuratibu tamasha la Kumbukizi ya Vita vya Majimaji NandeteKilwa. Halikadhalika, Shirika limeshiriki Onesho la Kimataifa la Biashara (Sabasaba), Nanenane Kitaifa, Karibu Utalii Kusini, Karibu Kili-Fair, Majimaji Serebuka na Swahili International Tourism Expo (S!TE).

**207. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Shirika limezindua Programu 2 ambazo ni Programu ya Museum Art Explosion (MAE) Plus na Programu ya Watoto wenye Mahitaji Maalum kwa kushirikiana na Ubalozi wa India. Aidha, vipindi 42 vya kutangaza huduma na mazao ya utalii wa malikale vimerushwa kupitia vituo 59 vya redio, vituo 65 vya televisheni,
Makala 17 kwenye Magazeti, Makala 36 katika mitandao ya kijamii na programu 10 za uhamasishaji zimefanyika katika Shule za Sekondari zilizopo Mkoa wa Arusha (3), Ruvuma (5) na Mtwara (2). Uendeshaji wa matamasha, programu na utangazaji wa mazao hayo ya utalii umeleta watalii wa ndani 1,000 kwa tamasha la Wachaga, Wandamba 200, Wanyakyusa 100, Mkole 300 na Majimaji 5,379. Vilevile, kupitia matamasha hayo jamii imepata elimu kuhusu uhifadhi wa urithi wa asili na uendelezaji wa malikale, kujenga uzalendo na kutambua fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo ya malikale.

**208. Mheshimiwa Spika,** Shirika pia limeboresha uhifadhi na ukusanyaji wa taarifa za mikusanyo kwa kuendelea kutumia mfumo wa teknolojia ya kidijitali ujulikanao kama Digital Record Archive and Management System – DRAMPS. Mfumo huu

umefanikisha usajili wa jumla ya mikusanyo 8,275, hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa matumizi ya utafiti na utoaji wa elimu kwa umma.

**209. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Mpango wa Miaka Kumi wa Kuenzi na Kusheherekea Urithi wa Mwl. Julius K. Nyerere wa Mwaka 2022 – 2032, Shirika liliandaa na kufanya programu maalum ya Mwl. Nyerere Marathon msimu wa pili iliyofanyika Butiama, Mara ambapo jumla ya wakimbiaji 500 walishiriki. Mpango huo unalenga kuendeleza uhifadhi na utalii unaohusiana na falsafa za Mwl. Julius Kambarage Nyerere. Sambamba na mbio za hiari za Mwl. Nyerere Marathon, matukio mengine yaliyofanyika ni pamoja na Usiku wa Mwl. Nyerere, zoezi la upandaji miti 101 katika msitu wa Mwitongo, kutembelea Makumbusho ya Mwl. Julius K. Nyerere, mchezo wa mpira wa miguu na bao.

**210. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Serikali imepitisha Muundo Mpya wa Utendaji kwa Shirika na Muundo wa Maendeleo ya Utumishi. Kupitia miundo hiyo, Shirika litakuwa na kurugenzi ya makumbusho na malikale itakayosimamia utekelezaji wa majukumu ya usimamizi na uendelezaji wa malikale na makumbusho Nchini yakiwemo uhifadhi, utafiti programu za maonesho na elimu. Pia, miundo hiyo imeanzisha kitengo kipya cha masoko na mahusiano ya umma ili kuimarisha utangazaji na uendelezaji malikale kwa ajili ya utalii. Halikadhalika, Shirika limewezesha watumishi 21 kuhudhuria mafunzo ndani na nje ya Nchi. Kati ya hao, watumishi 9 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 12 wanapata mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ili kuongeza ufanisi.

### 3.3.4.3 Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA

**211. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 kwa lengo la kuwezesha majukumu ya uhifadhi na utafiti wa malikale. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mfuko umewezesha uandaaji wa Mpango wa Urejeshwaji wa Malikale

na Masalia ya Miili ya Binadamu iliyochukuliwa wakati wa Ukoloni.
Vilevile, umewezesha kufanyika kwa tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo ya malikale 27 yaliyopo Tanga 19, Tabora 3 na Pwani 5. Zoezi hili limefanikisha upatikanaji wa taarifa za hali ya uhifadhi wa rasilimalikale katika maeneo hayo. Aidha, mfuko umewezesha utekelezaji wa Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi na Kusheherekea Urithi wa Mwl. Nyerere.

### 3.3.5 Utekelezaji wa Masuala Mtambuka

### (i) Kuimarisha Utendaji wa Wizara (Utawala na Rasilimaliwatu)

**212. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utendaji kazi, Wizara imekamilisha ujenzi wa jengo la ofisi awamu ya pili lenye vyumba 114 lililopo katika Mji wa Serikali Mtumba na kuwezesha Watumishi kuhamia katika jengo jipya mwishoni mwa Disemba 2023. Watumishi 218 wamehamia kwenye jengo jipya kati ya 315 waliopo Makao makuu. Nitumie fursa hii kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uratibu mzuri na uwezeshaji uliofanikisha jengo kukamilika na kuifanya Wizara ya Maliasili na Utalii kuwa Wizara ya kwanza kukamilisha ujenzi wa jengo awamu ya pili. Aidha, tayari Wizara imewasilisha maombi Ofisi ya Waziri Mkuu kupata ridhaa ya kuanza ujenzi wa jengo la ofisi awamu ya tatu litakalokuwa na nafasi zaidi ya ofisi kwa ajili ya watumishi pamoja na huduma muhimu kwa watumishi na Wizara kwa ujumla.

**213. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara imepokea watumishi 642 wa kada mbalimbali wakiwemo askari wa uhifadhi 488 ili kuimarisha uhifadhi, kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na biashara haramu ya nyara na mazao ya misitu na nyuki. Aidha, Wizara imewawezesha watumishi 401 kujiunga na mafunzo ya muda mrefu, watumishi 1,194 kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 912 kupata mafunzo ya jeshi la uhifadhi. Hivyo, kufanya jumla ya watumishi waliopata mafunzo kufikia 2,507. Mafunzo hayo yamekusudiwa kuwajengea uwezo watumishi kumudu majukumu yao kwa ufanisi zaidi, kupata sifa za kimuundo ili kuwawezesha kupata sifa za kupanda vyeo pamoja

na kuwaandaa watumishi wanaotarajia kustaafu kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali itakayowawezesha kumudu maisha baada ya kustaafu. Vilevile, watumishi wa kada mbalimbali 452 wamepandishwa vyeo.

**214. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kwa kuwahudumia watumishi waathirika waliojiweka wazi kwa kuwapa posho kwa ajili ya lishe bora na kutoa posho ya kuwahudumia watumishi wenye ulemavu. Pia, Wizara inaendelea kutoa vifaa kinga kwa watumishi wa Wizara na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutunza afya zao kupitia vipeperushi na vikao rasmi vya idara na Wizara. Aidha, Wizara imeendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi kwa kuweka mikakati mbalimbali na kuwahimiza watumishi kutoa huduma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu, maadili ya utumishi wa Umma, uwajibikaji pamoja na utekelezaji wa majukumu wakizingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

**215. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kutoa stahili za watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo. Aidha, katika kuimarisha afya za watumishi kwa njia ya michezo Wizara imeshiriki katika michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Mkoani Iringa Oktoba, 2023 ambapo ilifanikiwa kutwaa makombe 6 na medali 8 na pia Wizara ilishiriki katika michezo ya maadhimisho ya Mei Mosi iliyofanyika Kitaifa Aprili, 2024 jijini Arusha. Katika mashindano hayo Wizara ilifanikiwa kutwaa makombe 2 na medali 4.

**(ii) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

**216. Mheshimiwa Spika,** Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa kwenye masuala ya uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii, Wizara imeshiriki katika mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa ikiwemo SADC, EAC, IORA, UNESCO, CITES, UNFCCC na UNPFII. Ushiriki katika matukio hayo umeendelea kuitambulisha Tanzania katika medani ya utalii wa kimataifa, pamoja na kuimarisha

ushirikiano wa kimkakati kwa muktadha wa kukuza Sekta ya Utalii, Malikale na Maliasili.

**217. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Wizara imeendelea kutekeleza mikataba mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira, maliasili, malikale na utalii. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya TabiaNchi (UNFCCC); Mkataba wa UNESCO unaohusu Uhifadhi na Ulinzi wa Maeneo ya Urithi wa Dunia ya Asili na Utamaduni; Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka (CITES); Mkataba wa Kupambana na Hali ya Kuenea kwa Jangwa na Ukame (UNCCD); Mkataba wa Wanyamapori Wahamao (CMS); na Mkataba wa Uhifadhi wa Bioanuai (CBD). Kwa kutekeleza mikataba hiyo, Tanzania imeendelea kushirikiana na Nchi nyingine duniani katika uhifadhi wa maliasili, malikale na ulinzi wa urithi wa Dunia.

### 3.4 Miradi ya Maendeleo

**218. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ilitengewa **Shilingi 168,166,759,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara na Taasisi. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi 109,879,593,000** fedha za ndani; na **Shilingi 58,287,166,000** fedha za nje. Aidha, fedha za Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 59,415,166,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali chini ya Wizara na **Shilingi 108,751,593,000** za Miradi inayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, NCAA, TAWA na NCT). Hadi kufikia Aprili 2024, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 143,940,386,782.24** sawa na **asilimia 85.59** ya fedha zilizoidhinishwa kwa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 99,609,274,531.16** ni fedha za ndani na **Shilingi 44,331,112,251.08** ni fedha za nje. Aidha, Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

**Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth - REGROW)**

**219. Mheshimiwa Spika,** mradi wa REGROW unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya Hifadhi za Taifa Nyerere, Mikumi, Ruaha, Udzungwa na katika Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Kilombero. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mradi uliidhinishiwa jumla ya Shilingi 41,877,638,496. Hadi kufikia mwezi Aprili 2024, jumla ya Shilingi 37,061,710,068.96 zimepokelewa na kutumika kutekeleza kazi zifuatazo: Uboreshaji na ujenzi wa viwanja 4 vya ndege katika hifadhi za Taifa Mikumi 1, Nyerere 1, na Ruaha 2; ujenzi wa nyumba za watumishi 14 katika Hifadhi za Taifa za Ruaha 3, Nyerere 7 na Mikumi 4 zenye uwezo wa kuhudumia familia 48, ujenzi wa malango 3 ya kuingilia hifadhini; nyumba 32 za kufikia watalii, ujenzi wa Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania (Southern Tanzania Destination Marketing Center) na Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa.

**220. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia mradi imewezesha ujenzi wa malambo 5 kwa ajili ya maji ya mifugo unaoendelea katika vijiji vya Ikanutwa, Mabadaga, Mahango, Manienga na Itamboleo katika Wilaya ya Mbarali. Pia, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu ya Madibira Wilayani Mbarali na skimu ya umwagiliaji ya Kimani - Chimala na Makangarawe unaendelea.

**221. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara kupitia mradi wa REGROW imewezesha mafunzo kwa wakulima 161 kuhusu matumizi sahihi ya njia za kukabiliana na tembo kama vile matumizi ya uzio wa pilipili, mabomu ya pilipili, uzio wa nyuki na mishumaa yenye kutoa harufu inayowaudhi tembo. Aidha, wanufaika hao wameweza kutoa mafunzo kwa wakulima wenzao 180 na kufanya jumla ya wakulima 341 kunufaika na mbinu hizo hivyo kupunguza migogoro kati ya wanyamapori hao na binadamu. Vilevile, jumla ya vijana 281 (wanawake 41, wanaume 240) kutoka vijiji 40 vinavyopakana na maeneo ya hifadhi katika Wilaya za Chamwino, Iringa, Kilolo, Kilombero, Morogoro, Kilosa, Mvomero, Kisarawe na Rufiji wamewezeshwa kupata mafunzo ya Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) katika Kituo cha Mafunzo

ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Aidha, VGS 113 waliopata mafunzo hayo wameweza kushiriki kwenye matukio 87 ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu katika vijiji 12 vinavyopakana na Hifadhi za Taifa Mikumi, Nyerere, Ruaha na Udzungwa.

**222. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia mradi wa REGROW imetoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 761 (Wanawake 457, Wanaume 304) na kiasi cha Shilingi 2,882,670,260 zimetumika kufadhili wanafunzi hao katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Vilevile, Wizara kupitia mradi wa REGROW imewezesha utekelezaji wa miradi 150 ya kujikwamua kiuchumi kwa jamii katika Vijiji 15 vya awamu ya kwanza vilivyopo katika Wilaya za Chamwino - vikundi 9, Iringa 25, Kilolo - 9, Kilombero - 56, Kilosa - 15, Mvomero - 10 na Morogoro - 26. Mradi umetoa kiasi cha Shilingi 3,234,086,579.20 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi hiyo. Miradi hiyo imesaidia vikundi kuimarika kiuchumi na kuweza kujiendesha ili kuepusha utegemezi katika maliasili na kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Wizara kupitia mradi imeratibu upatikanaji wa vikundi vinavyojiendesha kwa mfumo wa Benki za Hifadhi za Jamii (Community Conservation Bank-COCOBA) katika vijiji 46 vya awamu ya pili ambapo jumla ya vikundi 602 vyenye wanachama 9,804 (wanawake 6,520 na wanaume 3,284) vimetambuliwa, kujengewa uwezo wa kujiendesha, kuanzisha miradi ya kujikwamua kiuchumi na kusimamia fedha. Vikundi hivyo, vitafanyiwa tathmini na kuongezewa fedha za mtaji wa kikundi na fedha za kutekeleza miradi watakayoiibua.

**223. Mheshimiwa Spika,** katika uhifadhi wa mazingira, Wizara kupitia mradi wa REGROW imewezesha jumla ya miche ya miti 90,000 kupandwa katika Wilaya za Mufindi (10,000), Mbarali (15,000), Makete (15,000), Wanging'ombe (20,000) na Mbeya (30,000). Miti iliyopandwa imekabidhiwa kwa Jumuiya za Watumia Maji - WUAs, Serikali za Vijiji na Wilaya ili kuhakikisha inakua kama ilivyotarajiwa. Pia, Wizara imewezesha kufukuliwa kwa mito iliyokuwa imepoteza mwelekeo (Mambi kilomita 15 na Kioga kilomita 6) katika Wilaya ya Mbarali. Hatua hiyo imeboresha mtiririko wa maji na kuimarisha shughuli za kilimo na

kupunguza siku za kukauka kwa mto kutoka 148 Mwaka 2018 hadi 126 Mwaka 2023. Vilevile, imesaidia kupunguza athari za mafuriko katika Kijiji cha Manienga ambapo zaidi ya kaya 100 zimeondokana na kero ya kuhama wakati wa msimu wa mvua.





Picha ya kwanza (kushoto) Utayarishaji wa mizinga, mradi wa ufugaji nyuki kikundi cha COCOBA Msufini-Udzungwa. Picha ya pili (kulia) ni mradi wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kikundi cha Upendo A, Kijiji cha Msolwa Station. Miradi hii ya vikundi vya COCOBA vinafadhiliwa kupitia REGROW.

**Mradi wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori (Combating Poaching and the Illegal Wildlife Trade in Tanzania)**

**224. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Kimataifa (Global Environmental Facility - GEF) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Programme - UNDP). Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, mradi uliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 2,916,531,100. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 2,383,156,284.12 zimepokelewa na kutumika kutekeleza kazi zifuatazo: kuwezesha maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili wa Mwaka 2023 – 2033; Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyampori za Jamii wa Mwaka 2023 - 2033; na Mpango wa Kutafuta Fedha wa Mwaka 2023 – 2033 kwa ajili ya kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili wa Mwaka 2023 – 2033; kuwezesha kufanyika kwa doria 7 katika kanda 6 za uratibu wa doria (TCGs). Doria hizo zimewezesha kukamatwa kwa vipande 52 vya meno ya tembo, vipande 222 vya nyamapori aina mbalimbali na watuhumiwa 68 ambao

wamechukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Katika kipindi husika kakakuona 1 na kasuku 43 hai, bunduki 19 zikijumuisha AK47 (3), Shotgun 5, Rifle 11 pamoja na magobore 31 na risasi 68 vimekamatwa. Aidha, mradi umewezesha kutungwa kwa Kanuni za Ufifilishaji wa makosa za Mwaka 2024 chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009; kufanya mapitio ya Mipango ya Ujumla ya Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za UMEMARUWA na WAGA na kuzijengea uwezo CBOs za Chamwino na WAGA.

**225. Mheshimiwa Spika,** mradi umewezesha ujenzi wa mfumo "Wildlife and Forest Crime Information System" kwa ajili ya kukusanya na kuchakata taarifa za ujangili na uhifadhi wa wanyamapori na misitu. Ujenzi wa mfumo umeendana sambamba na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya chumba maalum cha kuhifadhi takwimu na kutoa taarifa.

**226. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, mradi umewezesha ununuzi wa mizinga 300 na vifaa vya ufugaji nyuki vikiwemo tenki la kuhifadhi asali, brush ya nyuki, pamoja na vifaa vya kujikinga na nyuki wakati wa kurina wa asali kwa ajili ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori WAGA. Pamoja na kuongeza kipato kwa jamii kutokana na mauzo ya asali itakayozalishwa, mizinga hiyo itawezesha jamii kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu akiwemo tembo. Aidha, Mpango wa Ufuatiliaji wa Kijamii katika mfumo ikolojia wa Ruaha-Rungwa umeandaliwa ili kusaidia usimamizi madhubuti wa bioanuai; ununuzi wa vifaa vya doria na ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia katika Kanda za Kiikolojia za Kupambana na Ujangili (TCGs); na kuwezesha kampeni ya kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara katika mfumo ikolojia wa Ruaha– Rungwa. Kampeni hiyo ililenga kujenga mtazamo chanya katika uhifadhi.

**Mradi wa Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)**

**227. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Panda Miti Kibiashara ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Ufini (Finland). Kwa

Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mradi uliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 3,360,500,000 ambazo ni fedha za nje. Hadi Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 2,367,877,077 zimepokelewa na kutumika kutekeleza kazi zifuatazo: kuwezesha shughuli za ugani kwa wakulima wa miti 5,000 katika Vijiji 40 vilivyopo katika Wilaya za Mafinga, Makete na Njombe; kuwezesha uandaaji wa mipango ya kupambana na moto katika Vijiji 6 wilayani Kilolo na Mufindi ambapo wanavijiji 200 walishiriki. Vilevile, mradi umewezesha utunzaji wa mashamba 15 ya mbegu za miti yenye hekta 200 kwa kusafisha barabara za kudhibiti moto kusambaa katika maeneo ya mashamba ya miti, kupunguza miti, tafiti za magonjwa na uvunaji wa mbegu za miti kilo 98 zenye thamani ya Shilingi 245,000,000 kutoka katika mashamba 2 kati ya 15 yaliyoanzishwa na Mradi.

**228. Mheshimiwa Spika,** Mradi umewezesha uzalishaji wa miche ya miti 5,500,000 iliyopandwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 5,000 pamoja na uandaaji wa kitini cha mafunzo ya namna ya kukabiliana na moto katika mashamba ya miti. Kitini hicho kinatumika kufundishia wadau wa sekta ya misitu ambapo wanavijiji 350 kutoka katika maeneo ya mradi wamepewa elimu ya namna ya kuzuia na kupambana na moto katika mashamba ya miti. Sambamba na hilo, Mradi umeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia katika Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu – FWITC; pamoja na kuanzisha kitengo cha kutoa huduma ya ugani kwa wananchi ili kufikisha huduma kwa wananchi katika maeneo yao.

**Mradi wa Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain Development Programme – FORVAC)**

**229. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Ufini (Finland). Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kiasi cha Shilingi 3,899,920,000 ambazo ni fedha za nje, kiliidhinishwa kwa ajili ya Mradi. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya Shilingi 1,388,368,821 zimepokelewa na kutumika kutekeleza kazi zifuatazo: kutoa mafunzo ya jinsi ya kuandaa mpango wa biashara ya mbao (Timber business plan

development) kwa maafisa 16 na wananchi 153 wanaounda kamati za maliasili za Vijiji katika Wilaya za Namtumbo, Tunduru, Songea, Liwale, Ruangwa na Nachingwea; kununua na kugawa pikipiki 3 kwa Wilaya ya Nachingwea kwa ajili ya kusaidia usimamizi wa misitu iliyopo katika Wilaya hiyo; kujenga uwezo kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha na utunzaji wa kumbukumbu kwa wananchi 344 katika Vijiji 15 vya Wilaya za Liwale, Nachingwea, Namtumbo na Tunduru.

**230. Mheshimiwa Spika,** Mradi umewezesha kuunda vikundi vya kupambana na moto katika Vijiji 5 pamoja na kutoa mafunzo ya mbinu za kupambana na moto kwa wananchi 75; kutoa mafunzo kwa waendesha mashine 4 za kuchakata magogo (Sawmills); na mitambo 2 ya kukaushia mbao kwa kutumia nishati ya jua (Solar kilns) zilizopo katika Halmashauri za Wilaya ya Liwale, Ruangwa, Nachingwea na Songea.

**Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC)**

**231. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya. Mradi unatekelezwa katika Mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mradi uliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 2,948,860,404 ikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Shilingi 1,130,000,000 zimepokelewa na kutumika kutekeleza kazi zifuatazo: kununua pikipiki 20 kwa maafisa ufugaji nyuki katika Wilaya 20 za mradi ambazo zinatumika kuwezesha maafisa hao kutoa huduma za ugani kwa wananchi; kununua mashine na vifaa vya maabara kwa ajili ya Maabara ya Utafiti wa Ufugaji Nyuki iliyopo Njiro Mkoani Arusha.

**232. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, Mradi umeanzisha na kuwezesha Kikundi Kazi cha Utafiti kwa ajili ya utekelezaji wa maeneo ya kipaumbele ya tafiti zilizobainishwa katika Mpango Mkuu wa Kwanza wa Utafiti (NABERM - I); kuwezesha uandaaji wa rajamu (branding) ya asali

inayozalishwa Tanzania kutoka katika uoto wa mimea mbalimbali. Vilevile, mradi umewezesha TAFORI kukamilisha utafiti wa aina na viambata vya asali katika mikoa ya Singida, Tabora, Katavi, Kigoma, Kagera, Geita, Tanga, Njombe, Iringa, Ruvuma na Pwani. Matokeo ya kazi hii yatachangia kukuza soko la asali la ndani na nje ya Nchi.

**233. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Mradi umewezesha mafunzo ya utengenezaji wa mizinga ya kisasa kwa mafundi 58 katika Mikoa ya Kigoma 19, Katavi 15, Singida 14 na Shinyanga 10. Mafunzo hayo yalitolewa kwa washiriki kutoka Chuo cha MATI-Mubondo, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora, Kijiji cha Nyuki, Afri-Life, TanziFarm, Salah and Sons Carpentry, na Abdullah Kahsim Bakar Carpentry. Mafunzo haya yamechochea upatikanaji wa mizinga kwa wafugaji nyuki katika Wilaya zote za utekelezaji wa Mradi. Vilevile, Mradi umewezesha kikao kimoja baina ya sekta binafsi na Serikali kwa lengo la kujadili changamoto zinazokabili sekta ya ufugaji nyuki (Private Public Dialogue – PPD) kilichokutanisha wadau 22 kutoka katika taasisi mbalimbali; na kuwezesha vikao viwili vya kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa vyama vya wafugaji nyuki ambapo kupitia vikao hivyo hati ya makubaliano (MoU) baina ya vyama hivyo ilisainiwa.

**234. Mheshimiwa Spika,** mradi umewezesha utambuzi na uanzishaji wa hifadhi za nyuki za vijiji 21 katika Mikoa ya Kigoma (Vijiji 8), Katavi (Vijiji 3), Tabora (Vijiji 2) na Singida (Vijiji 8); na kuwezesha Makampuni 6 ya kitanzania ya uuzaji wa mazao ya nyuki kushiriki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (International Trade Fair) Nchini Ujerumani. Aidha, ushiriki huo umewezesha kufungua masoko mapya ya asali katika Nchi za Umoja wa Ulaya (EU) ikiwemo Poland. Vilevile, Mradi umewezesha wazalishaji wa asali 21 kushiriki katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba); pamoja na kuwezesha semina za kujenga uwezo wa vikundi 19 vya VICOBA na SACCOS za wanawake wanaojishughulisha na ufugaji na biashara ya mazao ya nyuki katika Wilaya za Nsimbo, Kibondo, Kakonko, Kasulu na Uvinza.

**235. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, mradi umewajengea uwezo viongozi 19 wa vyama vya ushirika wa wafugaji nyuki; kufanya mikutano katika Vijiji 297 ya kuhamasisha jamii kutenga na kuhifadhi maeneo ya misitu kwa ajili ya kufugia nyuki; kuunganisha wafanyabiashara 6 wanaouza asali nje ya Nchi na wafugaji nyuki 296 na vikundi 29 vilivyo katika maeneo ya Mradi. Vilevile, Mradi umewezesha mafunzo kwa makampuni 30 kuhusu utayari wa usafirishaji wa mazao ya nyuki nje ya Nchi; kuwezesha Kiwanda cha Central Park Bees kilichopo Jijini Dodoma kupata cheti cha ubora (HACCP) kinachotolewa na Shirika la Viwango vya Ubora Tanzania (TBS) na kuongeza idadi ya viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki vyenye cheti cha HACCP kufikia 3. Cheti hiki pamoja na uwepo wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mabaki ya Kemikali kwenye Asali kinawezesha wafanyabiashara kuuza asali katika masoko mbalimbali nje ya Nchi.

## 4.0 MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**236. Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 - 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025; Sera na Sheria mbalimbali; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026; Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge, maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

**237. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:

(i) Kuendelea kutangaza utalii ndani na nje ya Nchi ikiwa ni mwendelezo wa programu maalum ya Tanzania – the

Royal Tour, filamu ya Amazing Tanzania pamoja na mikakati mingine mikubwa kupitia matangazo katika ligi kuu za michezo mashuhuri duniani, matangazo kwenye ndege; misafara ya utangazaji utalii; matamasha makubwa ya kimataifa na mitandao mbalimbali ya Kimataifa na Vyombo vya Habari;

(ii) Kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo maeneo ya malikale pamoja na utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli, michezo, tiba na utamaduni;

(iii) Kuboresha miundombinu katika maeneo ya hifadhi ili kuwezesha shughuli za utalii kufanyika;

(iv) Kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale;

(v) Kuendelea kutekeleza mipango na mikakati ya uhifadhi pamoja na kuongeza kiwango cha uzalishaji na thamani ya mazao ya misitu na nyuki;

(vi) Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, ufugaji nyuki na malikale;

(vii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu mbalimbali na kufanya tafiti za kimkakati na kutoa huduma za ushauri zinazohusu masuala ya uhifadhi endelevu wa wanyamapori, misitu na nyuki, malikale na uendelezaji utalii; na

(viii) Kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato na kuimarisha usimamizi na mifumo ya ukusanyaji wa mapato na fedha za kigeni.

### 4.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**238. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 968,842,018,480** kutoka kwenye Idara na Taasisi zake.

### 4.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**239. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 348,125,419,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 250,884,083,000** zitagharamia Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 97,241,336,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Mishahara **Shilingi 125,366,391,000** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 125,517,692,000**. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 18,074,661,000** fedha za ndani na **Shilingi 79,166,675,000** fedha za nje.

**240. Mheshimiwa Spika**, fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 250,884,083,000 zinajumuisha **Shilingi 30,695,909,972** kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 220,188,173,028** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, **Shilingi 8,463,022,058** ni Mishahara na **Shilingi 22,232,887,914** ni Matumizi Mengineyo. Fedha za taasisi zinajumuisha **Shilingi 116,903,368,942** za Mishahara na **Shilingi 103,284,804,086** za Matumizi Mengineyo.

### 4.3 Kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake

#### 4.3.1 Sekta ya Wanyamapori

##### 4.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

**241. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya Shilingi 45,144,308,496.73 zimetengwa kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa helikopta 2 kupitia taasisi za uhifadhi za TANAPA 1 na NCAA 1; na uchimbaji wa mabwawa 30 kupitia TANAPA 12, TAWA 2 na TWPF 16. Mabwawa hayo yatachimbwa katika Hifadhi za Taifa

Serengeti 5, Ruaha 1, Tarangire 2, Katavi 2, Nyerere 2, Saadani 2, Mikumi 2 na Mkomazi 3; na Mapori ya Akiba Rungwa 2, Kizigo 2, Selous-Liwale 2, Muhesi 2, Maswa 2 na Msanjesi 1.

**242. Mheshimiwa Spika,** kazi nyingine zitakazofanyika ni ujenzi wa vizimba 50 katika maeneo yenye changamoto kubwa ya mamba na viboko. Maeneo hayo yanajumuisha Halmashauri za Wilaya za Bunda 3, Buchosa 3, Busega 3, Rufiji 3, Sengerema 3, Uvinza 4, Morogoro Vijijini 3, Tandahimba 3, Kibiti 3, Nsimbo 3, Nanyumbu 2, Nkasi 2, Tanganyika 4 Newala 2, Ukerewe 3, Muleba 2, Musoma Vijijini 2 na Ulanga 2.



Kizimba kilichojengwa kwa ajili ya kuzuia mamba kutowadhuru wananchi Ziwa Rukwa katika Halmashauri ya Songwe.

**243. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau itawajengea uwezo Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 200 kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo ya mbinu rafiki za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi 320 watakaotumika kama Wakufunzi katika Wilaya 16 zenye changamaoto ya wanyamapori wakali na waharibifu. Katika hatua nyingine, Wizara itanunua pikipiki 39 zikiwemo 22 kwa ajili ya Maafisa Wanyamapori wa Wilaya na 17 za Askari wa Jeshi la Uhifadhi ili kuwawezesha kufika kwenye maeneo ya matukio kwa wakati.

**244. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara kupitia taasisi zake itaongeza ajira ya Askari 850 (TANAPA 454, NCAA 51 na TAWA 345) ili kuimarisha shughuli za uhifadhi na doria za kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu;

kuendelea na ujenzi wa vituo 10 vya askari katika Wilaya za Mbarali, Kalambo, Kilwa, Bariadi, Manyoni, Kilosa, Rufiji, Morogoro Vijijini, Babati na Monduli.

**245. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kutumia teknolojia katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kununua ndege zisizo na rubani (drones) 16 kupitia TANAPA 13, TAWA 2 na NCAA 1; na mikanda maalum ya mawasiliano 100 (GPS Satellite Collars) kupitia TWPF kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori hao. Mikanda hiyo itafungwa kwa tembo viongozi katika maeneo ya Kusini (Nachingwea, Liwale, Namtumbo, Mchinga na Tunduru); Kaskazini (Mwanga, Same na Korogwe); na Kanda ya Ziwa (Biharamulo, Karagwe, Meatu, Bariadi, Itilima na Busega). Vilevile, Wizara itanunua na kusambaza vifaa vya kudhibiti tembo yakiwemo mabomu baridi 35,000. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kufanya tafiti za kimkakati kwa ajili ya kugundua mbinu mpya za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

**246. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022 - 2026 kwa kukamilisha hatua za utambuzi wa mipaka na kuweka mabango kwenye shoroba 20 kati ya 61 zilizoainishwa ili kuwawezesha wananchi kuyatambua na kutoyatumia maeneo hayo kwa shughuli za kibinadamu zisizoendana na uhifadhi. Vilevile, Wizara imepanga kuondoa mimea vamizi katika eneo la hekta 11,509 katika Kasoko (Crater) ya Ngorongoro na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

**247. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wanaoathirika na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi.

**248. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori, Wizara kupitia Taasisi zake za Uhifadhi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa Mwaka 2023-2033 na Mkakati wa Kusimamia na Kuhifadhi tembo Nchini wa

Mwaka 2023-2033. Utekelezaji wa Mikakati hiyo utawezesha udhibiti wa matukio ya Ujangili na biashara Haramu ya Nyara Nchini.

**249. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushirikishwaji wa jamii kwenye shughuli za Uhifadhi, Wizara ya Maliasili na Utalii itaandaa Mpango wa Kanda wa Kusimamia Rasilimali za Maliasili (Resource Zone Management Plan) kwa ajili ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Ifinga (Madaba) na kufanya tathmini ya maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Ndonda (Nachingwea) na Ikungi kwa ajili ya uanzishwaji wa Jumuiya hizo.

**250. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara itafanya ukaguzi wa ranchi, mashamba na bustani za wanyamapori na vituo vya kuuzia nyamapori. Vilevile, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya wanyamapori, Sura ya 283 na Kanuni za Wanyamapori (Uwindaji wa Kitalii, Uwekezaji Mahiri katika Maeneo Maalum ya Wanyamapori, Usimamizi wa Maeneo ya Ufugaji wa Wanyamapori, Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Biashara ya Nyara) kwa lengo la kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori.

#### 4.3.1.2 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

**251. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika linatarajia kupokea wageni takriban 1,950,000 sawa na ongezeko la asilimia 6.5 Shirika litaendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato kwa kufunga smart gates 30 katika hifadhi 8 za Arusha, Mkomazi, Ziwa Manyara, Mikumi, Nyerere, Ruaha, Kilimanjaro na Serengeti, kuboresha huduma za vibali vya kielektroniki (e-Permits) kwa kufungamanisha na mifumo mingine ya Serikali katika malango 5 ya Naabi, Ndabaka, Seronera, Kogatende na Ikoma.

**252. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ulinzi wa wanyamapori hasa walio hatarini kutoweka, Shirika litaendelea kuimarisha na kuboresha mawasiliano ya kidijitali kwa kuweka

mfumo wa kufuatilia faru (LoRa WAN rhino tracking system) katika Hifadhi za Taifa Serengeti na Mkomazi na kuboresha matumizi ya mfumo wa redio kidijitali kwa ajili ya vituo vya askari ndani ya Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro na Katavi.

**253. Mheshimiwa Spika,** Shirika litaendelea kuimarisha miundombinu ya uhifadhi na utalii kwa kufungua barabara mpya zenye urefu wa kilomita 448 katika Hifadhi za Taifa 6; na kukarabati kilomita 3,988 za barabara katika Hifadhi za Taifa 15; kukarabati kilomita 686.8 za njia za watembea kwa miguu katika Hifadhi za Taifa Kisiwa cha Saanane, Milima ya Mahale, Gombe, Kilimanjaro, Arusha na Milima ya Udzungwa; na ujenzi wa malango 5 katika Hifadhi za Taifa Nyerere 2, Mikumi 1, Mkomazi 1 na Saadani 1. Kazi nyingine zitakazofanyika ni ujenzi wa viwanja vidogo 4 vya ndege katika Hifadhi za Taifa Ruaha 2, Mikumi 1 na Nyerere 1; kukarabati viwanja 6 vidogo vya ndege katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ruaha na Tarangire; Shirika litaendelea kuimarisha usalama katika viwanja vya ndege kwa kununua gari maalum 1 katika Hifadhi ya Taifa Mikumi. Vilevile, Shirika litakarabati hosteli 5, mabanda 61 na nyumba za kupumzikia wageni 5 katika Hifadhi 16 za Taifa; na kujenga vituo 3 vya kutolea taarifa katika Hifadhi za Taifa za Serengeti, Ruaha na Mikumi.

**254. Mheshimiwa Spika**, Shirika litaanzisha na kuendeleza mazao mapya ya utalii katika Hifadhi za Taifa ikiwa ni pamoja na kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa uwanja wa mchezo wa Golf katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na kukamilisha ujenzi wa daraja la juu (Canopy walkway) katika Hifadhi ya Taifa ya Milima Udzungwa. Aidha, Shirika litaanzisha utalii wa faru kwa kujenga uzio wa faru (Rhino sanctuaries) katika Hifadhi za Taifa za Mikumi na Burigi-Chato na kuendeleza utalii wa faru katika maeneo mengine ya hifadhi. Katika hatua nyingine, Shirika litawezesha uanzishwaji wa shughuli za utalii (tourism activities) zinazolenga kuongeza siku za watalii kukaa katika Hifadhi za Taifa. Shughuli hizo ni pamoja na utalii wa nyota (star gazing na sleep out under the stars) Hifadhi ya Taifa za Serengeti na Ziwa Manyara, (hot spa) katika Hifadhi za Taifa za Ruaha na Ziwa Manyara. Sambamba na hilo, Shirika litaendelea kutangaza vivutio vya

utalii ndani na nje ya Nchi kwa kurusha matangazo ya moja kwa moja (live streaming) na kutumia njia nyingine ili kuvutia watalii kutembelea Hifadhi za Taifa.

**255. Mheshimiwa Spika,** Shirika litajenga jumla ya nyumba 17 za watumishi katika Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro, Mahale na Ruaha na miundombinu ya usambazaji wa maji katika Hifadhi za Taifa za Mikumi, Serengeti na Tarangire.

#### 4.3.1.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA

**256. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za wanyamapori nje ya maeneo ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka itaendelea kudhibiti ujangili na biashara haramu ya nyara kwa kuimarisha doria ambapo jumla ya doria 15,620 zitafanyika. Sambamba na hilo, Mamlaka, itanunua boti maalum – air boat 1 kwa Pori la Akiba Kilombero na trekta 1 kwa ajili ya Pori la Akiba Luganzo Tongwe ili kuimarisha doria katika maeneo yenye ardhioevu. Mamlaka itanunua magari 5 ya doria ambayo yatagawanywa katika Kanda 5 na kujenga madaraja 4 katika Mapori ya Akiba Kizigo 1, Wami-Mbiki 1, na Selous 2 pamoja na vituo 3 vya askari katika Mapori ya Akiba Moyowosi, Kizigo na Kilombero.

**257. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya utalii Mamlaka itajenga Kilomita 315 na kufanya ukarabati Kilomita 73.5 za barabara katika Mapori ya Akiba ya Wami-Mbiki, Luganzo Tongwe, Rungwa, Pande na Mpanga Kipengere na Hifadhi ya wanyamapori ya Makuyuni. Mamlaka pia itajenga lango la watalii katika Hifadhi ya Makuyuni na vituo viwili vya kukusanya mapato katika Pori Tengefu Lake Natron. Vilevile, Mamlaka itashiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kutangaza utalii wa picha na uwindaji wa kitalii pamoja na fursa za uwekezaji.

**258. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga ofisi 2 za Kanda za Uhifadhi za Magharibi na Ziwa; na ofisi 2 za Mapori ya Akiba Wami-Mbiki na Kilombero; kukarabati nyumba 5

za watumishi kanda ya Uhifadhi Kaskazini na Ghala Kuu la Nyara. Vilevile, Mamlaka itanunua basi la watumishi kwa ajili ya Mapori ya Akiba Ikorongo na Grumeti. Sambamba na hilo, Mamlaka itawezesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 268 katika fani mbalimbali na mafunzo ya ukakamavu na utayari kwa watumishi 200 pamoja na kuwezesha watumishi kushiriki katika mashindano ya SHIMUTA.

**259. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea na utatuzi wa migogoro ya mipaka, Mamlaka itaboresha na kutengeneza barabara ya kuzunguka mpaka (mkuza) wenye urefu wa kilomita 243 katika Pori la Akiba Maswa. Aidha, Mamlaka itaandaa Mipango ya Jumla ya Usimamizi (GMP) kwa ajili ya Mapori ya Akiba Rukwa, Lukwika-Lumesule, Msanjesi na Liparamba.

#### 4.3.1.4 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro – NCAA

**260. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori kwa kufanya doria 312 na ununuzi wa magari 6 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika eneo la hifadhi. Sambamba na hilo, Mamlaka itajenga vituo 4 vya askari katika maeneo ya Kakesio, Ndorobo, Mbulumbulu na Acacia. Vilevile, Mamlaka itasafisha mpaka wenye kilomita 200 ili kuzuia moto kichaa na kuweka vigingi 50 kuepusha migogoro ya mipaka. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea kuimarisha ushirikiano na jamii zinazopakana na Hifadhi kwa kufanya mikutano 120 ya ujirani mwema kwa lengo la kutoa elimu ya uhifadhi na kutatua migogoro.

**261. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kuboresha nyanda za malisho kwa kudhibiti mimea vamizi kupitia moto mpango, kung’oa, kufyeka na kuwezesha utafiti. Zoezi hili litafanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekta 3,500 lililoathirika zaidi katika maeneo ya Ndutu na Kasoko ya Ngorongoro (Ngorongoro Crater). Katika hatua nyingine, Mamlaka itaotesha miche ya miti 164,231 ambayo itapandwa katika maeneo yaliyoathirika na ukataji miti na mingine itagawiwa kwa wadau

mbalimbali wanaopakana na eneo la hifadhi na maeneo mengine.

**262. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea kusimamia zoezi la wananchi wanaohama kwa hiari kutoka ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwenda Msomera, Kitwai, Saunyi na maeneo mengine waliyochagua. Zoezi hilo litaenda sambamba na programu ya utoaji elimu, uhamasishaji wa wananchi kuhama kwa hiari, uandikishaji na uthaminishaji wa maendelezo katika Vijiji 25 ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, Mamlaka itaendelea kulipa stahiki ya fidia na motisha kwa wananchi watakaojiandikisha kuhama ndani ya eneo la hifadhi kwa hiari. Sambamba na hili Mamlaka itaendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba 2,500 katika Vijiji vya Msomera, Kitwai na Saunyi kwa ajili ya wananchi watakaohama kwa hiari kuelekea katika maeneo hayo na kutoa chakula kwa kipindi cha miezi 18 kwa kaya zote zilizohamia katika maeneo hayo.

**263. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu ya utalii, Mamlaka itajenga barabara yenye urefu wa kilomita 29.5 kutoka lango la Loduare hadi Malanja kwa kiwango cha tabaka gumu na kufungua barabara ya Endulen-Eyasi yenye urefu wa kilomita 21 kwa kiwango cha Changarawe. Vilevile, Mamlaka itafanya ukarabati wa mtandao wa barabara wenye kilomita 421 na ukarabati wa viwanja vidogo vya ndege vya Ngorongoro na Ndutu. Sambamba na hilo, katika kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya wageni na askari, Mamlaka itajenga miundombinu ya maji na kusimika pampu 2 za maji katika visima vya eneo la Olduvai na Ndutu na kukarabati miundombinu ya maji katika eneo lote la hifadhi. Kwa upande mwingine, Mamlaka itafanya matengenezo ya njia ya umeme kutoka Loduare mpaka ofisi za Makao Makuu ya zamani Ngorongoro.

**264. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kujitangaza na kushiriki katika matukio na maonesho mbalimbali ya utalii na uhifadhi ndani na nje ya Nchi ili kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea hifadhi pamoja na kuvutia wawekezaji wenye

tija watakaojenga miundombinu ya huduma za malazi ambazo zitaongeza idadi ya vitanda ndani ya Hifadhi. Sambamba na hili, Mamlaka itaendelea kuboresha na kutumia njia za kidijitali ikiwemo Ngorongoro live streaming kutangaza mubashara vivutio na matukio mbalimbali kutoka hifadhini.

**265. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea kuongeza thamani ya vivutio vya malikale kwa kujenga Makumbusho ya Hifadhi ya Jiolojia, sehemu ya kupumzikia wageni na kuboresha njia za miguu (walking trails). Aidha, Mamlaka itaandaa utaratibu wa kufukua nyayo za Zamadamu zilizopo katika kituo cha Laetoli na kujengea jengo maalum kwa lengo la uhifadhi endelevu na utalii. Vilevile, katika kuongeza thamani ya Makumbusho ya Bonde la Olduvai, Mamlaka itaweka vifaa maalum vitakavyotumika kumuongoza mtalii (self audio guide) kwa lugha 9 tofauti.

**266. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi itakamilisha ujenzi wa ofisi za Makao Makuu katika eneo la Kamyn Karatu na kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwawezesha kupata mafunzo ya muda mfupi watumishi 250 na mafunzo ya muda mrefu watumishi 25.

### 4.3.1.5 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI

**267. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Taasisi itaendelea kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi na utalii endelevu. Maeneo ya kipaumbele katika tafiti zitakazofanyika ni pamoja na mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori, matumizi ya teknolojia katika uhifadhi, afya ya mifumo ikolojia, nyuki na mazao yake, mahusiano ya viumbe na ikolojia zao, uhifadhi wa bioanuai na urejeshwaji wa baadhi ya wanyamapori katika mifumo ikolojia mbalimbali. Aidha, Taasisi itafanya zoezi la kuidadi wanyamapori kwenye mifumo ikolojia yote Nchini na kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam na kusambaza matokeo ya tafiti kwa watumiaji.

**268. Mheshimiwa Spika,** TAWIRI itaendelea Kujenga uwezo wa kutoa huduma ikiwa ni pamoja na kukarabati majengo 2 katika kituo cha utafiti wa wanyamapori Serengeti na kuboresha vitendea kazi. Aidha, TAWIRI itaendelea kuwapa watumishi stahiki zao, kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao, kupandisha madaraja watumishi 49 wanaostahili, ajira mpya 82, watumishi 12 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na Watumishi 48 watapata mafunzo ya muda mfupi, kutoa elimu na kuhamasisha kujikinga na magonjwa ya VVU/UKIMWI, magonjwa yasiyoambukiza, kushiriki michezo na semina za ujasiriamali kwa watumishi wote. Vilevile, TAWIRI itaanza kutumia mfumo wa TEHAMA/Teknolojia unaohusu tafiti za wanyamapori ambao umeunganishwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) utaowezesha usajili na upatikanaji wa vibali vya utafiti kidijitali.

#### 4.3.1.6 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka – CAWM

**269. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka, kitaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo kwa kudahili wanafunzi wapatao 1,000 katika fani za Usimamizi wa Wanyamapori na Utalii. Aidha, Chuo kitakamilisha mitaala 13 ya kozi za Usimamizi wa Mazingira na Taka (Environmental and Waste Management), Uwindaji wa Kitalii (Proficiency Course in Professional Hunting), Usimamizi wa Utalii (Tourism Management) na Ushirikishwaji wa Jamii katika Usimamizi wa Maliasili (Community Based Natural Resources Management). Kozi hizi zitatolewa katika ngazi mbalimbali kuanzia cheti cha msingi hadi shahada ya uzamili.

**270. Mheshimiwa Spika**, Chuo kitaendelea kufanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji wa mafunzo na kutoa mchango katika utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazokabili Sekta za Wanyamapori na Utalii. Aidha, Chuo kitaendelea kutekeleza jukumu la kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani kwa wadau mbalimbali wakiwemo Serikali na Taasisi zake pamoja na sekta binafsi.

**271. Mheshimiwa Spika**, ili kuweka mazingira rafiki ya kufanyia kazi kwa watumishi na ya kujifunzia kwa wanafunzi, katika Mwaka ujao wa Fedha Chuo kimepanga kujenga na kuiboresha miundombinu ikiwemo ujenzi wa ukumbi wa mikutano, ukarabati wa hosteli 4, madarasa 4, nyumba 4 za watumishi na kilomita 0.4 ya barabara za ndani za Chuo kwa kutumia vitofali vya sakafu (paving blocks) katika kampasi ya MWEKA. Aidha, Chuo kitanunua na kufunga vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kununua lori 1 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Chuo kitaimarisha maeneo yake ya mafunzo kwa vitendo kwa kujenga vyoo vya kisasa (Arash, Loliondo), hanga/bweni (Kwakuchinja), kuweka mipaka na kukamilisha taratibu za kupata hati miliki (Kihesa Kilolo na Nyumba ya Mungu).

**272. Mheshimiwa Spika**, ili kuwajengea watumishi uwezo wa kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija, Chuo kitawawezesha watumishi 17 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na 100 ya muda mfupi. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa stahiki za watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu ili kuongeza ufanisi.

**4.3.1.7 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC)**

**273. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii–Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo kwa wanafunzi 515, kati yao 253 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu ya kozi ya Utalii na Uongozaji watalii na 262 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, kituo kitaendelea kutangaza mafunzo yatolewayo kwa wadau kupitia maonesho/maadhimisho mbalimbali.

**274. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyingine, kituo kitakamilisha ujenzi wa bweni 1; madarasa 2; ukarabati wa bweni 1 la wanafunzi wa kike na jengo la Utawala; na kununua vifaa mbalimbali vya malazi na mafunzo ikiwemo vitanda (double deckers) 100, magodoro 200, madawati 200 na mahema 14.

**275. Mheshimiwa Spika,** Kituo kitawezesha watumishi 2 kupata mafunzo ya muda mfupi hapa Nchini. Vilevile, watumishi 2 wataendelea na masomo ya muda mrefu ambapo mmoja ataendelea na ufadhili wa masomo ya Shahahada ya Uzamili katika usimamizi wa Utalii wa Kimataifa (Masters of Science International Tourism Management) Nchini Indonesia na mwingine ataendelea na Stashahada (Diploma) ya uhifadhi wanyamapori katika Chuo cha Wanyamapori MWEKA.

#### 4.3.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi – PWTI

**276. Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Taasisi ya Taalum ya Wanyamapori Pasiansi itadahili wanafunzi 800 wa kozi ndefu katika fani za Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji Watalii na usalama kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali; na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 200. Katika hatua nyingine, Taasisi itaanzisha mtaala katika ngazi ya Stashahada katika Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji Watalii na kuanza kutumika Mwaka wa Masomo 2024/2025. Taasisi itawezesha watumishi 3 kuendelea na masomo katika Shahada ya Uzamili na Uzamivu na watumishi 8 katika masomo ya muda mfupi.

**277. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mazingira ya utoaji mafunzo na kujifunza, Taasisi imepanga kutekeleza yafuatayo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025: kuimarisha kitengo cha TEHAMA na kujenga ghala la kisasa la kutunzia silaha za mafunzo; kukamilisha ujenzi wa maktaba; kukarabati mabweni na madarasa ya wanafunzi; kukarabati mifumo ya maji na umeme na kujenga bwalo la chakula litakaloweza kutumiwa na wanafunzi 500 katika kambi ya mafunzo ya Fort Ikoma. Sambamba na hilo, taasisi itaendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa uzio wa ukuta kipande chenye urefu wa mita 100 ili kuimarisha ulinzi na usalama katika Kampasi ya Pasiansi Jijini Mwanza.

### 4.3.1.9 Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania – TWPF

**278. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mfuko utaendelea kuwezesha: utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu mbalimbali za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu; kulipa kifuta jasho na machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu; kuwezesha Kikosi kazi cha Taifa cha Kudhibiti Ujangili; utatuzi wa migogoro kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa; upandishaji hadhi maeneo yaliyohifadhiwa; na kujenga uwezo katika usimamizi wa rasilimali za wanyamapori. Aidha, Mfuko utawezesha ujenzi wa Zahanati 1 katika Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga.

### 4.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

### 4.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

**279. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara itaandaa Mkakati na Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma za Ugani wa Misitu; Mkakati wa Mazao Yasiyo Timbao; Mwongozo wa Kitaifa wa Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Mashamba ya Miti; Mwongozo wa Kitaifa wa Barabara za Msituni; Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Makundi ya Nyuki Wasiodunga; Mwongozo wa Kitaifa wa Misitu Mjini; Mwongozo wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkakati wa Kilimo Msitu; Mwongozo wa Kitaifa wa Utalii wa Nyuki; Mwongozo wa Kitaifa wa Kushirikisha Vikundi vya Wakulima na Wazalishaji wa Mazao ya Misitu; na Kuandaa Sheria Ndogo ya mfano kwa ajili ya usimamizi wa hifadhi za misitu ya Serikali za Mitaa. Kwa upande mwingine, Wizara itafanya mapitio ya Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii; na Mwongozo wa Uvunaji Endelevu katika Misitu ya Asili. Aidha, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Misitu, Sura ya 323 na Sheria ya Ufugaji Nyuki, Sura ya 224. Vilevile, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Miongozo mbalimbali inayohusu Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki.

**280. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa jamii inaendelea kushiriki kwenye uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali

za misitu na nyuki, Wizara itaanza utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Ufugaji Nyuki; kuandaa mikutano 2 ya wadau wa misitu na nyuki; kutoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa vikundi 6 vya wafugaji nyuki wanawake pamoja na kuanzisha manzuki 6 za mfano katika Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo ya uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki kwa wadau wa kisekta kwenye kanda 7 za TFS. Vilevile, Wizara itaratibu vikao 4 vya Kamati Kuu ya Maandalizi ya Mkutano Mkuu wa 50 wa Wafugaji Nyuki Duniani (Apimondia) na kufanya Mikutano ya kujenga uelewa kwa wadau kuhusu Mkutano huo. Wizara pia itaratibu vikao 4 vya Kamati ya Ushauri wa Misitu - NAFAC, vikao 3 vya Kamati ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki – NABAC; vikao 4 vya Kamati ya Uendeshaji ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa; na kuanzisha Baraza la Wataalam wa Misitu.

**281. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazao yatokanayo na misitu na nyuki, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya viwanda vya misitu na nyuki, uzalishaji wa mkaa mbadala, vituo vya kukusanyia mazao ya nyuki na miradi inayosimamiwa na Idara; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii wa Mwaka 2021 - 2031 kwenye misitu ya hifadhi 10 ya Taifa na Halmashauri; kushiriki mikutano na warsha za kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Apimondia, Vikao vya Mashirikiano katika Sekta ya Misitu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, na Kamati ya Misitu ya Dunia (COFO); na kuratibu ushiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Siku ya Kitaifa ya Upandaji Miti na Siku ya Misitu na Nyuki Duniani.

#### 4.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

**282. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala utaimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kupandisha hadhi misitu 4 ya hifadhi kuwa hifadhi za misitu ya mazingira asilia; kutangaza kisheria hifadhi za misitu 40 na hifadhi 4 za nyuki; kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi 29 za Misitu yenye ukubwa wa hekta 1,215,883 na kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa Misitu 40 ya Hifadhi. Aidha,

Wakala utaendesha jumla ya doria 4,576 katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wakala utaimarisha mipaka ya misitu 153 kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 429.27; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,641.3; kuweka vigingi 881 na mabango 286; kuchimba mitaro 180 inayoonesha uelekeo wa mipaka ya Hifadhi za Misitu na Hifadhi za Nyuki.

**283. Mheshimiwa Spika**, Wakala utajenga vituo 17 vya ulinzi wa misitu ili kuimarisha uhifadhi katika misitu, ujenzi wa Ofisi ya Wakala - Makao Makuu Dodoma. Aidha, Wakala utaweka mifumo maalum ya mawasiliano katika Hifadhi 4 za Misitu ya Asili na shamba 1 la miti, minara 2 mipya ya kubaini matukio ya moto na kusimamia mingine 18 na kununua ndege nyuki (drones) 2. Aidha, Wakala utasafisha njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 5,067; na kutoa elimu ya kupambana na kuzuia moto kwa jamii katika Vijiji 169 vilivyopo katika Kanda 7 za Wakala za usimamizi misitu na nyuki.

**284. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaimarisha miundombinu ya utalii katika Hifadhi za Misitu zenye vivutio vya utalii ikolojia kwa kujenga kilomita 21.7 za njia za watalii, barabara mpya zenye urefu wa kilomita 156 kwa kiwango cha changarawe za kuwezesha kufika kwenye hifadhi, nyumba ndogo 13 za kulala watalii na kambi 25 za watalii. Aidha, Wakala utakarabati kilomita 394.9 za njia za watalii, kilomita 2,290 za barabara katika hifadhi, madaraja 36, kalvati 44 na mabanda 5 ya kupumzika watalii. Vilevile, Wakala utaimarisha vituo vya utalii wa malikale kwa kujenga kambi 2 za watalii na kukarabati barabara yenye urefu wa mita 100, majengo 2 ya ofisi katika vituo vya Michoro ya Miambani Kolo - Kondoa, Mji Mkongwe - Bagamoyo, Tembe la Kwihara - Tabora, Magofu ya Tongoni - Tanga na Kaole - Bagamoyo.

**285. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza kampeni ya Tanzania ya Kijani na kukidhi mahitaji makubwa ya malighafi ya mazao ya misitu Nchini, Wakala utaongeza uzalishaji wa mbegu za miti kwa kuanzisha vyanzo 9 vya kuzalisha mbegu za miti; kuzalisha tani 26.3 za mbegu za miti jamiii mbalimbali na miche ya miti milioni 34.4. Aidha, Wakala utaendeleza mashamba ya

Miti 24 kwa kupanda miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 7,655; kurudishia miti iliyokufa kwenye eneo la hekta 2,244; kupalilia eneo lenye hekta 32,386; kupogolea hekta 10,789; na kupunguzia miti kwenye hekta 4,727. Vilevile, Wakala utarejesha uoto katika maeneo ya misitu ya mikoko iliyoharibika kwa kupanda miche ya mikoko katika eneo la hekta 24.

**286. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendeleza mashamba 3 ya ufugaji nyuki na manzuki 82 na kuzalisha tani 43.5 za asali; tani 2.9 za nta na kilo 121 za chavua; kusimamia viwanda 3 vya nyuki; kutoa elimu kwa wafugaji nyuki 580; na kutengeneza mizinga ya nyuki 1,000.

**287. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaboresha mazingira ya kazi kwa kununua magari 25, pikipiki 38, boti 3, lori 1, mtambo 1, kujenga ofisi 15 na nyumba 3 za watumishi. Vilevile, Wakala utaendelea kutoa elimu kwa jamii pamoja na kushiriki katika maonesho mbalimbali. Sambamba na hilo, ili kuongeza weledi na kuboresha utendaji kazi Wakala utaendelea na programu za kuendeleza watumishi wake ambapo watumishi 95 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu, watumishi 310 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi katika nyanja mbalimbali na watumishi 255 watapatiwa mafunzo ya Jeshi la Uhifadhi.

#### 4.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

**288. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, TAFORI itaendelea kufanya tathmini ya rasilimali za misitu kwa ajili ya kuongeza tija katika viwanda vya mazao ya misitu kwenye mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Mashariki na Kusini; kukamilisha tathmini ya mchango wa Sekta ya Misitu kwenye Pato la Taifa (GDP) kwa kutumia njia ya "green accounting". Kazi nyingine zitakuwa kuendeleza tafiti za idadi ya miti, hali ya masoko, na mchango wa aina 3 za miti ya asili yenye fursa kubwa kibiashara; kufanya tafiti kwa kutumia teknolojia bora ya kuzalisha nishati mbadala; na kufanya utafiti wa kuangalia jinsi wadudu wachavushao wanavyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. TAFORI pia, itafanya tathmini ya ukuaji wa miti aina ya mianzi kwenye Mikoa ya Kanda ya Mashariki, Kusini-Mashariki na

Nyanda za Juu Kusini; kufanya tathmini ya miti dawa na matumizi yake kwa ajili ya kuboresha maisha na uhifadhi wa misitu katika eneo la Milima ya Tao la Mashariki; kufanya utafiti wa faida na hasara ya biashara ya utomvu unaozalishwa kutoka kwenye miti katika Mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Ziwa; na kuchunguza athari za mizunguko ya uvunaji wa spishi za misindano na mikaratusi kwenye uzalishaji na ubora wa mbao.

**289. Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, TAFORI itaendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kuwezesha watumishi 28 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 17 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, TAFORI itajenga jengo la Kituo cha Utafiti cha Tabora na kukamilisha ukarabati wa jengo la Kituo cha Utafiti cha Malya. Pia, Taasisi kwa kushirikiana na wadau wa nje na ndani ya Nchi itaandaa Kongamano la 3 la Kimataifa la Sayansi linalotegemewa kukutanisha takriban wadau 500 wa ndani na nje ya Nchi. Mada kuu katika Kongamano hilo ni "Urejeshaji wa Mandhari ya Misitu kwa Maendeleo Endelevu ili Kukabiliana na Mabadiliko ya TabiaNchi (Restoring Forest Landscapes for Sustainable Development and Climate Change Mitigation)". Kongamano hili linatarajiwa kufanyika tarehe 11-13 Disemba, 2024, Jijini Arusha.

#### 4.3.2.4 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora – BTI

**290. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitadahili wanafunzi 420 wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada, kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam juu ya masuala mbalimbali katika mnyororo wa thamani. Aidha, Chuo kitakamilisha ujenzi wa kumbi 2 za mihadhara (Lecture theatre) na kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana. Chuo kitakarabati bweni 1 na nyumba 2 za watumishi. Vilevile, Chuo kitawezesha mtumishi 1 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 3 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi 6 watawezeshwa kuhudhuria mikutano ya mwaka ya kitaaluma. Katika kuongeza mapato ya ndani, Chuo kitanunua mashine 1 kwa ajili ya karakana ya mbao.

#### 4.3.2.5 Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI

**291. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 500 katika teknolojia ya viwanda vya misitu (Astashahada ya awali 200, Astashahada 150 na Stashahada 150). Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam katika matumizi endelevu ya mazao ya misitu na nishati mbadala kwa wananchi. Kwa upande mwingine, Chuo kitashirikiana na wadau mbalimbali katika kutoa mafunzo na kuandika maandiko ya Miradi ya maendeleo kwa Chuo na wananchi.

**292. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kinatarajia kuendelea na maboresho ya miundombinu ikiwa ni pamoja na hosteli, madarasa, karakana ya mbao, mashine ya kukaushia mbao, mashine ya kutibu mbao, ununuzi wa vifaa vya maabara ya kupimia ubora wa mbao na vifaa vingine vya kufundishia. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi, kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na kuongeza wafanyakazi wenye ujuzi.

#### 4.3.2.6 Chuo cha Misitu, Olmotonyi - FTI

**293. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo cha Misitu - Olmotonyi kitadahili wanafunzi 930 wa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Katika kuimarisha ufanisi wa kazi, Chuo kitawezesha watumishi 4 kupata mafunzo ya muda mrefu na 6 kupata mafunzo ya muda mfupi na kushiriki katika michezo mbalimbali. Vilevile, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi ya misitu na uhifadhi wa maliasili kwa washiriki 200. Pia, Chuo kitatoa huduma za ugani kwa shule 10 za msingi na sekondari katika Wilaya ya Arumeru na Jiji la Arusha.

**294. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha na kuboresha mazingira ya mafunzo, Chuo kitaotesha miche ya miti 200,000 na miche ya miti ya matunda na maua 200,000. Aidha, Chuo kitapanda miche ya miti 100,000 katika shamba la miti la chuo na miche 100,000 ya matunda na maua katika maeneo ya

Chuo. Aidha, Chuo kitagawa miche ya miti 50,000 na kuuza miche ya miti 50,000 na 100,000 ya matunda na maua. Vilevile, Chuo kitachakata magogo yenye mita za ujazo 1,400 na kuuza mazao yatakayotokana na uchakataji huo. Sambamba na hilo, Chuo kitakarabati mabweni 4, ukumbi 1 wa mihadhara, madarasa 3 na kununua samani mbalimbali za ofisi.

#### 4.3.2.7 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

**295. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mfuko utaendelea kuwezesha na kugharamia miradi 201 inayoendelea na miradi mipya 124 ya uanzishwaji wa vitalu vya miti, upandaji miti, ufugaji nyuki na miradi ya nishati safi ya kupikia hususan biogas kupitia utoaji ruzuku. Aidha, ruzuku itatolewa kwa watu binafsi; vikundi vya kijamii vikiwemo vikundi vya vijana na wanawake; mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs); Asasi za kiraia (CSOs); taasisi za dini (FBOs); taasisi za mafunzo na taasisi za utafiti; na taasisi za Serikali zikiwemo shule za msingi na sekondari, idara, mashirika na Wakala wa Serikali, na Mamlaka mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, Mfuko utaendelea kuwezesha ujenzi wa jengo la mihadhara katika Chuo cha BTI, mafunzo ya shahada ya uzamili na uzamivu katika fani ambazo hazina wataalamu katika sekta ya misitu ambazo ni magonjwa ya mimea (Plant Pathology) na uzalishaji wa mimea kwa kutumia teknolojia za kisasa (Tree Breeding) na kuiwezesha TAFORI kufanya tafiti 5 za kimkakati zenye manufaa katika uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki.

**296. Mheshimiwa Spika**, Mfuko utaandaa Mkakati wa Muda Mrefu wa Kutafuta Fedha kutoka kwa wadau mbalimbali (Strategic Financial Plan) kwa kushirikiana na Mfuko wa FUNDESNAP kutoka Nchi ya Bolivia Amerika ya Kusini. Aidha, Mfuko utaendelea kutoa tuzo na ufadhili wa masomo kwa wanafunzi watakaofanya vizuri katika mafunzo ya Astashahada, Stashahada na Shahada ya kwanza katika fani za misitu, ufugaji nyuki na teknolojia ya viwanda vya misitu. Vilevile, Mfuko utaendelea kugharamia vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC); Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki

(NABAC); Kamati Endeshi ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa - EWP na vikao vya Kikundi kazi cha Misitu chini ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC).

**297. Mheshimiwa Spika**, Mfuko utaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kununua magari 2 na kuanza ujenzi wa ofisi katika Jiji la Dodoma. Aidha, Mfuko utaandaa utaratibu wa kutekeleza muundo wa Mfuko ulioidhinishwa Mwezi Aprili, 2024 kwa kufanya tathmini ya mahitaji ya rasilimaliwatu ili kubaini idadi ya watumishi wanaohitajika katika kutekeleza majukumu ya Mfuko, kuandaa muundo wa maendeleo ya kiutumishi (scheme of service), kuandaa muundo wa mishahara (salary strucure), kuandaa maelezo ya kazi (job list and job descripition) na kuandaa Mpango wa Kurithishana madaraka (succession plan). Vilevile, katika kuwajengea uwezo watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Mfuko utagharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 16 na mafunzo ya muda mrefu (Shahada ya Uzamili) kwa mtumishi 1.

### 4.3.3 Sekta ya Utalii

#### 4.3.3.1 Idara ya Utalii

**298. Mheshimiwa *Spika***, kwa kuzingatia malengo yaliyopo ya kukuza na kuendeleza Sekta ya Utalii Nchini, Wizara kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 itatekeleza yafuatayo: kufanya mapitio ya Sheria ya Utalii, Sura ya 65, Kanuni na Miongozo ya Biashara za Utalii Nchini; kufanya ukaguzi, uhakiki na utambuzi wa Wakala wa Biashara za Utalii Nchini; kufanya tathmini ya hali ya utoaji wa leseni za Wakala wa Biashara za Utalii Nchini; na ufuatiliaji wa uendelezaji wa mazao ya utalii Nchini. Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni kuratibu na kuandaa vikao 4 vya Kamati ya Kitaalam ya Ushauri ya Utalii; kuandaa Kanuni, Miongozo ya kufanya uhakiki na kupanga huduma za malazi na chakula katika Madaraja ya Ubora wa Nyota; na kufuatilia utekelezaji wa Vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sambamba na hayo, Wizara itaendelea kuandaa Orodha ya Huduma za Malazi zinazopaswa kukusanya Tozo ya Kitanda Siku (Bed Night Levy) na kutangazwa katika Gazeti la

Serikali pamoja na kufanya tathmini ya uhakiki wa usajili wa wageni wanaolala katika huduma mbalimbali za malazi Nchini. Lengo ni kufahamu uwezo wa kuhudumia watalii katika huduma za malazi hususan kupata idadi ya vyumba na vitanda vilivyopo Nchini.

**299. Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi Nchini katika Madaraja ya Ubora wa Nyota kwenye Mikoa ya Mbeya, Kilimanjaro na Mwanza pamoja na kufanya tathmini ya ubora wa huduma katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Aidha, Wizara itafanya mikutano 4 ya wadau kuwajengea uelewa kuhusu Sheria ya Utalii, Kanuni na Miongozo mbalimbali. Vilevile, katika kupunguza mianya ya upotevu wa mapato yatokanayo na Sekta ya Utalii, Wizara itajenga Mfumo wa "Tanzania Online Safari Booking System".

**300. Mheshimiwa Spika,** Wizara itafanya mikutano 3 ya Wadau wa Utalii kuhusu uendelezaji wa mazao ya utalii ya kimkakati ya Fukwe, Meli, Mikutano na Matukio; kufanya mapitio ya Mpango Kamambe wa Kusimamia Utalii wa Mwaka 2002 (Tourism Master Plan); kuandaa Programu ya Kitaifa ya Uendelezaji Utalii – NTDP; na kukamilisha Mwongozo wa Pamoja wa Kuendeleza Utalii. Shughuli nyingine zitakazofanyika ni: kushiriki katika matamasha, misafara ya utalii, matukio na maonesho ya Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kukuza utalii; kufanya mkutano 1 wa Jukwaa la Uwekezaji la Utalii (Tanzania Tourism Investment Forum) na mikutano 2 ya Majadiliano na Wadau wa Sekta - PPD kuhusu masuala ya usimamizi na uendelezaji utalii; na kuendelea kushiriki katika matukio ya ushirikiano ya Kikanda na Kimataifa inayohusu masuala mbalimbali ya Sekta ya Utalii.

**301. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa mazingira ya biashara ya utalii nchini yanaimarika kuendana na matokeo chanya ya filamu ya Tanzania - the Royal Tour, Wizara imefanya vikao vingi na wadau wa Sekta mbalimbali na imechukua juhudi za makusudi na za kimageuzi kufanya maboresho kama ifuatavyo:

Mosi, imeendelea kutekeleza maelekezo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Kitaifa wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) katika Sekta za Utalii na Misitu;

Pili, imechukua pia juhudi mahsusi za kuboresha Kanuni na Sheria ikiwemo Kanuni za Tozo za Utalii za Mwaka 2015 na maboresho yake ya Mwaka 2017 pamoja na Kanuni za Usajili na Ulipaji wa Leseni za Wakala wa Biashara za utalii za Mwaka 2015 na maboresho yake ya Mwaka 2017.

**302. Mheshimiwa Spika,** maeneo mahsusi yatakayoboreshwa na utekelezaji wake kuanzia Julai, 2024 na mengine kuanzia Disemba kama tutakavyoainisha baadaye katika kanuni ni pamoja na kuhuisha muda wa kulipa Ada ya Leseni ya Biashara za utalii na kuwa katika kipindi cha miezi 12 kuanzia siku ya mwisho ambayo wakala wa biashara za utalii amelipia leseni yake badala ya utaratibu wa sasa hata kama mtu amekata leseni Novemba zote zinafikia ukomo Disemba, kupunguza Ada ya Leseni ya Biashara za utalii kwa wakala wa kupandisha watalii mlimani (mountain climbing), kufuta tozo kwa waongoza watalii wenye leseni hai kila wanapoingia hifadhini, wadau kulipa Ada ya Leseni ya Biashara za utalii kwa kutumia shilingi ya Tanzania badala ya Dola za Marekani pamoja na kuongeza muda wa Leseni ya Biashara za utalii kwa Waongoza watalii ambapo kwa sasa itadumu kwa kipindi cha miaka mitatu badala ya mwaka mmoja wa sasa.

**303. Mheshimiwa Spika,** tunatambua umuhimu wa sekta ya utalii katika kuchangia Pato la Taifa hivyo, pamoja na maboresho haya, maboresho mengine yanayohusu maboresho ya kodi mbalimbali katika sekta ya utalii yataainishwa kwenye hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali itakapowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

### 4.3.3.2 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB

**304. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kutekeleza jukumu la kutangaza na kuhamasisha utalii ndani na nje ya Nchi kwa

kushirikiana na wadau mbalimbali. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kutangaza utalii kupitia Ligi mbalimbali na mashindano ya michezo yenye wafuatiliaji wengi zaidi Duniani, kutumia watu mashuhuri na wenye ushawishi, Mabalozi wa hiari wa utalii, vyombo vya habari vya Kimataifa vyenye ushawishi pamoja na mitandao ya kimataifa ya utalii kama vile TripAdvisor na Expedia Group.

**305. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada nyingine, Bodi ya Utalii Tanzania itashirikiana na wadau mbalimbali katika kutangaza utalii kupitia misafara ya utangazaji utalii (Road Shows) katika masoko yetu ya utalii hususan Nchi za Ghuba, Scandinavia, China, India, Brazil, Urusi na Poland; ziara maalum za mafunzo za utalii (Familiarization Trips) kwa wakala wakubwa wa utalii, waandishi wa habari wa kimataifa na watu mashuhuri wenye ushawishi kutoka Nchi ambazo ni masoko yetu ya utalii; pamoja na ushiriki katika Maonesho na Matukio mbalimbali ya utangazaji utalii ndani na nje ya Nchi. Aidha, Bodi itaandaa Onesho la 8 la Swahili International Tourism Expo - S!TE 2024 ambalo hushirikisha waoneshaji na wanunuzi wa Kimataifa wa bidhaa za utalii. Maonesho haya ni jukwaa muhimu la kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji zilizopo.

**306. Mheshimiwa Spika,** Bodi itaendelea kuandaa filamu na makala zenye viwango vya Kimataifa kwa lengo la kuitangaza Tanzania katika Soko la Utalii Kimataifa. Aidha, Bodi itaendelea kutangaza mazao ya utalii ikiwemo utalii wa meli, fukwe, mikutano na matukio, michezo, uwindaji wa kitalii, utamaduni, malikale, ikolojia, miamba, kilimo, matibabu, nyuki na vyakula kwa kushirikiana na Wadau. Bodi pia itaendelea kutangaza vivutio vya utalii kwa kushirikiana na mashirika ya ndege ya kimataifa yakiwemo Qatar Airways, Emirates, Ethiopian Airlines, na Turkish Airlines.

**307. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kushirikiana na ofisi za Balozi za Tanzania katika Nchi mbalimbali kwa lengo la kuvutia uwekezaji kwenye utalii na kuimarisha utangazaji utalii katika masoko ya msingi, kimkakati na yale yanayochipukia katika Bara la Amerika, Ulaya, Asia, Australia,

Mashariki ya Kati na Afrika. Juhudi hizo zitaenda sambamba na kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika masuala ya utangazaji utalii Kwa upande mwingine, Bodi itaendelea kuratibu na kusimamia Programu na Kampeni Maalum kwa muktadha wa kujenga hamasa ya utalii kwa makundi mbalimbali ya kijamii.

**308. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa kufanya mapitio ya miundo ya maendeleo ya utumishi, mpango wa motisha na maboresho ya mishahara. Sambamba na hilo, Bodi itawajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo.

### 4.3.3.3 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

**309. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kitadahili wanafunzi 1,500 katika ngazi ya Astashahada 1,100 na Stashahada 400. Aidha, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa utalii. Vilevile, Chuo kitakamilisha ujenzi wa Jengo la Mafunzo kwa Kampasi ya Arusha na kufanya ukarabati wa miundombinu ya Jengo la Mafunzo katika Kampasi ya Bustani, Jijini Dar es Salaam.

**310. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kitaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kufanya huduma mkoba (Outreach programs) za uhamasishaji, kushiriki maonesho pamoja na kuandaa vipindi vya televisheni na redio kwa ajili ya kunadi Programu za Mafunzo kwa Wanafunzi wa Shule za Sekondari na Wadau wa Utalii. Hatua hiyo inalenga kuongeza udahili zaidi wa wanafunzi na kuboresha utoaji huduma za utalii na ukarimu Nchini.

**311. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kitaandaa Kongamano la 3 la Kimataifa (The 3rd Linking Industry with Academia in the Tourism and Hospitality in Developing Countries (LIATH-DC) linalokutanisha Wadau na Wanataaluma katika masuala ya Utalii na Ukarimu. Kongamano hili linaandaliwa kwa

kushirikiana na Chuo Kikuu cha Teknolojia cha Tshwane cha Afrika Kusini pamoja na Chuo cha Kenya Utalii College na linatarajiwa kufanyika Mwezi Novemba 2024.

**312. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kitaendelea na utekelezaji wa Mpango wa mafunzo kwa Watumishi 30 kuwezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya Nchi ambapo watumishi 4 watapata mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Uzamili (Masters) na Uzamivu (PhD) na watumishi 26 watawezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi. Utoaji wa mafunzo hayo utajikita zaidi katika fani za ukarimu, utalii na uratibu wa matukio.

### 4.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale

#### 4.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

**313. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara itatangaza maeneo 15 ya malikale katika Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa; kuendelea na utatuzi wa migogoro ya mipaka katika maeneo 4 ya malikale na kuhuisha taarifa za maeneo 21 yaliyotangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa katika Mikoa ya Dodoma, Singida na Lindi. Aidha, Wizara itafanya warsha 3 za Wadau wa Malikale kuhusu usimamizi na uendelezaji wa maeneo yenye malikale Nchini. Vilevile, Wizara itaandaa Mwongozo na Taratibu za kutwaa na kuhamisha umiliki wa rasilimali za malikale kutoka kwa wamiliki kwenda kwa Wadau wenye uwezo na nia ya kuyaendeleza kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uhifadhi. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kufanya vikao 2 vya Wadau katika Mikoa 2 kwa ajili ya kuidhinisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malikale ya Mwaka 2008; kushiriki katika maonesho na matamasha ya kitaifa na kimataifa; na mikutano ya kikanda na kimataifa.

#### 4.3.4.2 Shirika la Makumbusho ya Taifa - NMT

**314. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika litaimarisha kazi za uhifadhi na usimamizi wa malikale Nchini kwa

kuhamasisha uwekezaji kwenye malikale na vituo vya makumbusho, kusimamia ukarabati wa majenzi ya kale 15 yaliyopo katika maeneo ya Mafia (Pwani) na Kigamboni (Dar es Salaam) pamoja na kutumia mifumo ya kidijitali kuhifadhi kumbukumbu za maeneo ya malikale Nchini. Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika shughuli za uhifadhi ikiwemo usajili wa mikusanyo. Vilevile, Shirika litafungua maonesho mapya 2 ya kudumu ya kidijitali katika vituo vya Makumbusho, Nyumba ya Utamaduni (Dar es Salaam) na Kituo cha Tendaguru (Lindi). Katika hatua nyingine, Shirika litajenga nyumba 2 za asili kwa jamii ya Wachaga 1 na Wafipa 1 katika Kijiji cha Makumbusho na kuanza mpango wa uboreshaji wa jukwaa la sanaa (theatre) katika Kituo cha Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni ili kuwezesha jukwaa hilo kuhudumia watu 600 kwa wakati mmoja.

**315. Mheshimiwa Spika,** Shirika litaendelea kushirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuhamasisha uhifadhi na uendelezaji malikale Nchini. Aidha, Shirika litafanya tafiti 5 za masuala ya urithi wa utamaduni na kutoa vibali vya utafiti katika maeneo ya malikale. Vilevile, Shirika litaendelea kuhamasisha jamii kuanzisha makumbusho binafsi, kutangaza vivutio vya urithi wa kiutamaduni kidijitali na kufanya programu za uhamasishaji utalii wa ndani kwa kuendesha kampeni ya makumbusho inayotembea (mobile exhibition), maonesho, matamasha, matukio na warsha zenye kujenga uelewa kuhusiana na utalii wa malikale. Katika hatua nyingine, Shirika litatekeleza Mpango wa uanzishwaji wa Makumbusho ya Marais, Dodoma. Aidha, Shirika litaendesha programu za kutekeleza Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi, Kutangaza na Kuhifadhi Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

#### 4.3.4.3 Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA

**316. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mfuko utawezesha uandaaji wa Mipango ya Usimamizi wa Maeneo 2 ya Malikale ya Mji wa Kihistoria wa Bagamoyo na Magofu ya Kaole; uwekaji wa vioneshwa katika Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa cha Tendaguru, Lindi; na kutambua maeneo 27 ya

malikale ili yaweze kutangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa. Aidha, Mfuko utaratibu utekelezaji wa Mpango wa Urejeshwaji wa malikale za Tanzania zilizopo nje ya Nchi; kuratibu shughuli za uhifadhi wa malikale katika maeneo 25 Nchini; kufanya vikao 2 vya wadau kujadili uhifadhi na ufukuaji wa Nyayo za Laetoli; kuandaa Kanuni za utafiti wa malikale pamoja na uanzishwaji wa Makumbusho Binafsi Nchini; kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwl. Nyerere; na mafunzo kwa vitendo ya uhifadhi wa maeneo na majengo ya kihistoria.

### 4.4 Miradi ya Maendeleo

**317. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 97,241,336,000** kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,074,661,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 79,166,675,000** ni fedha za nje. Fedha za maendeleo **Shilingi 97,241,336,000** zinajumuisha **Shilingi 52,845,774,134** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara; na **Shilingi 44,395,561,866** za Miradi itakayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, TAWA, NCT na NMT).

**318. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:

**Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programe VI)**

Mradi wa Programu ya maboresho ya usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI) ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi utatumia **Shilingi 95,794,606** fedha za ndani na **Shilingi 1,405,250,000** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuhuisha teknolojia zilizotumika kutengeneza moduli za Mfumo wa MNRT Portal, kuongeza moduli mpya pamoja na kufungamanisha mfumo wa MNRT Portal na mifumo ya taasisi zingine (TRA, Uhamiaji, NCAA, NIDA na BRELA);

(ii) Kufanya zoezi la majaribio la ukubali wa mfumo wa kielektroniki wa upangaji wa huduma za malazi na chakula katika Madaraja ya Ubora ya nyota;

(iii) Kufanya mafunzo ya Mfumo wa kielektroniki wa tathmini ya upangaji wa huduma za malazi na chakula katika Madaraja ya Ubora (AserT) kwa watumiaji na wadau katika kanda 4;

(iv) Kuwawezesha watumishi 8 kupata mafunzo ya muda mfupi ya usalama mtandaoni;

(v) Kuandaa nyaraka za usimamizi wa TEHAMA (ICT Documents – Enterprise Architecture Document na ICT Security Guideline Document).

**Ujenzi wa Tanzania Online Safari Booking System**

Ujenzi wa Mfumo huu una lengo la kupunguza mianya ya upotevu wa mapato yatokanayo na Sekta ya Utalii ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii itajenga Mfumo wa Tanzania Online Safari Booking System. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ujenzi wa mfumo utatumia kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya ukusanyaji wa mahitaji ya mfumo, usanifu, ujenzi, kufanya majaribio, kupandisha mfumo, mafunzo, matengenezo na maboresho ya mfumo.

**Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)**

Mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi utatumia **Shilingi 92,672,655** fedha za ndani na **Shilingi 40,880,000,000** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutekeleza mikakati ya kutangaza Utalii na kuendeleza Utalii wa utamaduni kusini mwa Tanzania;

(ii) Kuwezesha ufuatiliaji wa njia mbadala za kujipatia kipato kwa jamii zinazoishi jirani na hifadhi za kipaumbele (Mikumi, Nyerere, Udzungwa na Ruaha) kwa kusimamia shughuli za jamii katika Vijiji 61, vikundi vya COCOBA, Ufadhili wa wanafunzi, miradi ya vikundi, na Askari Wanyamapori wa Jamii (VGS);

(iii) Kuwajengea uwezo wa kusimamia vikundi wawezeshaji jamii 46, wajumbe 460 wa kamati za kusimamia utekelezaji wa shughuli za wananchi, watendaji wa Vijiji 46 pamoja na wawakilishi wa Mradi kwenye Wilaya 10 za Kilolo, Iringa, Mvomero, Kilosa, Chamwino, Ifakara, Rufiji, Kisarawe, Mbarali na Morogoro;

(iv) Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania (Southern Tanzania Destination Marketing Center) na Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa;

(v) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za mabonde madogo ya mito Chimala na Kimani kwa ujenzi wa skimu za Mbuyuni-Kimani na Makangarawe katika Wilaya ya Mbarali;

(vi) Kuwezesha upandaji wa miti rafiki katika vyanzo vya maji katika kingo za mito Ndembera, Mfyamba, Kioga, Mbarali, Kimani, Chimala, Mpolo, Mambi, Mswiswi, Mlowo, Gwiri, Mkoji, Balali, Halali, Mtitafu na Lumbizi katika Wilaya za Mufindi, Mbarali, Makete, Mbeya na Wanging'ombe;

(vii) Kuwezesha shughuli ya kurejesha mikondo ya mito iliyopoteza muelekeo (River trainings) katika Mto Mbarali;

(viii) Kuwezesha usimamizi wa fedha, manunuzi, usalama wa jamii na mazingira kwenye maeneo ya mradi, mafunzo pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi kwa watekelezaji wa mradi; na

(ix) Kuwezesha usimamizi na uratibu wa mradi kwa kufanya tathmini na kuratibu ufuatiliaji wa shughuli za mradi.

**Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili (Capacity Building in Game Reserves)**

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani, Kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 mradi utatumia **Shilingi 1,123,563,539** kutekeleza shuguli zifuatazo:-

(i) Kukamilisha malipo ya ununuzi wa eneo na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ghala la nyara Jijini Dodoma;

(ii) Kununua vitendea kazi kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi;

(iii) Kuperemba na kufanya tathmini ya pamoja ya shughuli za mradi;

(iv) Kuwezesha uratibu na usimamizi wa shughuli za mradi; na

(v) Ununuzi wa visukuma mawimbi (GPS Collars) 50 na mabomu baridi 20,000.

**Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Combating Poaching and illegal Wildlife Trade in Tanzania)**

Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inatekeleza Mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira **"Global Environmental Facility – GEF" katika Mwaka wa** Fedha 2024/2025 mradi utatumia **Shilingi 3,660,500,000** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ununuzi wa vifaa vya doria kwa ajili ya Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili (NTAP) na Kanda za Kiikolojia za Kuratibu Doria (TCGs);

(ii) Kutoa mafunzo maalum kuhusu intelijensia, usimamizi wa kesi na operesheni kwa maafisa kutoka NTAP, TCG na Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu;

(iii) Kuwezesha doria za ki-intelijensia katika TCG 10 na doria za pamoja za kikanda kwenye maeneo ya mifumo ikolojia inayovuka mipaka ya Nchi;

(iv) Kutoa elimu kuhusu athari za ujangili na biashara haramu ya nyara kwa Wabunge, Majaji na Waendesha Mashtaka;

(v) Kukamilisha maandalizi ya kanzidata kwa ajili ya kutunza taarifa na kumbukumbu mbalimbali za ujangili na biashara haramu ya nyara;

(vi) Kuwezesha mikutano ya kikanda ya kupambana na ujangili;

(vii) Kununua samani kwa ajili ya chumba maalum cha kuratibu kazi za kudhibiti ujangili; Kuwezesha uwekaji wa alama za kudumu na mipaka ya eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Chamwino;

(viii) Kuwezesha jamiii kutekeleza miradi ya kuongeza kipato na kupunguza utegemezi wa rasilimali za wanyamapori;

(ix) Kujengea uwezo hifadhi ya wanyamapori ya jamii (WMA) ya Chamwino kwa kuinunulia vifaa;

(x) Kuwezesha mtandao wa jamii wa ufuatiliaji wa masuala ya ujangili katika mfumo ikolojia wa Ruaha – Rungwa;

(xi) Kuwezesha utekelezaji wa mbinu za kujikinga na wanyamapori hatari na waharibifu; na

(xii) Kuwezesha kampeni za kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara.

**Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping)**

Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mradi utatumia **Shilingi 92,672,655** za fedha za ndani kwa ajili ya kujenga maabara ya mafunzo kwenye Chuo cha Ufugaji Nyuki – Tabora (BTI).

**Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC)**

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Umoja wa Ulaya. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi utatumia **Shilingi 1,587,948,290** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuwezesha mafunzo ya utalii wa nyuki, uzalishaji wa malkia na utengenezaji wa vifaa vya kukusanyia chavua kwa wakufunzi wa taasisi za mafunzo;

(ii) Kuwezesha ununuzi wa vifaa vya maabara ya utafiti wa ufugaji nyuki iliyopo Njiro;

(iii) Kuwezesha ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora;

(iv) Kutoa mafunzo ya utengenezaji wa mizinga ya nyuki inayofaa na utengenezaji wa mavazi ya kinga kwa mafundi seremala na cherehani mtawalia katika eneo la mradi;

(v) Kuboresha ugavi wa asali kwa kuanzisha vituo vya kukusanyia asali, masoko mahsusi ya kuuzia asali jirani na maeneo yaliyohifadhiwa pamoja na kuwezesha uanzishwaji wa vibanda maalum vinavyohamishika kwa ajili ya kuuzia asali maeneo ya barabarani;

(vi) Kuwezesha vitendea kazi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya nyuki kwa kuzingatia mbinu bora kwa vikundi vinavyotekeleza shughuli katika hifadhi za nyuki zilizoanzishwa;

(vii) Kuandaa ramani na vigezo vya kuanzisha manzuki za mfano na kuwezesha uanzishwaji wa manzuki hizo katika Wilaya za mradi;

(viii) Kuwezesha utafiti-vitendo katika masuala ya teknolojia za ufugaji nyuki, kuchapisha na kusambaza mbinu na matokeo ya tafiti hizo; na

(ix) Kuwezesha uanzishwaji wa kambi bora za ufugaji nyuki na kufanya ziara za kubadilishana uzoefu wa teknolojia za ufugaji wa malkia na uvunaji wa chavua.

**Mradi wa Kurejesha Mifumo ya Chakula na Matumizi Bora ya Ardhi (Food Systems, Land use and Restoration Project – FOLUR)**

Mradi huu unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira "Global Environmental Facility – GEF" utatumia **Shilingi 2,474,900,000** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutekeleza Mpango Kazi wa Usimamizi Shirikishi wa vyanzo vya maji katika Bonde la Kilombero (SMT);

(ii) Kuwezesha maandalizi ya mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi za Vijiji katika maeneo ya kipaumbele katika ikolojia za Kilombero;

(iii) Kutoa mafunzo na kujenga uelewa kuhusu usimamizi shirikishi wa ikolojia za Kilombero;

(iv) Kuwezesha tathmini ya vihatarishi kwenye maeneo yenye thamani kubwa ya uhifadhi na kubainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya uongoaji kwenye maeneo yaliyoharibiwa katika ikolojia ya Kilombero; na

(v) Kusimamia maeneo yenye thamani kubwa ya uhifadhi katika ikolojia lengwa kupitia mbinu zilizofanya vizuri kwenye maeneo mengine kwa ikolojia za Kilombero.

**Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE Tourism Development Project)**

Mradi huu utatumia **Shilingi 432,472,388** fedha za ndani kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa michoro ya ujenzi wa ukumbi wa mikutano.

**Ujenzi wa Makumbusho ya Marais - Dodoma**

Ujenzi huu una lengo la kuongeza wigo katika uhifadhi wa urithi wa asili na utamaduni wa Mtanzania, kuhifadhi historia za Waasisi na Viongozi Wakuu wa Nchi, kuimarisha na kuhamasisha tafiti za masuala ya historia pamoja na kuongeza vivutio vya utalii vya utamaduni. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ujenzi huu utatekelezwa na fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa makumbusho ya Marais wa Tanzania itakayojengwa Jijini Dodoma.

**Mradi wa Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii**

Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi huu utatumia fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 2,757,658,485** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la taaluma (Academic block) kwenye Kampasi ya Arusha. Jengo hilo litakuwa na miundombinu ya madarasa yenye uwezo wa kutumika kutoa kwa wanafunzi 1200, kumbi za mihadhara, kumbi za mikutano na vifaa vya mafunzo vikiwemo majiko, chumba cha kufulia (Laundry), mgahawa na yumba vya wageni (application rooms).

**Miradi ya TANAPA**

Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) litatumia kiasi cha **Shilingi 18,633,325,000** fedha za nje ili kutekeleza baadhi ya shughuli zifuatazo: -

(i) Ujenzi wa Miundombinu ya kijamii (29 katika Wilaya ya Serengeti na 29 katika Wilaya ya Ngorongoro);

(ii) Ujenzi wa Kituo cha kutolea taarifa kwa wageni (Serengeti Visitors Interpretive Centre (SVIC) eneo la Seronera;

(iii) Kugharamia shughuli za Ikolojia katika Hifadhi za Mahale na Katavi;

(iv) Kugharamia kazi ya uzoeshaji wa Sokwe matu (Habituation of Chimpanzee at Mahale Mountains NP);

(v) Ujenzi wa miundombinu ya kijamii katika Ushoroba wa Katavi – Mahale;

(vi) Ujenzi wa miundombinu ya kudhibiti mwenendo wa magari;

(vii) Utoaji elimu kwa wadau; na

(viii) Ujenzi wa jengo la Utawala kwa Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Mahale na ujenzi wa nyumba 6 za Maafisa katika Hifadhi ya Taifa Katavi.

**Miradi ya TAWA**

Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori itatumia kiasi cha **Shilingi 22,004,578,381** ambapo kiasi cha **Shilingi 11,479,826,671** ni fedha za ndani na **Shilingi 10,524,751,710** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa vivuko vya barabara, Jengo la Ofisi, Nyumba ya Wageni na Mnara wa Tangi la Maji, Karakana Kubwa, Bweni katika Pori la Akiba la Selous;

(ii) Ukarabati wa mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 593 na viwanja vidogo 4 vya ndege katika Pori la Akiba la Selous;

(iii) Ununuzi wa injini mpya ya ndege (5H SGR), kamera 3 kwa ajili ya programu ya uhamasishaji, magari 6 pamoja na gari 1 ya kubeba wagonjwa (Ambulance), vifaa vya ujenzi wa mfumo wa usambazaji wa maji katika vituo 8 vya Askari wa kudhibiti

wanyamapori wakali na waharibifu na basi dogo kwa ajili ya wafanyakazi wa Mapori ya Akiba Ikorongo – Grumeti;

(iv) Kununua na kufunga mfumo wa umeme wa jua (solar system) katika Kituo cha Askari wa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu Mboliboli;

(v) Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa katika Shule ya Ngumbu-Liwale, shule ya Sekondari Mwaseni-Rufiji na Shule ya msingi MiguruweKilwa;

(vi) Upanuzi wa Zahanati ya Miguruwe - Kilwa pamoja na ununuzi wa dawa;

(vii) Ujenzi wa daraja la Lung'onya na Matandu;

(viii) Ujenzi wa kilometa 255.1 za mtandao wa barabara katika mapori ya Akiba Wami-Mbiki, Mpanga Kipengere, Luganzo na Hifadhi ya wanyamapori Makuyuni;

(ix) Ujenzi wa ofisi 4 kwa ajili ya Kanda za Uhifadhi Magharibi, Ziwa na Mapori ya Akiba Wami-mbiki na Kilombero;

(x) Kununua boti maalum (air boat) 1 na trekta 1 katika Pori la Akiba Kilombero;

(xi) Kujenga lango la kuingia na kutoka katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni; na

(xii) Ukarabati wa nyumba 5 za watumishi na ujenzi wa uzio katika Ofisi ya Matumizi Endelevu – Arusha.

## 5.0 SHUKRANI

**319. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kumshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameendelea kutoa dira na maelekezo ili kuimarisha zaidi Sekta yetu ya Maliasili na Utalii na kuwezesha kufikia malengo yetu. Pia, kutumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti

wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

**320. Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini sio kwa umuhimu, nitumie fursa hii tena kipekee kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mailiasili na Utalii. Kwa hakika Naibu Waziri Wangu amekuwa wa Msaada Mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu, wakati wote. Aidha, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kusimamia vyema utekelezaji wa kazi mbalimbali za Wizara. Vilevile, nawashukuru Wakurugenzi na Vitengo vya Wizara; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinipatia wakati wote na juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba tunatimiza ipasavyo majukumu tuliyokabidhiwa. Naomba waendelee na juhudi hizo ili tuweze kutimiza malengo tuliyojiwekea.

**321. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kuwatambua wadau wote wa Wizara yetu ikiwa ni pamoja na Washirika mbalimbali wa Maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa Programu, Miradi na Mipango mbalimbali ya Wizara.

**322. Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kuzishukuru Nchi marafiki, Jumuiya za Kikanda, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali pamoja na wadau wengine wakiwemo Sekta Binafsi kwa ushirikiano wao katika kukuza na kuendeleza Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii ili kuchochea maendeleo ya jamii na uchumi wa Nchi kwa ujumla. Nachukua fursa hii kuzishukuru Serikali za Canada, China, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya.

**323. Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii pia kuyashukuru na kuyatambua Mashirika na Taasisi za Kimataifa zikiwemo: EU, AfDB, AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, RTI, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNTourism, IORA,

USAID, Honey Guide Foundation, CIFOR, ICRAF, INBAR, GATSBY, FOREST- FARM FACILITY, SIX RIVERS, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF.

**324. Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru pia wadau wote wa ndani wa Sekta ya Maliasili na Utalii wakiwemo: TCT, TATO, HAT, TAHOA, TLTO, TTGA, KGA, NTSGS, IGS, TGS, KTGA, NGTF, KPA, TPO, TACTO, TAOA, TAHA, TAWTO, TWEA, CWMAC, TABEDO, TAF, TTGAU, API-SUPPORT, HEAT, SHIVIMITA, Nature Tanzania na wadau wote wanaoshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale, uendelezaji na utangazaji utalii ikiwemo ofisi zetu za Ubalozi nje ya Nchi.

**325. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kutambua mchango wa Viongozi wetu wa Dini na Viongozi wa Kimila kwa jitihada wanazozionyesha katika kuhakikisha kuwa rasilimali zetu zikiwemo wanyamapori, misitu na malikale zinaendelea kulindwa na kuhifadhiwa kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vijavyo. Aidha, Viongozi hawa wamekua mstari wa mbele katika kupiga vita shughuli zinazoharibu mazingira zikiwemo; ukataji miti ovyo, uchomaji wa mkaa kiholela, na kufanya shughuli za kilimo ndani ya hifadhi kinyume na Sheria. Kwa upande mwingine, natambua mchango mkubwa unaotolewa na wenzetu wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Shule za Sekondari na Msingi kwa namna walivyojikita katika utunzaji wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kuanzisha vitalu vya miti na miradi ya ufugaji nyuki katika maeneo yao. Vilevile, natambua mchango wa taasisi za tafiti kwa namna zinavyoshirikiana na Wizara kwa kutafuta majawabu ya changamoto mbalimbali zinazokabili sekta ya Maliasili na Utalii.

**326. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee, navishukuru Vyombo Vya Ulinzi na Usalama, Taasisi za Himasheria pamoja na Vyombo vya Habari kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Maliasili na Utalii katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji Utalii.

**327. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Wizara yangu inatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau hawa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**328. Mheshimiwa Spika,** napenda kwa mara nyingine kuwashukuru Sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika utekelezaji wa majukumu yetu katika uhifadhi wa Maliasili, Malikale na Utalii na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

**6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025**

**329. Mheshimiwa Spika,** ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 348,125,419,000** kwa matumizi ya Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 250,884,083,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 97,241,336,000** ni za Miradi ya Maendeleo.

**330. Mheshimiwa Spika,** fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 125,366,391,000** za Mishahara na **Shilingi 125,517,692,000** za Matumizi Mengineyo. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 18,074,661,000** fedha za ndani na **Shilingi 79,166,675,000** fedha za nje.

**7.0 HITIMISHO**

**331. Mheshimiwa Spika,** napenda kuhitimisha kwa kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kushiriki katika uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji wa Utalii. Aidha, ninatoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**332. Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: https://www.maliasili.go.tz

**333. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava aje awasilishe Maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 kwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisishisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano: -

(i) Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaotoa msingi wa uchambuzi na mawanda ya uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayochambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iii) Sehemu ya tatu inayochambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iv) Sehemu ya nne inayofafanua maoni ya Kamati na ushauri unaotolewa kwa Serikali; na

(v) Sehemu ya tano ni hitimisho na msimamo wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024; katika eneo hili Kamati imezingatia mambo yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge;

(iii) Utekelezaji wa majukumu na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(iv) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na

(v) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati; katika kulisaidia Bunge lako Tukufu kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 2 Juni, 2023 wakati wa uwasilishwaji wa Hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo 19, sehemu kubwa ya ushauri imezingatiwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo na kuendelea kusisitiza kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa na Kamati, pamoja na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya maoni na ushauri ambao bado utekelezaji wake hauridhishi kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa minne ya Lindi, Pwani, Dar es Salaam na Tanga ili kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, katika maeneo hayo. Miradi hiyo ni: -

(a) Mradi wa Kuwezesha Watalii katika Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara

unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapori Tanzania *(TAWA)*.

(b) Mradi wa UVIKO–19 Pugu/Kazimzumbwi unaotekelezwa na Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)*.

(c) Mradi wa Kituo cha Kutangaza Utalii Kidigitali *(Destination Digital Marketing Command Centre – DDMCC)* unaotekelezwa na Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)*.

(d) Mradi wa Kukuza Utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Wizara; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara imefanya majukumu mbalimbali ikiwa ni utekelezaji wa vipaumbele vyake. Majukumu hayo yanaonekana katika ukurasa wa 37 hadi 66 wa Randama ya Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati ilifanya uchambuzi juu ya utekelezaji vipaumbele hivyo na taarifa kamili ya Kamati inaonekana kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa maduhuli, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 773,268,687,705.4. Hadi kufikia Februari, 2024 hatua ya ukusanyaji wa maduhuli ilifikia shilingi 664,993,203,299.66 sawa na 86% ya lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge. Kiwango hicho kinaashiria mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli. Uchambuzi zaidi unaonekana katika taarifa yetu na kielelezo namba moja cha taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kutoka Hazina; kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 654,668,208,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2024 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 406,884,441,886 sawa na 62% tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo 68.03% zilikuwa za matumizi ya kawaida

na 45.14% zilikuwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Taarifa zaidi inaoneshwa kwenye kielelezo namba mbili.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo si wa kuridhisha hali inayoweza kuathiri upatikanaji wa tija ilikusudiwa katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa. Changamoto hii inachangiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kushindwa kuwa na mpango bora wa matumizi ya fedha zinazopelekwa na Hazina. Hali hii ilionekana kwa Wizara hii kupewa kibali cha matumizi ya fedha ya baadhi ya miradi ya maendeleo jumla ya shilingi bilioni 52 zilizovuka mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2024 Wizara hiyo ilikuwa imetumia kiasi cha shilingi bilioni 47 tu ya fedha hizo, huku kiasi cha shilingi bilioni tano zikiwa hazijatumika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ni uchambuzi wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; Kamati ilichambua na kujadili mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; na

(iv) Mambo muhimu yanayogusa sekta ya maliasili na utalii

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025; kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 inakadiriwa kukusanya maduhuli ya shilingi 968,842,018,480. Makadirio haya yameongezeka kwa shilingi 195,573,330,774.6 sawa na 25.29% ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha unaokwisha. Taarifa zaidi inaoneshwa kwenye kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 inakadiria kutumia shilingi 348,125,419,000 ukilinganisha na makadirio ya matumizi ya shilingi 693,083,661,00 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taswira halisi ya matumizi inaonekana katika kielelezo namba nne.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo muhimu yanayogusa Sekta ya Maliasili na Utalii; changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu; nchi imeshuhudia migogoro kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. Kamati imebaini sababu mbalimbali zinazochangia migogoro hiyo hali ambayo imegeuka kuwa changamoto kubwa inayoikabili sekta ya maliasili na utalii nchini. Sababu hizo ni pamoja na ongezeko la watu na uanzishwaji wa shughuli za kibinadamu karibu na maeneo yaliyohifadhiwa na kwenye shoroba za wanyamapori, kukosekana au kutokuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinavyopakana na maeneo yanayotumiwa na wanyamapori, mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa na ongezekeo la wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mamlaka za serikali za mitaa 184 nchini, takribani halmashauri 91 zinakabaliwa na changamoto hii ikiwa ni sawa na 49.5% ya halmashauri zote nchini. Hata hivyo, miongoni mwake halmashauri 44 zimeonekana kukumbwa na changamoto kwa kiasi kikubwa zaidi ukilinganisha na nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari zinazotokana na migongano ya binadamu na wanyamapori ni pamoja na uharibifu mkubwa wa mazao, mifugo kujeruhiwa na kuuawa, binadamu kujeruhiwa na kuuawa, uharibifu wa miundombinu kama vile barabara, nguzo za umeme na miundombinu ya maji. Wanyama wanaoleta

changamoto kubwa ni pamoja na tembo, mamba, viboko, nyumbu, ngedere na nyani. Hali hii inaongeza kiwango cha umaskini miongoni mwa wananchi wanaokabiliana na changamoto hii hivyo kuzorotesha ustawi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto hiyo. Kamati imeipongeza Serikali kwa hatua ambazo imechukua. Pamoja hatua hizo, bado changamoto hii ni kubwa kwa hiyo, Kamati inaitaka Serikali kuongeza juhudi zaidi kuhakikisha inatekeleza mipango iliyojiwekea kwa wakati katika kukabiliana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Serikali imekuwa ikitoa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi walioathirika na matukio ya wanyapori wakali na waharibifu kwa mujibu wa Kanuni ya Kifuta Jasho na Machozi za mwaka 2011. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko miongoni mwa wananchi waliothirika kuwa kiwango kinachotolewa ni kidogo na hakitolewi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya migogoro baina ya askari wa uhifadhi na wananchi; Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa na nzuri inayofanywa na askari wa uhifadhi nchini, kwani wamesaidia katika kukabaliana na kudhibiti matukio ya ujangili wa wanyamapori na kuzuia uvamizi wa maeneo ya hifadhi. Hata hivyo, kumekuwa na baadhi ya matukio ya migogoro baina ya askari wa hifadhi na wananchi. Migogoro hiyo imezaa uhasama ambao umesababisha matukio ya kushambuliana na kusababisha majeraha, ulemavu na wakati mwingine vifo baina yao.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na malalamiko ya wananchi kukamatwa, kuteswa na kubambikiwa kesi na baadhi ya askari wa uhifadhi hali inayoongeza uhasama baina yao. Mathalani, katika moja ya matukio ambayo mahakama imethibitisha mwananchi kubambikiwa kesi na askari wa uhifadhi ni lile la mwananchi aitwae Richard Changei Ng'ombe, mkazi wa Wilaya ya Serengeti. Maelezo zaidi kuhusu kesi ambayo ni Rufaa ya Jinai Namba 40809 ya mwaka 2023 katika Mahakama ya

Tanzania, Kanda ya musoma ni kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Kwa rejea na kumbukumbu nzuri za Bunge lako ninaomba pia kuweka mezani kwako hukumu ya kesi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba si tu malalamiko ya watu kubambikwa kesi, bali kumekuwa na matukio ya wananchi kulalamikia kutaifishwa kwa mifugo yao kinyume na utaratibu. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa inafanya uchunguzi na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria baadhi ya askari wanaokiuka maadili ya kazi yao na kutenda kinyume na sheria. Pia Wizara ianze mchakato wa kuboresha Mtaala wa Jeshi Usu utakaosaidia kuboresha utendaji wa jeshi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya ufinyu wa bajeti na rasilimaliwatu kwa Taasisi za *TAFORI* na *TAWIRI;* pamoja na umuhimu wake katika sekta ya maliasili na utalii, taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti na rasilimaliwatu, hali inayochangia taasisi hizi kuwa na madeni, uchakavu wa miundombinu ya majengo na kukosa vifaa vya kisasa vya kufanyia tafiti. Kwa mfano, Taaisi ya *TAFORI* ina upungufu wa wafanyakazi kwa zaidi ya 55% huku ikidaiwa jumla ya shilingi 1,390,919,622. Kwa upande wa Taasisi ya *TAWIRI* changamoto kubwa ni kukosekana kwa fedha kiasi cha shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya kufanya sensa ya wanyamapori katika mifumo ya ikolojia 11 iliyopo nchini. Aidha, taasisi hii tangu kuanzishwa kwake mwaka 1985 haina jengo la ofisi za makao makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshwaji wa fedha za jumuiya za wanyamapori; kabla ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020, suala la kukusanya na kugawa fedha za *WMA* lilikuwa chini ya Wizara kupitia *TAWA*. Baada ya mabadiliko hayo ya sheria jukumu la kukusanya fedha za wanufaika linatekelezwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kisha kuhifadhiwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hali hiyo inachangia kucheleweshwa kwa mgao wa fedha za *WMA* hivyo kusababisha kukosekana kwa fedha uendeshaji wa ofisi, ulinzi wa rasilimali za

wanyamapori na kudhoofisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu upungufu wa huduma za malazi ya watalii nchini; Tanzania ina huduma za malazi takribani 10,432. Miongoni mwa huduma hizo za malazi huduma 1,437 sawa na 13.8% zina hadhi ya juu ya kulala wageni. Huduma za malazi zilizopo katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii ni 261 kati ya huduma zote1,437. Huduma za malazi 8,995 sawa na 86.2% ni nyumba za kulala wageni *(guest houses)* ambazo zina huduma za chini.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango wa ubinafsishaji Serikali ilifanya uamuzi wa kubinafsisha hoteli na *lodge* 23 ambapo kati ya hizo, *lodge* nne zipo ndani ya Hifadhi. *Lodge* hizo ni Seronera na Lobo zipo katika Hifadhi ya Serengeti, *Mikumi Wildlife Lodge* iliopo katika Hifadhi ya Mikumi na *Ngorongoro Wildlife Lodge* iliopo katika Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ongezeko kubwa la watalii wanaoingia nchini na hali ya huduma ya malazi iliyooneshwa hapo juu, Kamati inaitaka Serikali kuzirudisha hoteli zote ambazo wawekezaji wake wamekiuka mikataba ya uwekezaji. Aidha, Serikali iweke mazingira rafiki ya utekelezaji ya mwongozo wa uwekezaji katika sekta ya utalii pamoja na kutumia fursa za matukio ya utangazaji wa utalii kutangaza na kuvutia uwekezaji katika huduma za malazi hususani ujenzi wa hoteli zenye hadhi ya kati na ya juu katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho katika mpango na makadirio mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; katika kikao cha kupitisha bajeti ya Wizara katika ngazi ya Kamati siku ya Ijumaa tarehe 22 Machi, 2024 Kamati ilipata nafasi ya kushauriana na Wizara hivyo kwa pamoja kubeba ajenda ya nyongeza ya ukomo wa bajeti kwenda kwenye kikao cha mashauriano na Serikali kuhusu ongezeko la bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Mei, 2024, Kamati ilipokea taarifa ya Serikali kupitia kwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu maboresho ya mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 katika maeneo mawili ambayo ni utaratibu mpya wa kukusanya mapato kwa taasisi za *TANAPA* na Ngorongoro na ongezeko la ukomo wa bajeti kwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa maeneo hayo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu mpya wa makusanyo na matumizi kwa taasisi za *TANAPA* na Ngorongoro; Kamati ilitaarifiwa kwamba Serikali imeridhia ushauri wa muda mrefu wa Bunge lako Tukufu kuruhusu taasisi za uhifadhi za *TANAPA* na Ngorongoro kukusanya na kutumia mapato yao. Kutokana na uamuzi huo Kamati ilitaarifiwa kuwa makadirio ya matumizi ya *TANAPA* yameongezeka kwa shilingi bilioni 70 na matumizi ya Ngorongoro yameongezeka kwa shilingi bilioni 27.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwani kwa uamuzi huu ni wazi kuwa Serikali inaheshimu ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo inalipa Bunge Mamlaka ya Kuisimamia na Kuishauri Serikali. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuweka usimamizi madhubuti katika matumizi ya fedha za umma kwenye taasisi hizi ili kuzuia matumizi mabaya na ubadhirifu katika fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ongezeko la bajeti kwa Wizara ya Maliasili na Utalii; Kamati ilipokea taarifa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 limeongezewa bajeti kwa kiasi cha shilingi bilioni 19 ili kupunguza baadhi ya changamoto zinazosababishwa na ufinyu wa bajeti. Katika fedha hizo, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara imepanga kutumia shilingi bilioni 14, sawa na 74% ya nyongeza hiyo katika matumizi mengineyo, na shilingi 5,000,000,000 sawa na 26% kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhika na mgawanyo wa nyongeza hiyo kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni baadhi ya taasisi za Wizara kutokuwa na ofisi, mzigo wa madeni, uchakavu wa miundombinu na changamoto ya wanyamapori wakali na waharaibifu kuvamia makazi ya wananchi. Hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba ongezeko hili halitakuwa na tija kwa Wizara kwa sababu haliendi kushughulikia changamoto za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba taasisi zimeruhusiwa kukusanya 6% na kutumia kwenye utangazaji wa utalii bado shilingi 1,000,000,000 imeongezeka kwenye Idara ya Utalii kwenye kutangaza utalii, safari za nje, kubaini vivutio na mazao mapya ya utalii na kufanya utafiti. Kazi hizi ni kazi za msingi za Bodi ya Utalii na si Wizara. Hata hivyo, katika nyongeza hiyo shilingi 2,000,000,000 zimeelekezwa katika ujenzi wa mifumo ya TEHAMA ujulikanao kama *Tanzania Safari Booking Platform*. Kamati ya imebaini kwamba fedha hizo zimetengwa kutekeleza mradi ambao hauna andiko la awali wala gharama halisi za mradi. Pamoja na manufaa yanayotarajiwa na mfumo huo, maandalizi ya utekelezaji hayajafanyika na hivyo fedha hizi zinaweza kutumika vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Kituo cha Kutangaza Utalii Kiditali *(DDMCC)* ambacho Kamati ilikitembelea, kuna sehemu ya mfumo wa kufanya miadi *(booking)* na kuwaunganisha watalii kutoka nje ya nchi na huduma za hoteli na usafiri ijulikanayo kama *Travel Companion.* Kwa hiyo, kujenga mfumo kama huo ndani ya Wizara hiyo ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati ya kutokubaliana na matumizi ya nyongeza, Serikali ilipewa siku 15 ili kutafakari na kuona namna ya kufanya mabadiliko. Serikali ilikubaliana na Kamati na kuahidi kwenda kushughulikia jambo hilo kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha, kikao kilichofanyika tarehe 21 Mei, 2024 ili kupokea utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati, Kamati ilitaarifiwa kwamba mabadiliko hayawezi kufanyika kwa sababu vitabu vimefungwa jambo ambalo si sahihi. Mchakato wa ufungaji wa vitabu vya bajeti unafanyika baada ya kupitisha Sheria ya Matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla; Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili utekelezaji wa miradi hiyo ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani upatikanaji wake siyo wa uhakika, jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie kikamilifu utendaji wa taasisi ambazo zinakusanya maduhuli kupitia Mfumo wa *MNRT Portal* na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ili kuhakikisha zinaongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, maoni mahsusi kuhusu maeneo mahsusi yanayogusa Wizara ya Maliasili na Utalii; changamoto ya migogoro ya mipaka katika maeneo ya hifadhi na vijiji vinavyozunguka hifadhi.

(i) Kamati inaishauri Serikali, Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara nyingine za kisekta ili iweze kupima na kufanya utambuzi wa mipaka halisi itakayoondoa migogoro kati ya hifadhi na wananchi wanaoishi kuzunguka maeneo ya hifadhi. *(Makofi)*

(ii) Iweke alama zinazoonekana katika mipaka ya hifadhi na ile ya ardhi za vijiji vinavyozunguka hifadhi ili kupunguza na kuondoa migogoro ya ardhi baina ya hifadhi na wananchi;

(iii) Ihakikishe panakuwa na ushirikishwaji wa Wizara za Kisekta, taasisi nyingine za Serikali na wananchi wakati wa uwekaji wa alama za mipaka, uanzishwaji wa hifadhi au uanzishwaji wa vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Ichukue hatua stahiki za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababishwa na muingiliano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. *(Makofi)*

(ii) Ishirikiane na Wizara ya nyingine za kisekta kuongoa shoroba za wanyamapori kupitia zoezi la kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi;

(iii) Iboreshe kanuni na viwango vya kifuta machozi kwa wananchi kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyama ili vizingatie hali halisi ya maisha na thamani ya uharibifu au madhara yaliyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya migogoro baina ya Askari wa Hifadhi na wananchi; Kamati inaishauri kuwa:

(i) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka hifadhi, ikiwa ni pamoja na Askari wa Hifadhi ili kuboresha mahusiano baina yao.

(ii) Ihakikishe inawachukulia hatua za kisheria na kutoa taarifa kwa wananchi na wawakilishi wao, juu ya hatua zilizochukuliwa kwa askari wa uhifadhi ambao watabainika wanashiriki katika vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wananchi wanaozunguka hifadhi. Hali hii itaongeza uwajibikaji kwa Askari wa Hifadhi na kuondoa dhana kwa

jamii kudhani kuwa Askari wa Hifadhi wanalindwa na Serikali hata katika makosa ya wazi. *(Makofi)*

(iii) Iweke utaratibu wa kufidia hasara inayotokana na kubainika kwa vitendo vya baadhi ya Askari wa Uhifadhi kuharibu mali za wananchi.

(iv) Itekeleze mpango wa kurejesha kwa jamii *(CSR)* kwa jamii zinazozunguka hifadhi ili kuhakikisha jamii hizo zinanufaika na shughuli za uhifadhi na utalii zinazoendelea katika maeneo wanayopakana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya vitendea kazi na rasilimali watu kwa taasisi za *TAFORI* na *TAWIRI*; Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Iandae mpango mkakati wa ajira za muda mfupi, kati na mrefu ili kupunguza na kuziba pengo la watumishi katika taasisi hizi muhimu kwa maendeleo ya Sekta za Uhifadhi na Utalii.

(ii) Iweke mkakati utakaoiwezesha *TAWIRI* kufanya Sensa ya Wanyamapori katika mifumo 11 ya Ikolojia nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya ucheleweshaji wa fedha za Jumuiya za Wanyapori *(WMAs)*; Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Irejeshe fedha za *WMAs* zinazodaiwa na Jumuiya hizo kwa mujibu wa kanuni ili kusaidia ufanisi katika kutekeleza majukumu yao ya uhifadhi na utalii. *(Makofi)*

(ii) Ifanye marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 ili kuruhusu fedha zinazotokana na shughuli ndani ya *WMAs* kulipwa moja kwa moja kwenye *WMAs* zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uhaba wa huduma ya malazi; Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Ichukue hatua za haraka kurudisha hoteli na *lodge* toka kwa wamiliki waliobinafsishiwa hoteli na *lodge* za Serikali ambao wamekiuka masharti ya mikataba yao ya kuziboresha, hali itakayopunguza uhaba wa huduma ya malazi ya watalii nchini. *(Makofi)*

(ii) Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwenye kutangaza fursa za uwekezaji wa huduma za malazi katika maeneo yanayomilikiwa na Wizara na sehemu zilizokaribu na vivutio vya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, utangazaji wa vivutio vya utalii; Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

(i) Iandae na kutekeleza kikamilifu mikakati madhubuti ya kutambua na kutangaza vivutio vingine vya utalii, kama ilivyo kwenye utalii wa wanyamapori ili kuongeza wigo wa mapato yatokanayo na utalii.

(ii) Ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha kwa ajili Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali *(DDMCC)* ili kiweze kufanya kazi kama ilivyotarajiwa na kuleta tija iliyokusudiwa. *(Makofi)*

(iii) Ishirikishe sekta binafsi na wadau wengine wa sekta ya utalii katika kuibua na kutangaza vivutio vipya vya utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; Kamati haijakubaliana na matumizi ya shilingi bilioni 16 kati ya bilioni 19 zilizoongezeka. Sababu za kutokubaliana na matumizi hayo ni kama nilivyozibainisha juu. Kamati inapendekeza ongezeko hilo lielekezwe katika maeneo yafuatayo: -

(i) Ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya *TAWIRI*;

(ii) Ukarabati wa miundombinu ya ujenzi na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika vyuo vya *FTI* – Moshi, Olmotonyi – Arusha na Pasiansi – Mwanza;

(iii) Kushughulikia changamoto ya wanyama wakali na waharibifu, ikiwa ni pamoja na kuongeza vizimba vya mamba na viboko, kwa kuzingatia kanda zenye changamoto kubwa;

(iv) Ujenzi wa vituo vya Askari wa Wanyamapori na ongezeko la fedha kwenda *TAWA* ili kuongeza idadi ya mabwawa katika mapori tengefu na mapori ya akiba. *(Makofi)*

(v) Fedha nyingine kwenda *TAFORI* kwa ajili ya kusaidia kulipa madeni na kushughulikia uchakavu wa vifaa na miundombinu ya ujenzi.

(vi) Kiasi kingine cha fedha hizo kielekezwe kwenye matumizi mengineyo *(OC)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili, Kamati imekusudia kuleta *addendum* ya mabadiliko ya Fungu 69 kuhusu matumizi ya fungu hili wakati wa kupitisha vifungu. Endapo itakupendeza, Kamati inaomba jambo hili ulielekeze Kamati ya Bajeti lishughulikiwe kwa mujibu wa Kanuni ya 124 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni kuhusu kufanya mabadiliko kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024; Serikali ifute marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 yaliyofanyika kwenye Sheria ya Hifadhi za Taifa na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kurejesha utaratibu ambao Kamati ilitaarifiwa umekwishakubaliwa na Serikali wa kukusanya na kutumia.

Mheshimiwa Spika, kuweka masharti maalumu yatakayotaka bajeti za taasisi hizo kuchambuliwa na kuidhinishwa na Wizara ya Fedha pamoja na Msajili wa Hazina kabla ya kila mwaka wa fedha kuanza ili kuzuia ubadhirifu wa fedha za umma unaoweza kujitokeza kwa taasisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; ninapenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo

mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kwa moyo wa dhati kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha na uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingine kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee na kwa upendeleo, ninatumia nafasi hii kuwashukuru Wana-CCM na wapiga kura wa Jimbo la Korogwe Vijijini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kazi yao ya kuwawakilisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki (Mb) na Naibu Waziri na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula (Mb). Pia ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hassan Abbas pamoja na Naibu Katibu Mkuu, *CP*. Benedict Wakulyamba, kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee ninaomba niwashukuru watumishi wote wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa kuongoza vyema uratibu wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii pamoja na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii - Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kama yalivyowasilishwa awali na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** ili kurahisishisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayohusu taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza inayotoa, Msingi wa Uchambuzi na Mawanda ya Uchambuzi;

(ii) Sehemu ya pili inayochambua na kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na

(iii) Sehemu ya tatu inayochambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Sehemu ya nne inayofafanua Maoni ya Kamati na ushauri unaotolewa kwa Serikali; na

(v) Sehemu ya mwisho inahitimisha taarifa ya uchambuzi na kuonesha msimamo wa Kamati.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi Wizara ya Maliasili na Utalii ni Masharti ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, ambapo Kanuni ya 6 (8)(b) ikisomwa kwa pamoja na kanuni ya 7(1)(a) zinatoa jukumu hilo kwa Kamati. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kuja na matokeo kama yalivyoainishwa katika taarifa hii.

## 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:-

(i) Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iii) Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(iv) Mambo muhimu katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa uchambuzi, Kamati iliongozwa na kigezo cha asilimia pamoja na kufanya tathmini ya jumla na ulinganisho wa mambo mbalimbali. Mambo hayo yaliiwezesha Kamati kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji na mantiki ya mpango na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokuja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) na (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii baada ya ziara ya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kupata uwiano utakaolisaidia katika uamuzi kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, sehemu hii inafafanua mambo matano yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushuri uliotolewa na Kamati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha na Bunge;

(iii) Utekelezaji wa majukumu na Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha, 2023/2024

(iv) Hali ya ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali; na

(v) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** mambo hayo kwa pamoja yameweka msingi wa kuliwezesha Bunge lako Tukufu kupata uwiano utakaolisaidia katika kufikia uamuzi baada ya mjadala wa hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika kulisaidia Bunge kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali, tarehe 02 Juni, 2023, wakati wa uwasilishwaji wa hotuba ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka fedha 2023/2024, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kuhusu mambo kumi na tisa **(19)**. Ili kupima tija ya Bunge kuendelea kuishauri Serikali, Kamati ilitaka kubaini iwapo ushauri uliotolewa umezingatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 22 Machi, 2024, Waziri wa Maliasili na Utalii alifika mbele ya Kamati aliwasilisha taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika kuzingatia ushauri wa Kamati. Kamati ilichambua taarifa na kubaini kwamba, sehemu kubwa ya ushauri imezingatiwa. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hiyo na kuendelea kusisitiza kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kuna baadhi ya maoni na ushauri ambao bado utekelezaji wake hauridhishi. Maoni na ushauri ambao utekelezaji wake hauridhishi ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa elimu ya kutosha kuhusiana na mipaka ya hifadhi ili kusaidia wananchi kutambua maeneo ambayo hawapaswi kuwepo kisheria;

(ii) Serikali kuandaa na kutekeleza mkakati madhubuti wa kutambua na kutangaza vivutio vipya vya utalii ili kuongeza mapato yatokanayo na utalii tofauti na sasa ambapo kiasi kikubwa mapato ya utalii yanatokana na utalii wa wanyamapori;

(iii) Ushirikishwaji usioridhisha baina ya Serikali, wawakilishi wa wananchi na viongozi wa vijiji katika kutatua migogoro inayotokana na mipaka ya hifadhi, uvamizi wa mifugo kwenye hifadhi, biashara ya mkaa na mazao ya misitu hali inayochangia uhasama baina ya wananchi na askari wa Uhifadhi; na

(iv) Serikali kushindwa kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye miradi ya maendeleo, badala yake katika mwaka wa fedha 2024/2025 utegemezi umeongezeka kwa **asilimia 36** kulinganisha na mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa ukomo wa bajeti na upatikanaji usioridhisha wa fedha za Maendeleo ni moja ya sababu za Wizara kushindwa kutekeleza baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati kwa ufanisi. Hali hii inaweza kupunguza manufaa ya Wizara hii katika Taifa na kupelekea kuzorotesha ustawi wa wananchi kinyume na lengo la Serikali kama inavyotakiwa na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 2.2 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha

### 2.2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa minne (4) ya Lindi, Pwani, Dar es Salaam na Tanga ili kukagua baadhi ya miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kamati ilikagua miradi minne (04) kama ifuatayo:-

**(a) Mradi wa Kuwezesha Watalii katika Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyapori (TAWA)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitekelezwa kwa thamani ya **Shilingi 1,449,387,245.00** zilizoidhinishwa na Bunge. Lengo lake ni kuwezesha shughuli za utalii katika Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara ambayo ipo katika Wilaya ya Kilwa Mkoa wa Lindi. Shughuli za utekelezaji wa mradi huu zilijumuisha

ukarabati wa Gati, Ukarabati wa ngazi ya Kasri ya Husuni Kubwa, Ukarabati wa Mnara wa Songo Mnara, Ujenzi wa maliwato, Ujenzi wa njia za watembea kwa miguu (pedestrian strips), Ununuzi wa boti mbili za kisasa kwa ajili ya wageni (Glass Bottom Boat'), Ujenzi wa eneo maalum la kupumzika wageni (Tourism Lounge) na Ujenzi wa mabanda ya kulala wageni (Tourism Banda).

**Mheshimiwa Spika,** taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati zilibainisha kuwa miradi huu umekamilika kwa **asilimia 100.** Aidha, Kamati ilijionea utekelezaji wa mradi huo na hatua zilizofikiwa ambazo ni sehemu ya mkakati wa kuirejesha sekta ya utalii baada ya athari za UVIKO -19.

**(b) Mradi wa UVIKO – 19 Pugu/Kazimzumbwi Unaotekelezwa na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa jumla ya **shilingi 579,142,176.00** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika msitu wa Pugu/Kazimzumbwi uliopo Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani. Aidha, ili kulinda miundombinu hiyo, TFS ililazimika kujenga makalavati na madaraja kwa **Shilingi 126,062,350.00** na kufanya gharama ya mradi kufikia jumla ya **Shilingi 658,267,957.19.** Kiasi cha fedha za ziada kwa mradi huu kilipatiakana kutokana na bakaa ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za utekelezaji wa mradi huo ni pamoja na ujenzi wa Barabara ya **kilometa 12** kutoka Kimani-Maguruwe na ukarabati wa barabara ya **kilometa 1** kutoka Minaki – Bwawani. Shughuli nyingine ni ujenzi wa **kilometa 7** za njia za watembea kwa miguu na Ujenzi wa lango la kuingilia kwenye ofisi, kituo cha taarifa za utalii, ofisi ya malipo na kibanda cha mlinzi. Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100,** na tayari umeanza kutumika katika shughuli za uhifadhi na utalii.

**(c) Mradi wa Kituo cha Kutangaza Utalii Kidigitali (Destination Digital Marketing Command Centre – DDMCC) unaotekelezwa na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni sehemu ya mikakati ya kutangaza Utalii nchini na unatekelezwa katika Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar Es Salaam. Kwa ujumla mradi umetumia

kiasi cha **Shilingi 1,372,256,210.07** kwa ajili ya miundombinu ikiwemo ujenzi wa chumba cha kurushia matangazo, ununuzi wa vifaa, samani na mifumo ya kurushia matangazo.

**Mheshimiwa Spika,** Kituo hicho kimekamilika kwa **asilimia 100**, na tayari kimeanza kutekeleza Mkakati wa Utangazaji uliokuwa umeandaliwa kama sehemu ya majaribio. Aidha, Kituo hicho kinafanya kazi kidijitali katika kutangaza vivutio vya utalii na kutoa taarifa sahihi kuhusu fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii.

**(d) Mradi wa Kukuza Utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unalenga kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii na unatekelezwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan iliyopo katika Mikoa ya Pwani na Tanga. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,023,128,519.23** zimetengwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi huu. Shughuli hizo ni ujenzi wa vyoo vya kisasa katika uwanja wa ndege wa Saadan na eneo la kupiga mahema, ukarabati wa barabara mbalimbali ndani ya hifadhi, ujenzi wa bwalo la chakula na kisima cha kuvuna maji ujazo wa lita 1000 pamoja na ununuzi wa samani kwa ajili ya matumizi ya hosteli.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu kwa wastani umefikia **asilimia 80**, hata hivyo mradi huu unatarajia kukamilika pale fedha zilizobakia za mradi zitakapopokelewa kutoka hazina.

**2.2.2 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi**

**Mheshimwa Spika,** Katika ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Lengo ilikuwa kulinganisha na kubaini iwapo taarifa zilizowasilishwa na Wizara zinawiana na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji pamoja na madhumuni ya miradi inayohusika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya Serikali chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii iliyotembelewa na kukaguliwa. Kamati

inalitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza miradi hiyo thamani ya fedha, uwekevu, ufanisi na tija vimezingatiwa. Tathmini ya kina, imebainisha yafuatayo:-

i. Utekelezaji wa miradi umewezesha ongezeko la Watalii na shughuli za Utalii katika maeneo ambayo miradi ya kuimaraisha utalii inatekelezwa. Mathalani, Katika katika Msitu wa Pugu/Kazimzumbwi kwa mwaka wa fedha, 2019/2020, wageni waliotembelea Msitu huu ni **1,822** na mapato yalikuwa **Shilingi 6,013,000.00** tu, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024, hadi kufikia Februari, 2024 wageni walikuwa **15,473** na mapato ya **Shilingi 115,650,000.00;** na

ii. Tija iliyokusudiwa katika mradi wa TTB, inakwamishwa na kutolewa kwa bajeti isiyotosheleza kwa ajili ya kuendesha Kituo cha Kidijali cha Kutangaza Utalii. Mahitaji ya fedha ni kiasi cha **Shilingi 5,831,846,284.08,** sawa na **asilimia 63.4** ya bajeti yote TTB. Lakini hadi kufikia Februari, 2024 TTB ilikuwa imepokea **asilimia 27** tu ya bajeti yake iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mambo hayo yaliyobainika, Kamati ilibaini kuwa Kuna uvamizi wa binadamu na ongezeko la shughuli za kibinadamu katika maeneo ya hifadhi hali inayochangia migogoro ya ardhi katika maeneo hayo. Mathalani, Katika hifadhi ya Taifa ya Saadani, kuna mgogoro wa mpaka kati ya hifadhi na wananchi wa Kitongoji cha Uvinje, vilevile katika hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara kumekuwa na changamoto ya kuongezeka kwa idadi ya watu na makazi ndani ya hifadhi. Aidha, kuna upungufu mkubwa wa miundombinu ya malazi na chakula, umeme na barabara katika kuwezesha shughuli za utalii kwenye maeneo hayo.

### 2.3 Utekelezaji wa Vipaumbele na Majukumu ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa vipaumbele vya Serikali nchini kwa ujumla unazingatia mipango na miongozo ya Kitaifa na Kimataifa. Mipango na miongozo hiyo ni pamoja na Dira ya Maendeleo ya Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa

wa Miaka Mitano (FYDP III) mwaka 2021/22 – 2025/26, Malaengo ya Maendeleo Endelevu chini ya Umoja wa Mataifa, Malengo ya Utalii Endelevu chini Shirika la Utalii Duniani na maelekezo mengine.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii ina dhamana ya kutekeleza vipaumbele vya Serikali kwenye sekta za Utalii, Wanyamapori, Mambo ya Kale na Misitu na Nyuki. Katika utekelezaji wake, Wizara hii inajukumu la kuhakikisha Ulinzi na Uhifadhi endelevu wa sekta hizo kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho. Ni dhamira ya Serikali kuwa, sekta hizi zitaleta manufaa kwa Taifa na kusaidia katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuchangia pato la Taifa, kutoa ajira na kupunguza umasikini hatimae kuleta ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara imefanya majukumu mbalimbali ikiwa ni utekelezaji wa vipaumbele hivyo. Majukumu hayo yanaonekana katika ukurasa wa 37 hadi 66 wa Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati unaonesha kwamba utekelezaji wa majukumu hayo umechangia mafaniko mbalimbali. Mafanikio makubwa na ya kupigiwa mfano ni Kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini kutoka **1,454,920** mwaka 2022/2023 hadi watalii **1,808,205** mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la **asimilia 24.3**. Ongezeko hili limeenda sambasamba na kuongezeka kwa Mapato yatokanayo na utalii kutoka Dola za Marekani **Milioni 2,527.72** mwaka 2022 hadi Dola za Marekani **Milioni 3,373.83** mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 33.5. Mafanikio hayo yamechangiwa na mikakati mbalimbali ikiwemo juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** katika kutangaza utalii kupitia program maalum ya Tanzania – *The Royal Tour.*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati umebaini kuwa katika kutekeleza vipaumbele na majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara hii inakabiliwa na bado changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja ufinyu wa bajeti,

ongezeko la matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu, upungufu wa watumishi na vitendea kazi, kuchelewa kupata fedha za wanufaika kutokana na shughuli za Jamuiya za Wanyamapori (WMAs), migogoro baina ya wananchi na askari wa uhifadhi na mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** hatua za haraka zinatakiwa kuchukuliwa na Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo kwani zinaweza kuwa kikwazo cha kufikia malengo ya ibara ya 67-70 ya ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020. Ibara hiyo inaitaka Serikali kukuza sekta ya utalii nchini ili kuongeza idadi ya watalii kufikia milioni tano na kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii nchini kufikia Dola za Kimarekani bilioni sita kufikia mwaka 2025.

### 2.4 Hatua iliyofikiwa katika Ukusanyaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la uchambuzi wa taarifa za makusanyo ya maduhuli ni kuliwezesha Bunge kubaini iwapo lengo la makusanyo lililoidhinishwa na Bunge limefikiwa. Aidha, uchambuzi huu unaliweka Bunge katika nafasi ya kutumia uzoefu unaopatikana kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kubaini uhalisia unavyostahili kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 773,268,687,705.40**. Hadi kufikia Februari, 2024 hatua ya ukusanyaji wa Maduhuli ilifikia Shilingi **664,993,203,299.66** sawa na **asilimia 86** ya lengo la makusanyo liliodhinishwa na Bunge. Kiwango hicho kinaashiria mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli ulionyesha yafuatayo:-

i. Ukusanyaji wa kutumia MNRT portal, umefikia **asilimia 58** ya lengo lililoidhinishiwa, huku ukusanyaji wa kutumia TRA imefikia **asilimia 96** ya lengo la njia hiyo. Kwa takwimu hizo njia ya TRA itafikia na hata kuvuka lengo na kwa upande mwingine njia ya MNRT portal ina hatari ya kutofikia lengo; na

ii. Wakati wa makadirio, makusanyo kwa utaratibu wa MNRT portal yalitarajiwa kuchangia kwa **asilimia 26** huku yale ya TRA yakitarajiwa kuchangia kwa **asilimia 74.** Hata hivyo, katika makusanyo halisi njia ya portal imechangia pungufu kwa kufikia **asilimia 18** wakati njia ya TRA imechangia zaidi ya makadirio ya mchango wake kwa kufikia **asilimia 82**. Taswira kamili ya ukusanyaji inaonekana katika **Kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na: 1 Ukusanyaji wa Maduhuli hadi Februari, 2024**

| Fungu 69 | % ya Makadirio | Makadirio | Makusanyo | % ya Makusanyo | % ya lengo njia |
|---|---|---|---|---|---|
| *MNRT Portal* | **26** | **200,363,068,234.48** | **116,494,574,362.27** | **18** | **58** |
| TRA (TANAPA, NCAA, TAWA) | **74** | **572,905,619,470.92** | **548,498,628,937.39** | **82** | **96** |
| **JUMLA** | **100** | **773,268,687,705.40** | **664,993,203,299.66** | **100** | **86** |

***Chanzo***: *Randama ya Wizara ya mwaka 2024na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mchanganuo huo ni dhahiri kuwa, Makusanyo taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA ndio yaliyofanikisha kwa kiasi kikubwa makusanyo kufikia **asilimia 86**. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua ya makusanyo iliyofikiwa. Hata hivyo, Kamati, inaitaka Wizara kuongeza usimamizi wa karibu katika taasisi zinazokusanya maduhuli kupitia mfumo wa MNRT Portal ili ziongeze kasi ya ukusanyaji wa maduhuli na kufikia lengo liliowekwa.

## 2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Bajeti unategemea upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi

**654,668,208,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2024, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 406,884,441,886.00** sawa na **asilimia 62.2** tu ya fedha iliyoidhinishwa. Katika fedha hizo, **Shilingi 330,972,018,516** sawa na **asilimia 68.03** zilikuwa za matumizi ya kawaida na **Shilingi 75,912,393,369.93** sawa na **asilimia 45.14** zilikuwa za kugharamia miradi ya maendeleo. Taswira ya Upatikanaji wa Fedha inaonekana katika **Kielelezo Na. 2.**

**Kielelezo Na: 2 Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha hadi Februari, 2024**

| Matumizi | | Kilichoidhinishwa | Kilichopokelewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Kawaida | OC | 302,212,953,000 | 195,455,009,252 | 64.67 |
| | Mishahara | 184,288,496,000 | 135,517,009,264 | 73.54 |
| | Jumla (A) | **486,501,449,000** | **330,972,018,516** | **68.03** |
| | | | | |
| Maendeleo | Ndani | 109,879,593,000 | 35,602,037,491.86 | 32.40 |
| | Nje | 58,287,166,000 | 40,310,355,878.07 | 69.16 |
| | Jumla (B) | **168,166,759,000** | **75,912,393,369.93** | **45.14** |
| **JUMLA KUU (A+B)** | | **654,668,208,000** | **406,884,441,886** | **62.15** |

*Chanzo: Randama ya Wizara 2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa bajeti, Kamati uchambuzi wa kina katika mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka hazina ambapo unaonyesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2024:-

i. Upatikanaji halisi ulitakuwa uwe usiopungua **asilimia 67** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa ili kuendana na muda wa utekelezaji wa bajeti, lakini Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 62.15** tu; ii. Katika **asilimia 45** ya bajeti iliyopokelewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha za Ndani ni **asilimia 32.40** tu, huku fedha za nje zikiwa ni **asilimia 69.16** ya bajeti iliyoidhinishwa.

iii. Kuwepo kwa changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uendeshaji wa shughuli za ofisi. Aidha, upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo si wa kuridhisha, hali inayoweza kuathiri upatikanaji wa tija ilikusudiwa katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto hii inatokana na Wizara ya Maliasili na Utalii kushindwa kuwa na mpango bora wa matumizi ya fedha zinazopelekwa na hazina. Hali hii ilionekana kwa Wizara hii kupewa kibali cha matumizi ya fedha ya baadhi ya miradi ya maendeleo jumla ya **shilingi 52,640,664,356.03** zilizovuka kutoka mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2024, Wizara hiyo ilikuwa imetumia kiasi cha **Shilingi 47,331,713,792.73** tu ya fedha hizo, huku kiasi cha **Shilingi 5,308,950,563.30** zikiwa hazijatumika.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, **Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua na kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

i. Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
ii. Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
iii. Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa;na
iv. Mambo muhimu yanayogusa sekta ya Maliasili na Utalii

### 3.1 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua uhusiano uliopo kati ya Mapato na Matumizi, Kamati ilipokea ufafanuzi kuhusu lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** inakadiriwa kukusanya maduhuli ya **shilingi 968,842,018,480.00**. Aidha, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa maduhuli kwa

mwaka wa fedha 2023/2024**.** Taswira ya ulinganisho wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 inaonekana katika **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na: 3Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| Fungu 69 | 2023/2024 | 2024/2025 | % Ongezeki |
|---|---|---|---|
| Maduhuli yanayokwenda Mfuko Mkuu wa Serikali | **773,268,687,705.40** | 105,558,757,000.00 | -86.40 |
| Maduhuli yanayokusanywa na kutumika na taasisi | **0.00** | 863,283,261,480.00 | - |
| **JUMLA** | **773,268,687,705.40** | **968,842,018,480** | **25.30** |

***Chanzo****: Randama ya Wizara 2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini yafuatayo:-

i. Makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezeka kwa **shilingi 195,573,330,774.60** sawa na **asilimia 25.29** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha 2023/2024;

ii. Makadirio ya Makusanyo ya maduhuli yanayokwenda mfuko mkuu wa Serikali yamepungua kwa **asilimia 86** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024. Upungufu huo umetokana uamuzi wa Serikali kuruhusu baadhi ya taasisi zilizochini ya Wizara kubaki na makusanyo yake. Aidha, katika lengo la Makusanyo ya Wizara, **asilimia 89.10** ya makusanyo, yatakusanywa na kutumika na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, huku **asilimia 10.90** makadirio yatakusanywa na kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi zaidi wa Kamati ulibaini kuwa ukuaji wa sekta ya utalii nchini umechangia ongezeko la makadirio ya maduhuli. Aidha, utekelezaji wa mkakati wa wizara wa kuimarisha sekta ya utalii baada ya athari za UVIKO-19 ni sehemu ya sababu za ongezeko la makadirio ya maduhuli. Hata hivyo, lengo hilo la maduhuli litaweza kufikiwa iwapo Serikali itatekeleza ipasavyo mikakati ya kutangaza vivutio vya utalii kwa ufanisi na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato.

### 3.2 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza mpango na vipaumbele vilivyowekwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69)** inakadiria kutumia Shilingi **348,125,419,000.00** kulinganisha na makadirio ya matumizi ya **Shilingi 693,083,661,00.00** katika mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge yamelenga kuliwezesha Bunge kutumia uzoefu wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kwa kuzingatia lengo hilo, Kamati imechambua makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kulinganisha makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Taswira ya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na 2024/2025 inaonekana katika **Kielelezo Na. 4.**

**Kielelezo Na: 4 Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| **Mwaka** | **Matumizi ya Kawaida** | | **Maendeleo** | |
|---|---|---|---|---|
| | PE | OC | Ndani | Nje |
| 2023/24 | 184,288,496,000 | 302,212,953,000 | 109,879,593,000 | 58,287,166,000 |
| 2024/25 | 125,366,390,974 | 125,524,892,027 | 18,074,661,000 | 79,166,675,000 |
| Pungufu | 58,922,105,026 | 176,688,060,973 | 91,804,932,000 | 20,879,509,000 |
| Asilimia - % | -32 | -58.46 | -83.55 | 35.82 |

***Chanzo**: Randamba ya Wizara 2024 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umeonyesha kuwa:-

i. Makadirio ya matumizi ya Wizara hii yamepungua kwa **Shilingi 344,958,242,000.00** sawa na **asilimia 46.8** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024;

ii. Fedha za mishahara zimepungua kwa **Shilingi 58,922,105,026.00** sawa na **asilimia 32** ilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024;

iii. Fedha za matumizi ya mengineyo yaani (OC) zimepungua kwa **Shilingi 176,688,060,973.00** sawa na **asilimia 58.46** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024;

iv. Fedha za miradi ya maendeleo zimepungua kwa **Shilingi 66,144,017,000.00** sawa na **asilimia 41.55** ikilinganishwa na mwaka 2023/2024. Fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo zimepungua kwa **asilimia 83.55** huku fedha za nje zikiongezeka kwa **asilimia 35.82.** Hali hii ni kiunyume na ushauri wa Kamati uliotolewa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 wa kuitaka Serikali kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo hayo ya uchambuzi yanatokana na uamuzi wa Serikali kuzingatia ushauri uliokuwa ukitolewa Bungeni juu ya kuziruhusu Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kuanza kubaki na makusanyo yake.

**3.3 Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya maliasili na utalii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi, hivyo ulinganisho wa bajeti ya Wizara hii dhidi ya bajeti ya Taifa ni jambo linalosaidia kuweka msingi wa ushauri kuhusu sekta husika. Kwa kuzingatia hilo, sehemu hii inatathmini mambo yafuatayo:-

i. Uwiano wa bajeti ya Wizara kwa bajeti ya Taifa; na

ii. Ulinganisho wa hali ya uwiano kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na hali hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taswira ya ulinganisho huo unaonekana katika **Kielelezo Namba 5.**

**Kielelezo Na: 5 Bajeti ya Wizara (Fungu 69) dhidi ya Bajeti ya Taifa**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2023/2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI YA MALIASILI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,578,433,000,000 | 302,212,953,000 | 5.42 |
| **MISHAHARA** | 10,882,126,000,000 | 184,288,496,000 | 1.70 |
| **MAENDELEO NDANI** | 11,873,900,000,000 | 109,879,593,000 | 0.93 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,282,100,000,000 | 58,287,166,000 | 1.8 |
| **DENI LA SERIKALI** | 12,771,500,000,000 | - | - |
| **JUMLA** | **44,388,059,000,000** | **654,668,208,000** | **1.50** |
| **BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2024/2025** | | | |
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI YA MALIASILI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,822,535,000,000 | 125,524,892,027 | 2.12 |
| **MISHAHARA** | 11,997,752,000,000 | 125,366,390,974 | 1.05 |
| **MAENDELEO NDANI** | 12,148,283,000,000 | 18,074,661,000 | 0.15 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,640,838,000,000 | 79,166,675,000 | 2.17 |
| **DENI LA SERIKALI** | 15,736,280,000,000 | - | - |
| **JUMLA** | **49,345,688,000,000** | **348,125,419,000** | **0.705** |

*Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Mfumo na Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/2024 na 2024/2025, Randama ya Wizara ya Maliasili na Utalii 2023/2024 na 2024/2025*

**Mheshimiwa Spika,** kwa tathmini hiyo, uchambuzi umeonyesha mambo yafuatayo:-

i. Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii dhidi ya Bajeti ya Taifa imepungua kutoka **asilimia 1.50** hadi **asilimia 0.75;**
ii. Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeshuka kutoka **asilimia 5.42** hadi **asilimia 2.12**;
iii. Bajeti ya mishahara imepungua kutoka **asilimia 1.70** hadi kufikia **asilimia 1.05**;
iv. Bajeti ya Maendeleo kutokana na fedha za ndani imepungua kutoka **asilimia 0.93** hadi **asilimia 0.15**; na
v. Bajeti ya maendeleo kutokana na fedha za nje imeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka **asilimia 1.80** hadi **asilimia 2.17**, hali inaonyesha kutakuwa na ongezeko la utegemezi wa fedha za maendeleo kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** kupungua kwa viashiria vya kibajeti katika mwaka wa fedha 2024/2025 ukilinganisha na ile ya mwaka 2023/2024 kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 5** imetokana na taasisi za TANAPA na NCAA kuanza kujitegemea katika makusanyo na matumizi, hivyo kufanya bajeti zake kuwa si sehemu ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

### 3.4 Mambo muhimu yanayogusa sekta ya Maliasili na Utalii.

i. Changamoto ya Wanyamapori wakali na Waharibifu

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni ni miongoni mwa nchi zenye sera nzuri za Uhifadhi ikiwa imetenga takribani **asilimia 32.5** ya ardhi yake kwa ajili ya uhifadhi wa rasilimali za maliasili mbalimbali ikiwemo wanyamapori na misitu. Hata hivyo, pamoja na sera hizo, Tanzania imeshuhudia migogoro kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini sababu mbalimbali zinazochangia migogoro hiyo hali ambayo imegeuka kuwa changamoto kubwa inayoikabili sekta ya Maliasili na Utalii nchini. Sababu hizo ni pamoja na ongezeko la watu na uanzishwaji wa shughuli za kibinadamu karibu na maeneo yaliyohifadhiwa na

kwenye shoroba za wanyamapori, kukosekana au kutokuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vinavyopakana na maeneo yanayotumiwa na wanyamapori, mabadiliko ya tabia nchi, ongezeko la mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa na ongezekeo la wanyamapori.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) 184 nchini, takribani halmashauri 91 zinakabaliwa na changamoto hii ikiwa ni sawa na **asilimia 49.5** ya halmashauri zote nchini. Hata hivyo, miongoni mwake, halmashauri 44 zimeonekana kukumbwa na changamoto kwa kiasi kikubwa zaidi ukilinganisha na nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** athari zinazotokana na migongano ya binadamu na wanyamapori ni pamoja na uharibifu mkubwa wa mazao, mifugo kujeruhiwa na kuuawa, binadamu kujeruhiwa na kuuwawa na uharibifu wa miundombinu kama vile barabara, nguzo za umeme na miundombinu ya maji. Wanyama wanaoleta changamoto kubwa ni pamoja na tembo, mamba, viboko, nyumbu, ngedere na nyani. Hali hii inaongeza kiwango cha umaskini miongoni mwa wananchi wanaokabiliana na changamoto hii hivyo kuzorotesha ustawi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto hiyo. Pamoja hatua hizo, bado changamoto hii ni kubwa kwa hiyo, Kamati inaitaka Serikali kuongeza juhudi zaidi na kuhakikisha inatekeleza mipango iliyojiwekea kwa wakati katika kukabiliana na tatizo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwingine Serikali imekuwa ikitoa kifuta machozi na kifuta jasho kwa wananchi walioathirika na matukio ya wanyapori wakali na waharibifu kwa mujibu wa Kanuni ya kifuta machozi na kifuta jasho za mwaka 2011. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi 1,580,783,750.00** zimelipwa kwa wananchi **6,551** walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu. Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko miongoni mwa wananchi waliothirika kuwa kiwango kinachotolewa ni kidogo na hakitolewi kwa wakati. Taarifa zaidi za Wizara zinaonesha kuwa,

Kuanzia Aprili hadi Mei, 2024 Wizara ilikuwa na mpango wa malipo ya **Shilingi 1,621,426,000.00** kwa wananchi **9008** katika Halmashauri za Wilaya 14.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara iliijulisha Kamati kuwa, Kanuni za kufuta machozi zinafanyiwa marekebisho na tayari Wizara ya Fedha imetoa kibali kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea na mchakato huu. Ni matumaini ya Kamati kuwa, Serikali itaharakisha mchakato huu ili kuongeza kiwango sambamba na kuboresha utaratibu ili Kifuta jasho kitolewe kwa wakati.

**ii. Changamoto ya Migogoro baina ya Askari wa Uhifadhi na Wananchi**

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ufanisi na tija katika za uhifadhi wa maliasili nchini, mwaka 2019 Serikali iliamua kuunda jeshi usu ambalo limekuwa na matokeo mazuri katika uhifadhi. Kamati inatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na askari wa uhifadhi nchini kwani wamesaidia katika kukabaliana na kudhibiti matukio ya ujangili wa wanyamapori na kuzuia uvamizi wa maeneo ya hifadhi. Hatua hii imesaidia katika kuongeza idadi ya wanyapori na misitu ikiwa ni pamoja na Serikali kunufaika na biashara ya utalii, uwindaji wa kitalii, hewa ukaa (carbon trading), kulinda vyanzo vya maji na kusababisha biashara endelevu ya mazao ya misitu na nyuki. Hali hii imechangia Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea kuongeza manufaa katika kuchangia pato la Taifa, kukuza uchumi, kuongeza pato la kigeni na kutoa ajira katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, katika maeneo yanayopakana na hifadhi nchini kumekuwa na baadhi ya matukio ya migogoro baina ya askari wa hifadhi na wananchi. Migogoro hiyo imezaa uhasama ambao umesababisha matukio ya kushambuliana na kusababisha ulemavu na wakati mwingine vifo baina yao.

**Mheshimiwa Spika,** pia kumekuwa na malalamiko ya wananchi kukamatwa, kuteswa na kubambikiwa kesi na baadhi ya askari wa uhifadhi hali inayoongeza uhasama baina yao. Mathalani,

katika moja ya matukio ambayo mahakama imethibitisha mwananchi kubambikiwa kesi na askari wa uhifadhi, ni lile la mwananchi aitwae Richard Changei Ng'ombe mkazi wa Wilaya ya Serengeti ambae alikamatwa siku ya tarehe 12 Agosti, 2022 majira ya saa 12:00 jioni na askari watano.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya mtuhumiwa huyo kufikishwa mahakamani, mahakama ilipitia ushahidi wa vielelezo mbalimbali vilivyowasilishwa mahakamani ikiwa ni pamoja na point za dira (cordinates) na nyara ambazo walidai wamemkamata nazo mtuhumiwa. Ushahidi wa askari ulitofautiana na kuonesha mtuhumiwa alibambikiwa kesi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hukumu ya kesi hiyo ambayo ni ''**Criminal Appeal No. 40809 of 2023'',** iliyosomwa tarehe 24 Aprili, 2024, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Musoma, Mhe. Kamazima Idd Kafanabo wakati anamuachia huru mtuhumiwa Richard Changei Ng'ombe alitoa onyo kwa kusema .''Mahakama haiwezi kufumbia macho jambo hili linaonekana kuzoeleka na kujirudia la kutofuata maadili ya kazi kunakofanywa na maofisa wengi wa uhifadhi na wengine katika haki jinai, hasa katika ukamataji wa watuhumiwa na uchukuaji wa vielelezo''.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini, sio tu malalamiko ya watu kubambikwa kesi, bali kumekuwa na matukio ya wananchi kulalamikia kutaifishwa kwa mifugo yao kinyume na utaratibu. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inafanya uchunguzi na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria baadhi ya askari wanaokiuka maadili ya kazi yao na kutenda kinyume na sheria. Pia, Wizara ianze mchakato wa kuboresha mtaala wa jeshi usu utakaosaidia kuboresha utendaji wa jeshi hilo.

iii. Changamoto ya Ufinyu wa Bajeti na Rasilimaliwatu kwa Taasisi za TAFORI na TAWIRI

**Mheshimiwa Spika,** taasisi za TAFORI na TAWIRI ndio muhimili wa sekta za uhifadhi na utalii katika Taifa letu. Taasisi hizi zinafanya tafiti katika maeneo mahsusi yanayohusu Misitu (TAFORI) na Wanyamapori (TAWIRI) na kutoa taarifa zinazoisaidia Wizara na

taasisi zilizochini ya Wizara kufanya maamuzi sahihi yanayolenga kuboresha na kuleta tija katika sekta hizi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wake katika sekta za Maliasili na Utalii, taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti na rasilimaliwatu hali inayochangia taasisi hizi kuwa na madeni, uchakavu wa miundombinu ya majengo na kukosa vifaa vya kisasa vya kufanyia tafiti. Kwa mfano, taaisi ya TAFORI ina upungufu wa wafanyakazi kwa zaidi ya **asilimia 55%** huku ikidaiwa jumla ya **Shilingi 1,390,919,622.00** ambazo zimetokana na gharama za watoa huduma, wakaguzi wa mahesabu, ada za wajumbe wa bodi, uhamisho na stahiki za watumishi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa taasisi ya TAWIRI, changamoto kubwa ni ufinyu wa bajeti ambayo imesababisha uchakavu wa miundombu ya nyumba za watumishi, uhaba wa vifaa vya kisasa vya kufanyia tafiti na kukosa fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 4** za kufanya sensa ya wanyapori katika mifumo ya ikolojia kumi na moja **(11)** iliyopo nchini. Aidha, taasisi hii iliyoanzishwa mwaka 1985 na kuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi wa rasimali za wanyamapori hadi sasa haina jengo la Ofisi za Makao Makuu.

iv. Ucheleweshaji wa Fedha za Jumuiya za Wanyamapori (WMAs')

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maliasili na Utalii inatekeleza dhana ya ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi kwa kuanzisha maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMA). Jumuiya hizi zinanufaika na moja kwa moja na rasilimali za Wanyamapori kupitia uwekezaji kwenye shughuli za Utalii. Aidha, fedha zinazopatikana katika maeneo hayo hugawanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 27 (o) na 72 ya Kanuni za WMA za mwaka 2018. Kabla ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020, suala la kukusanya na kugawa fedha za WMA lilikuwa chini ya Wizara kupitia TAWA. Baada ya mabadiliko hayo ya Sheria, jukumu la kukusanya fedha za wanufaika linatekelezwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kisha kuhifadhiwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo kumekuwa na ucheleweshaji wa mgao wa fedha za wanufaika kuwafikia kwa wakati. Kuchelewa kwa mgao wa fedha za WMAs kunasababisha kukosekana kwa fedha za uendeshaji wa ofisi, ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, na kudhoofisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo vijijini. Hali hii inahatarisha ustawi wa uhifadhi katika maeneo ya Jumuiya hizi ambapo vitendo vya ujangili wa wanyama vinaongezeka na kushindwa kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Januari, 2024, jumla ya madai ya fedha za wanufaika (WMAs 13, Vijiji 50, Halmashauri za Wilaya 29) zilizowasilishwa Wizara ya Fedha ni **Shilingi 8,010,647,911.58.** Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2024, Serikali ilikuwa imelipa **Shilingi 1,437,223,351.87** tu ikiwa ni mgao wa mwezi Julai, 2023. Ni muhimu kukumbuka kuwa, WMA siyo hifadhi ya Taifa na Wala siyo muendelezo wa hifadhi za Taifa.

v. Upungufu wa Huduma za Malazi ya Watalii Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina huduma za malazi takribani **10,432.** Miongoni mwa huduma hizo za malazi huduma **1,437** sawa na **asilimia 13.8** zina hadhi ya juu ya kulala wageni. Huduma za malazi zilizopo katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii ni **261** kati ya huduma za malazi **1,437**. Huduma za malazi **8,995** sawa na **asilimia 86.2** ni nyumba za kulala wageni yaani guest houses ambazo zina huduma za chini.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kupitia mpango wa ubinafsishaji nchini, Serikali ilifanya uamuzi wa kubinafsisha Hotel na Loji 23, ambapo kati ya hizo, Loji 4 zipo ndani ya Hifadhi. Loji hizo ni Seronera na Lobo (Hifadhi ya Serengeti), Mikumi Wildlife Lodge (Mikumi) na Ngorongoro Wildlife Lodge (Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro).

**Mheshimiwa Spika,** Hoteli 10 zimewekezwa kulingana na masharti ya Mikataba ya mauziano. Loji na Hotel 6 uwekezaji uliofanyika haulingani na matakwa ya Mikataba ya Mauziano ambapo

wawekezaji wametekeleza chini ya viwango vilivyokubalika na Hotel 7 zipo kwenye hatua mbalimbali za ukarabati.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia ongezeko la idadi wa watalii wanaoingia nchini na hali ya huduma ya malazi iliyooneshwa hapo juu, Kamati inaitaka Serikali kuzirudisha hoteli ambazo wawekezaji wake wamekiuka mikataba ya uwekezaji. Aidha, Serikali iweke mazingira rafiki ya utekelezaji ya mwongozo wa uwekezaji katika sekta ya utalii pamoja na kutumia fursa za matukio ya utangazaji wa utalii kutangaza na kuvutia uwekezaji katika huduma za malazi hususani ujenzi wa hoteli zenye hadhi ya kati na ya juu katika maeneo yanayosimamiwa na Wizara.

vi. Maboresho katika Mpango na Makadirio Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Maliasili na Utalii ilikabiliana na changamoto mbalimbali. Moja ya changamoto hizo ni ufinyu wa bajeti kama ilivyoripotiwa katika ukurasa wa **70** wa Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** katika kikao cha kupitisha Bajeti ya Wizara katika ngazi ya Kamati siku ya Ijumaa tarehe 22 Machi, 2024, Kamati ilipata nafasi ya kushauriana na Wizara hivyo kwa pamoja kubeba ajenda ya nyongeza ya ukomo wa bajeti kwenda kwenye kikao cha mashauriano na Serikali kuhusu ongezeko la bajeti ya Wizara hii. Tarehe 06 Mei, 2024, Kamati ilipokea taarifa ya Serikali kupitia kwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu maboresho ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 katika maeneo mawili (02) ambayo ni; utaratibu mpya wa makusanyo na matumizi kwa Taasisi za TANAPA na NCAA na ongezeko la ukomo wa bajeti kwa Wizara ya Maliasili na Utalii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa maeneo hayo kama ifuatavyo:-

**a) Utaratibu Mpya wa Makusanyo na Matumizi kwa Taasisi za TANAPA na NCAA**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kikao cha Kamati na Wizara tarehe 06 Mei, 2024, Kamati ilitaarifiwa kwamba Serikali imeridhia ushauri wa muda mrefu wa Bunge lako Tukufu kuruhusu taasisi za Uhifadhi za TANAPA na NCAA kukusanya na kutumia mapato yao. Kutokana na uamuzi huo Kamati ilitarifiwa kuwa makadirio ya matumizi ya TANAPA yameongezeka kwa **Shilingi 70,879,823,326.53** kutoka **shilingi 263,901,922,507.00** hadi **Shilingi 334,781,745,833.53** na kwa upande wa NCAA makadirio ya matumizi yameongezeka kwa Shilingi **27,910,355,827.00** kutoka **Shilingi 118,689,644,193.00** hadi **Shilingi 146,600,000,000.00** Uamuzi huo utakuwa na manufaa yafuatayo:-

i. kuziwezesha taasisi hizo kujiendesha kwa ufanisi na kuongeza kasi ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika hifadhi; ii. utaimarisha mchango wa sekta ya utalii katika uchumi na kuimarisha ustawi wa Taifa; iii. kuwa na uhakika wa fedha za kutangaza utalii kupitia Tozo ya Maendeleo ya Utalii nchini NCAA kwa kutenga **asilimia 6** ya mapato ghafi kama tozo ya maendeleo ya utalii, (Tourism Development Levy).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwani kwa uamuzi huo ni wazi kuwa Serikali inaheshimu ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inalipa Bunge Mamlaka ya Kuisimamia na Kuishauri Serikali. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuweka usimamizi madhubuti katika matumizi ya fedha za umma kwenye taasisi hizi ili kuzuia matumizi mabaya na ubadhirifu katika fedha za umma.

**b) Ongezeko la Bajeti kwa Wizara ya Maliasili na Utalii**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea taarifa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii (Fungu 69) limeongezewa bajeti kwa kiasi cha **Shilingi 19,000,000,000.00** ili kupunguza baadhi ya changamoto zinazosababishwa na ufinyu wa bajeti. Katika fedha hizo, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara imepanga kutumia **Shilingi bilioni 14** sawa na **asilimia 74** ya nyongeza katika matumizi mengineyo na **Shilingi bilioni 5** sawa na **asilima 26** kwa ajili ya matumizi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na mgawanyo wa nyongeza hiyo kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni baadhi ya Taasisi za Wizara kutokuwa na Ofisi, mzigo wa madeni, uchakavu wa miundombinu na wananchi kuvamiwa na wanyamawakali na waharibifu. Hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba ongezeko hili halitakuwa na tija kwa Wizara kwa sababu haliendi kushughulikia changamoto za msingi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Taasisi zimeruhusiwa kukusanya asilimia 6 na kuitumia kwenye utangazaji wa Utalii bado shilingi bilioni 1 imeongezeka kwenye Idara ya Utalii kwenye utangazaji wa Utalii, safari za nje, kubaini vivutio na mazao mapya ya utalii, utafiti kuhusu utalii na grading. Kazi hizi ni kazi za Msingi za Bodi ya Utalii na Sio Wizara. Hata hivyo, Idara hiyo katika bajeti ya awali ilikuwa imetengewa kiasi cha **Shilingi 2,553,813,000.00** kama OC kiasi ambacho kwa maoni ya Kamati kinatosha kufanya shughuli hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika nyongeza hiyo **Shilingi Bilioni 2** zimeelekezwa katika ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA ujulikanao kama Tanzania Safari Booking Platform. Kamati ya imebaini kwamba fedha hizo zimetengwa kutekeleza mradi ambao hauna andiko la awali *(Concept Note)* wala gharama halisi za mradi. Pamoja na manufaa yanayotarajiwa ya mfumo huo maandalizi ya utekelezaji hayajafanyika na hivyo fedha hizi zinaweza kutumika vibaya.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia kituo cha Kutangaza Utalii Kiditali **(DDMCC)** ambacho Kamati ilikitembelea, kuna sehemu ya mfumo wa kufanya miadi (booking) na kuwaunganisha watalii kutoka nje ya nchi na huduma za hoteli na usafiri ijulikanayo kama Travel Companion. Kwa hiyo kujenga mfumo kama huo ndani ya Wizara hiyo ni matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati ya kutokubaliana na matumizi ya nyongeza, Serikali ilipewa siku 15 ili kufanya Mabadiliko. Serikali ilikubaliana na Kamati na kuahaidi kwenda

kushughulikia jambo hilo kwa kuzingatia ushauri wa Kamati. Jambo la kusikitisha kikao kilichofanyika tarehe 21 Mei, 2024 hadi tarehe 21 Mei, 2024 ili kupokea utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati, Kamati ilitaarifiwa kwamba mabadiliko hayawezi kufanyika kwa sababu vitabu vimefungwa jambo ambalo si sahihi. Mchakato wa ufungaji wa Vitabu vya Bajeti unafanyika Baada ya kupitisha Sheria ya Matumizi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo; -

### 4.1 Maoni ya Jumla

(a) Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili utekelezaji wa miradi hiyo ufanyike kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa;

(b) Serikali iendelee kupunguza utegemezi wa fedha za nje kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwani upatikanaji wake siyo wa uhakika, jambo linaloweza kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo; na

(c) Serikali isimamie kikamilifu utendaji wa taasisi ambazo zinakusanya maduhuli kupitia mfumo wa *MNRT - Portal* na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ili kuhakikisha zinaongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kwa ufanisi.

### 4.2 Maoni mahsusi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii

**(a) Changamoto ya migogoro ya mipaka katika maeneo ya hifadhi na vijiji vinavyozunguka hifadhi**.

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i. Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara nyingine za Kisekta ili iweze kupima na kufanya utambuzi wa mipaka hali itakayoondoa migogoro kati ya hifadhi na wananchi wanaoishi kuzunguka maeneo ya hifadhi ;

ii. Iweke alama zinazoonekana katika mipaka ya hifadhi na ile ya ardhi za vijiji vinavyozunguka hifadhi ili kupunguza na

kuondoa migogoro ya ardhi baina ya hifadhi na wananchi; na

iii. Ihakikishe panakuwa na ushirikishwaji wa Wizara za kisekta,Taasisi nyingine za Serikali na Wananchi wakati wa uwekaji wa alama za mipaka, uanzishwaji wa hifadhi au uanzishwaji wa vijiji.

**(b) Changamoto ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu**

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i. Ichukue hatua stahiki za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazosababishwa na muingiliano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu;
ii. Ishirikiane na Wizara ya nyingine za Kisekta kuongoa shoroba za wanyamapori kupitia zoezi la kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi; na
iii. Iboreshe Kanuni na viwango vya fidia ya kifuta machozi kwa wananchi kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyama ili vizingatie hali halisi ya maisha na thamani ya uharibifu au madhara yaliyotokea.

**(c) Changamoto ya Migogoro baina ya Askari wa Hifadhi na Wananchi**

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i. Iendelee kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka hifadhi ikiwa ni pamoja na askari wa hifadhi ili kuboresha mahusiano baina yao; ii. Ihakikishe inawachukulia hatua za kisheria na kutoa taarifa kwa wananchi na wawakilishi wao juu ya hatua zilizochukuliwa kwa askari wa uhifadhi ambao watabainika wanashiriki katika vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wananchi wanaozunguka hifadhi. Hali hii itaongeza uwajibikaji kwa askari wa hifadhi na kuondoa dhana kwa jamii kudhani kuwa askari wa hifadhi wanalindwa naSerikali hata katika makosa ya wazi; iii. Iweke utaratibu wa kufidia hasara inayotokana na kubainika kwa vitendo vya baadhi ya askari wa uhifadhi kuharibu

mali za wananchi kama mifugo na mazao; iv. Itekeleze mpango wa kurejesha kwa jamii (CSR), kwa jamii zinazozunguka Hifadhi ili kuhakikisha jamii hizo zinanufaika na shughuli za uhifadhi na utalii zinazotekelezwa katika hifadhi mbalimbali nchini ; na

**(d) Changamoto ya Vitendea kazi na Rasilimaliwatu kwa Taasisi za TAFORI na TAWIRI**

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i. Iandae mpango mkakati wa ajira za muda mfupi, kati na mrefu ili kupunguza na kuziba pengo la watumishi katika taasisi hizi muhimu kwa maendeleo ya sekta za Uhifadhi na Utalii; na
ii. Iweke mkakati utakaoiwezesha TAWIRI kufanya sensa ya Wanyamapori katika Mifumo kumi na moja (11) ya ikolojia nchini.

**(e) Changamoto ya Ucheleweshaji wa Fedha za Jumuiya za Wanyapori (WMAs')**

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i. Irejeshe fedha za WMAs zinazodaiwa na Jumuiya hizo kwa mujibu wa kanuni ili kusaidia ufanisi katika kutekeleza majukumu yao ya Uhifadhi na Utalii; na
ii. Ifanye marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 ili kuruhusu fedha zinazotokana na shughuli ndani ya WMAs kulipwa moja kwa moja kwenye WMAs.

**(f) Changamoto ya Uhaba wa Huduma ya Malazi ya Watalii**

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i. Ichukue hatua za haraka kurudisha hoteli na loji toka kwa wamiliki waliobinafsishiwa hoteli na Loji za Serikali ambao wamekiuka masharti ya mikataba yao ya kuziboresha hali itakayopunguza uhaba wa huduma ya malazi ya watalii na kuleta tija iliyokusudiwa; na
ii. Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwenye kutangaza fursa za uwekezaji wa huduma

za malazi katika maeneo yanayomilikiwa na Wizara na sehemu zilizokaribu na vivutio vya utalii nchini.

**(g) Utangazaji wa Vivutio vya Utalii**

Kamati inaishauri Serikali kuwa:-

i. Iandae na kutekeleza kikamilifu mikakati madhubuti ya kutambua na kutangaza vivutio vingine vya utalii kama ilivyo kwenye utalii wa wanyamapori ili kuongeza wigo wa mapato yatokanayo na utalii; na
ii. Ihakikishe inatenga bajeti ya kutosha kwa ajili Kituo cha Kutangaza Utalii Kidijitali **(DDMCC)** ili kiweze kufanya kazi kama ilivyotarajiwa na kuleta tija iliyokusudiwa; na
iii. Ishirikishe sekta binafsi na wadau wengine wa sekta ya utalii katika kuibua na kutangaza vivutio vipya vya utalii ili kuvutia watalii wengi zaidi.

**(h) Mpango na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijakubaliana na Matumizi ya Shilingi Shilingi bilioni 16 kati ya bilioni 19 zilizoongezeka. Sababu za kutokubaliana na matumizi hayo ni kama nilivyozibainisha awali. Kamati inapendekeza ongezeko hilo lielekezwe katika maeneo yafuatayo:-

i. Ujenzi wa Makao Makuu ya Ofisi ya TAWIRI;
ii. Ukarabati wa miundombinu ya ujenzi na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika vyuo vya FTI Moshi, Olmotonyi Arusha na Pasiansi Mwanza;
iii. Kushughulikia changamoto ya wanyama wakali na waharibifu ikiwa ni pamoja na kuongeza vizimba vya mamba na viboko kwa kuzingatia kanda zenye changamoto kubwa, ujenzi wa vituo vya askari wa wanyamapori na ongezeko la fedha kwenda TAWA ili kuongeza idadi ya mabwawa katika mapori tengefu;
iv. Kwenda TAFORI kwa ajili ya kusaidia kulipa madeni na

kushughulikia uchakavu wa vifaa na miundombinu ya ujenzi; na
Kiasi kingine cha Fedha hizo kielekezwe kwenye matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekusudia kuleta addendum ya mabadiliko ya Fungu 69 kuhusu matumizi ya Fungu hili wakati wa kupitisha vifungu. Na endapo itakupendeza, Kamati inaomba jambo hili ulielekeze Kamati ya Bajeti lishughulikiwe kwa Mujibu wa kanuni ya 124 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023.

**(i) Kufanya Mabadiliko kupitia sheria ya Fedha ya Mwaka 2024 kurejesha utaratibu wa ukusanyaji wa mapato na kuyatumia**

i. Serikali ifute marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2020 yaliyofanyika kwenye Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura 284 ili kurejesha utaratibu ambao Kamati ilitaarifiwa umekwishakubaliwa na Serikali; na

ii. Kuweka masharti maalumu yatakayotaka Bajeti za Taasisi hizo kuchambuliwa na kuidhinishwa na Wizara ya Fedha pamoja na Msajili wa Hazina kabla ya kila mwaka wa fedha kuanza ili kuzuia ubadhirifu wa fedha za umma unaoweza kujitokeza kwa taasisi hizo.

## SEHEMU YA TANO

### 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa weledi mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi

chote cha ziara za ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha na uchambuzi wa bajeti ya wizara hii hadi kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wake, ningependa kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Muntazar Giga, Mb – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Shaabani Omar Shekilindi, Mb
4. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb
5. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb
6. Mhe. Ester Lukago Midimu, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
9. Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb
10. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
11. Mhe. Alaudin Hasham Salim, Mb
12. Mhe.Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mb
13. Mhe. Festo Richard Sanga , Mb
14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
16. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
17. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
19. Mhe. Ask. Dkt Josephat Mathias Gwajima, Mb
20. Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb
21. Mhe. Dkt. Florence G. Samizi, Mb
22. Mhe. Asha Abdullah Juma, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Angela Jasmin Kairuki (Mb) na Naibu Waziri, Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi hasa katika sekta hii. Aidha, nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Katibu Mkuu, Dkt.

Hassan Abbasi, pamoja na Naibu Katibu Mkuu, CP Benedict Wakulyamba, kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, kwa namna ya pekee nawashukuru watumishi wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (ndc), kwa kuongoza vyema uratibu wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii na kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii pamoja na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii **(Fungu 69),** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

Timotheo Paul Mnzava, Mb
MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

31 Mei, 2024

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, anaenda mbali sana huyo. *(Makofi/Kicheko)*

Haya, ahsanteni sana, ameamua kukaa njiani, ahsante sana, Mwenyekiti ahsante sana kwa kuwasilisha Maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada tutaanza na uchangiaji wa Wabunge ambao wameomba kuchangia, lakini sasa Wizara hii ina waombaji wengi, maombi ni mengi. Kwa hiyo, ili kila mmoja aliyeomba kuchangia Wizara hii aweze kupata nafasi, Waheshimiwa Wabunge mtachangia kwa dakika nane ili kutoa fursa kwa Wabunge wote kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine orodha inavyoletwa hapa mbele mnakuwa mmenakili ama mmekariri ile namba inayoletwa hapa mbele, halafu akiitwa Mbunge mwingine unaona mimi nimerukwa, unaanza kumtafuta Mwenyekiti ama Spika hapa mbele. Ni kwamba hapa mbele pia huwa kuna maombi, ukiacha jina lako halitaachwa utaitwa, lakini mpangilio ule unaweza kubadilika kwa sababu ya watu wanakuwa wameomba kuchangia wana dharura, wengine wanaenda kwenye Kamati zetu za Bunge ambazo zinaendelea kufanya kazi sasa. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi; maadamu jina limekuja hapa mbele utapata fursa ya kuchangia. *(Makofi)*

Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia na ninakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii na hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote, kwa hotuba nzuri ya bajeti waliyoitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii nii Wizara muhimu sana kwa sababu ndiyo inayosimamia rasilimali za nchi yetu ambazo zina thamani kubwa isiyomithilika na ndiyo sura ya nchi yetu, ndiyo hifadhi ya nchi yetu, ndiyo hazina ya nchi yetu. Kwa hiyo, ni Wizara muhimu sana na mimi ninaanza kabisa kwa kuunga mkono hoja na kuomba Wizara hii iongezewe fedha ili iweze kuyafanya mambo hayo kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia mambo matatu; la kwanza ni kuhusu mazungumzo kuhusu madhila yanayotokana na ukoloni wa Wajerumani na kurejeshwa kwa malikale na mali za kitamaduni ambazo ziko Ujerumani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninaomba kuanza na tanbihi au indhari *(caution)*. Mazungumzo ambayo yameanza ningetoa indhari kwamba inaonekana sasa wenzetu wa Ujerumani badala ya kujua kwamba sisi ni Taifa, wameanza wao moja kwa moja kwenda kwenye jamii hizo, moja kwa moja kwenda kwenye makabila hayo na kusahau kwamba sisi leo siyo mkusanyiko wa makabila ambayo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo.

Maafisa ambao hamjatangazwa bado, subiri mtangazwe halafu mtatoka. Watoke wale ambao wameshatangazwa, wale ambao bado kutanganzwa mtulie kidogo hapo mtatoka mkishatangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, hilo ni muhimu sana kwa sababu kuna kila dalili sasa kuonekana kwamba ni maeneo fulani tu ndiyo yaliyopata madhila ya ukoloni wa Kijerumani, wakati ni nchi nzima na maeneo yote yalipata madhila ya kikoloni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina muda wa kusema kwa sababu leo nimekuja na kitabu ambacho ningependa watu wakisome waone kwamba Tanzania nzima ya leo iliathirika na ukoloni wa Kijerumani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba jambo hili liratibiwe, lisimamiwe na liongozwe na Serikali yenyewe, kwa sababu yako mambo ya msingi Serikali ya Ujerumani lazima ikiri na iwajibike kwa mambo mabaya yaliyofanyika na isitake tena kuturudisha kwenye mikataba kama ya Mangungo ya kwenda kwenye familia moja moja na jamii moja moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni utajiri na utalii wa lugha, niliizungumzia kwenye bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na ninaomba tena kulileta hapa.

Mheshimiwa Spika, tuna utajiri mkubwa wa lugha ambao tunaweza pia kuutumia kama utalii, Tanzania ndiyo nchi pekee katika Bara la Afrika na duniani kote ambayo makundi yote makuu ya lugha yapo hapa. Ninaomba makundi haya makuu ya lugha yaifanye Tanzania kupeleka maombi *UNESCO* ili Tanzania iorodheshwe katika urithi wa Kimataifa yenye makundi hayo ya lugha, yaani Wabantu, Wakushi, Wakhoisani na Waniloti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa Wakhoisani ndiyo hawa Wasandawe na Wahadzabe, lakini pia wale wanaozungumza Lugha ya *Afro-Asiatic* yaani Wairaqw na Wambulu. Hili ni jambo muhimu sana, ni kitu cha pekee na adhimu na tutumie nafasi hii, siyo tu kuzitangaza lugha hizi, makundi haya makuu manne ya lugha pamoja na *Afro-Asiatic* kuwa urithi wa Kimataifa, lakini tuwekeze katika kutunza lugha hizi za asili kwa sababu zinabeba maarifa, zinabeba hazina kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru sana wale wote ambao wamefanya utafiti kuhusu lugha hizi na tukifanya hivyo haturejeshi ukabila, bali tunatunza utajiri wetu mkubwa na anuai kubwa tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa maeneo ya malikale na uendelezaji wa utalii wa kihstoria.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara kwa kupanua wigo wa utalii kutoka kwenye utalii wa wanyama tu, sasa kwenda kwenye utalii wa maeneo mbalimbali. Iwe ni utamaduni, iwe ni mila, iwe ni desturi, iwe ni vyakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nianze kwa ule utalii wa hifadhi; Hifadhi ya Kitulo tuipe kipaumbele ya juu sana kuitangaza kama Kitulo na ninaiomba Wizara tusipeleke wanyama katika hifadhi hiyo. Watu hawaji kuona tu pundamilia na swala, watu wanakuja kuona maua ya asili. Ile ndiyo hifadhi ya aina ya peke yake duniani. Sasa kwa sababu hifadhi ile imeanza kukabiliwa na matatizo ya ukame, tutafute njia ya kuwa na *sprinklers* za

kumwagilia maji ili mwaka mzima yawepo na yale maua yaliyokauka yavunwe, yahifadhiwe na yauzwe nje kama maua pekee yanayotoka kwenye Bustani ya Mungu iliyoko Kitulo na tuepuke sana kudhani utalii ni wanyama tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninachukua nafasi hii kukupongeza sana kwa jambo ambalo umelifanya ambalo limeongeza Utalii wa Ndani, haya matamasha ya ngoma za kienyeji. Sasa, sijui Tamasha hilo ni *Tulia Traditional Dances* au kama ni *Dr. Tulia Traditional Dances* na katika tamasha hili, marathoni imenishinda lakini tamasha hili kwa sababu ambazo wewe unazifahamu siwezi kulikosa, lakini hii iwe kwa nchi nzima. Tuwe na matamasha ya aina hiyo ya utamaduni wetu na iwe ni sehemu ya kuendeleza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Makumbusho ya Taifa na Idara ya Mali ya Kale iongezewe fedha ya kutosha ili kufanya utafiti na kuhakikisha maeneo haya yanahifadhiwa ili yawe sehemu ya urithi wa Taifa, sehemu ya urithi wa Kimataifa, lakini pia sehemu ya utalii.

Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara kwa kutoa fedha katika bajeti ya maendeleo ya kuanza kujenga Nyumba ya Makumbusho ya Marais na hii ingefuatiwa na Jumba la Makumbusho mengine hapa Dodoma, lakini kila mkoa sasa ufikirie kuwa na nyumba ya makumbusho ambayo itatunza maeneo na utamaduni na mila na desturi za aina ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona katika nchi za wenzetu, ukifika tu unakwenda kwenye makumbusho. Mji wa Addis Ababa peke yake Ethiopia, sitaki kuzungumzia Ulaya, Mji wa Addis Ababa una zaidi ya makumbusho 12 na ukifika pale utaona utamaduni wote wa Addis Ababa na sehemu ya mwisho ambayo watakupeleka kwenda kuiona ni Kanisa Kuu Utatu Mtakatifu, Addis Ababa ambako wamezikwa wafalme wote ikiwa ni pamoja na Haile Selassie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi pia maeneo hayo tungeyatambua, tungeyabainisha ili tuyahifadhi, ikiwa ni pamoja na Ikulu ya

Chamwino, ikiwa ni pamoja na majengo mbalimbali hapa Dodoma, Boma la Dodoma lakini pia ikiwa ni pamoja na Jamatin hii ya Dodoma na Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu la Waanglikana la *Diocese of Central Tanganyika* ambalo ni miongoni mwa majengo ya kale na limejengwa kwa mfano wa Hekalu la Jerusalem, lakini kikubwa lilijengwa wakati wa njaa kubwa ili watu hawa wamkumbuke Mungu yupo na wasife na njaa, waliweza kuvuka awamu hiyo na wakajenga kanisa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo yote hayo yahifadhiwe, lakini pia iwe ni pamoja na reli yote ya kati na stesheni zote ambazo zilijengwa na Wajerumani. Inaanza kuleta hofu tunapoanza kubadilisha mwonekano wa majengo haya ya reli ya zamani. Tuyatunze, tuitunze Meli ya MV Liemba na iwe ni sehemu ya rasilimali za watu kija kuziona. Ninachukua hatua hii kuipongeza sana Serikali kwa kuyatangaza Mapango ya Kipatimu kuwa ni mapango yaliyohifadhiwa na yaliyotumika wakati wa Vita ya Majimaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo hilo ninalisema kwamba wengi tunadhani kwamba Vita ya Majimaji ilikuwa sehemu moja tu ya Tanzania lakini Vita ya Majimaji iliyoanzia kwa Wamatumbi ilisambaa kwenda Kilosa kwa Wavidunda, ilishuka kwenda kwa Wangoni, Songea. Kwa hiyo, ninaipongeza sana hatua hii ambayo imechukuliwa na ninaomba Wizara sasa pia iweke juhudi hiyo katika Mapango ya Magubike kule Kilosa, Mamboya kule Kilosa ili nayo yawe katika hifadhi hii ikiwa ni pamoja na Kituo cha Stesheni cha Kondoa ambacho leo hakitumiki na ndiyo ilikuwa mahali waliposhushwa watuma lakini baadaye Wajerumani walijenga stesheni ya reli pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningepanda kulizungumza ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzjai)*

**SPIKA:** Dakika moja malizia Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, ni kuhusu kuhifadhi Misitu ya Itigi *(Itigi Thickets)*. Hii ni misitu ambayo iko Tanzania na Zambia tu, tumeanza sasa kulima korosho, alizeti, lakini tuchukue hatua ya kuitunza *Itigi thickets* na kuhakiksha tunaziorodhesha katika urithi wa Kimataifa ili zitunzwe, lakini pia zitusaidie kupata asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa jimbo langu tunaomba fedha ya malipo ya athari za tembo au ndovu, lakini pia, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilosa, ili kuhakikisha watalii wanaokwenda Mikumi wanaingia pale. Nilipoomba uwanja wa ndege watu wengine hawakuelewa kwamba, hiyo mbuga ipo huko.

Mheshimiwa Spika, nilianza kwa kuunga mkono hoja, ninaomba kuunga mkono hoja na mengine nitatafuta njia ya kuyachangia. Ndiyo maana nakushukuru sana na nilikuja na vitabu vyote, ili kuonesha mambo haya yote, ikiwa ni pamoja na hawa *dinosaur* na vitabu vipo hapa kuhusu mafuvu yote ya vichwa, vitabu vipo hapa, lakini muda hautoshi. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na kunivumilia. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Ole-lekaita Kisau, lakini Mheshimiwa kabla hujachangia keti kidogo tutangaze wageni.

Waheshimiwa Wabunge ninao wageni ambao ni Mabalozi wa Bima pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)*. Yupo Mhandisi Zena Said, ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Mabalozi wa Bima Tanzania. Karibu sana. *(Makofi)*

Ameongozana na *CPA* Moremi Marwa, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Bima, karibu sana. Yupo Dkt. Suleiman Mohammed, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Bima pamoja na bwana Justine Mwandu, Mjumbe wa Bodi ya Taifa ya Bima. Yupo Dkt. Bagayo Sakwale, Kamishina wa

Bima na Mtendaji Mkuu wa MAMIAKA; Mamlaka, samahani wamekosea kuandika. Kamishna wa Bima na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania. *(Makofi)*

Yupo pia, Bi. Khadija Issa Said, Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Halima Mwinyi, Msaidizi wa Katibu Mkuu, Kiongozi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, ipo Menejimenti ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)*. Haya, sijui wamekaa upande gani? Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Yupo Kamishna Benedict Wakulyamba, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. Pia, Mheshimiwa Saning'o Kaika Ole-Telele, ambaye aliwahi kuwa, Mbunge na pia, aliwahi kuwa Naibu Waziri, karibu sana Bungeni. Huyu alikuwa Mbunge wa Ngorongoro, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, hawa ni Makamanda wa Kanda za Uhifadhi kutoka *TANAPA, TAWA, NCAA* na *TFS*. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo pia, Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)*. Sasa sijui kama ni hawahawa halafu wameorodheshwa tena? Naona orodha ndefu hapa. Mamlaka ya Usimaizi wa Wanyamapori *(TAWA)*, ni haohao? Sawa, basi karibuni sana, lakini pia, wapo Waandishi wa Habari na Wadau wa Utangazaji wa Utalii. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Wasanii wa *Bongo Movie* wakiongozwa na Steve Nyerere, karibuni sana. Pia, wadau wa benki na wawakilishi wa Wakazi wa Msomela, karibuni sana. *(Makofi)*

Ipo klabu inayojishughulisha na uelimishaji na utunzaji wa misitu na mazingira *(Green Awareness)* kutoka chuo cha Misitu Olomotonyi, Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kamati ya *RUAHA*, hii nayo ni ya kwako? Kamati ya *RUAHA Marathon,* au ni ya Mheshimiwa Cosato? Nimeona mahali ameandika.

Haya, Kamati ya *RUAHA Marathon*, karibuni sana. Nadhani hawa wageni wana-*share,* Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Cosato David Chumi. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Minza Mjika, ambao ni wazee wa Kanisa kutoka Kanisa la Mshikamano Meatu. Wengine ni wageni tisa wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi ya Wilaya ya Korogwe Vijijini wakiongozwa na ndugu Ali Waziri, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya. Karibuni sana viongozi. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo:-

Wanafunzi 70 na walimu sita kutoka Chuo cha Utalii Arusha. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya tangazo hilo anakuja Mwenyekiti kunipokea.

*(Hapa, Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na michango. Namuita sasa Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

Mheshimiwa Mama Kaboyoka! Haya, Mama Kaboyoka alishaitwa. Endelea Mheshimiwa Mama Kaboyoka. *(Kicheko)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Maliasili na Utalii. Kwa kweli, na mimi nachangamana na wenzangu

waliopita kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi alivyochagiza katika kuleta utalii wa hali ya juu sana Tanzania. Kwa kweli, nchi yetu sasa hivi imefunguka na ninajua kwamba, tutaendelea kupata mapato mengi kutokana na watalii. Pia, ninampongeza Spika wetu, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, maana na yeye kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani amesaidia pia, kututangaza Tanzania kwa hiyo, ni sehemu ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii na watendaji wake wote, Waziri, Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii na mashirika yake. Kipekee pia, naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ripoti yake ambayo kwa kweli, imetaja maeneo muhimu sana ambayo yanatakiwa yaangaliwe na Bunge hili kwa undani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wakati napitia hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii nilikuwa najiuliza maswali, hivi ni kwa kiasi gani tembo wanaonekana ndiyo wanyama ambao wanatakiwa wahifadhiwe kwa gharama zozote zile, ili watalii waweze kuja? Je, Serikali imeshawahi kufanya hata utafiti kidogo kuona hawa watalii wengi wanaokuja wanavutiwa na kitu gani zaidi? Kwa nini nauliza hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivi kutokana na sababu moja kubwa kwamba, kwenye Biblia, Hosea Nne, Mstari wa Sita, imeandikwa "Watu wangu wanaangamizwa kwa kuokosa maarifa." Pia, ukiangalia Mwanzo Moja, Mstari wa 26, inasema "Mungu ametupa mamlaka ya kutawala wanyama wote na kila kiumbe chenye uhai," lakini inaelekea kama sasa hivi tunaelekea mahali tutatawaliwa na wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kilio cha wananchi kila sehemu na umetajiwa na kamati yako hapa. Halmashauri ambazo zinakumbwa na tataizo hili la wanyamapori kuingilia wananchi kwenye mashamba yao, kuharibu mimea, mazao, kuua wananchi ni janga ambalo linatakiwa tusilifumbie macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninauliza, hivi hawa tembo tumeshawahi kufanya utafiti kuona *carrying capacity* yao kwa maeneo yaliyotengwa itachukua muda gani, ili yasiweze yakazidi lile eneo mpaka ikabidi wananchi watolewe tena, ili tembo wapate nafasi za kuishi? Nimeona ambavyo Serikali au wizara imejitahidi kweli, wanafanya jitihada kubwa, lakini mimi ninaangalia nikiwa pia, ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu inayoangalia Matumizi ya Fedha ya Serikali. Ni *helicopter* ngapi zinahitajika tununue? Ni walinzi wangapi ambao watasimama tu kungojea tembo aje, ili wamrudishe kwenye hifadhi bila kuzalisha? Je, ukiangalia wenzetu wanasema *cost benefit analysis* ukiifanya, unaweza kuangalia hizi gharama ambazo zinawekwa kulinda tembo au wanyama waharibifu zinalingana na kile tunachopata kwenye utalii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge aliyepita ameongea sana kuhusu maeneo mbalimbali ambayo yanaweza kuleta watalii wengi. Kwa nini Tanzania tumeonekana kwamba, wanyama sasa ndiyo wana umuhimu na ndiyo wana hadhi au wana thamani kuliko binadamu? Hili ni jambo ambalo lina hatari sana. Itafika mahali ambapo wanyama wanaweza kuzidi binadamu halafu ikawa matatizo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri inapoonesha kwamba, wanyama wanaweza kuvunwa, ili tukaacha kiasi kile kinachotakiwa kutokana na eneo lililopo na kwa muda gani wanyama hawa wanaweza kuishi katika eneo hilo bila kuhitaji kufukuza tena wananchi kwenye maeneo yao. Mimi kweli, ninamefurahi kwamba, tunajitahidi. Wizara ya Serikali inajitahidi, lakini unaposema unampa mwananchi mabomu ya kufukuza hawa tembo, je, wanafukuzwa mchana au wanafukuzwa usiku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni usiku, mwanchi amelala na mabomu yake, tembo huyo anamuamsha kwamba, amka nakuja, ili bomu lifanye kazi au atamvamia kabla hata hajatumia lile bomu? Kwa hiyo, unaangalia wananchi wetu usiku wapigane na tembo, mchana, ngedere na ndege kweleakwelea, sasa huyu mkulima kweli, maisha yake yatakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba, tuna haja ya kuangalia pia, njia nyingine za kuweza kudhibiti hawa wanyama. Kwa mfano, tukitumia *traditions* au njia za asili, kuchimba mitaro yale maeneo ambayo tembo hawezi kuvuka naamini kwamba, mitaro ile itasaidia wale tembo hawavuki kuingia kwenye maeneo ya wakulima maana watajua kwamba, wakishuka wanaakili, tembo wanajua wakiingia kwenye mitaro hawatatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu jambo lingine ni sisi jana tulikuwa na kikao na semina na wenzetu wa Mamlaka ya Usimaizi wa Bima Tanzania *(TIRA)*. Tukaongelea kama kuna wadau wa bima ambao wanaweza kusaidia wakulima wakipatwa na maafa ya mafuriko au jua kali, ukame; je hawawezi kuwa na bima ya kusaidia hawa watu, wakulima, ambao wanapata adha ya kuliwa mazao yao na kuuwawa, hasa na Tembo? Wenzetu *TIRA* walisema hilo linaongeleka na wakasema wapo tayari kukaa na *TANAPA* kuongea na kuona jinsi ambavyo wanaweza kuwasaidia hao wakulima, ili kuona kwamba, mazao yao yatakapoharibiwa na hawa Wanyamapori watawezaje kuwasaidia, pamoja na wale watakaouwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana kama mlivyosikia kamati ikisema kwamba, wakulima wanataka wafidiwe sawasawa na thamani ya mazao yao *more than* kusema nampa laki au nampa ngapi, laki moja ni sawa na mbolea ya nusu ekari tu. Sasa huyo mkulima amepoteza, kwa mfano kule kwetu mpunga ambao akiuza mazao ya eka moja anapata shilingi milioni tatu, leo unampa shilingi laki moja kwa kweli, hilo ni uonevu mkubwa sana kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri *TANAPA*, kupitia Wizara hii, wakae na wenzetu wa *TIRA* waone jinsi ambavyo wanaweza kuwasaidia hawa wakulima. Kama kuna bima ya afya kwa wote pia, inawezekana kuwa na bima ya maisha kwa wote. Ripoti ya *CAG* imeonesha kwamba, katika Mwaka 2022/2023 *TTB* ilikuwa na bajeti ya shilingi bilioni moja na milioni 100.13 na hiyo ilikuwa kwa ajili, ya kuwa na matamasha mbalimbali, mikutano mbalimbli huko Ulaya, Bara la Asia, Marekani, Kusini na Kasikazini,

lakini haikutolewa hata senti moja ya hawa wenzetu wa *TTB* kufanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajiuliza hili shirika lipo, kwa ajili gani? Kama hatuwezi kuliwezesha liendeleza *promotion* ya watalii sasa lipo, kwa ajili ya kufanya nini? Kwa hiyo, tunaomba Serikali iliangalie hilo, ili kuona jinsi ambavyo wataweza kuisaidia hii *TTB* iweze kufanya kazi yake kikamilifu. Pia, kuongeza walimu wa lugha katika vile vyuo vya ufundishaji watalii kwa mfano, sasahivi tunapata watalii wengi wanaoongea Kifaransa, Kichina, Kirusi na Kijerumani. Inatakiwa na sisi tujipange vizuri kwamba, wale wanaoongoza utalii na wao wawe *competent* katika hizi lugha, hii itatusaidia sana kutoa *impression* kwamba, tupo *serious* katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawapongeza pia, Wakala wa Misitu kwa kazi wanayoifanya. Tunaomba waendelee kupanda misitu kila sehemu inayowezekana, ili tuongeze ukaa ambao utatuletea fedha kitaifa na kupunguza gharama nyingine katika bajeti zetu. Naomba kusema kwamba, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru sana. Namuita sasa Mheshimiwa Edward Ole-lekaita Kisau, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Mheshimiwa Mrisho Gambo, ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa *Royal Tour,* nadhani itafanya nchi yetu ijulikane zaidi na tupate watalii, ili maeneo haya tunayojaribu kuyahifdhi yawe na manufaa na tija kwa nchi yetu. Ninampongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na kwa kweli, leo nitachangia hii bajeti nikiwa na furaha kidogo kwa sababu moja; kwanza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira mmenifurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli, Mheshimiwa Mwenyekiti shikamoo na Wajumbe wako wote. Hii inaweza ikawa ndiyo ripoti ya kwanza ya Bunge hili, nzuri sana, ya Kibunge,

hongereni sana. Mmezungumza yale yanayowasibu Watanzania, hongereni sana, lakini vile vile nitachangia kwa upole kwa sababu, Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki wakati anaanza hapa amesema hii ndiyo hotuba yake ya kwanza akiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, nikianza kutwanga hapa wakati ndiyo hii ya kwanza, itakuwa siyo uungwana. Kwa hiyo, leo nashauri sana tu na kwanza nakupongeza kwa kuanzisha ile mijadala ya kuwaita Wabunge wa Mikoa yote na kuzungumza nao, ili upate wanachotaka Watanzania kupitia Wabunge wao, ukiendelea hivyo, utajifunza mambo mengi sana. Kwa hiyo, kwa kweli, nakupa *big up* sana, hii itakuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ya kwanza ambayo nachangia nikiwa *a bit calm*. Vile vile Naibu Waziri wako ni mtu mwema na atakusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kamati imepunguza kazi yangu kubwa sana, leo niseme Mheshimiwa Waziri, kitu ambacho hatutaki ku-*negotiate* ni mahusiano ya wananchi na watu wa hifadhi na ni kwa kuwa, kwenye hotuba yako umezungumza habari ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Ukurasa wa 113, inasema hivi, "kuimarisha mahusiano kati ya maeneo ya hifadhi na wananchi" kwa hiyo, siyo takwa tu, *is not just a speech* ni *commitment* ya Chama Cha Mapinduzi. Nakuomba sana uwe mkali sana linapokuja jambo la mahusiano kati ya wananchi na watu wako wa hifadhi, uwe mkali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ilikuwa inasema hivi; "Ili kuwa na uhifadhi endelevu ni lazima mjali haki na maslahi ya wananchi." Ilani imezungumza vizuri sana. Mali zao zilindwe, mashamba yao yalindwe, mifugo yao ilindwe na *more importantly,* maisha yao kila wakati, ukifanya hili utakuwa Waziri mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ushauri wangu mwingine Mheshimiwa Mchengerwa alipokuwa Waziri hapa alikuwa na kauli zake mbili nzuri sana, ambazo ningekuomba uazime. Wananchi wa Tanzania ni wahifadhi namba moja na kwamba kazi za nyinyi

mnaohifadhi kazi zenu zitapimwa kwa kusikiliza Wananchi wa Tanzania wanataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza Mheshimiwa Profesa Kabudi hapa kwenye utalii na uhifadhi; sisi tunafikiri utalii ni kuwa na mbuga za wanyama nyingi tu na mapori tengefu, hapana siyo kweli. Ukiangalia nchi 10 Barani Afrika ambazo zina maeneo ya hifadhi na hiyo mka-*update* na nyinyi *list* yenu *Wild Atlas* bado inasema Tanzania ina mbuga 16 wakati tunajua zipo 21 ambayo inafanya Tanzania ya tano, sita huko wakati ilitakiwa *actually* iwe ya pili, ya kwanza ni Kenya, halafu Tanzania, halafu Zambia, lakini bado hawaja-*update*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia nchi ambazo zinafanya vizuri ni *Egypt* ina watalii karibu 11,000,000 unajua wana mbuga ambazo hazizidi hata tano. Maana yake utalii lazima tufikiri *more broadly* kuliko tunavyofikiri. Ukitembelea *Washington DC* utalii watu wanakwenda *African American Museum, John Kennedy Memorial Centre* na *Luther King Junior*. Ukienda *Italy* wanakwenda kwenye *St. Peters Basilica Church yaani n*i vitu vingi sana kuliko sisi tunavyofikiri ni kwenda tu kuangalia Wanyama pori na maeneo mengi. Kwa hiyo, lazima tufikiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia nchi kama *Morocco* haina mbuga nyingi sana, lakini watalii ni wengi, kwa sababu *factors* nyingi zinazoleta watalii. Vilevile ukiangalia Tunisia hawana mbuga nyinyi, lakini watalii ni wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunazungumza habari ya 33% ya nchi hii ipo kwenye hifadhi; ushauri wangu mwingine usikubali *proposal* nyingine ya aina yoyote ya namna ya kuongeza maeneo ya hifadhi, kwa sababu *is not sustainable, population* yetu inaongezeka sana. Ni afadhali tuweke nguvu kwenye haya tuliyonayo yawe *well managed* na ilete *return* kwa nchi yetu. Siyo namba tu ya mbuga za wanyama na mapori yanaongezeka, lakini uhalisia ukiangalia hatuoni *benefit*. Halafu mnaongeza kwa kuwatoa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshauri Mheshimiwa Waziri kuhusu *WMAs* na mimi ninazungumza hapa kama Mwenyekiti wa Wabunge wenye *WMA*. Nikushukuru umewaalika watu wa *WMA* hapa. Mahusiano tunataka kuona hapa hawa ni wahifadhi na nyinyi ni wahifadhi mnauza nchi yetu na mnafanya kazi mmoja mdumishe mahusiano. Tunataka mtu wa *TANAPA* apande ndege aende akauze mbuga zake na mtu wa *WMA* aende akauze mbuga zake wote mpo kwenye ndege moja. Mmoja ana banda pale, mwingine banda pale, mwekezaji aliyepo *WMA* ni kama aliyepo Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, kama walivyosema Kamati ya Bunge, mwaka jana na leo wamerudi, tunakuomba Maazimio ya Bunge, yalishapitishwa hapa kwamba pesa za *WMAs* zinazodaiwa na *WMAs* zirudi, lakini Bunge lilisema hivi tengenezeni mfumo ambao utawezesha kila mdau na kwa sababu tumeshaweka mpango huu kwa mujibu wa Sheria kila mtu anapata pesa zake kwa wakati. Kila mtu akipata pesa zake kwa wakati uhifadhi utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni migogoro; Mheshimiwa Waziri *WMAs* zinafanya kazi za uhifadhi kama unavyofanya wewe. Mimi sioni *logic* ya kugombana kuhusu mipaka kwa sababu wote tunafanya kazi hiyo hiyo moja. *It illogical* kufikiri eti pori linaweza chukua sehemu ya *WMA for conservation* wakati hata wao wanafanya shughuli hiyo hiyo ya *conservation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea ku-*promote WMAs* na kuna Wabunge wengi wanataka kuanzisha *WMA*. *WMA* ni nzuri, kwa sababu ni *modal* ambayo inafanya wananchi washiriki moja kwa moja kwenye uhifadhi. Nchi kama Namibia, Kenya, Botswana, Zimbabwe na *South Africa* wote wanafanya hivyo. Ni *modal* nzuri sana, zitauza Wizara yako vizuri sana, kwa sababu ni *modal* ambayo ina-*empower* wananchi wenyewe washiriki kwenye *conservation*. Kwa hivyo, tutafika mahali wewe utakuwa uhangaiki, kwa sababu wanyama pori wanalindwa sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

*(Hapa kengele ililia kuashira kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umeisha.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ala muda umekwisha kumbe? Haya. Basi nashukuru kwa kuwa, leo nina furaha basi nitaishia hapa. Ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimwite sasa Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuata, Mheshimiwa Ester Bulaya, ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza katika Bunge lako Tukufu. Kwanza, nipende kutoa shukurani na pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya kazi nzuri ndani ya miaka mitatu ya utawala wake, kuongeza watalii wengi katika nchi yetu na hivyo kuliongezea Taifa letu mapato mengi kama ambavyo amesoma Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimpongeze Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Menejimenti nzima ya Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa Kilwa. Katika Wilaya yetu ya Kilwa kama mnavyofahamu katika karne ya 13 mnamo mwaka 1,331 Mwanazuoni maarufu aliwahi kuzuru katika Wilaya ya Kilwa kwa shughuli za utalii. Aliandika kitabu mnamo waka 1,332 akiusifu sana Mji wa Kilwa Kisiwani, ukiwa ni mji maarufu kabisa kuliko miji yote kwa wakati ule katika Pwani ya Afrika Mashariki na Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tukirudi nyuma tunakumbuka kati ya karne ya 12 mpaka karne ya 15, Dola ya Kilwa Kisiwani ilikamata kasi kwa maendeleo, lakini hapa katikati tulipoteana. Kilwa ikashuka, Kilwa ambayo ilikuwa na Dola yake, ilikuwa na

fedha zake na ilikuwa na utawala wake, ilipotea katika uso wa dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa wa Rais, ameweza kufanya mambo makubwa katika Wilaya ya Kilwa na sasa Kilwa inakwenda juu kwa kasi kubwa. Ukiachia kwenye sekta nyingine, lakini kwenye sekta ya utalii peke yake wamewekeza. Wizara ya Utalii imewekeza fedha nyinyi kwa ajili ya uendelezaji wa Makumbusho ya Magofu Kilwa Kisiwani ya pamoja na Makumbusho ya kule Songomnara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru mwezi Machi, mwaka huu tulipata *GN* ya Kumbukizi za Majimaji. Kumbukizi ambazo tulizihangaikia kwa miaka mingi tangu baba zetu hadi leo. Tunashukuru kwamba sasa zimeweza kupatikana. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri, ambaye anahusika na Wizara hii, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumelipwa fidia kwa watu wetu wengi, fidia zinazotokana na madhila yaliyotokana na wanyama waharibifu na wanyama wakali. Tunashukuru watu wengi wamelipwa, ni jambo jema sana ambalo tulikuwa tunalipigania kwa miaka zaidi ya mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi nyuma kusisitiza kwenye utalii wa utamaduni na historia *(cultural and historical tourism)* kama nilivyosema mwanzo Kilwa ilikuwa imeshamiri sana kwa utalii wa aina hii tangu karne ya 13. Kumbukumbu za kihistoria zinasema wakati *Ibn Battuta*, alipofika Kilwa aliikuta Kilwa Kisiwani yenye ukubwa usiozidi *square kilometer* mbili ilikuwa na misikiti 99, ukiwemo msikiti wa karne ya 11. Msikiti ambao ulijengwa kwa umahiri mkubwa haijawahi kutokea katika zama zile katika Ukanda wote wa Pwani ya Afrika Mashariki. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, alikuta watu wa Kilwa, wamestaarabika sana kiasi kwamba, walikuwa wanajua hadi kusoma na kuandika. Walikuwa ni hodari wa kuandika mashari kwa Lugha ya Kiswahili. Nisema nasisitiza kwenye utalii huu, kwa

sababu hata walipotokea wavamizi katika Kilwa Kisiwani ile misikiti 99, ilihusika katika kuomba dua kiasi kwamba, ile merikebu ambayo ilikuja kuvamia Kilwa Kiswani iligeuka kuwa jiwe la jahazi lipo mpaka leo. Utalii wa kihistoria na utamaduni umenufaisha nchi nyingi ikiwemo: Nchi ya Misri, Algeria, *Morocco,* Israeli, Saudi Arabia, Jordan, Palestina, Uturuki, Iraq, Syria na Tunisia. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuwekeza kwenye utalii wa utamaduni na kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimimiwa Mwenyekiti, ukienda Misri unakuta kuna yale ma-*pyramid* ya Mafarao likiwemo lile pyramid kubwa kabisa lililopo kule Giza, la Farao *Khufu* au *Cheops***,** ambaye aliishi katika karne ya 26 kabla ya Kristo. Ukienda Uturuki unakuta kuna mjini unaitwa Antioch una kumbukumbu muhimu sana za kidini, hasa dini ya kikristo. Wakati Mtume Paulo alipokuwa anafanya kazi zake kule Antioch**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sisi tumejitahidi kuwekeza kwa kushirikiana na taasisi za dini na kadhalika. Israeli mambo yapo hivyo hivyo, Palestina yapo hivyo hivyo. Sasa ningeomba Serikali iendelee kuwekeza kwa kutangaza hivi vivutio vya utalii, kuendeleza utafiti lakini pia kuendeleza kuboresha miundombinu kuelea kwenye vivutio vyetu vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya Kilwa, kulikuwa na *Rhapta* Makao Makuu ya Mji wa Dola ya Azania, nyuma kidogo kabla ya Dola ya Kilwa. Pia, kuna Visiwa vya *Fanjove* pale Songosongo, kuna Kilwa Kiswani, Songomnara Kumbukizi za Majimaji, Mapango ya Namaingo na Nan'goma ambayo yapo pale Kilwa Kaskazini. Pia kuna viboko *albino* kule Mpindilo, kuna Kumbukizi Dainosari (mjuzi mkubwa). Kwa hiyo, nina imani hivi vyote vikiunganishwa vikitangazwa vizuri vikiendelea kutafitiwa vikawekewa miundombinu mizuri ya kufikika, ni wazi kwamba tutaongeza tija na ufanisi katika sekta ya utalii na tutapata fedha nyingi pengine kuliko nchi yoyote Barani Afrika. Kwa hiyo, niiombe Serikali iongeze nguvu katika hayo maeneo. Pia, kule kwenye Kumbukizi za Majimaji ninaomba Mheshimiwa Waziri, tuteue taasisi ambayo itasimamia kumbukizi zile baada ya kuwa zimepata *GN. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuweke bajeti kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025, bajeti hii tunayokwenda kuipitisha tarehe 3, kwa hiyo, ningeomba iwekwe bajeti pia. Kwa hiyo, niseme tu kwa ujumla tutatoboa sana. Kwa ujumla, nirudie kupongeza Wizara na Mheshimiwa Rais kwa ujumla, kwa kufanya kazi nzuri. Kwa ujumla, nasema Mungu ibariki Kilwa, Mungu ibariki Tanzania, Mungu akubariki sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri unayofanya na Mungu ambariki Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Ni wazi kwamba, tutatoboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ndulane. Nimwite sasa Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya, wajiandae Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya changamoto ya muda, mimi nitajielekeza kwenye maeneo makubwa mawili; eneo la kwanza ni eneo la changamoto na eneo la pili ni mawazo yangu kwenye namna gani tunaweza tukafikia idadi ya watalii 5,000,000 kama ambavyo Ilani ya CCM imeelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kwenye eneo la *service levy*, ambayo kwa mujibu wa sheria inatakiwa wafanyabiashara walipie 0.3%. Changamoto iliyopo kwenye sekta ya utalii fedha ambazo wanazipokea siyo zote ni fedha zao. Wanapokea kama hela kwa ajili ya *park fee,* nyingine kwa ajili ya *concession fee*, nyingine kwa ajili ya masuala mbalimbali yanayohusiana na suala la utalii, ambayo mwisho wa siku wao wanakwenda kuyalipa pengine Ngorongoro, *TANAPA* na kwenye hoteli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hiyo, inakwenda ku-*charge*-iwa kwa mwenye hoteli kwa maana ya *service levy* lakini pia ana-*charge*-wa na *tour operator*. Tulidhani kwamba ni vizuri Sheria

ikaangalia badala ya ku-*charge* kwenye *turnover* pengine tuka-*charge* kwenye *gross profit* ya wafanyabiashara. Pia, kuna hali ya kutumia nguvu kwenye kukusanya nadhani masuala kama haya yamepitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni changamoto kuhusiana na *mountain climbing TALA* ambao wanalipa wale wanaopandisha watu wa utalii. Kubwa zaidi wanaofanya hiyo kazi ni Vijana wa Kitanzania ambao wamejiajiri kwenye fursa hizo na gharama yake ni dola 2,000. Tulikuwa tumetoa mawazo toka huko nyuma badala ya dola 2,000, walipe dola 500 kwa sababu mchakato huu ulifanana na *tour operators.* Zamani walikuwa wanalipa dola 2,000, utaratibu ukabadilika ikatoka dola 2,000 ikawa gari moja mpaka tatu dola 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunadhani kwamba kwa wenzetu *mountain climbing TALA* wao gharama ya kupandisha watalii; pengine kwa wanaopandisha watu 50 mpaka 100 walipe dola 200; wanaopandisha watu 100 mpaka 300 labda walipe dola 300; watu 300 mpaka 500 walipe dola 500; na 500 na kuendelea iwe dola 1,000, kadiri ambavyo Wizara itaona inafaa ili kutoa fursa ya ajira hasa kwa Vijana wa Kitanzania ambao wanatumia fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, changamoto tatu, Mheshimiwa Waziri, wale watu wote wenye *camp* kwenye hifadhi zetu labda Serengeti, ukienda Ngorongoro wanapokwenda kule ndani wafanyakazi wa *camp* wenyewe wanalipishwa fedha na Serikali yetu shilingi 3,500 kila siku. Mtu ameajiri watu wanakwenda kutoa huduma ya kupika, kuhudumia watu na kufua, lakini bado Serikali pia inakwenda kuwa-*charge* fedha mpaka hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili jambo Serikali ingetengeneza vitambulisho maalumu vya kuwatambua wafanyakazi wote wanaofanya kwenye *camp*. Wasilipe chochote, kwa sababu wao ni wafanyakazi tu, kuwapa mzigo wa kulipa nadhani siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata magari ambayo yanapeleka vyakula na vitu vingine, kila yakipita kwenye mageti yana-*charge*-iwa fedha. Tunadhani kwamba magari pia yangetambuliwa yasilipe chochote ili kuendelea kutoa motisha na fursa kwa watu wetu wa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamo ya nne ni kuhusiana na ile *guiding fee; guiding fee* hii ni leseni tu, ni utambuzi tu. Leo Serikali inachukua dola 50 kwa kila *guide*. Wakati leseni ya magari pia wanalipia 70,000 kwa miaka mitatu. Tulidhani kwamba kama hatuwezi kutumia leseni ya magari kuwatambua, kwa sababu hawa ma-*guide* ni madereva. Basi pengine uweke utaratibu wa miaka mitatu basi leseni yao ya utambuzi izisidi kiasi cha shilingi 70,000 kwa hiyo miaka mitatu ili Serikali iwatambue na iwe rahisi kuweza kufanya shughuli zao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto pia kubwa ya barabara kwenye hifadhi zetu; nenda Ngorongoro, nenda Serengeti hali ya barabara ni mbaya sana, kwa sababu Serikali imechukua fedha zote. Halafu kwenye kurudisha imekuwa ni mtihani. Tumefurahi kuona mwaka huu umekuja na pendekezo ya kwamba fedha zile waachiwe Ngorongoro na *TANAPA* na mamlaka nyingine ili waweze kukusanya na kuweza kutumia inaweza kuwa ni rahisi pia kwenda kusimamia hali ya barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, hoja yangu ya pili, ni kuhusiana na mwenendo wa utalii duniani. Leo ukiangalia sisi Tanzania tumepeana *target* ya watalii 5,000,000 lakini tuangalie dunia ipoje? 5,000,000 yenyewe ambayo hata hatujaifikia bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda nchi kama Afrika Kusini kwa mwaka 2022, wao walipata watalii 8,500,000, lakini idadi yao ya watu ni milioni 60.4 na walipata mapato kiasi cha bilioni 13.2. Ukienda Morocco mwaka 2022 idadi yao ya watalii waliopata ni 14,000,000 kwa mwaka 2022, watu wao wapo 38,000,000 na walipa 9*.8 billion*, ukienda Ufaransa wao walipata watalii milioni 21.6, wapo milioni 64.8 na walipa bilioni 58.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi leo tumejiwekea *target* kama Watanzania ya kupata shilingi 6,000,000,000 na watalii 5,000,000 na ukizingatia kwamba, kwa mwaka 2022, Tanzania tulikuwa na watalii milioni 1.8, tupo milioni 69.4 na tulipa *3.4 billion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nadhani kwa maoni yangu, ili tuweze kuanza hata hawa tuliojiwekea wachache wa 5,000,000. Je, tuna mpango gani kama Taifa? Tumejipangaje? Je, viwanja vyetu vya ndege vina uwezo wa kuwa-*accommodate* watu hao? Ukiangalia leo ili uweze kupokea watalii 5,000,000 kwa mwaka maana yake unahitaji kuwa na *international flights* 68 kila siku zitue katika ardhi ya Tanzania. Utahitaji pia kila siku uweze kupokea watalii 13,698 na utahitaji pia uweze kuwa na magari ya uhakika kiasi cha 3,424.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua magari 3,424 yakiondoka na watalii kwa mfano kwa siku sita na kila siku kama wanaingia 13,698. Maana yake siku sita zilizobaki hizo wakati magari yale yapo porini unahitaji pia idadi ya magari kama hayo. Kwa hiyo, utahitaji magari 20,544. Je, tumejipangaje kama Taifa kwenye eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *accommodation* na kwenyewe, kama tunapokea kwa siku 13,698 ili tufikie hao 5,000,000 kwa mwaka mzima. Tutahitaji vitanda 13,698, lakini vitanda hivyo kama leo wamekuja 13,698 na wakikaa siku sita, je, wakija wengine kesho na kesho kutwa watakaa wapi? Maana yake utahitaji vitanda 82,188 kama watalii watakuja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utahitaji pia kuwa na *international brands* kama *Meliá* pamoja na *Hyatt* na nyingine ambazo zinasaidia pia kuleta idadi ya watalii. Pia, utahitaji pia *human resources* tumejipangaje kwenye *human resources* sisi kama Taifa? *Waiters* kwa ajili ya kudumia watu, wapishi, *room attendants'* na *mangers,* kwa sababu ukiangalia watu wetu wahifadhi hao kwa asilimia kubwa wanapambana kupata wahudumu wazuri. Ndiyo maana wengi wanawatoa mpaka nje ya nchi kwa ajili ya kuja kuhudumia. Je, sheria zetu zimekaaje kwenye hii hii tunayouizungumzia *human resources? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *TDL (Tourism Development Levy) one percent* inafanya nini toka imeanzishwa imekusanya kiasi gani? *Impact* yake ni nini kwenye kukuza utalii wetu, kuna *skills development levy* ambayo ni *four percent,* toka imeanza kukusanywa imeongeza ujuzi wa kiwango gani kwa Watanzania ambao wanatakiwa kuhudumia sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia je, sheria zetu zimekaaje na zenyewe. Kwa mfano unaangalia kwenye *VAT,* Tanzania *VAT* 18% ukienda Zanzibar tu, nchi moja na Tanzania yenyewe ni asilimia 15, ukienda Kenya asilimia 16, Africa Kusini asilimia 15, Namibia asilimia 15. Kwa hiyo, unaona kuna changamoto kubwa sana katika sheria zetu ni lazima tuzi-*harmonize*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kumalizia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gambo ahsante sana hitimisha.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani dakika moja tu. Hata kwenye wawekezaji wetu kule hifadhini wanapewa maeneo ya kuwekeza lakini hawapewi hata *title* kwa ajili ya kuwekeza, wanawezaji ku-*access finance* kwenye maeneo mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kuna changamoto ya muda lakini kuna mengi ya kuchangia kwenye sekta ya utalii.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimuite sasa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, Mwenyekiti makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa niipongeze Kamati ya Maliasili na Utalii, imefanya kazi ya Kibunge, imetusaidia kazi, wajibu wetu Wabunge, Bunge hili kuiheshimisha Kamati ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa 33 ongezeko la bajeti kwa Wizara ya Maliasili na Utalii bilioni 19. Bilioni 5 iende kwenye miradi ya maendeleo, bilioni 14 *OC*. Maombi ya hovyo ambayo Bunge hili tusikubali kuyapitisha. Maombi ya matumizi mabaya ya fedha za umma, maombi ya kifisadi, maombi ya anasa. Mnaleta maombi kama haya? Kuna taasisi chini ya Wizara hii haina ofisi? Mnatuletea maombi kama haya ya kwenda kuzurura, kuna taasisi chini ya Wizara hii ina madeni? Mnatuletea maombi kama haya kwenye hotuba ya Waziri ametenga bilioni mbili kwenda kulipa wananchi fidia walioathiriwa na tembo? Mnatuletea maombi kama haya tumetoka kwenye bajeti ya maji mmepunguza pesa za wananchi kutopata maji, mnatuletea maombi kama haya kwenda kwenye *OC*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana hapa bajeti ya Ujenzi ilikuwa hatari, barabara zimeharibika huko wananchi wanashindwa kupita? Mnataka Bunge kama hili tupitishe anasa hizi, *no*, Hapana! Hizi pesa za walipa kodi zitalindwa zikafanye mambo ya msingi katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naangalia hapa hii Wizara, Bodi ya Utalii imejenga kituo kizuri kabisa cha kutangaza utalii kidijitali, imetumia bilioni moja, huu mwezi wa 20 hakitumiki. Halafu kuna watu wanataka kwenda kuzurura tu huko. Wenye kazi yao hapa ya kutangaza utalii mnawanyima hela, haya Kamati wamewaambia huko tangu mwaka jana hamsikii, kwenye ripoti ya CAG ameandika aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili kituo kimekamilika mmeshindwa kulipa milioni 228 kwa ajili ya kuanza kazi. Mnategemea tu Mheshimiwa Mama Samia na *royal tour* yake nyinyi mnashindwa kutimiza majibu yenu ya msingi, halafu mnataka tufikie idadi ya milioni 5 ya watalii katika Taifa letu kwa mambo haya ya hovyo. Hatuwezi kuruhusu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bodi ya Utalii imetengewa bilioni 4 hawajawapa yote, wamewapa bilioni 3 wanatuletea huku maombi ya bilioni 14 ya anasa huku vitu vya

msingi vya kuongeza utalii Serikali yetu, nchi yetu ipate mapato mnashindwa kupeleka pesa huku? Mnatuomba bilioni 14 sisi ya *OC* huko? Hii si sawa, hili ni Bunge la wananchi tufanye kazi ya wananchi. Mnatenga bilioni mbili watu huko wamekatwa miguu na tembo wenu, hamuwalipi fidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja Nyatwali, Kata ya Nyatwali yenye mitaa mitatu, mtaa wa Tamau, mtaa wa Serengeti na Nyatwali iliyopo Jimbo la Bunda Mjini Mkoa wa Mara. Hatukuzaliwa Mkoa wa Mara kwa bahati mbaya, sikuzaliwa Bunda Mjini kwa bahati mbaya, nimezaliwa kutetea haki za wananchi mnaowanyanyasa, wananchi wa Nyatwali. Aibu, Serikali kwenda kutaka kupora ardhi kwa dhuluma ili tembo wapiti! Hatukatai tutawaachia ardhi lakini hatutaki muwaache wananchi wa Nyatwali na umaskini wa kutupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kaya 1,200, kuna wakazi 13,000. Mmefanya tathmini miaka miwili, mmewaacha na umaskini kule. Mnataka kwenda kuwatoa kwa *square meter* shilingi 490? Ardhi ambayo ni lango kuu la kuingia Serengeti. Maeneo ya jirani kwenye Halmashauri ya Mji wa Bunda wametangaza *square meter* moja inauzwa shilingi kuanzia 2,200 - 5,000. Mnawachukuwa ardhi yao wawe maskini? Mnawalipa 470? Shilingi? Hata hela ya *coca* ni kubwa kuliko ardhi yetu ya Bunda. Wananchi mmewaacha kwenye umaskini, mmewafanyia tathmini hawawezi kufanya maendelezo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba zimechakaa mmewakataza kujenga zaidi ya familia 300 zinalala nje, yamepita mafuriko wengine mmewasaidia, watu kule wanakaa juu ya bati kwa sababu mnataka kutwaa ardhi yao. Mmefanya tathmini hamjawaandalia mahali pa kwenda, mnataka kuwaondoa kwa gharama ndogo kwa ajili ya tembo. Sawa, mnawapeleka wapi? Tumesikia sijui wapi huko, mmewajengea nyumba, mmewafanyia nini. Wale hata pa kuwapeleka hamuwaambii. Eneo mnawapa *square meter* shilingi 470, waende wakanunue ardhi kwa *square meter* shilingi 5,000, waende wakanunue ardhi kwa mita shilingi 2,200? Kwa nini mnataka kunyanyasa wananchi maskini? *Why?* Hili halitakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale wapo kama kwenye kisiwa halafu mnaenda kuwatisha tisha na wamesema hawataki ziara za viongozi tena kwenda kuwatumia kisiasa, wanataka muwalipe pesa kwa hadhi na thamani ya ardhi yao. Leo hawajui hatima yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza daftari la kuandikisha wapiga kura enhe! wao wanaenda wapi? Wakose haki yao ya kupiga kura? Mtawapeleka wapi? Hili halitakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ya tembo, Halmashauri ya Mji wa Bunda wamefanyiwa tathmini mwaka 2021, zaidi ya wananchi 1,200 mpaka leo hamjawalipa fidia halafu mnataka tuwapitishie bilioni 14 hapa kwenda kuzurura? Sisi hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao tangu mwaka 2021 wanadai, sasa leo mfugaji akosee kidogo tu hatusemi waingie kwenye hifadhi, akosee kidogo tu aingie kwenye hifadhi milioni moja, akichelewa mnaenda kuuza akiingia kwenye hifadhi. Hili hatuwezi kukubali. Tulipeni fidia, mpaka sasa ivi jumla ya wananchi 2,000 wanadai waliofanyiwa tathmini ni hawa hawa 1200 na zaidi, 1,008 bado hamjafanyia kazi, hamjawaingiza kwenye mfumo wa malipo. Hatuwezi kukubali mnyanyase wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tutafutieni maeneo kama maeneo mengine na mtulipe fidia kutokana na thamani ya ardhi yetu. Wale siyo takataka wale. *(Makofi)*

**MWEMYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Bulaya. Nimuite sasa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei atafuata.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia Wizara hii nyeti sana ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na

Makamu wake na Wanakamati wote, kwa kweli wamefanya kazi nzuri ambayo inaonesha kule ambako wananchi wameelekea. Pamoja na pongezi hizo nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dada yangu Mheshimiwa Angellah Kairuki, Naibu Waziri Kaka yangu Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Katibu Mkuu Dkt. Abbas pamoja na Naibu Katibu Mkuu CP. Benedict Wakulyamba kwa sababu kwa kweli pamoja na changamoto nyingi zilizopo kwenye Wizara yao, nao wamefanya kazi kubwa, bado tunaendelea kuona namna ambavyo wanapambana, ujangili umepungua, uhifadhi umekuwa bora haya mapungufu kwa pamoja tunaona namna ya kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza kwa hatua zao za kusudi kabisa za kuinua utalii. Niliona kwenye habari wiki mbili zilizopita kwamba waliamua kupunguza gharama za leseni zile za utalii kutoka dola 2,000 kwenda dola 1,000 nawapongeza sana na hii ndiyo itakachowasaidia kupata idadi ya watalii. Kwa mfano, Mlima Kilimanjaro *target* mmeonesha ni kutoka watalii 56,000 kwenda watalii 200,000 hongereni sana na naomba tuwaombee kwamba haya yakazae matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze zaidi pale mlipoona umuhimu wa kupunguza *fee* au leseni ile ya u-*guide* kutoka dola 50 kwa kila mwaka mkaweka shilingi 100,000 kwa miaka mitatu. Hii itaongeza kipato cha wale watumishi kabisa ambao ni ma-*guide* ambao tunawahitaji sana katika kuwaongoza watalii lakini niwaombe mkaangalie sasa maslahi ya hao wengine huko chini, wale wapishi, ma-*porter* na kadhalika. Hawa wanaweza kupata faida zaidi kama mtaweza kuwaangalia hawa wafanyabiashara wa utalii kuwapunguzia zile kodi ambazo zinaonekana nyingi ni za kujirudia rudia ili basi na wao waweze kuwaangalia wale makuli - *porters* na wapishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungumzaji waliotangulia walishaongea, moja ya eneo la kuangalia ni barabara. Pamoja na kwamba mmesema fedha zile zitarudishwa kukusanywa kule, hili suala la barabara mimi nadhani, mbona ni kazi ndogo tu, mkiwa na vifaa ninyi mnaweza mkawa mnatumia wale wataalam wa *TARURA*. Kwa nini katika kila Wizara ama kama Wizara

yenyewe msiwe na vifaa kuendana na *zone* kwa ajili ya kurekebisha zile barabara hasa zile za kwenye mbuga kama Serengeti, Ngorongoro ili kupunguza gharama lakini ili kuweza kuzifanya ziwe nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi watalii, teknolojia inakwenda mbali watalii hawataki tena kurushwa rushwa, vumbi iliyozidi, barabara ni vizuri ziwe nzuri zaidi kwa sababu hata magari yanayokuja *model* mpya hayastahimili hizi barabara mbovu sana. Kwa hiyo naomba ma-*tour operators* wanapata hasara sana kwenye gharama ya kurekebisha yale magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona kwenye habari, wanahabari walienda kutembelea hoteli ya Burigi kule Chato, nimeona inaendelea kutengenezwa taratibu, wasiwasi wangu ni kwamba, kasi ya kuweka hela pale naona ni ndogo, ile hoteli nimeisikia muda mrefu. Ni vizuri tupeleke fedha ya kutosha miradi kama hiyo ikamilike lakini iweze kuleta tija haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho, Serikali haitaweza kuziendesha, nimesikia mchangiaji mmoja amesema na zile hoteli za Serikali zirudishwe, Hapana! hata kama zitarudishwa tutafute wabia. Kuna watu wame-*specialize* kwenye *management*, makampuni makubwa tufanye nayo na hii tunaweza kuangalia hata ile Hoteli ya Ngurdoto ambayo nasikia ilikuwa inakufa lakini juzi juzi naona tumefanikiwa kurudisha tena mikutano ya Afrika Mashariki. Namna ya Serikali kulipa lile deni na kununua *share* na kutafuta *management companies* hasa hizi za nje ili kuendesha hoteli kama hizo ziweze kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa Wizara ya Mipango kunatakiwa kulete tija ya haraka sana kwenye Wizara mbalimbali. Kwa mfano tu, Wizara ya Utalii kuna *component* ya *conference tourism* naona ipo Mambo ya Nje, *AICC* ipo pale lakini na ile Julius *Nyerere Convection Centre* sasa ule ni utalii mkubwa kwa sababu kwanza unaleta biashara kwenye hoteli na baadae wanaenda kutembelea vivutio. Nilikuwa naomba hii Wizara ya Mipango ione namna ya ku-*link,* vitu kama *AICC* wanapoenda kwenye utalii hawa *TTB* wanapoenda kutangaza wana- *incorporate* vipi?

Wanaangalia vipi namna ambavyo inaweza ikaunganishwa pamoja na utalii wetu huu wa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sehemu kama *ATCL* linawezaje kusaidia utalii nchini maana kwa mfano tu, kumekuwa na shida kubwa sana ya *cancellation* kwenye *ATCL* lakini tulitegemea *ATCL* ndiyo i-*compliment* utaliii. Ni namna gani Wizara ile ya Mipango itafanya kazi na Wizara hii ifanye na Uchukuzi ili kuleta tija.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye mahoteli, uwekezaji pamoja na kuweza kupata *man power*. Kwa hiyo kuna mahali pa kuweza kufanya hizi Wizara ziongee. Wameelezea namna ambavyo wanaangalia *man power* lakini nataka nikuambie, kwenye *man power* Tanzania tuna shida kubwa ya *customer care,* tuna shida kubwa ya kiingereza na lugha nyingine, masoko mapya, Kirusi, Kichina, Kituruki. Ni vyuo gani vinafundisha hayo masomo vizuri ili hao watalii tunaotaka milioni tano watakaotoka kwenye masoko mapya wapate watu ambao wataongea nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuhimu sana hayo mambo yaweze kuunganishwa. Nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tarimo. Basi nimuite Mheshimiwa Festo Richard Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei na muda ukiruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Jambo la kwanza ninaunga hoja mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nipende kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii ambayo mimi pia ni Mjumbe, Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kazi kubwa ambayo ameifanya ya Kibunge ya kuheshimisha Bunge lakini pia kuangalia mustakabali mpana

wa Taifa letu, maono na vipaumbele vya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba Kamati inaleta ripoti ambayo inaakisi maisha halisi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na mambo machache. Jambo la kwanza Mheshimiwa Waziri hatuna nia mbaya na Wizara yako, haya yote tunayafanya kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu. Mheshimiwa Waziri hatuna kabisa nia mbaya na watendaji wako, haya yote tunayazungumza kwa mustakabali wa wananchi wetu walioko nje ambao nao wanategemea sisi kama Wawakilishi wao tuguse maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Makete tuna hoja moja Mheshimiwa Waziri kuhusu *re-grow*. Mradi wa *re-grow phase two* tunawaomba sana mtupangie hifadhi yetu ya Kitulo iweze kuingia katika mradi wa *re-grow phase two*. Tuna uhitaji wa barabara, tuna uhitaji wa kiwanja cha ndege pale Kitekelwa nashukuru wataalam walikuja lakini kuna uhitaji wa *accommodation*. Mheshimiwa Waziri *re-grow* ikija Kitulo itaisaidia hifadhi hii ya kipekee Barani Afrika, hifadhi ya maua lakini pia tulileta pendekezo kwenu la kuongezewa idadi ya wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wanyama mlituletea nadhani utafiti utakuwa umekamilika kwa sababu wanyama wamekaa zaidi ya miaka kumi pale. Inawezekana umeshakamilika utafiti huo, tunahitaji kuongezewa idadi ya wanyama ili tuongeze idadi ya watalii kwa maana ya Jimbo la Makete. Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana kwenye *re-grow phase two* Kitulo isisahaulike.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye suala la bilioni 19. Waheshimiwa Wabunge kama Kamati tuliliona hili jambo la bilioni 19. Kwanza nia njema ya Mheshimiwa Rais, kwa sababu sisi kama Kamati tulishapitisha Bajeti ya Wizara ya Maliasili kwenye Kamati yetu lakini Mheshimiwa Rais akaona ni vyema Wizara hii aiongeze bilioni 19. Sisi kama Kamati tukaangalia mgawanyo wa fedha ulioletwa na Wizara hauna tija kwa maslahi mapana ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyongeza ya bilioni 19 unatoa bilioni 5 pekee ndiyo unapeleka kwenye shughuli za maendeleo, *the rest* bilioni 14 inaenda kama *OC,* wakati Wizara tayari ilishapitisha *OC* yake kwenye miradi mbalimbali. Hii sisi kama Kamati tumeona hatuwatendei haki Watanzania, tumeona ni vema Bunge na kama ambavyo Mwenyekiti ametushauri kwenye ripoti yake mtusaidie jinsi gani tuweze kuokoa fedha hizi ziweze kwenda kuleta tija kwa Watanzania. Sisi Wabunge tuliona ni vema fedha za maendeleo zikawa ni nyingi kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi ya leo tulitaka tuahirishe Bunge hapa kwa sababu ya changamoto ya mamba kule Buchosa. Wale watu wanachokihitaji ni kuona mamba wanavuliwa na ni fedha hizi zinatakiwa zitumike.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, achana na hiyo ukienda kwenye hifadhi zetu, moja kati ya hifadhi sisi tunatanganzwa kama kivutio namba mbili kwa utalii duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya changamoto kwenye hifadhi ni changamoto ya miundombinu mibovu ya barabara. Achana na hivyo, nenda kwenye suala la kupamba na tembo. Tuna changamoto ya vituo vya askari havipo. Wizara haina fedha ya kujenga vituo vingi. Tuliona kwamba fedha iwelekezwe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi lukuki zinazoibeba Wizara ambazo kama tutatumia fedha hizi kugusa maslahi ya Watanzania, tutakuwa tumeokoa jambo kubwa sana. Kwa hiyo, mimi naliomba Bunge lako na ninamuomba Mheshimiwa Waziri, hatuna nia mbaya; tunajua ni mchapakazi sana na kwa kweli ametuhusisha sisi Waheshimiwa Wabunge kwenye shughuli nyingi za utatuzi wa matatizo ya wananchi wetu, lakini kwenye hili la shilingi bilioni 19, sisi kama Waheshimiwa Wabunge hatuwezi tukawa tayari. Lazima tulinde fedha ya Serikali yetu na ni lazima tuguse maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana mgawanyo wa fedha hii tukaachana na mambo ya *OC* ambayo

mlikuwa mmeyapanga ya hizo shilingi bilioni 14 kwenda kwenye matumizi ya kawaida twende kwenye utaratibu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *issue* ya nchi. Tukizungumza wataalamu wanakuja na lugha nyingi za kwamba, unajua ukomo wa bajeti *framework,* kikaenda yaani panda shuka nyingi. Sisi tunazungumzia maisha halisi ya Mtanzania ambaye ukimwambia suala la ukomo wa bajeti au *framework* ya bajeti haifanyi kazi hawezi kufahamu. Anachofahamu kuna tembo wanasumbua kwenye eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Kamati tuliona ni vyema Mheshimiwa Waziri utusaidie hizi fedha ziende kuleta tija kwa wananchi wetu. Hatuko tayari kuona kwamba huu mgawanyo wa fedha unaenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naipongeza Serikali. Watu wa *NCAA* na Watu wa *TANAPA* fedha imerudi kwenu; mnakusanya na mnapanga matumizi. Hili lilikuwa ni kilio kikubwa cha Wizara kuona hili jambo linafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu ni moja. Moja kati ya kashfa kubwa za *TANAPA* na *NCAA* ni matumizi mabaya ya fedha. Ninayo *Report* ya *CAG*, ukisoma *Report* ya *CAG*, *TANAPA* na Ngorongoro hawana *record* nzuri kwenye *Report* ya *CAG* kwenye matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kurudisha fedha hizi hatutegemei kuona tena bodi zinaenda kukaa Ulaya. Hatutegemei tena kuona matumizi ya fedha yakiwa mabaya. Tunategemea udhibiti mkubwa wa fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua baada ya kurudisha fedha hizi kukusanywa *TANAPA* na *NCAA,* kuna msururu wa watendaji wa Serikali wataanza kuomba kazi kwenye *NCAA* na *TANAPA* kwa sababu tayari wameshaona kichaka na asali ya fedha iliyoko kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunakuomba Mheshimiwa Waziri, simama imara, dhibiti matumizi. Mheshimiwa Rais anakutegemea uta-*control* hili jambo, baadaye Serikali isituone *burden* kwa sababu moja kati ya hoja ya Serikali kuondoa hizi fedha kukusanywa na Serikali Kuu ilikuwa ni matumizi mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumezirudisha, tunaomba Mheshimiwa Waziri simamia fedha hizi zikusanywe vizuri ziweze kuleta tija na hifadhi zetu lazima tuone *development*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu haya magari ametoka kuzungumza hapa Mheshimiwa Mbunge wa Moshi, magari ya *four wheels* hizi zinazotumika sasa hivi kwenye hifadhi zetu zimepitwa na wakati. Sasa hivi watu wanataka kutumia magari ya kisasa lakini barabara zetu haziruhusu. Ni fedha hizi zitaenda kutumika kusaidia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo yalikuwa ni ya kwangu. Mwisho kabisa, tunaiomba Bodi ya Utalii ndiyo *custodian* wa utangazaji wa utalii... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua. Jambo moja tu kwenye suala la utalii kwa sababu Mheshimiwa Rais ameonesha njia, siyo kila mtu anafaa kutangaza utalii. Mheshimiwa Waziri unajua hata wewe mtu wa kukuombea kura, siyo kila mtu atakuombea kura ushinde. Kuna mtu akikuombea kura unaanguka. Tunaomba utalii wetu utangazwe na watu *smart* na muwaachie *custodian* wa utalii watangaze utalii wa nchi hii... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga, muda wako umeisha; umeeleweka.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na Mungu akubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei na huyo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunifanya niwe wa mwisho kwenye kipindi hiki cha asubuhi. Mimi nianze kwa kumsifu na kumshukuru mtukufu Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwa mdau wa kwanza wa Sekta hii ya Utalii na kujua kwamba, Sekta hii ya Utalii ilitakiwa iwe ni Sekta ya kipaumbele baada ya Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utalii pekee ndiyo inaweza ikatuletea ukuaji mkubwa wa Pato la Taifa kwa wakati bila kuwekeza sana. Halafu pia, inaweza ikatusaidia sana kuongeza fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwamba, unapozungumza kwa mfano Sekta ya Madini ambayo tumeichangamkia. Sekta ya Madini fedha yote ya mapato yake inayopatikana, mapato yake yote makubwa yanaishia nje na fedha za kigeni zinazokuja pengine unaambulia asilimia sita ile ya mrahaba tu. Kwa hiyo, mimi nasema hii ni Sekta muhimu na bila kupoteza muda ninataka nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Utalii, Mheshimiwa Kairuki pamoja na Naibu wake na viongozi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hiyo kwa mambo tuliyosikia toka asubuhi yakisomwa kutoka Buchosa, halafu baadaye tukasikia kutoka kwa Kamati na kwenye hotuba yenyewe ya Mheshimiwa Waziri inahitajika pengine tufanye upya tathimini ya sera, sheria na kanuni za hifadhi za wanyamapori na hifadhi za misitu kwa sababu kuna changamoto nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona kwamba tunaendelea kutenga hifadhi bila kujali kwamba wanadamu nao wanahitaji sehemu za kukaa na halafu hizi hifadhi zinakuwa ni *heritage* ya dunia nzima. Sasa inavyokuwa vile, ni lazima Dunia nzima iwe inachangia kwenye kufidia wale watu au wananchi wanaohamishwa au wale wanaopata athari mbalimbali. Kwa hiyo, *somehow* tutafute njia ya kuwalazimisha wenzetu kwenye

hizo nchi tajiri waweze kuwa wanachangia kwenye athari zinazotokana na uhifadhi huu wa hifadhi za wanyama pamoja na misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, kwa mfano pale kwangu, kwenye Jimbo langu la Vunjo, Kijiji cha Komela, Kitongoji cha Komela, tarehe 09 Mwezi Mei, mwaka huu, askari wa hifadhi walimpiga risasi mbili kijana wangu na mpigakura wangu mwenye miaka 39, Octavian Temba. Baada ya kumpiga kijana huyo alikufa pale pale. Kijana huyo aliacha familia ya watu watano, mmoja akiwa bado hajazaliwa lakini wanne wakiwa ni wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nikasema, kweli nilitakiwa nilete hoja binafsi Bungeni hapa lakini nikajizuia sana. Nikatumia nguvu zangu sana kujizuia nisilete ile hoja wakati ule kwa sababu walisema ngoja uchunguzi ukamilike; lakini zaidi nilisaidiwa na Mheshimiwa Waziri msikivu. Mheshimiwa Waziri alinipigia simu akaniambia subiri tuone sheria itachukua mkondo wake na kweli wale askari walikamatwa na kuwekwa rumande. Sijui wamefikia wapi lakini tunafuatilia jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba, pamoja na kwamba *KINAPA* walishiriki katika mazishi ya yule kijana baada ya wananchi kuwa wakali sana na kuvuruga miundombinu lakini nafikiri lazima Serikali itoe tamko lingine, kwamba hata rambirambi hawajatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe rambirambi kwa familia iliyobakia. Ni watu masikini na ni watoto. Watoe rambirambi na ninaomba kwamba Serikali iweze kutoa neno au kauli kwa suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba Kamati na pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea kwamba, inataka kuongeza fidia kwenye maeneo hayo yanayotokana na hifadhi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu kijana alikuwa anakata majani tu ya ng'ombe. Kwa hiyo, alikuwa hakati mti au hafanyi

chochote. Naomba hicho kifanyike na hiyo Sheria sasa ikiwa *reviewed,* tuweze kuona ni namna gani tutaingiza masuala mazima ya kuvuna wanyama, masuala mazima ya *carbon trade*. Hii *carbon trade* inatakiwa kuleta fedha za kufidia wale watu wanaokaa jirani ambao walikuwa wananufaika kukata majani na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hile *concept* ya *carbon trade* mimi niliizungumza hapa baada ya hili suala la nusu maili kushindikana, nikasema basi tufanye *carbon trade* hela ikipatikana, sehemu ya ile hela iende kwa wale wananchi wa vijiji vinavyozunguka ile milima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utalii, natoa pongezi sana kwa *TATO* na *TAHOA*, ambao wameingia wenyewe wanaanza ku-*market*. Wanaenda kwenye Soko la Dunia na kwenye mikutano ile mikubwa wanaenda kuuza utalii wetu wakati hapo zamani ni Serikali ndiyo ilikuwa inafanya yenyewe. Sasa hivi binafsi wanaenda na ndiyo sababu wanaleta tija na ongezeko kubwa linatokana na jitihada za kutangaza za watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi, lazima tuwasaidie. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ametangaza kwamba, tozo zinatolewa na leseni zinafanywa upya kwa mfumo mpya. Nasema kwamba, tatizo la watu wanao-*operate* biashara hapa nchini, wote tunaowasikia wanasema tatizo pamoja na hizo tozo kuwa utitiri lakini zikusanywe na mamlaka moja. Hiyo mamlaka moja izisambaze kwenye zile mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *issue* ya kwamba mtu mmoja anaenda kulipia leseni au kulipia *levy* mahali kwa watano na hajui ni wangapi kwa sababu wanaongezeka siku hadi siku inakuwa inaongeza sana gharama ya kufanya biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sasa pamoja na haya yanayofanyika basi kwa kusaidia wafanyabiashara wote basi Mheshimiwa Waziri azungumze na Mheshimiwa Waziri mwenzake ili tuhakikishe kwamba hizi tozo zinakusanywa mahali

pamoja. Pia, tozo hizo kuna zingine hata hazi-*apply*. Kuna hizi mamlaka zote za *NEMC, CAMARTEC, LATRA, TBS, TARA* kwa upande wa hawa, *Local Government Authority* na wenyewe wanakusanya *service levy,* inakuwa *very difficult*. Kwa hiyo, naomba hilo suala lichukuliwe na litiliwe maanani na mambo haya yakamilike kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha. Nina matangazo machache. Tangazo la kwanza ni wageni.

Tunao walimu na wanafunzi wa Chama cha *Scout Tanzania* wa Shule za Msingi na Sekondari za Kilimani, Carisa, Hekima, Waldorf, Kiluvya, Balewa na Mshikamano kutoka Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani. Hebu wasimame tuwaone. Karibuni sana. Watoto simameni kwa kujiamini; karibuni sana. *(Makofi)*

Baada ya hilo kuna tangazo lingine. Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi wanaombwa kuelekea *Speaker's Lounge* mara baada ya Bunge hili kusitishwa.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporejea tutaanza na Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Abbas Tarimba na Mheshimiwa Riziki Said Lulida. Hawa ndiyo tutakaoanza nao mchana.

Baada ya kusema hayo nasitisha Kikao hiki cha Bunge mpaka saa 11. 00 jioni.

*(Saa 7.11 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deudatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano kwenye Wizara hii. Wachangiaji wetu tutakaoanza nao, nitamwita Mheshimiwa Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa na Mheshimiwa Mhata ajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika ratiba hii ya jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye Wizara moja kwa moja naomba nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali, hasa kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameweza kukuza utalii na hasa kupitia ile *Royal Tour*. Tumeona sehemu kubwa mapato ya kitalii yameongezeka sasa maradufu. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu pia niseme kuwa ninawapongeza sana Mawaziri katika Wizara hii, Mheshimiwa Kairuki pamoja na Mheshimiwa Kitandula. Wizara hii huwa ina changamoto nyingi sana, lakini wanafanya kazi nzuri sana, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tulipewa dakika nane mimi niende *chap chap* kwenye masuala ambayo ninayaona kuwa ninaweza kuyazungumzia ili nisirudie ya wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta yetu ya utalii inakuwa sana, lakini ukiangalia hata kwenye maoni ya Kamati, mimi nipo kwenye Kamati hii ya Ardhi, Maliasili na Utalii, utegemezi bado ni mkubwa, ukiangalia bajeti kwenye maendeleo katika Wizara hii bajeti kubwa ni tegemezi, kwa maana ya kwamba tuna kama 32% ambayo sasa ndiyo mapato ambayo ni ya ndani, lakini asilimia takribani sitini na kitu ni mapato ya nje, hii ni hatari. Tunatakiwa tutoke hapo, Wizara iangalie namna ya kuweka mkakati ili tuweze kupandisha mapato yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 32 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna lile suala la uvunaji wa wanyama wakali na waharibifu. Kuna kitu kimenishangaza kidogo, kwa mwaka 2022/2023 ukiangalia ile orodha nimeshtuka kidogo kwamba wanasema waliweza kuvuna nyani 10, viboko 28, mamba 21 na wanyama wengine, lakini nikiangalia tatizo la nyani lilivyo kubwa mwaka 2022/2023 nyani 10? Hawa kila mimi ninapokwenda Tabora naweza nikakutana nao tu pale Nyahua zaidi ya nyani 100 wapo barabarani wanavizia mahindi ya watu na mazao mengine. Sasa kwa nyani 10 tu sijaelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata upande wa viboko, kwa viboko 28 ni kidogo sana. Mimi nina tatizo kubwa sana, kwa mfano kule Tabora tuna Bwawa la Igombe, viboko ni wengi na nimeshawahi kuzungumza hata kwenye Wizara, kwamba tuangalie namna gani ya kuvuna wale viboko ili kuwapunguza, kwa sababu watu wengi sana wanauwawa maeneo yale, hasa Kata ya Kabila na Kata ya Misha - Tabora Mjini kumekuwa na majanga makubwa sana ya viboko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa uvunaji huu niliouona hapa wa kweli Mheshimiwa Angellah pamoja na ndugu yangu, Naibu Waziri Mheshimiwa Kitandula mzidishe *speed* kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mbuga nyingi ambazo zina upungufu wa wanyama, zipo. Kuna mbuga nyingine unaweza kukuta kuna nyati tu na wanyama wengine, wengine hawapo. Waangalie namna mnavyoweza kuvuna wale wanyama na kuwapeleka mbuga zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanyama kwa mfano tembo, mimi ninavyofahamu tembo ni mmoja kama siyo wa kwanza basi hawezi kuvuka wa pili. Tembo ana kumbukumbu kubwa nadhani kuliko wanyama wengine wote. Zile njia zile ambazo zinaitwa shoroba, tembo hata kama alipita miaka 100 iliyopita leo anaweza kupita tena pale pale. Sasa wangeangalia namna ili sehemu kama zile wakaweka uzio *(fence)*. Uzio uwe katika maeneo yale tu ambayo wanaweza kutoka, inaweza ikasaidia sana, kwa sababu lazima apite pale pale. Hata hapa Chuo Kikuu cha Dodoma wamewahi kuja kwa sababu inaonekana miaka hiyo walikuwa wanakuja kula sehemu zile. Kwa hiyo waangalie namna mnaweza kuwadhibiti wanyama katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malikale, tulikwenda Kilwa na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake wanahudhuria sana ziara za Kamati. Mali kale ni muhimu sana, tume-*base* sana kwenye wanyamapori zaidi na tunasahau malikale. Ule Mji wa Kilwa, aliongea hata Mheshimiwa Ndulane asubuhi, una historia kubwa sana. Mji kama Kilwa kuwa na *currency* yake, si tu kwamba ilitumika *East Africa,* tuliambiwa mpaka Australia. Leo ile misikiti 99 iliyotajwa hapa tulikwenda tukakuta misikiti kama minane tu hivi nayo tunaambiwa ilifukuliwa fukuliwa. Kule chini ya ardhi kuna misikiti isiyopungua 90 ya miaka hiyo kwa mujibu wa watu wa maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna historia kubwa, ndugu yangu Mheshimiwa Ndulane naona hakuitaja hapa, wale wazee si tu kwamba walijua kuandika wakati ule, kwa ndugu zetu Waislamu tulipokwenda pale tuliwaambia wale wazee miaka hiyo kuna wazee waliondoka na melikebu walikwenda kuonana na Mtume Mohamad kule Saudi Arabia na walionana naye na wakarudi. Wazee wale hakuna historia yao, wazee wale hata majina yao tulipouliza hayakuhifadhiwa, kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kubwa sana la utalii hata kidini. Ule Mji wa Kilwa tulielezwa kwamba katika miaka hiyo ule mji ndio ulikuwa kati ya miji 200 ya dunia ambayo ilikuwa inaongoza kwa uzuri na biashara. Wakati ule baada ya biashara

ya utumwa kuwa *ceased,* wale walikuwa wnaongoza kwa biashara ya dhahabu na biashara zingine. Haya mambo yamekufa kwa kiwango kikubwa, mji ule unazidi kuwa ni mji ambao sasa vile vyanzo vya utalii vinaendelea kupotea. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri, kama inapatikana nafasi, kufukua maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la migogoro ya mipaka; migogoro hii ya mipaka ni lazima iwepo kwa sababu ongezeko sasa ni kubwa, tupo watu milioni 62 *plus,* watu wameongezeka sana, kwa hiyo na makazi pia lazima yaongezeke. Watu wetu lazima watafutiwe sehemu za kukaa, kuwe na mpango ambao ni endelevu ambao hautaleta vurugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kipekee niungane na wengine waliotangulia ku-*appreciate* kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais kwenye kukuza utalii, amekuwa *champion* wa utalii katika nchi hii, kwa hiyo na mimi niungane na wengine kwenye kumpongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake kwa hotuba nzuri, kwa usimamizi wa maandalizi ya hotuba hii na bajeti hii ambayo aliikuta njiani ambayo wameendelea nayo na sasa wanaimalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mimi jambo moja tu la muhimu, nitakuwa na uchangiaji kama sehemu mbili, hasa mambo yanayohusu jimbo langu, halafu baadaye nitakwenda kwenye mambo ya jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *record* za Bunge nadhani nimekuwa nikiongelea sana suala la ardhi kwa wananchi. Mwaka 2022 Mheshimiwa Rais akiwa Bukoba kwenye Uwanja wa Kaitaba tarahe 9 Juni alitoa maelekezo *specific* kwa Mkoa wa Kagera kwamba tutafute maeneo kwa ajili ya kufanya shughuli za kilimo na ufugaji ili tuweze kunyanyua uchumi wetu na Ilani pia ya CCM imehaidi kwenye habari ya kuongeza maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kelele yangu kubwa au jambo ambalo nimekuwa ninaliongea ndani ya Bunge ni kwamba maeneo hayo hayapo kwenye mikono ya watu, ni maeneo ya Serikali, kwa sababu Mheshimiwa Rais anavyoelekeza akasema maeneo yatafutwe, maana yake anaelekeza watu wake watafute maeneo. Sidhani kama anaelekeza wananchi watafute maeneo na wananchi kama walikuwa na maeneo hawana haya ya kuomba maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa habari ya Wilaya ya Biharamulo; nataka tu nitoe rekodi nzuri niingia katika rekodi za Bunge. Sensa ya mwaka 2002 Biharamulo ilikuwa na wakazi 159,055, lile eneo letu la makazi na kilimo likiwa hekta 183,400. Mwaka 2012 tumetoka laki moja tukaenda 323,486, eneo bado ni lile lile 183,400. Mwaka 2022 457,114 eneo bado ni lile lile 183,400. Niliposimama hapa Jimbo la Biharamulo ndilo jimbo linaloongoza kwa idadi ya watu kwa Mkoa wa Kagera, lakini miaka zaidi ya 20 eneo la makazi na kilimo bado ni lile lile. Ni jimbo la 20 kwa wingi wa watu Tanzania kati ya majimbo 264.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuwezi kila siku idadi ya watu inaongezeka, hatuna shughuli nyingine, sisi hatuna maeneo ya viwanda kama Njombe, shughuli yetu kubwa Biharamulo ni kilimo na ufugaji. Kama idadi ya watu inaongezeka, lakini hatupewi maeneo ya kulima wala kufuga, *what is the meaning* ya watu kuwepo pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikihamasisha watu wazae na kuongezeka, miundombinu inaletwa, lakini watu hawapewi maeneo ya kufanya shughuli za uchumi. Hii inasikitisha na inaumiza. Watu wangu wamekuwa wanaishi kama wakimbizi kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe na Mheshimiwa Waziri anaelewa kwamba nilishapeleka maombi ya kata nne kwakwe. Kata ya Nemba nikaomba hekta 5,000 tu tuanzie, nikaomba Kata ya Nyanze eneo la Rukako hekta 5,000 tu tuanzie, nikaomba pia Kata ya Nyakahura waongezewe eneo, nimeomba Nyakanazi waongezewe eneo pale hekta 5,000, pia nimeomba na Kata ya Katahoka waongezewe eneo. Tukishapewa haya maeneo hawa watu wanaofuga na kulima wataweza kupata maeneo mengine, hatuwezi kuongeza idadi ya watu ambao hawana maeneo ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi mifugo yao hata na maisha yao ya kawaida wananchi wanateseka. Mimi niliuliza hapa kwenye taarifa za Kamati wakati uliopota, nadhani ilikuwa Bunge la mwezi wa pili, hivi mtu anayekwenda kuokota kuni, kama kweli mnatufanya sisi maeneo yale yapo kwetu, tumezaliwa hapa na sisi ndio wahifadhi wa kwanza, kwa sababu muhifadhi ambaye ametoka darasani si muhifadhi wa kwanza, asingeyakuta, wahifadhi wa kwanza ni wananchi wa lile eneo wale watu lazima washirikishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi unashangaa ulinzi shirikishi ni wa nini? Mbona polisi hawa wa kawaida tunashirikiana nao vizuri, tunakuwa na ulinzi shirikishi? Wanajeshi mbona hawagombani na wananchi? Shughuli nyingine au vyombo vingine mbona havigombani na wananchi? Kwa nini kila siku *TFS* tu?

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba tusaidiwe kupitia Bunge hili, hawa watu ni Watanzania na hili Bunge ni lao lazima nije niwasemee hawawezi kuja humu. Ninachoomba tuongezewe maeneo ili watu wapate maeneo ya kufanyia kazi kwa sababu shughuli zao za uchumi zinakwama. Hilo jambo ninaomba niliweke

*specific*. Wafugaji wangu wanateseka, kwa laki moja, moja hizi sasa imefikia *stage* watu wamekuwa watumwa. Tulikwishaomba maeneo tuongezewe mule ndani ya hifadhi naamini Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hilo atalifanyia kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninayo Hifadhi ya Burigi pale kwangu, hii hifadhi Mheshimiwa Rais alipopita Biharamulo tarehe 8 Juni, 2022 nilimuomba eneo na geti la kuingilia kwenye hifadhi kupitia Biharamulo Mjini. Hayo ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, alisema amepokea na akatoa maelekezo lifanyiwe kazi. Kwa hiyo, ninaomba kwenye kuhitimisha Mheshimiwa Waziri, nadhani yeye hakuwepo, lakini Serikali ni ile ile, ningeomba nipate majibu pia wakati anahitimisha ili nijue tunaishia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Hifadhi hii ya Biharamulo – Burigi, Mheshimiwa Waziri alipokuwa na kikao na Wabunge wa Kagera nilisema, kwamba watu wangu wanakamatwa kwa sababu ng'ombe wanaingia mule, lakini kuna makundi ya ng'ombe wa wageni wengi sana ambao wameingizwa mle. Hii inaharatisha usalama wa nchi yetu na usalama wa Wilaya yetu ya Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama unaweza ukahesabu simba ukajua ni wangapi ukatuambia hapa, ukahesabu nyati, ukahesabu chui na vitu vingine, kipindi mnahesabu hawa wanyama hizo helikopta zinazohesabu hao wanyama hao ng,ombe hamuwaoni kweli? Kwa hiyo nilikuwa naomba ng'ombe wale waondoke kwenye hifadhi kwa sababu hauwezi kuweka ng'ombe wa watu wengine, tena si Watanzania, ni wageni halafu ng'ombe wa watu wetu kwenye hifadhi tu ya *TFS* wanakamatwa. Nilikuwa naomba hilo nipate jibu, nilisema pale wakanihaidi kufanya *operation* maalumu, *operation* sijaiona hadi leo naingia kwenye bajeti, kwa hiyo naomba mnisaidie kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine cha muhimu, Mheshimiwa Waziri alinihaidi kwamba wanahamisha tembo Kimisi mnawaleta Burigi. Sasa ndugu yangu, kelele za tembo hapa zimekuwa kubwa. Watu wa Nyakahura kwangu pale hawalali usingizi. Sasa tena uchukue tembo zaidi ya 200 uwatoe Kimisi

uwalete pale, jamani hivi kweli hapa si kuniongezea matatizo Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba, kama wanyama wanakuwa wengi tufanye kazi ya kuwavuna, hamuwezi kuwa na vitu visivyovunika, kwa nini tusiangalie jinsi ya kupunguza hawa wanyama? Huenda wamezaliana sana, hivyo tuwapunguze ili wananchi waweze kuishi kwa ahueni hali kadhalika na wanyama wasilete vurugu kwa wananchi. Nilikuwa naomba hilo mliangalie, ni jambo la muhimu sana sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nina kata moja inaitwa Kata ya Kalenge, Mheshimiwa Naibu Waziri anaelewa, kuna viboko zaidi ya 20 kwenye mto ambao upo kijijini. Alikwishatuma watu kutoka Kigoma wakaja wakaangalia. Tunachoomba wale viboko waondolewe, kile ni kijiji cha wananchi siyo hifadhi, waondoeni muwapeleke sehemu nyingine ili wananchi waweze kufanya kazi kwa amani, kwa sababu wamekwishaharibu mazao mengi sana na wamekwishawaumiza wananchi kule na hiyo mnayotuambia fidia kila siku ninapiga simu kwa ajili ya hiyo fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameshaumiza na wananchi kule, kuna nyati amepiga mwananchi akamuua. Shilingi milioni mbili anayosema wameongeza haina thamani ya kifo cha mtu, hata kama wangeweka milioni 100. Fedha hii bado ni ndogo kwenye kulipa fidia. Nilikuwa naomba aangalie jinsi ya kufanya ili angalau wananchi wanaoumia na wanaoumizwa na hawa wanyama waharibifu kiwango kiongezeke kidogo ili na wao wapate ahueni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Chiwelesa. Nimwite sana Mheshimiwa Yahya Ally Mhata atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha mchana huu kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba Wizara hii inafanya kazi ya kuinua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni mashahidi tumeona jinsi alivyoshiriki katika filamu ile ya *Royal Tour* na jinsi gani filamu ile ilivyoweza kuongeza mapato ya nchi yetu, lakini pia yeye pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar walivyoshiriki katika hii filamu ya *Amazing of Tanzania* ambayo nina uhakika ita-*boost* uchumi wa nchi yetu na kuwavutia watalii kwa wingi. *(Makofi)*

Naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii kwa jinsi alivyoingia katika Wizara hii na alivyowashirikisha Wabunge wote, kukutana nao na kuweza kutoa changamoto zetu mbele yake. Nina imani yale ambayo tulimweleza Mheshimiwa Waziri atayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Naibu wake kwa kweli amekuwa msikivu sana. Naibu muda wowote ukimpigia simu anapatikana na anatoa ushirikiano mkubwa sana. Kwa hiyo, ninaombwa nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba anaye naibu makini na afanye naye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie maeneo yafuatayo; kwanza kuhusu wanyama waharibifu. Tumekuwa na changamoto sana katika nchi hii ya wanyama waharibifu. Kwa mfano, ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu tunao hawa wadudu wanaoitwa tembo au wanyama tembo. Wanyama hawa wamekuwa waharibifu na huhatarisha maisha ya watu wetu. Tarehe 9 Mei, 2023 kuna mama mmoja Bi. Mwanaali alipoteza maisha kwa kushambuliwa na tembo, lakini juzi tarehe 10 Mei,

dada yetu Zena Maganga alipokuwa nyumbani kwake, akienda kuchota maji alishambuliwa na tembo na kupoteza maisha, lakini jambo la kusikitisha Wizara haijatoa rambirambi kwa wafiwa hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba Wizara ijiongeze itoe rambirambi kwa wafiwa pindi wanapopata taarifa hizi za kuhuzunisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wamekuwa kikwazo ndani ya jimbo langu, ndani ya mwaka huu wameshambulia ekari 460 za mazao, lakini mpaka hivi navyozungumza ni ekari 11 watu watatu wamelipwa fidia, ekari 460 unalipa ekari 11, hii tunafanya mchezo na maisha ya watu, wale watu shamba ndiyo maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Sengenya, Nangomba na Lumesule wananchi wameathirika na mazao yao, lakini mpaka sasa hivi wizara imekaa kimya pamoja na kuwapatia taarifa. Kwa hiyo, ni matarajio yangu kwamba hili kesho atakapohitimisha Mheshimiwa Waziri lazima atoe kauli, wananchi wangu watalipwa lini fidia ili na wao waweze kujikwamua na maisha yao, vinginevyo, kesho hatutaelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni wanyama waharibifu (mamba), mimi napakana na Mto Ruvuma. Hivi ninavyozungumza zaidi ya watu kumi wameawa na mamba na mpaka leo ni watu watatu tu wamelipwa kifuta jasho. Maisha ya binadamu yanapotea kwa sababu ya wingi wa mamba ndani ya Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hotuba ya Waziri, hakuna mahali palipozungumziwa jinsi gani ya kuwapunguza mamba katika Mto Ruvuma au kujenga vizimba ndani ya Mto Ruvuma, hili jambo halikubaliki. Tumepoteza watu zaidi ya kumi, watu zaidi ya 30 ni walemavu, hili jambo linahuzunisha sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakuomba kesho utakapokuja utupatie utaratibu utakaoutumia kupunguza mamba wale au jinsi gani ya kujenga vizimba ndani ya Mto Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hizi pesa ambazo zimeongezwa na Mheshimiwa Mama Dkt. Samia ndani ya Wizara hii. Mimi naomba nitoe ushauri, kwanza nakubaliana na mawazo ya Kamati, naomba sasa fedha hizi zitumike kwenda kulipa fidia kwa wananchi ambao wameathirika na wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wananchi wanateseka halafu pesa zitoke zikafanye shughuli ambayo haina tija. Hebu jichukulie Mheshimiwa Waziri kama ungekuwa wewe shamba lako limeliwa, halafu fedha inaletwa inakwenda kutumika vile, ungekubali? Usiruhusu mambo yanafanyika ndani ya Wizara yakow ewe unayatazama, hili jambo halikubaliki Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba sana fedha hizi zitumike kwenda kuwalipa fidia wananchi ambao wamepoteza mali zao na wengine wamepoteza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kuzungumzia kuhusu *WMAs* hizi ambazo ni hifadhi za wanavijiji wetu. Wanavijiji wameanzisha hizi hifadhi kwa lengo zuri la kuhifadhi wanyamapori wetu, lakini Wizara au Serikali haiwaungi mkono, hivi ninavyozungumza fedha nyingi za hizi *WMAs* ziko chini ya Serikali na wananchi sasa wamekwishaanza kuona kwamba hawanufaiki na jitihada wanazozifanya katika kuwatunza hawa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuchukue wazo la Kamati, fedha zote ambazo zimechukuliwa na Hazina zirejeshwe kwa wananchi, zirejeshwe ndani ya vijiji ili wanavijiji waweze kuzitumia fedha hizi kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani fedha hizi ndizo ambazo zilikuwa zinajenga shule, vituo vya afya kule vijijini na kulipa mishahara ya hawa watu wanaolinda maliasili zetu. Leo hii kila kitu kimekuwa *abandoned* na matokeo yake ujangili umeongezeka kwa sababu wananchi hawaoni faida ya kuwa na hizi maliasili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tumerudisha fedha kwa *TANAPA*, kama tumerudisha pesa kwa Ngorongoro na hizi *WMAs*

zirejeshwe ili wananchi zirejeshwe ili wananchi waweze kuzitumia kwa shughuli za kuleta maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwangu ninayo *WMA* ambayo imejenga madarasa mpaka usawa wa *lintel*. Wameshindwa kuendelea kwa sababu hawana fedha, fedha zimechukuliwa na Serikali na hazirejeshwi. Kwa hiyo, nashauri fedha hizi zirejeshwe ili wananchi waweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna maombi yasiyopungua 16 ndani ya wizara yako wananchi wanaanza kutaka ku-*register* hizi *WMAs*, bado hazijafanyiwa usajili. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri mara baada ya kupitisha bajeti yako hebu nenda kazipitishe zile *WMAs* ambazo zimebaki ili wananchi waweze kwenda kuzifanyia kazi na hatimaye kulinda maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ila hili ambalo nimelizungumza kama kesho sitapata majibu nitashika shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhata, namwita sasa Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru sana na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kupata afya njema na kuwepo hapa. Vilevile, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa nafasi aliyoipata ya kuwa Makamu wa *WTO* Duniani, yeye sasa hibvi ni Makamu Mwenyekiti. Hii ni nafasi kubwa sana atakuwa amekaa kule akitutangazia utalii wetu wa Tanzania. Pia ninaamini kwa kazi na nafasi aliyoipata ni eneo sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia siyo hivyo tu, sasa hivi naona Tanzania inaanza kusisimkwa kwa ajili ya *Royal Tour.* Tumemuona mama ametangaza *Royal Tour* vizuri sana na kutokana na kuitangaza *Royal Tour* ndiyo maana sasa hivi tunaona mapato ya utalii wa ndani yameruka mpaka 161%, mapato ya Kimataifa

imeruka kwa 276%, haya ni mafanikio makubwa sana. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Dkt. Abbas Mwenyezi Mungu awabariki sana. Kwa kweli Dkt. Abbas alifanya kazi kubwa sana akiwa katika Wizara ya Michezo. Mimi baada ya kuja hapa nikasema kweli nimepata jembe, maana yake natamani angerudi kule, lakini huku nako naona mambo yamezidi kuwa mazuri. Kwa mafanikio haya Mwenyezi Mungu awabariki sana na muendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Watendaji, Wakurugenzi Wakuu wa *TANAPA*, Ngorongoro, pamoja na matatizo makubwa tuliyokutana nayo ya *Covid,* lakini naona uchumi umekuwa sana kwa asilimia kubwa sana. Tuwapongeze kwa kazi kubwa wanayofanya na wanakutana na changamoto nyingi, lakini Mwenyezi Mungu hii Wizara ni Wizara ya kuitegemea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi ina mapungufu sana ya *foreign currency* (fedha za kigeni), lakini kwa kupitia watalii wa nje tunapata fedha za kutosha. Pia hii inaweza kusaidia yale mapengo tuliyokuwa nayo yakasababisha na sisi kuweza kutatua Wizara hii. Pia mimi nasema kazi inahitajika kuendelea. Kazi iendelee ili mapato makubwa katika hii wizara yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Rais ya kutangaza *Royal Tour* na mimi ninaamini tuna Royal Tour kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Katika dunia siyo watu wote ambao wanahitaji na walemavu wanatkiwa wawepo katika Utalii. Kwa vile katika Sheria ya 2024 ya *Disability and Tourism* ni lazima isimamiwe, *inclusion*. Sasa tunatamani sana na sisi tuwe na *Royal Tour* na tuaalike wenzetu walemavu duniani. Kuna maprofesa, kuna watu wameingia katika vita, lakini walikuwa na pesa za kutosha na bado ni haki yao ya kimsingi ya kupata utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa hivi walemavu mpaka wanapanda Mlima Kilimanjaro, wanatembea na kuna

mazingira mazuri ya mahoteli ambayo kwa kweli ni lazima tuseme ahsante kwa Wizara yako kwa kazi kubwa mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia suala la migogoro; hii nchi kuna sheria, taratibu na kanuni. Tukisimama na sheria migogoro mnayoiona yote hii haitakuwepo, lakini kama hatusimamia na sheria, tukajichukulia sheria kama tunavyotaka sisi, basi kwa kweli migogoro hiyo haitakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tujifunze na tujiulize na kama kila mtu akijiuliza hivi ninachokifanya basi atajiona kabisa kuwa kuna mambo mengine tunafanya ni ya makusudi kusababisha migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Mama Riziki Said Lulida, Mama Tembo, Mama Mjusi, Mama Mazingira, lakini vilevile mimi ni Mama Selous. *Selous National Park* au *Selous Game Reserve* ilikuwa ni *reserve* ya nchi na ilikuwa ina wanyama wengi hasa tembo, lakini ninachokwambieni sasa hivi ningetamani ututoe Wabunge hapa utupeleke ukaone vurugu la ng'ombe liliko ndani ya Selous na Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza yule ng'ombe ameingia Selous, yule tembo amabaye alikuwa amehifadhiwa kule Selous atakwenda wapi? Ni lazima atakwenda vijijini mwa watu. Ina maana mlimharibia njia yake ya kupita ndani ya Selous na siyo katika mashamba ya watu, wafugaji wako Selous. Wafugaji wametoka walikotoka mpaka wamefika Selous na sasa hivi wanataka kuvuka Mto Ruvuma kwenda Mozambique, sasa huu ni uvunjifu wa taratibu na sheria na ndiyo matokeo yake migogoro ambayo haifuati sheria itaendelea kuwa mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukimaliza Bunge namuomba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri twende Tendeguru, lile ni eneo la hifadhi ambalo tayari walishapima wakinamama Jane Goodall, wafugaji wamepewa maeneo yao makubwa Mkoa wa Lindi na Pwani yote, wako Tendeguru na pale wanahakikisha wanamaliza msitu wa mipingo ambao ni *indigenous species* ambayo

tunaitegemea duniani kwa sababu bado miti michache tu ya mipingo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunasema nini ikiwa baadhi ya taratibu na sheria zinavunjwa na zikivunjwa watu watalalamika lakini unalalamika kwa mazingira yale, kama leo Tendeguru wangeiachia eanyama wakafika pale kama asili ya *corridor* yao, wale tembo wasingehama kwenda vijijini, maana yake tembo anatoka Niasa – Mozambique anavuka Namtumbo – Mbalang'andu anakuja mpaka Kiyegeyi, yule mnyama anakuja mpaka Liwale, akifika pale anakuta tayari ng'ombe na binadamu wamekuja wanakaa pale. Tembo atafika hapo? Tembo anabadilisha njia, akibadilisha njia anakwenda kwa binadamu. Bado tuko na sheria, sheria haijasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda na Naibu Waziri wakati huo akasema wafugaji watatolewa, mpaka leo wako pale pale. Hivyo, msitegemee kumaliza migogoro kama hamuwezi kufuata sheria na taratibu. Nchi isiyokuwa na sheria na taratibu haiwezekani kumaliza migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hatuna shida ya ardhi, tembea kutoka Dodoma na ninaomba mchukue vichwa vyenu mviangalia. Dodoma msitu, Singida msitu, Tabora mpaka Igunda yote msitu, hao mnakwenda mpaka Shinyanga mpaka mnaingia Mwanza msitu. Bado watu hawajaweza kukaa kwenye maeneo yale, lakini wanakimbilia kwenye maeneo ambayo ni tengefu kwa vile ardhi ile haijatumika, ina mbolea ya kutosha na maji, lakini kama tungekuwa tumetengeneza maendeleo makubwa katika halmashauri zetu ya kuhakikisha maeneo ya wafugaji wetu yamesimamiwa, wasingehama. Leo wafugaji waliopewa ardhi kusini wote maeneo waliyopewa wamekimbia wamekwenda maeneo mengine, sasa hii migogoro mingine ni ya sisi wenyewe kutokusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwana mazingira, tukimaliza misitu yote Tanzania tunategemea nini? Tunategemea mvua? Je, kipindi cha ukame tutafanya nini na nchi yetu ambayo tunategemea iwe na maendeleo? Haiwezekani, sisi Wabunge

tuwe vinara wa kusimamia mazingira, Tusiwe vinara wa kuchochea migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Balozi wa Utalii, tulipewa nafasi ya fulani ya kuzunguka na Wabunge, waliporudi hapa wote walinyamaza vichwa vyao. Walipofika ndani ya Selous pamejaa ng'ombe, ndani ya *Serengeti National Park* kuna simba, tembo na nyati, ndani kuna ng'ombe. Hivi jamani kwa nini mnavunja sheria? Kwa nini mnavunja taratibu kuifanya Wizara ionekane ngumu wakati tunategemea hii wizara ituletee mapato ya kutosha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapata mapato ya 17.2% ni fedha za kigeni, leo tunakwenda kwenye mabenki hakuna fedha za kigeni. Tunategemea hela za kigeni kutoka katika Wizara hii, hii Wizara ni ya kuisimamia, tuungane Wabunge, naomba kila mara mje mtufanyie semina ya kutuelewesha na baadhi ya Wabunge waende katika maeneo yao na kanda wakajionee haya mazingira ili watuletee majibu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Niasa Selous corridor,* ile *corridor* nafikiri hata Wizara wenyewe walifanya makosa. Maeneo anayopita tembo katika *corridor* njia ni nyembamba, basi wamepewa vitalu wanawinda kipindi tembo anapita, unategemea nini? Fujo tu. Sasa matokeo yake, mazingira magumu ambayo yanatengenezwa inayaathiri nchi katika mazingira yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia maeneo matatu, *TANAPA*, Ngorongoro hawa watu ndio wanatuingizia pesa za kutosha. Katika mabadiliko ya tabianchi mwaka huu wameathirika vibaya sana kwenye haya maeneo na watalii wanahitaji kupita katika sehemu ambayo ni salama, *security* yao iwe imelindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali, niko chini ya miguu yenu, pelekeni hela Ngorongoro na *TANAPA* ili barabara zile zijengwe mara moja ili inapofikia kipindi cha msimu wa watalii kuja Tanzania wasikutane na mahandaki, makorongo na

mabalaa ya barabarani. Maana yake wanahitaji kupita katika barabara ambayo iko salama na tunaamini nchi yetu iko salama. Mama ameiweka nchi iko *peace* kabisa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, niwashukuru sana Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, namwita sasa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza najua hii wizara ina Waziri mgeni, anatengeneza mifumo Wizara, lakini anakwenda vizuri. Nampongeza sana Mheshimiwa Kairuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri ndugu yangu Kitandula naye ameingia ni mgeni na anamsaidia kufanya kazi vizuri, lakini vilevile tuna Katibu Dkt. Abbas ambaye ni mzoefu anafanya kazi vizuri na watendaji wote na Makamishina wote wa *TANAPA*, *TAWA*, *TFS* wanafanya kazi vizuri. Tatizo lilikuwa kwenye hela na sasa kwa sababu tunawarudishia hela tunajua watafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo mawili katika Wizara hii, kwanza wapo watu wa *philosophy* wanaosema kwamba, katika utawala bora ufanye kuliko kutokufanya. Mheshimiwa Rais alipoanza kutembea porini watu walimuona kama anazurura tu, walisema kazi gani hiyo atafanya? Hata hivyo, leo kila mahali pameongezeka, watalii wameongezeka, fedha imeongezeka. Ni miaka mingi sana

hatujawahi kufika watalii milioni moja na kitu, sasa imekwishafika. Kwa hiyo, amefanya kazi kubwa ile ambayo watu walikuwa ni kazi ya kawaida, lakini imetoa matokeo makubwa sana, nimpongeze kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Rais wetu ni msikivu sana, tumezungumza mara nyingi sana kwamba, hawa watu wa *TANAPA*, *TFS* na *TAWA* wana maeneo makubwa sana ya utawala asilimia 32 *point*. Kuna hifadhi 21, lakini hifadhi zinazotoa hela ni tano tu au tatu, zote tunalinda. Tuna mapori 29 na mengine tengefu karibu 23 na tuna misitu karibu mia nne na kitu, yote haya yanahitaji fedha za kuyalinda haya mapori, vinginevyo yatabaki matupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulinda haya mapori hatuhitaji yote yaje na faida, kwa sababu kuna mambo mengine yako kwenye *environment type*. Unaweza kuzungumza kwa maana ya mazingira lazima kuwepo miti na mambo mengine ambayo yanatunza nchi yetu, siyo lazima yalete faida, kwa hiyo, yote yanalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekubali kuwapa zile fedha ambazo zilikuwa zimerudi kwa makusanyo yao na sasa zinakwenda kukaa na wao, maana yake ni yake ni kwamba watakuwa na uwezo mkubwa wa kulinda tembo na kuzuia ujangili kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hilo jambo ambalo amelifanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie fidia ambayo ni kifuta jasho na kifuta machozi, sasa sijui tatizo liko wapi, kila mara Wizarani wanatuambia fedha za kulipa kifuta machozi, lakini kila mara wanakwenda kufanya tathmini kwenye maeneo yetu ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo yangu ya Hunyari, Kihumbu, Mariwanda, Sarakwa, Tingirima, Kyandege, Mugeta na maeneo mengine yote wanafanya tathmini, lakini malipo

hayatoki. Sasa Mheshimiwa Waziri, tusemeje sasa, kama malipo hayatoki tunasemaje na mnasema pesa zipo?

Mheshimiwa Kitandula nimekuja kwako mara nyingi tu mnazungumza kesho watalipa, kesho watalipa na hawalipi. Sasa mtuambie kwenye bajeti hizo fedha za kuwalipa hawa watu waathirika wa tembo zipo au hazipo? Maana yake sasa kila siku tunakwenda kuwaambiaje wananchi? Tutawambia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe hilo na sasa mjue kwamba tembo siyo kwamba wanakwenda kwenye vijiji vilivyopakana na hifadhi, sasa hivi tembo wanatembea nchi nzima, kwenye maeneo yangu wako karibu vijiji vyote 30, wanakwenda Nyang'aranga, Manchimweru, Mahanga, Mikomariro, Salama, Nyangere, Nyabuzume, kila mahali wanakwenda na watu wanadai fedha hazipo. Mheshimiwa Waziri nikuombe, bahati nzuri wewe ni mtu wa mifumo, tusaidie kutengeneza mfumo ambapo mkulima mazao yake yakiharibika anakuwa na karatasi ambayo itaweza kufika kwako mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo ya makaratasi ya fomu za kuleta malipo. Iende sijui wapi, aitwe Afisa Kilimo naye apewe hela, iende wilayani watoe hela, wananchi wanatoa wapi, wanakata tamaa. Kwa hiyo, niombe tutengeneze hiyo mifumo ikae vizuri ili tuweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ya kuzuia tembo, sasa mimi sijui tumeleta mabomu, hivi sasa najiuliza, juzi tulikuwa tunasema tuongeze hela za kununua mabomu. Hivi yanatumika na nani? Kwa hiyo, tuombe sasa haya mabomu kuna wale watu wanaitwa *VGS* tumieni, kila kijiji kwa mfano pale kwangu wako 15 kila kijiji, watumieni na muwape mafunzo na vifaa walinde tembo. Maana yake vinginevyo ninyi wenyewe hamuwezi hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo anaweza kuja kwa siku mara tatu, hamuwezi kwenye hayo mambo, lakini kwenye kifuta machozi kulipa yale malipo ya fidia mnakuja saa 10.00 mnaondoka saa mbili, halafu mnaondoka na hela mnarudi nazo Wizarani, Hapana. Mna *KDU* pale kwenye maeneo yenu, zile

fedha zinapokuja kama mtu hayupo, wananchi siyo wa kuwapigiwa kengele kama wanafunzi. Mtoe matangazo, mkilipa fedha yake kwa siku hiyo anaumwa, mgonjwa mpeleke pale *KDU* aifuate, kama ana uhalali wa kuipata, aipate karibu kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, malipo ya Nyatwari. Hapa wamezungumza Wabunge wengi, amezungumza dada yangu pale Esther nikamwangalia, sasa najiuliza hivi kweli, amezungumza Waziri wa Ardhi hapa, Mheshimiwa Jerry kwamba, Serikali na mtu yeyote anayetwaa eneo la wananchi kama hana fedha za kulipa asiende kutwaa eneo hilo. Sasa mmeahidi miezi tisa, imepita, sasa inaenda mwaka Nyatwari Tamau na Serengeti hawajalipwa na wananchi wameathirika sana, sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninachosema ni twendeni mkaiambie Serikali, washaurini kwenye upande wanaohusika kwamba, malipo ya Nyatwari Tamau na Serengeti yamegoma. Waambieni wananchi waishi, kwani shida iko wapi? Sasa haya mateso ni ya nini sasa? Yaani mnawapa watu mateso mpaka wanakata tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huwa najiuliza hivi sasa tunafanyaje kwa mfano? Hivi hawa wananchi tunaendaje kuwaambia wapige kura? Wanapiga kura kwa namna gani? Wana mateso, hawalimi, hawajengi, hawafanyi chochote, wanafanyaje? Waambieni bwana malipo hayapo, fedha haipo, tutakuja kuwapa sijui 2040, waambieni wajenge waendelee kuishi, kama wanavyoishi kwa sababu, sasa malipo yameongezeka ina maana hatutakuwa na hiyo hali ya malipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara na Serengeti. Sisi tuna matatizo, Mkoa wa Mara na Serengeti asilimia 80 ya Hifadhi ya Serengeti ambayo ndiyo hifadhi bora Tanzania na Africa ambayo ndiyo inatoa hela nyingi Tanzania iko Mkoa wa Mara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, hitimisha. Muda umeisha.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninakuomba Mheshimiwa Waziri ujue tuliomba kujengewa *VETA* ambayo itaitwa *VETA* ya Serengeti, ambayo hata wananchi wa huku wanaokuwa wanakufa kule ndani wanapopata matatizo haya wao wanajua kuna kitu tunakiona. Miaka karibu 60 sasa ile hifadhi iko kwetu na haina maana sana kwa Serengeti, hata ajira ya Watu wa Mara haipo kwenye mambo ya *TANAPA, TAWA* na *TFS*.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe sasa watu wa Mara wafikiriwe kwa sababu, asilimia 80 ya hifadhi ya Serengeti iko mara. Ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere. Namuita sasa Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, atafuatiwa na Jesca Jonathani Msambatavangu. Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, ajiandae.

Washa kisemeo hapo. Sogea hapo jirani.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi jioni nichangie kuhusiana na ajenda yetu iliyoko Mezani. Kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia 100, lakini ninawashukuru sana Wizara hii kwa kuja na utaratibu wa kutengeneza mabomu baridi, kwa ajili ya kufukuzia tembo. Nadhani hii itasaidia angalau kupunguza adha kubwa iliyopo katika maeneo yetu hasa Tunduru Kaskazini na Tunduru Kusini kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunduru ni moja ya waathirika wa tembo. Pamoja na kuwa na haya mabomu, lakini jitihada hizi zinaweza zikakwama kwa sababu zifuatazo, moja ni, kuna tatizo la askari. Tulipaswa kuwa na vituo vitano, kwa ajili ya kufukuzia hawa Wanyama, lakini tumepata kimoja tu, kipo pale kwenye Kata ya Muhesi na tunahitaji katika tarafa tano, kila tarafa

angalau iwe na kituo chake, ili kiweze kusaidia kufukuza hawa tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na kituo kimoja na cha pili pale Mbesa kina askari nane tu, Wilaya nzima ambayo kwenye jimbo langu ina vijiji 38 vilivyo kwenye kata kumi, ndivyo vinaathirika na wanyama hawa wakali ambao wengine wanatoka Msumbiji, kwa maana ya tembo na wengine wanatoka Mbuga ya *Selous.* Sasa tukitaka haya mabomu yafanye kazi ni lazima tuongeze askari. mahitaji ya askari ni makubwa kwa sababu, kila kijiji tembo wa Msumbiji wanasumbua upande huu, tembo wa *Selous* wanasumbua upande mwingine kwa hiyo, wafanyakazi hawa, askari waliokuwepo wanne kwenye Kituo cha Mbesa wanashindwa kwa kweli, ku-*meet* hizi changamoto ambazo zinatokea, kwa ajili ya wanyama wakali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili naomba niseme kidogo. Kwenye jitihada hizi tuna *TAWA*, tuna *TANAPA* tuna *TFS* ambao kwetu wanashirikiana kuhakikisha kwamba, hili jambo linaweza kusaidia, lakini kuna malalamiko ambayo naomba Wizara ikayafanyie kazi, hawa askari wote wanafanya kazi ya aina moja, lakini tatizo *level* zao ni sawa, lakini mishahara inatofautina kulingana na taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo halijakaa vizuri kwa sababu, wote wanafanya kazi ya aina moja, *level* yao ni moja, wote ni askari, kwa nini watofautiane mishahara? Hii changamoto inaonekana katika maeneo haya, wengine kwa kweli, wanakosa imani, kazi ile ni kubwa na ni nzito, mbaya zaidi na wale mgambo *VGS* tunaowatumia wanaweza wakakaa miezi miwili mpaka mitatu hawajapata ile posho ambayo wanatakiwa wapewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana kwenye jambo hili Wizara ilishughulikie wale *VGS* tunaowatumia pamoja kwamba, ni wachache na ile kazi ni ngumu basi hata zile posho zao wanazolipwa wapewe kwa wakati, ili waone kwamba, wanathaminiwa. Ombi langu kubwa sana ni kuhakikisha kwamba, tunaongezewa askari katika eneo hili, ili madhara ya tembo yapungue. Faida ya mabomu itaonekana kama askari watakuwa

ni wengi kwa sababu, watasaidia kuhangaika kwenda sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa lingine ni suala la vifaa, mabomu ni machache na usafiri hakuna. Halmashauri nzima tunalo gari moja. Tunaomba sana usafiri, kwa maana ya gari lipatikane, kwa ajili ya kusaidia harakati za hawa askari katika kufukuza hawa tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Wilaya ya Tunduru ina *WMA*, ziko mbili moja ni Narika na nyingine ni Chingori. Zote ziko katika Jimbo la Tunduru, Kaskazini moja na Kusini moja, na zinapakana na Hifadhi ya *TFS* na Hifadhi ya *Selous.* Hizi zote zina changamoto, naomba kabla sijasoma changamoto, Serikali itakavyokuja Waziri aje atuambie Maazimio ya Bunge la Januari ambayo yalitokana na Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati yamefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu:-

(i) *"Serikali ihakikishe imerejesha kiasi chote cha fedha kinachostahili kurejeshwa kwenye WMAs kwa mujibu wa Kanuni ili ziweshe katika kuendesha kuratibu shughuli zao za kiuhifadhi kwa ufanisi."*

(ii) *"Serikali iandae mpango kazi wa ukusanyaji mapato ambao utatofautisha mapato ya Serikali na yale ya WMAs ili fedha za jumuiya hizi ziende moja kwa moja kwenye account zao."*

(iii) *"Serikali ishughulikie kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi ya WMAs na hifadhi zingine pamoja na makazi ya watu."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni Maagizo ya Kamati yalitolewa Januari. Nafikiri leo ni Mei, nadhani kuna hatua ambayo mmepiga kuhakikisha haya mambo yanatekelezeka, tusipo tekelezeka *WMAs* zinaathirika. Zinaathirika kwa sababu, wale wana kazi ya kufanya, wana watumishi, mnaposhindwa

kuwapelekea ile fedha maana yake ni wanakwama. Miradi ambayo ilitakiwa itekelezwe kutegemea kwa hizi pesa haiwezi kutekelezeka kwa sababu, pesa inachelewa kupelekwa kwa *WMAs,* ili kuhakikisha kwamba, wanatekeleza hii miradi iliyokuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya mipaka kwenye *WMAs*. *WMAs* wananchi wamezianzisha wenyewe, mkiona zimenawiri *TFS* anakuja anataka kumega, ukiona inanawiri hifadhi ya taifa nao wanataka, ya wanyamapori nao wanamega, *TANAPA* wanakuja wanataka eneo eti. Sasa wote kazi yao ni moja na hizi *WMAs* zimeanzishwa na wananchi wenyewe, kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, sasa ni kwa nini msiwaachie waendelee kuhifadhi kwa sababu, wote lengo letu ni moja? Sasa kila siku mnapokwenda kumega maana yake ni kwamba, changamoto hii haikamiliki kwa hiyo, shughulikieni ile migogoro ya *WMAs* pamoja na hifadhi zetu, ili muwaachie waendelee kuhifadhi maeneo hayo, ili iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ninaomba Wizara watusaidie ni Narika wana kiwanja cha kitalu cha uwindaji. Wana mwekezaji amewekeza pale, lakini hailipi Nnarika, *TAWA* wanapolipwa wanashindwa kuwasaidia watoto wao, nao walipwe, hili jambo halijakaa vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe Mheshimiwa Daimu Mpakate. Muda wako umeisha.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali, hasa *TAWA,* wakati wanapolipwa malipo waisaidie na *WMA* hii ya Narika iweze kupata malipo, ili waweze kutimiza shughuli zao walizojipangia. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante sana. Namuita sasa Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Vuma Augustine Holle. Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii katika nchi yetu na hoja yangu ya kwanza kabisa itakuwa kwa heshima na taadhima kubwa kutoa pongezi na shukrani kwa uongozi wa Wizara hii nikianzia na Mheshimiwa Waziri mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri anipelekee salamu zangu kwa Mheshimiwa Rais za kumshukuru sana. Sisi kama wana-Nyanda za Juu Kusini tuna kila sababu ya kumshukuru sana Rais. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuona umuhimu wa kupanua wigo wa utalii kwenye nchi yetu kuja Kusini, kama *Southern Circuit* na hilo amelifanya kwa matendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikianzia katika Jimbo langu la Iringa, kwanza Mheshimiwa Rais kwa Awamu ya Sita, kupitia Wizara zake, ameweza kutujengea uwanja wa ndege mkubwa ambao umekamilika kwa asilimia 86 ambao unaleta watalii wengi, lakini pia, matendo mengine aliyotuonesha ni kuimarisha miundombinu ya barabara zinazoingia kwenye mbuga yetu kubwa ya *Ruaha National Park*. Barabara ya Iringa – Samora kama kilomita 103 ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami, Barabara ya Ruaha – MR – Itunundu – Pawaga na yenyewe tumetengewa kilomita 20, tuna uhakika 25 zitajengwa mwaka huu, lakini pia, Iringa *By Pass,* kwa ajili ya kuweka mji wetu kuwa wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu. Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi ulikuja wakati wa Maonesho ya Kusini pale, kile kituo ambacho tumekuwa tukilalamika. Tumeuliza humu maswali zaidi ya nane na hapa nachukua nafasi hii kumpongeza sana Naibu Waziri aliyekuwepo, dada yangu, Mheshimiwa Mary Masanja ambaye mimi huwa namuita kivutio cha utalii, yaani yeye mwenyewe ni kivutio cha utalii, kwa kazi kubwa aliyofanya tukiwa tukipambana, kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Leo Naibu Waziri, dada yangu, Mheshimiwa Mary kile kituo kimeanza kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi imesababisha sasa mimi kutoa hoja, kwa ajili ya kuwatetea tembo waliopo ndani ya nchi yetu. Kwa nini nawatetea tembo? Ninawatetea tembo na wanyamapori wengine, lakini ninawatetea tembo nikiwa nina sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *species* ya tembo duniani, wanasema miaka ya milioni sitini iliyopita 37 mpaka 34 tembo, walikuwa wa aina karibu 175 mpaka tunapoongea leo tembo wamebakia *species* tatu tu. *Specie* mojawapo ipo Asia, *specie* nyingine iko Savannah na *specie* nyingine tuko nayo sisi *Forest Africa* ambao ni tembo tulionao huku Tanzania na *East Africa in General,* wakiwemo tembo kwenye mbuga zetu za Tanzania na tembo waliopo Mbuga ya Ruaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wamekuwa wakipambana muda mwingi. Inasemekana, unajua Waheshimiwa Wabunge tukilia sana Mungu anaweza akasema sawa, nyie wote ni viumbe wangu, kama hawa wanawasumbua sana ngoja niwachukue wote kama alivyowachukua kwenye nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa hatueleweki kwa sababu, tembo, kama Wanyama, ni moja kati ya *big five* na ni moja kati ya wanyama wanaovutia watalii wengi kuja *Africa* baada ya kuwa zile *species* zimepotea huko kwao. Tembo ni mnyama kati ya wanyamapori wengine wanaotusaidia katika kupambana na umaskini wa nchi hii, kupambana na maradhi, kupambana na wale maadui watatu ambao tuna changamoto nao. Hawa wanapokuja kuwaona tembo wanalipa fedha za kigeni, tunaweza kununua dawa, tunaweza kujenga vituo vya afya, tunajenga shule na tunajenga miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inanisababisha kuona kwamba, hawa wanyamapori sisi tunaweza tukaishi nao. Ndio maana hata Mungu alivyomuumba Adamu alimuweka kwenye bustani na wanyama. Tunachotakiwa sisi kutumia ni akili zetu, sisi ni binadamu, tumepewa utashi, wao hawajapewa utashi. Wakati mwingine unajiuliza, sisi kila wakati tunaenda *Ruaha National Park* tunakwenda kutalii, tunakutana na wanyamapori, tunakutana na

simba na tembo, tunarudi tukiwa salama tume-*enjoy,* afya zetu za akili zimekaa sawa, lakini wao wakija kwetu tayari shughuli inakuwa ni nzito, sisi tunashindwa kutumia akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachowaomba, kama Wizara, hebu fanyeni utafiti wa kina. Tembo wame-*undergo evolution* mbalimbali, inaonekana tembo wa zamani kwanza walikuwa wadogo tu, wana kilo kama tano tu, sasahivi tuna tembo wana kilo 4,000 wame-*undergo evolution* ya kukua *size,* kuongezeka zile *trunk* zao, wameongezeka *skull* ya kichwa, wameongezeka *rims* zao mpaka yamekuwa majitu yale ya kilo 6,000/7,000 kwa tembo tulionao sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isijekuwa tembo hawa nao wanabadili tabia baada ya sisi kwenda kuwatembelea sana manukato yetu yanawavuta na wao kuja huku kwetu. Mnachotakiwa ninyi ni mkasome, tembo wasijekuwa wana-*undergo evolution* wanatamani, kwani India jamani, tembo wao si wanapakia maharusi? Hamuoni kule India wanapakia maharusi? Inawezekana na wa kwetu wameshatokea *species* nyingine inayotaka kuishi karibu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitoa ushauri kama huu wataalam wanatujibu tu, tukianza kuwaruhusu waje huku kwa watu watabadili tabia, watakuwa na tabia za watu, wanabadilika ndio. Kwa sababu, hata wale wa India walikuwa kwanza wa pori, lakini baadae wamekuja kuwa huku, kama wapo huku tujifunze, muwafundishe wananchi wanaokaa karibu na hao tembo, maeneo yanayosumbua zaidi, ili wawe marafiki na wale Wanyamapori kwa sababu, wanatusaidia kutuletea fedha za kigeni na ni katika *species* ambazo Mungu amezilinda amezilinda *Africa* na anatuamini kwamba, tutaendelea kuwalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, sisi tulikuwa tunaongea siku moja nikawaambia hivi kama tembo wanakuja huku wanafuata matikiti, wanafuata mpunga, sisi ni binadamu na wale ni *herbivores. Herbivores* wanakula *vegetation,* wameamua kula mpunga, wanakula matikiti, ni *vegetation*. Kwa nini msiwapandie

kwenye *buffer zone* hayo matikiti nao wakiwa wanatoka, kabla hawajaingia kwenye matikiti ya wananchi wakutane na matikiti yao kwenye *buffer zone* kule? Mnasema ooh, watabadili tabia, kule ndani kuna mibuyu gani saa hizi wanayopata maji ya kutosha? Wanakutana na *climate change,* wanakutana na kupungukiwa kwa makazi kutokana na wanadamu kuwasogelea. Tembo wanakutana na changamoto ya kuibiwa viungo vyao zikiwemo pembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu kama hivi wale nao Mungu ametupa tu, kama tunaona tabu sana sawa, watu watafunga na kuomba tembo watapotea *and then* tutapata wapi hela za kigeni? Hata kama tuliambiwa tuwatawale, Mungu alimwambia Adamu awatunze maana yake ni kwamba, mwishoni tutaulizwa, uliwatunza vipi? Sasa inaonekana kama akili zetu sisi zinazidiwa na akili za tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tembo wanatuzidi akili sisi binadamu? Tumeshindwa ku-*control* kuishi na Wanyama? Mbona leo tuko na simba hapa? Kule kwenye maonesho hatuko na simba? Iringa, simba wamekuja wametutembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba ninyi fanyeni utafiti. Tumekutana na kundi la simba walivyokuja pale, sijui wale wazee wamefanyaje kwa sababu, mhifadhi wa kwanza kuwa *Ruaha National Park* alikuwa ni *Chief* Mkwawa, ulikuwa hauruhusiwi kwenda kuwinda kwenye ile mbuga bila kibali cha *Chief* na alikuwa anakuelekeza wanyama wa kuwinda, hauwindi tu kila mnyama. Leo wamekuja simba, wazee wanaenda, muulize Mkuu wa Mkoa wa Iringa dada yangu Halima Dendegu yuko pale, wakamwambia usiwe na wasiwasi hawa tunajua jinsi ya kuishi nao hapa. Walichofanya wale ni kuwazuia wale simba wasile watu na wasile mbwa, lakini waliwaruhusu kula vitu vinginevingine, ng'ombe, mbuzi na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, simba wamekula ng'ombe, wamekula mbuzi, hawajala mtu hata huyu. Wana akili timamu, lakini ninyi kama binadamu mmekaa tu, utafiti wa kwenda kusoma utakuta watu wanasema tunaenda Dubai kwenda

kusoma jinsi ya kuishi na tembo, sasa Dubai wana tembo? Unaenda Ulaya kujifunza jinsi ya kuishi na nyani, wanapata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hao ndio ujanja-ujanja, wasomi wetu watusaidie, wafanye uchunguzi watuambie Watanzania kuishi na tembo unaishi naye hivi, sisi tuta-*enjoy*. Wakija wakakaa sehemu nyingine, mmeshajua wanapita, mnasema wanafuata kule walikofanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tembo wana akili sana. Sisi wengine tangu tuondoke kwa bibi zetu hatujawahi rudi, lakini wao kwa babu zao na bibi zao wanarudi. Wanaenda kutembea ndio wanakutana na majengo, sasa tujifunze kama wanapita zone hii tunawalindaje?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja. Tembo walindwe kwa gharama yoyote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hatimaye tembo wapata msemaji.

Namuta sasa Mheshimiwa Vuma Augustine Holle, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, ajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi jioni ya leo na mimi nichangie kidogo juu ya hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza kiongozi namba moja wa utalii Tanzania Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia nampongeza dada yangu Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki, Mheshimiwa Naibu Waziri, kaka yangu Kitandula pia na Katibu Mkuu wa Wizara hii kaka yangu Dkt. Abbas, hongereni sana kwa kazi kubwa mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayofanyika Wizarani hapa ni kubwa sana. Nilikuwa napotia *Data* za *BOT* nikaona kwamba mwaka 2021 sekta hii ya utalii iliingiza dola billioni 1.3, 2022 iliingiza dola bilioni 2.3 lakini mwaka jana mpaka Disemba iliingiza zaidi ya dola bilioni 3.3, hii siyo kazi ya kubeza ni kazi kubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa sababu tunahitaji fedha hizi kwa ajili ya kwenda kuleta maendeleo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa namna ambavyo tunafanya kazi, tunaendelea kushirikiana na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu tunaamini kwamba mtafanya makubwa zaidi kwa sababu huku Bungeni kumejaa mawazo mengi sana ya kuweza kusaidia Wizara hii. Hata hii namba 20 ambayo tunayo maana yake ripoti ya mwaka jana inasema tuko namba 20 kwa wanaofanya vizuri; naamini tunaweza tukafanya vizuri zaidi na kupata watalii wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la Kitalu cha Uwindaji cha Makere, Uvinza *Open Area;* hiki kitalu mara ya kwanza kilikuwa chini ya Halmashauri ya Kasulu *DC,* miaka ya nyuma kidogo. Baadaye Serikali ikakichukua kikawa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Maana yake sasa hivi hatusaini mikataba na wao tena kama wawekezaji ila Wizara ndiyo inayosaini mikataba kupitia *TAWA* na mwekezaji huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninavyoongea hapa kuna vilio vya hali ya juu sana; kuna kilio kikubwa sana kwenye Jimbo la Kasulu Vijijini. Vijiji ambavyo vinazunguka na ambavyo vinapakana na mipaka ya kitalu hiki wanapitia machungu makubwa ambayo sijawahi kuyashuhudia tangu niwe Mbunge. Machungu gani? Kwanza, kuna changamoto ya mipaka kutofahamika vizuri; hakuna *clarity* ya mipaka. Yaani mpaka wa vijiji na kitalu cha uwindaji haifahamiki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo imesababisha wananchi kulima maeneo ambayo mwekezaji anadai kwamba ni eneo la kitalu. Jambo la kwanza hatujui kwamba wapo kwenye kitalu au hawapo kwenye kitalu, *that is number one;* lakini mbaya zaidi ni

kwamba mwekezaji anafanya *operation* ambazo kimsingi zinatumia nguvu kubwa. Ukienda pale utatoa machozi; anachoma mazao na mali za wananchi bila kuwa na huruma yoyote. *We know that* amewekeza pesa, tunajua. Tunajua wamewekeza pesa pale lakini kama hakuna *clarity* mipaka hiyo nguvu ya kwenda kuchoma mazao na mali za wananchi anaipata wapi? Mheshimiwa Waziri, hili jambo huwezi kulikimbia dada yangu, linakuhusu kwa sababu Wizara yako ndiyo imesaini mkataba na yule mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko umuhimu na ulazima wa Wizara kuweka utaratibu wa kuweka *clarity* ya mipaka ili wananchi waweze kujua kwamba huu ndiyo mwisho wa mpaka wa mwekezaji; wasije kwenda kulima kule na hatimaye wakaenda kupambana na mwekezaji wakaingia kwenye hasara ambayo wanaendelea kuipata mpaka sasa hivi; lakini kwa sababu hakuna *clarity* ya mipaka Mheshimiwa Waziri nakuomba sana utakapokuja kuhitimisha hapa, kwa sababu huyu najua ndiye aliyewekeza na najua dhana ya kuheshimu wawekezaji ambao wamekuja kuwekeza kwenye nchi yetu kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika dhana nzima ya ujirani mwema Wizara yako iweze ku-*contact* naye; iweze kuzungumza naye angalau awaruhusu wananchi ambao wamelima na wakapalilia mazao yao yakaiva, sasa hivi wanavuna wanaenda kuwachomea mazao. Wawaruhusu mazao yao wayatoe halafu baada ya hapo wekeni mipaka inayoeleweka ili wananchi tuweze kuwapa elimu ya kutosha kwamba msivuke mipaka ya kitalu kwenda kulima kwenye kitalu. *Otherwise* hakuna anayejua mipaka hasa iko namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuhusu *TFS* na kama hili halitapata majibu ya kutosha kwa kweli nitashika shilingi. Nilizungumza kuhusu *TFS*, *TFS* kwa kweli mimi ninawapongeza sana chini ya Kamishna Silayo. Kama miaka mitatu iliyopita tulikubaliana na tukaweka utaratibu kwamba kwenye Hifadhi ya Msitu ya Pori la Kagera Nkanda yaani Makere Kusini, kulikuwa kuna changamoto kwa maana kwamba msitu kwanza

umepoteza uhifadhi na wananchi wakienda kulima kule *TFS* wanawatandika viboko ikawa ni changamoto kwelikweli; tukakubaliana tuligeuza kuwa ni shamba la miti. Kazi imeanza, ekari 1,500 zimeshapandwa na kwa sababu shughuli za kibinadamu haziathiri kilimo cha miti waliwaruhusu wananchi kwa utaratibu maalumu waende kulima na mwaka jana tuligawiwa ekari 21,000, hongera sana *TFS* kwa hilo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna changamoto kidogo, kuna baadhi ya vishoka kule vijijini ambao wanakuwa katikati pale, nimetumiwa taarifa kutoka kwa wananchi. Yale mashamba tulikubaliana kwamba wananchi wagawiwe bure lakini kuna vishoka ambao wanajipenyeza kwa ajili ya kuwakodishia wananchi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Silayo kwa sababu hili jambo tumekuwa tukilifanya wote uingilie kati katika jambo hili ili wananchi waendelee kunufaika na matunda ya kitalu ambacho mmekifanya na wananchi kama ambavyo tuliwatangazia maana yake baada ya kukubaliana nilienda kwa wananchi kuwatangazia mashamba ni bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unavyoenda kule unawaambiwa watoe shilingi elfu 20 tukupe ekari moja, siyo utaratibu tuliokubaliana na kwa sababu msimu wa kilimo umekaribia kuanza naomba sana chonde chonde tufunge safari twende tukawaambie wananchi vishoka tuwakatae mashamba ya *TFS* Makere Kusini tunayagawa bure kwa sababu haiathiri shughuli ya kilimo cha miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mchache nilitaka kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma wajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kunipa fursa ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu

ambayo ni hotuba ya Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wote kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ndugu yetu Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Naibu Waziri Ndugu Dunstan Kitandula (Mbunge), Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya maliasili kwa kuandaa hotuba yenye mwelekeo wa kuleta tija katika sekta ya utalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake binafsi kwa kutangaza utalii Duniani kupitia *Film* yake ya *Royal Tour* lakini pia *film* hii ya hivi karibuni kwa jina la *The Amazing Tanzania and really Tanzania is amazing* kwa sababu ya baraka ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu kwa vivutio vyote hivi ambavyo tunavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu utaegemea katika maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020 hadi 2025 Ibara ya 7(a) kwamba, pamoja na mambo mengine ni kubuni na kutekeleza mikakati ya kuongeza na kukuza wigo wa bidhaa na mazao ya utalii ili kufikia watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa tatu amezungumzia kuongezeka kwa watalii wa nje kutoka watalii 922,962 mwaka 2021 hadi watalii 1,808,205 kwa mwaka 2023. Pia, watalii wa ndani kutoka 788,993 kwa mwaka 2021 hadi watalii wa ndani milioni 1.9 mwaka 2023. Naipongeza sana Wizara kwa mikakati ambayo inaifanya kwa nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba utalii unaendelea kuingiza Pato la Taifa na kweli tumeona katika taarifa ya Wizara hakika hatua ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba nizungumzie kwanza kuhusiana na utalii wa ndani, kutokana na sensa tuko Watanzania zaidi ya milioni 60 au kama milioni 62 hivi lakini idadi ambao wameshafika labda katika maeneo mbalimbali ni kama milioni 1.8. Kwa hiyo, ushauri wangu ni

kwamba tunahitaji msukumo mkubwa sana kwa Wananchi wa Tanzania wa ndani ili kusudi waweze kuona vivutio na huu urithi ambao mwenyezi Mungu ametupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo ni kwamba watalii milioni tano ndiyo wanahitajika pengine itakapofika 2025 waweze kuwa wamefika. Bado napata mashaka, leo hii tuko 2024 mwakani Mungu akitujaalia tutafika 2025. Kwa hiyo, mimi naomba niendelee kuishauri Wizara ni vizuri kuendelea kutoa elimu na matangazo zaidi. Tunatambua kabisa kwamba Wizara imekuwa ikifanya mbinu mbalimbali kwa kutumia balozi, makundi mbalimbali na kadhalika, lakini naamini kabisa msukumo zaidi ukifika kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutaweza kufikisha zaidi ya watalii milioni tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurusa wa 100 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amebainisha juhudi za Serikali kupitia Bodi ya Utalii kwamba wameanzisha ushirikiano mkubwa sana Duniani na kampuni *Expedia Group* ya Marekani. Inasemekana kwamba kampuni hii imefanikiwa sana katika masuala ya utalii, mimi nawapongeza sana lakini nilikuwa nina ushauri kwamba kuwe na mkakati wa muda mrefu wa kuongeza *hotels* na *camps* za utalii hasa kwenye hifadhi ambazo zinatembelewa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa naomba nishauri kwamba gharama za kuwekeza kwenye malazi ziwe rafiki ili wawekezaji wa ndani waweze kuvutiwa na waweze kuwekeza. Sambamba na hilo wenzangu wengi wamezungumzia kuhusu suala la miundombinu hasa barabara. Tumejua kabisa kwamba kipindi cha *El-Nino* kumetokea shida sana. Kwa hiyo, naomba nishauri kwamba kwenye hili suala la miundombinu liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo natamani nilizungumzie ni kwamba naipongeza sana Wizara kwa kuendelea kupambana na hawa wanyama waharibifu ambao ni tembo. Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamezungumzia kuhusu hili jambo lakini sisi pia katika mkoa wa Dodoma Wilaya ya Chamwino tuna kata kadhaa ambazo kwa kuzitaja ni Kata ya

Manda, Chiboli, Chinugulu na Nghambaku, kata hizi nazo pia kuna shida sana ya hawa wanyamapori tembo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tarehe 13 Mei Wizara ilikuwa imezindua suala zima la vilipuzi na kukabidhi haya mabomu 4,000 kwa Wizara. Basi naomba nishauri, kwa sababu katika hotuba hii ameandika kwamba halmashauri 20 za mwanzo ndizo zitakazofaidika na vilipuzi hivi. Mimi natamani kwamba katika yale maeneo ambayo pia bado kuna taarifa kwamba tembo bado wapo basi pia waendelee kuona ni jinsi gani na wao pia wanapata vilipuzi hivi ili kusudi waweze kukabiliana na hawa tembo, kwa kweli tembo wamekuwa ni shida sana, wamekuwa wanaharibu mazao na watu wanapoteza maisha yao. Kwa hiyo, na sisi tunaomba katika Wilaya ya Chamwino hili jambo liweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba sisi tunahifadhi zaidi ya 20. Naamini kwamba tukijipanga vizuri kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutaweza kufikia zaidi ya watalii milioni 10 kwa sababu nikitoa mfano, tuna Nchi za Afrika ambazo wenzetu nao wamefikia hatua kubwa. Mfano Egypt wameweza kufikia hatua ya kupata watalii milioni 14.9 kwa mwaka, Morocco milioni 14.5, Tunisia milioni 9 na South Africa milioni 7. Kwa sisi vivutio tulivyonavyo naamini kabisa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na najua kabisa kwa mipango ya Wizara na hii kazi ambayo Rais wetu amekuwa akiifanya mwisho wa siku tutaweza kupata watalii wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niunge mkono ushauri wa Kamati. Baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Shally Josepha Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa kipekee namshukuru Mungu kwa sisi sote tuliopo hapa na wanaotusikiliza kuzungumzia mambo mazuri

haya ya nchi yetu. Namshukuru Mungu kutupa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongoza nchi hii kwa amani na utulivu katika kipindi hiki Tanzania. Ni chaguo la Mungu na tuendelee kumtii na kusikiliza na kumpa *support. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Rais kututeulia Waziri wetu wa Utalii binti yetu huyu ambaye sasa ndiye Waziri wa Utalii, Mheshimiwa Angellah Kairuki. Niseme kwamba ana uwezo na anapenda kujisomea ndiyo maana hii kazi siyo ngeni kwake na amepata Naibu Waziri Mheshimiwa Dunstan Kitandula ambaye pia ni mtu anayependa kujisomea sana, kwa hiyo, hakuna ugeni kwenye Wizara. Wameweza na wamechukua na Katibu Mkuu Abbas waendelee kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ni mashahidi tumeoina wenyeviti wa taasisi zilizo ndani yao; tumeona ma-*General* wastaafu wawili wa nchi hii ni watu wakubwa sana. Tumemwona *General* Mabeyo na tumemuona *General*... limenitoka lakini yule mkubwa zaidi wa siku nyingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** *General* Waitara.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** *General* Waitara, tumemwona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale watu ukiwapa Chombo chako nataka tujue sote kwamba kiko salama. Kuna mambo yaliyojitokeza hapa mengi, labda hela zinaliwa na labda hela zinatapanywa. Nataka niseme hivi tumeomba miundombinu iende kwenye maeneo ya mbuga za wanyama. Sasa tunapoenda kupeleka miundombinu hiyo nani apite huko? Hawa wanyama wanataka hiyo miundombinu? Tunataka watalii wengi na ndiyo maana Mungu akampa maono Mheshimiwa Rais akaja na *Royal Tour.* Watalii wameanza kuingia nchini, hawa watalii wanapenda amani na utulivu na safari salama. Hakuna mtalii atatoka nchini kwake aje kuvunjika kiuno hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuwezesha jambo hilo liende inabidi hii Wizara ipewe hela za kutosha. Rasmi kabisa naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuwaunge mkono na

tuwapatie hela iliyoombwa na Mheshimiwa Waziri shilingi bilioni 348,125,419,000 wakafanye kazi na wasilale. Kwanza, ni vijana wadogo hawa. Tuone matokeo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tuendeshe hili gari tukiangalia kwenye *wind screen,* mambo ya kuangalia *side mirror* huko nyuma ikawaje na ilikuwaje, ilishakuwa; sisi tusonge mbele. Waheshimiwa Wabunge nawaomba sana tuweze kuwapa *support.* Nakubaliana kabisa na hotuba aliyosoma Mwenyekiti wa Kamati hii, nakubali. Tutaendelea kuyafanyia kazi na yatarekebishika lakini kwa leo tunapoenda kuhitimisha tuwape hii hela wala haifiki hata nusu trilioni; ni hela kidogo tu wameomba na wazalishe. Mimi naamini hii Wizara ya Utalii Tanzania ingewekwa vizuri, wakapewa nafasi hao wanaofanya kwenye hizo taasisi nyingine za utalii wakapewa *exposure* wakaenda nje na wakaenda huko katika *trade fair* kama ilivyokuwa zamani, *TTBS* wakajitangaza, tungepata hawa watalii kabla hata mwaka huu kuisha lakini hatutaki kutoa hela, tunataka tu tuwafinye. Tutawaminya halafu tutapata nini? Ukitaka hela lazima uweke hela, halafu ndiyo utapata faida zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa vile muda ni mchache naomba niende moja kwa moja kwa wanawake kufikiriwa katika hii sekta ya utalii. Wanawake wa Tanzania bado hatujapewa fursa na pale tulipopewa hata kama ni madereva hatujaweza kufikiriwa na kupewa *support.* Mheshimiwa Waziri nakuomba sana *research* zimefanyika na wengi, wanawake siyo kama wanaume kuna nyakati ambapo watajifungua wapeni likizo zao inavyobidi. Pia, siyo hayo tu kuna kuonewa kule yaani kutofanyiwa kama inavyotakiwa. Naomba uwalinde wanawake waliopo katika sekta hii ya utalii ambao ni kama 54%; wapatiwe haki zao walindwe na pia wapatiwe nafasi ambazo ni za mishahara ambayo inakidhi matumizi yao na matumizi ya familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hii Sekta ya Utalii hata ukiangalia walivyokuwa wanatambulishwa waliopo juu hatukuona hapa wanawake wengi tumeona wanawake kama wawili ama watatu tu, nao sijui wamepatikana kwa bahati. Sasa

kwenye *level* zote kwenye taasisi zako, Mheshimiwa Waziri, wewe ni *gender* ya (ke) sisemi kwamba ukawape ambao hawana uwezo, kwani walipoanza shule, wakaenda sekondari mpaka vyuo vikuu wakahitimu iweje walioweza ni wanaume tu? Ina maana miaka hiyo wanawake walikuwa hawawezi? Naomba uwafikirie sana hawa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba sana Mheshimiwa Waziri uangalie ni jinsi gani sasa wanaoishi tambarare ya Mlima Kilimanjaro ambao pia ni kivutio na ni maajabu ya dunia, ile theluji inaondoka kwa sababu ya tabianchi lakini tunaweza kurekebisha uoto wa asili kwa kurejesha tena kuotesha miti na mengineyo. Watu hawa wanaanzia toka kule Siha wanakuja Hai, Moshi Vijijini ambako na Vunjo ipo lakini mpaka Rombo, kumekuwa kukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utatoa mradi ambao tumeona huyu Prof. Dos Santos Silayo, anagawa miche kwa ukarimu kabisa, nimuombe tena aendelee kugawa katika shule zote, aendelee kugawa hata kwenye kaya za watu, waoteshe tu, ukishaotesha mti ukaumwagia maji au ukatafuta chochote, yaani kadri ya uoto utakavyoendelea lazima ule mlima utarejea katika hali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri ikimpendeza, atoe *pilot project* ya wanawake hawa kuweza kuwa na vitu vya asili. Tumeona asali inatengenezwa na inaweza kuwekwa katika kufuga nyuki. Hata kuku pia wale wazungu wakija wasile tena yale mayai waliyozoea yale makapi makapi yale, wale mayai ambayo ni *organic* kama wanavyokula mboga *organic* hapa wanafurahi. Ndizi *organic*, ndizi haiwekwi hata siku moja *fertilizer* yoyote ambayo ni ya nje, hivyo ndiyo vivutio vyenyewe. Wanatoka kule walishavizoea, tuwape vitu vyetu vya jadi, waweze kufurahia hata kukaa kwao hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia 100, nawatakia kila la heri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namuita sasa Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipatia nafasi kusimama hapa kuchangia kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi anayoifanya hasa ya kutangaza utalii, ukichukulia filamu ya *Royal Tour* ambayo imevutia watu wengi na kuleta watalii wengi Tanzania, kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa kazi hii nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ameweza kuitangaza na watalii wameweza kuongezeka kuanzia milioni 1.4 kwa mwaka 2022 mpaka milioni 1.8 kwa mwaka 2023. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Pili, ameweza kuongeza bajeti kwa kuwa anaithamini sana Wizara hii hasa kwa upande wa utalii kwa kuongeza bajeti ambayo mpaka sasa hivi tunasema ni shilingi 348,125,119,000. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa namna anavyoithamini sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nampongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Angellah Kairuki, kwa kweli anafanya kazi kubwa sana, pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa kazi wanayoifanya. Ninyi wenyewe ni mashuhuda mmeona kuwa licha ya matatizo yanayojitokeza lakini kwenye hotuba yake amesema kuwa pato linalotokana na utalii limeongezeka, watalii wameongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kufika namba moja kwa nchi zote za Afrika kwenye mambo ya utalii. Kwa kweli mimi nampongeza na nawapongeza watendaji wa Wizara wote kwa kazi nzuri mnayoifanya, kama kuna matatizo mengine yatatuliwe, naamini kuwa Wizara itakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ninaloongea hapa ni kuongeza vivutio vya utalii. Naomba sana ili watalii waweze kuongezeka pamoja na pato la nchi liweze kuongezeka lazima tuongeze vivutio vya utalii. Vivutio vya utalii kila Kanda na kila Mkoa vilikuwepo, kulikuwa na himizo la kusema kila Mkoa uweze kuvumbua na kutangaza vivutio vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nikija kwenye Mkoa wangu wa Morogoro, tuna vivutio vingi sana. Nikianza na Bwawa la Mwalimu Nyerere, tunamshukuru sana Dkt. Samia kwa jambo hili alilolifanya. Nikija kwenye milima ya Uluguru, nikija kwenye barabara, nikija kwenye hoteli, kwa kweli tuna mambo mengi, utamaduni, utalii siyo lazima uwe ni wanyama, hata maua, hata vyakula na uvaaji wa watu wanaoishi kwenye Mikoa hiyo nayo ni utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie kuvutia na kuongeza vivutio ambavyo vitaweza kuongeza utalii kwenye nchi yetu ili kusudi watalii waweze kuwa wengi na tuweze kuongeza vivutio na uchumi uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanyama waharibifu. Mheshimiwa Waziri Angellah, wanyama waharibifu wamekuwa tatizo. Tembo wamekuwa ni tatizo, tembo kwenye Mkoa wangu wa Morogoro kwa wastani, Mikoa yote ya Tanzania kwa wastani ni tembo ndiyo wanaoongelewa. Hata hivyo, ninawashukuru na kuwapongeza kwa jitihada mnayoichukua ya kufanya utafiti wa jinsi ya kuwadhibiti hawa tembo. Kwa mfano, mabomu baridi, kwa kweli mmefanya kazi nzuri tumeiona, ila mimi najiuliza, mkishawatupia wakakimbia, je, hapo baadaye hawarudi? Kwa hiyo, naomba sana tuangalie huo utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmesema mnawafunga mikanda na helkopta, safi, tumieni tafiti tuweze kuona tafiti zinafanya kazi kusudi tembo waache kuharibu mazao ya wananchi. Wanaharibu mazao ya wananchi, wanaua watu, kwa hiyo naomba sana Tembo ni mzuri lakini kwa mfano ukipita pale Mikumi, wewe mwenyewe unafurahia kuwaona walivyo, ni

mnyama mkubwa sana anapendeza, lakini tuangalie wasiharibu mazao ya watu pamoja na kuleta vifo kwa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi na hifadhi. Imekuwepo lakini wananchi wengine hawaelewi kuwa kuna sheria, wanaingia kwenye hifadhi wanadhulumiwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, natoa ushauri kuwa elimu iendelee kwa hawa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi, waweze kujua ni sheria ambayo inawakataza kuingia kwenye hifadhi, waelewe vizuri, kuwe na ushirikiano wa kupima mipaka kati ya ardhi ya wananchi pamoja na ardhi ya hifadhi. Waweze kuelewa na kushirikishwa kuwa hii huwezi kuingia na hii huwezi kufanya nini ili kusudi tupunguze migogoro inayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rasilimali misitu. Misitu ni mali, misitu ina faida, inaleta hewa, inaleta mvua, inazaa *carbon* kwa hiyo ni utajiri kwa nchi yetu. Kwa hiyo, naomba ile miche inayozalishwa iweze kupelekwa kwenye taasisi mbalimbali na ikiwezekana na wananchi wagawiwe kama mnavyofanya *TFS*. Mnafanya vizuri, tuendelee kustawisha hii miche. Angalizo ni kuwahimiza watu wa halmashauri kwa kushirikiana na TAMISEMI kuwa hii miche inayogawiwa iweze kutunzwa, isiwe ni kupanda tu na kuisahau, iweze kufuatiliwa ili kusudi iweze kustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuongeza utalii tumeona kuna ujenzi wa viwanja vya ndege ambavyo vitajengwa na kukamilika mwezi huu wa Nane. Kwa mfano, kuna kiwanja cha ndege Mikumi kitajengwa, kuna kiwanja cha ndege Nyerere kitajengwa, kuna viwanja viwili Ruaha, vitajengwa. Kwa kujenga hivi viwanja vya ndege vitaongeza watalii kuja nchini kwetu na hapo hapo tutaweza kuongeza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri, pamoja na hivyo tuendelee kuboresha na kujenga viwanja vya ndege kwenye hifadhi zetu ili kusudi watalii waweze kuja kwa wingi tuongeze kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa nyuki. Ufugaji wa nyuki ni kitu kizuri sana hasa kwenye kuhifadhi misitu. Ukiweka

nyuki kwenye misitu, watu hawawezi kuingia hovyo hovyo kukata hiyo misitu. Kwa hiyo, nilikuwa nasema hivi, elimu iendelee kutolewa kwa wananchi hasa kwenye vikundi vya vijana pamoja na akinamama, waweze kupewa mizinga kama mnavyofanya ili kusudi waweze kufuga hao nyuki na waweze kupata ajira kwa kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya nyuki ni dawa, nyote mmeona asali, nta, kwa hiyo ni jambo zuri pamoja na mazao mengine yaweze kutolewa elimu ili watu waweze kuendelea kufuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufinyu wa bajeti. Licha ya kumshukuru Mheshimiwa Rais lakini naomba waongezewe bajeti ili kusudi iweze kuwatosheleza na iweze kuonekana vizuri na kusimamiwa vizuri kusudi iweze kufanya mambo yaliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ubarikiwe na Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunao wageni, waliopo ndani ya Ukumbi wa Bunge ningependa tuwatambue ambao ni:

Wageni 27 wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii, hawa ni wanafunzi wa Chuo cha Biashara (*CBE*) cha Jijini Dodoma wanaosomea utalii. Tuwaone, karibuni sana Bungeni, ahsanteni. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya, Mbunge na Naibu Waziri, hawa ni wanafamilia kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana, wako pale. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, Mbunge ambao ni Watangazaji kutoka Wasafi *Media*, wako pale juu. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wapo humu kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni walimu na wanafunzi 50 wa Chama cha *Scout* Tanzania wa shule za msingi Karisa, Waldorf na Mshikamano kutoka Kibaha na Ubungo. Simameni tuwaone, haya karibuni sana naona *scouts* wengi tu pale. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 70 wa umoja wa *scouts* wa shule za msingi NABA kutoka Jijini Dar es Salaam, wale *scouts* tuwaone nao. Haya karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa nimuite Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARGARET S. SITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mezani, pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na wakati huo huo nawashukuru wananchi wa Urambo kwa ushirikiano wao wanaonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia, Rais wetu, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutafuta maendeleo ya nchi hii. Pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioko katika Wizara hii ambayo inajadiliwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urambo uchumi wetu unategemea sana tumbaku na asali. Wananchi wanaofuga nyuki wameunda umoja wao wa wafuga nyuki, waliniomba mimi nikapeleka barua rasmi Wizara ya Maliasili na Utalii ili kupewa mashine ya kusaidia kuchenjua asali ili na sisi tusafirishe ndani ya nchi na nje ya nchi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ilikubali ikamtuma Mkurugenzi akaja, akakagua eneo letu na wakakubali kwamba watatupa mashine. Nawashukuru sana kwa sababu walitupa moyo wa kuongeza mizinga katika mapori yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, Serikali ikaja na wazo zuri la kuwa na hifadhi ya Mto Ugala ambako ndiyo kwetu sisi na maeneo yanayoguswa karibu sana ni Kata za Nsenda, kwenye maeneo ya Lunyeta, Utenge, Mkola na Mtakuja. Pia, Kata ya Ukondamoyo kwenye maeneo ya Tumaini, Nholongo na Utewe na pia Kata ya Kasisi katika maeneo ya Azimio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Urambo, naomba nilete ombi siku ya leo. Kwanza kuishukuru Serikali kwa kutupa hifadhi ya Mto Ugala, tunathamini hifadhi hiyo na ninajua kabisa Serikali ilifanya hivyo, kugeuza ule msitu ukawa hifadhi ya Mto Ugala kwa maksudi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, tunathamini kuwa na hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi tunaloleta kwako Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla ni kwamba, kwa kuwa uchumi wetu unategemea sana asali, tuna haja ya kupeleka mizinga. Kwa bahati mbaya ndani ya hifadhi ya Mto Ugala haturuhusiwi kupeleka mizinga lakini ni zao ambalo tunalithamini na tulikuwa tumeshapata watu wa nje ambao walikuwa tayari kununua asali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi ambalo ninalileta kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba tupewe eneo la kuweka mizinga, kwa sababu ni zao ambalo tunalitegemea kiuchumi. Tatizo moja lililotokea ambalo ninaamini ni kwa bahati mbaya kwa sababu Serikali yetu ni nzuri tu, hawakutoa elimu ya aina yoyote walipokuwa wanageuza huu msitu kuwa hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawakuelimishwa kwamba kuwa na hifadhi maana yake ni nini, wao watafaidika vipi na wajibu wao ni nini ili kujenga mahusiano na ujirani mwema. Kwa sababu, tunaamini kabisa mlinzi wa kwanza wa hifadhi hiyo ni mwananchi lakini kwa bahati mbaya elimu haikutolewa kwa hiyo hakukuwa na ushirikishwaji wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali yetu sikivu ifanye utaratibu wa kuja kuongea na wale wananchi, wajue maana ya hifadhi ni nini na watanufaika nini na wajibu wao. Pia,

tunaomba tupewe angalau kilomita 5.5 za eneo ili wananchi waweke mizinga yao kwa zao wanalolitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo tunalileta ni kwamba, sisi tuna *WMA* ambayo ni kitu kizuri sana, tunaomba Serikali ilipe stahili zao. Kwa bahati mbaya mwaka 2021/2022 na mwaka 2022/2023 bado Serikali ilikuwa haijalipa lakini tunayo imani na Serikali yetu, tunaomba *WMA* ipewe fedha zake ambazo Serikali iliahidi kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, bado tunarudi kwa Serikali yetu. Mheshimiwa Waziri nakuheshimu, nakuamini pamoja na Naibu na Wizara yote kwa ujumla. Mlikuja mkatoa ahadi kwa wananchi kwamba mtawapa mashine, mtawasaidia kuwa na umeme, mtawapa kisima, wakafurahi na bado wana imani na Serikali yao. Tunaomba mashine ya kuchenjua asali, pia mje mtembelee muone eneo lile, kwa sababu wananchi wamejiunga wana imani na Serikali yao kwamba wataendeleza zao la asali ili waweze kusafirisha na kuinua uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nisingependa kuendelea na maneno zaidi kwa sababu shida zangu ni hizo hizo. Naomba uniruhusu nimalizie kabla kengele haijalia. Kwanza, tunaomba mje muongee na wananchi, kuwapa elimu na wajibu wao. Pili, tunaomba muwape eneo lao la kuweka mzinga, kilomita 5.5 ndiyo pendekezo letu. Tatu, tunaomba *WMA* ilipwe fedha zao na mwisho tunaomba mashine ya kuchenjua asali kama tulivyoomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele haijalia, mwisho kabisa labda nikumbushe kidogo tu, hili suala siyo la leo tu. Mheshimiwa Kigwangalla akiwa Waziri alikuja, bahati mbaya mvua ikanyesha akashindwa. Alikuja Mheshimiwa Ramo Makani kama Naibu Waziri naye akashindwa lakini pia Mheshimiwa Josephat Hasunga naye alifika ili kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa Mheshimiwa Waziri aliyepo sasa hivi na Naibu Waziri naamini watakuja waone

maeneo haya na nyinyi mtakubaliana na maombi ya wananchi wetu, hayo ambayo nimeyatanguliza siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nina imani na Serikali yetu na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namuita sasa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuata na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya mwaka huu 2024 /2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada nichukue nafasi hii kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri na ubunifu mzuri katika sekta hii ya utalii. Wakati anaanza na ajenda ya *Royal Tour*, tuliona kama ni kitu cha kawaida lakini sasa tumeona matunda ya ubunifu wake, kwa kweli tunampongeza sana Mama apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Angellah Kairuki, Waziri wa Maliasili na Utalii, pia nimpongeze Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu Dkt. Abbas kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kuifanya na delegation yenu yote, kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nampongeza Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu Dkt. Abbas kwa kazi nzuri ambayo mnaendelea kuifanya na *delegation* yenu yote. Kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mafanikio kama hayo, hakukosi changamoto. Nimeona hapa kuna suala linahusiana na utambuzi wa maeneo ya malikale nchini na kuyatangaza kuwa Urithi wa Taifa. Nilipokuwa napitia hii bajeti, kwa kweli nimekutana

na kitu ambacho kilinisononesha sana. Yametajwa maeneo kama 11 ambayo yatawekwa kama urithi na kumbukizi ya maeneo hayo yakiwepo Morogoro, Rukwa, Songwe, Mbeya, Katavi, lakini Ruvuma haijatajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ruvuma sisi tuna Makumbusho ya Majimaji, Wajerumani walikuja pale sisi ndiyo mashujaa wenu Wangoni. Tulisimama tukapigana kuhakikisha kwamba adha ile haiwakuti huku lakini mnashindwa kutambua kwamba kuna Makumbusho ya Majimaji. Kwa kweli hatujatendewa haki, tunataka Wizara iweke suala hili la Makumbusho ya Majimaji na iletewe pesa ili Makumbusho ya Majimaji iendelee kukua na iweze kuletewa watalii wengi kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo kumbukumbu kubwa sana, kwa sababu ya muda, naamini kabisa katika historia ya vitabu, kila Mtanzania anajua. Pia, naomba kusema, katika kumbukumbu hizi za Makumbusho ya Majimaji, yuko Chifu Mbano, babu yetu sisi. Alikatwa kichwa chake na kichwa chake kikapelekwa Ujerumani, mpaka leo kichwa kile hakijarudishwa. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, mnapokezana tu hapo, Mheshimiwa Waziri huyu, Mheshimiwa Waziri huyu, Mheshimiwa Waziri huyu lakini hamrudishi kichwa cha babu yetu, tunadai kichwa cha babu yetu Mbano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuletee kichwa cha babu yetu, kinafanya nini Ujerumani? Yule ni Mngoni na wala siyo Mjerumani. Tafadhali sana tunaomba mturudishie kichwa cha babu yetu ili tuweze, katika yale Makumbusho ya Majimaji, sasa kichwa kile kitatuletea watalii wengi sana. Watakuja kuona kile kichwa kilikuwa na madini ya aina gani na hata aliweza kunyongwa karibu mara tatu alishindwa kufa mpaka wakaamua kumpiga risasi. Mheshimiwa Waziri tutaelewana mimi na wewe, utakuwa *best* yangu kama kichwa cha babu yangu Mbano kitarudi kule. Wanaruvuma wanahitaji kichwa cha babu yao Mbano, ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye Ziwa Nyasa. Ziwa Nyasa ni ziwa ambalo kimsingi limezungukwa na

mambo mengi mazuri yanayohusiana na utalii. Nataka kusema tu kwamba, kuna Kisiwa cha Ndumbi pale, kisiwa kile kipo hakiendelezwi. Jamani kwa nini katika nchi hii mnapoamua kuendeleza masuala ya utalii mnaendeleza upande mmoja tu lakini Ruvuma, upande wa Kusini hamuendelezi utalii? Mbona kila siku tunalia humu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi, Waheshimiwa Wabunge wa Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, sisi tunahitaji kukuzwa utalii kule kwetu. Tunahitaji na sisi tuone watalii wanakuja, tuweze kuendelea kukuza uchumi lakini pia watalii wakiendelea kuja, na ajira zitaongezeka, tunaomba tafadhali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la Ziwa Nyasa, pia kuna samaki wazuri sana wa mapambo; wako aina 400, nayo pia ni sehemu ya utalii. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, katika kukuza maeneo ambayo ni vivutio vya utalii, basi na Nyasa nayo itengewe pesa ili iweze kukua kiutalii. Kuna ngoma za asili, na wachezaji tupo wa ngoma hizo. Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, mchezaji mzuri wa ngoma za asili, zimejaa kule kwetu Ruvuma, Nyasa, Songea na maeneo mengine, Namtumbo, Tunduru na maeneo mengine yote mpaka Songea Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tukifunga kibwewe, tunafunga kwelikweli, kwa hiyo ni sehemu ya utalii. Tunaomba sana, Mheshimiwa Waziri, tunaomba u-*promote* hivi vitu. Mimi nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, ambaye ni Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukuza ile *Tulia Festival* ambayo kila mwaka anaendeleza masuala ya mila na desturi, mambo ya ngoma na nini. Nayo pia ni sehemu ya raha, ni sehemu ya utalii, inaleta raha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naomba Mheshimiwa Waziri, katika kazi zako unazoendelea kufanya, tunataka tuone mageuzi katika vitu hivyo vidogo vodogo ambavyo vitatuingizia pato kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ni suala linalohusiana na tembo. Kwa kweli nataka kusema, nampongeza Mheshimiwa mama Lulida, kachangia vizuri sana, lakini mama yangu Mheshimiwa Jesca Msambatavangu mmh! Yaani tembo wale waanze kuja huku, ameoanisha tembo wa India na tembo wa Tanzania. Tembo wa Tanzania, tembo kwelikweli, huwezi kulinganisha na vitoto vile vya India, vile vya India ni vitoto, Mheshimiwa Jesca tafadhali naona unataka kuwasha *mic*, utanipotezea muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema, tafadhali sana, hoja yake inawezekana ni nzuri na ina mashiko, lakini itachukua umri mrefu sana mpaka kwenda kuanza kuwafundisha, kuwaelekeza. Kubwa ambalo nataka kuuliza Wizara; je, wamewahi kufanya utafiti kwa nini tembo wanatoka kule porini wanakuja huku? Wamewahi kufanya utafiti? Kama wamefanya utafiti, basi watuletee majibu hapa utafiti walioufanya ni kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi miaka mitano iliyopita, nimepiga kelele sana kuhusu tembo lakini wakati huu, sitaweza kupiga tena zaidi ya kushauri Serikali hii kwamba kule ndani kwenye mapori yale ambayo ya wanyamapori, sasa hivi yamekuwa siyo mapori ya wanyamapori, ni mapori ya wanayamawatu kwa sababu wafugaji wamejaa huko, wanatembeza ng'ombe wao kila mahali. Wanyama kama Wanyama sasa hivi, siyo tembo tu tunawaona tembo kwa sababu wamekuwa na athari kubwa sana katika jamii lakini wanyama wengi: fisi, tumbili, nini, wote tunapishana nao huko mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu wale wafugaji wanakuwa wana ng'ombe wao, wale ng'ombe wamewafunga kengele, wanapopiga kengele kule katikati ya misitu, tembo wanakimbia na wanyama wengine wanakimbia. Waende wapi? Wanakuja huku kwa binadamu. Kwa hiyo iko haja ya kufanya utafiti na kuhakikisha kwamba tunaondoa wale watu walioko huko ambao wanafanya uharibifu, ambao wanachunga ng'ombe huko tofauti na taratibu na Sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nasema kwamba, pamoja na jitihada za Serikali ambayo zinaendelea kuleta mabomu ya kuwaondoa tembo, kuongeza askari, kuongeza risasi baridi, napo itakuwa haitoshelezi kwa sababu tembo watazidi kuwa wanafika tu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu, sekunde moja. Ulikuwa unakaa hapa, baadaye umehamia hapo, sekunde moja nimalizie. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, anataka hawa tembo awaone wanaingia Ikulu? Eeh?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru. Namwita sasa Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Naipongeza Serikali kwa jitihada ambazo zinafanywa ambazo zimekuwa za kuleta mafanikio makubwa sana hasa kwenye Sekta ya Utalii; tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumzia mazingira ya migogoro kati ya Pori la Msitu wa Tongwe Mashariki na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ambao ndio wamiliki wa huo msitu. Mheshimiwa Waziri unaujua vizuri mgogoro huu na tulikuwa tunategemea kabisa kwamba ungekuwa umefanya

jitihada za karibu kumaliza huu mgogoro ili wananchi wa Wilaya ya Tanganyika waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchelewa kwa kutokutoa maamuzi ya haraka, kumefanya eneo hilo ambalo lina mgogoro kuingia hasara karibu ya thamani ya shilingi 30,000,000,000 tumezipoteza kwa sababu ya mgogoro uliopo. Kama unavyofahamu Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Tanganyika inavuna *carbon credit* na imekuwa wilaya ambayo ni ya mfano katika nchi yetu. Wewe mwenyewe unafahamu, karibu halmashauri 50 zimekuja kujifunza huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, juzi alikuwepo, ameshuhudia maendeleo makubwa sana ambayo yapo kwenye vijiji vile nane ambavyo vinapata *carbon credit*. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, uje na majibu ili tuweze kumaliza mgogoro huu ambao kimsingi ukiumaliza, utakuwa umewasaidia wananchi karibu vijiji 32 watanufaika kwenye misitu inayozunguka maeneo hayo karibu na vijiji hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ushauri kwa Serikali. Mheshimiwa Waziri, tumejielekeza sana kwenye Sekta ya Utalii, jambo ambalo ni jema. Nawaomba sana, ili tuweze kukuza utalii, matangazo ni muhimu sana katika nchi yetu. Utalii mahali popote pale ambapo umetangazwa kwa kina, umetoa faida kubwa na tija kubwa kwa nchi zilizofanya hivyo. Kwa hiyo elekezeni nguvu kuweka matangazo ya Kimataifa ambayo yatatangaza hifadhi tulizonazo na zitaleta fedha za kifgeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri, nawaomba Wizara muelekeze nguvu sasa kuitumia rasilimali tuliyonayo hasa misitu tunayomiliki, tuweze kuvuna *carbon credit*. Mheshimiwa Waziri, tuna misitu yenye hekta 48,000,000 kwa nchi nzima. Hii misitu haijafanya kazi ya aina yoyote ambayo tungeweza kupata faida kama nchi. Mimi naamini, kama Serikali itakuwa ina nia ya dhati, hata kodi tunazokuwa tunaongeza kwenye vinywaji, tusingekuwa tunaelekea huko kwenda kudai kodi hizo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna rasilimali ambazo naamini tukiwekeza kwa kiwango kikubwa sana, tuna nafasi ya kupata kati ya shilingi 10,000,000,000,000 au zaidi kupitia kwenye misitu kwa idadi ya misitu tuliyonayo. Inawezekana Waheshimiwa Wabunge wasilielewe hili na wakaona kama miujiza, lakini huo ndiyo ukweli. Zipo nchi ambazo zinanufaika kupitia uvunaji wa *carbon credit*, wao wamenufaika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba na kuishauri Serikali, iwekeze kwenye eneo hili, tuweze kubadilisha Sheria ambazo ni vikwazo vinavyoweza vikatufanya tukakosa kupata hizo fedha. Ni matumaini yangu ushauri huu mtaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, namuomba sana Mheshimiwa Waziri aje atusaidie. Tuna mgogoro kati ya wawekezaji ambao wanafanya shughuli za uwindaji kwenye Msitu wa Nkamba. Sisi Msitu wa Nkamba tumepakana na Msitu Msitu wa Luwafi. Muwekezaji yule anaenda kulipa mapato kwenye Msitu wa Luwafi ambao uko Mkoa wa Rukwa, lakini uvunaji anafanya kwenye eneo la Wilaya ya Tanganyika. Naomba hili, mtupatie mapato yetu ambayo ni stahiki ya Wilaya ya Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwenye mkoa wetu sisi, tuna Hifadhi ya Katavi. Hifadhi ya Katavi haijatangazwa ipasavyo. Tuna wanyama wakubwa pengine kuzidi wale ambao tunawaona kwenye Hifadhi ile ya Mikumi. Mfano tembo, tunao mpaka tembo ambao ni wakubwa sana na tuna twiga mweupe yupo kule Katavi. Sasa, hawajaweza kuitangaza hii hifadhi na matokeo yake inatumia rasilimali kubwa kutoka kwenye hifadhi nyingine ili kuendesha ile hifadhi. Naomba hili muweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, aje na majibu sahihi juu ya mgogoro wa Msitu wa Tongwe Mashariki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakoso. Namwita sasa Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuata wakati huo Mheshimiwa Amsabi Mrimi ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwanza nasema, bila shaka Wizara hii ni miongoni mwa Wizara chache ambazo ni kwa bahati nzuri zimepata nyongeza ya bajeti tofauti na Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na nyongeza hii waliyopata, imekuwa pia ni bahati mbaya nyongeza hii haijaelekezwa kwenye mambo muhimu na ya msingi ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi wa wananchi, hapa ndani ya Bunge, mara zote tumekuwa tukisema na tukieleza, na katika mijadala mbalimbali hata kama siyo ya hapa, kwenye Kamati, nje ya vikao hivi, lakini adha ambazo wanapata wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi wetu kwenye maeneo yetu, tumekuwa tukijadili habari ya wanyama wakali na waharibifu katika maeneo yetu. Bahati mbaya pamoja na bahati hiyo waliyoipata Wizara hii, fedha hizo ambazo wamepata kama nyongeza, hakuna ambayo imeelekezwa kuweka nguvu kubwa katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu, karibia asilimia 49.5 ya halmashauri zetu kwa maana ya halmashauri 91, ndizo halmashauri ambazo kwa kiwango kikubwa zimeathirika na suala la wanyama wakali na waharibifu kuingia katika maeneo yetu, kumaliza mazao, wananchi kuuawa na wengine kujeruhiwa. Kwa bahati hiyo waliyoipata, sisi kama wanakamati, hawajatushawishi kuonesha ni namna gani wanakabiliana na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati hiyo waliyopata ya nyongeza ya fedha ya shilingi 19,000,000,000, matokeo yake

wanasema katika fedha shilingi 19,000,000,000 walizopata, shilingi 14,000,000,000 inaenda kwenye matumizi ya kawaida, na shilingi 5,000,000,000 peke yake inaenda kwenye fedha za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitarajia tuone mikakati hiyo kutokana na hii nyongeza. Tulitarajia pia, tuone mikakati ya namna gani tunaokoa shoroba kwa sababu mwisho wa siku pia wanyama wanaingia kwenye maeneo yetu shoroba zote zimevamiwa, namna gani wanakuja na mkakati. Pia, namna gani mkakati wa kutangaza utalii kwa sababu utalii kwa nchi hii ni sehemu ambayo inaingizia Pato la Nchi na ni Sekta ambayo pia inasaidia nchi kupata fedha za kigeni, imekuwa ni bahati mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imetusikitisha kama wanakamati na mimi ni mmoja wa Kamati lakini tunaamini, kupitia Bunge hili sasa na Waheshimiwa Wabunge, tutahakikisha hiki ambacho wameongezewa, kinaelekezwa katika maeneo muhimu ya kukabiliana na masuala yote ambayo tumesema na changamoto ambazo wananchi wanakutana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hizi taasisi zetu ambazo zimeachiwa kitu kinaitwa *retention*, huko nyuma walikuwa wanapewa *retention*, baadaye ikaja ikaondolewa, na sasa hivi tumerudi kwenye ule mfumo kwa maana ya *TANAPA* na *NCAA* kwa maana ya Ngorongoro. Lengo la kuachia hizi fedha wakusanye wenyewe na wazitumie, na baadhi ya *percent* iende kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inaeleweka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia kuona kwamba baada ya fedha hizi kubaki mikononi mwao, tutarajie kuona ufanisi wa taasisi katika utendaji wao wa kazi. Hatutarajii kuona upigaji ukifanyika wa hizi hela, tunatarajia kuona hizi taasisi zinafanya vizuri katika suala zima la kuhifadhi maeneo yetu yote ya hifadhi kama ni Ngorongoro, ni *TANAPA*, lakini miundombinu iliyoko ndani ya hifadhi hizi zinaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tuna barabara ya kutoka Ngorongoro kuelekea Serengeti, kipindi cha mvua, na tunaenda kupindi cha *high season*, ile barabara ni mbovu, ni mbovu, ni mbovu. Tunatarajia sasa, kwa sababu mmepewa *retention* hii, tuone matokeo ambayo tunatamani kuyasikia na kuyaona kwa macho tukitembelea na kuona vitu hivyo kwa maana ya kwamba kuboresha miundombinu kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msifanye ule wakati ambao ni *high season*. Bahati mbaya sana ikifika tena wakati wa *high season*, Wazungu mfano, watalii wameingia *crater,* unakutana na ma-*grader* ndiyo vifusi vinaanza kumwagwa huko, ndiyo ma-*grader* yanaanza kusambaza, sasa *what's that*? Hiyo ni nini? Huo ni utalii au ni vurugu? Maana yake magari yanapita yanatembeza watalii, humohumo unakuta ma-*grader* tena yanaanza kuchonga barabara, mara sijui imefanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia sasa, baada ya hili, kwa sababu tuliliomba muda mrefu na tulilisemea, tuone mabadiliko makubwa yanafanyika katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, asilimia 32.5 ya ardhi ya nchi hii, ni kwa ajili ya uhifadhi kwa maana ya maeneo ya hifadhi pamoja na misitu. Hii maana yake ni kwamba, hizi ni ardhi ambazo tayari ziko katika eneo hilo. Tunatambua ardhi haiongezeki, watu huongezeka, mahitaji ya utumiaji wa ardhi yanaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutarajie na kuona kwamba hiki ambacho kimetengwa kwa ajili ya hifadhi kibaki hapo hapo. Kwa sababu tukiendelea kuongeza maeneo ni sahihi kabisa, ukija kwenye *logic* kwamba umuhimu wa utalii na umuhimu wa uhifadhi na vitu vyote vinavyohusiana na utalii kwenye kiuchumi, lakini kwa ajili ya mapato ya nchi ni suala zuri kabisa, lakini tukiendelea kusema kwamba tunapandisha baadhi ya mapori, tunachukua baadhi ya maeneo na kuyafanya hifadhi, nafikiri hapo tulipofika inatosha, hebu tuyatunze haya tuliyonayo kwanza tuyahifadhi, kwa sababu tukiendelea kupanua ndivyo tunavyendelea kuwa na migogoro na wananchi, ndivyo

ambavyo tunaona hawa askari wetu wa Jeshi Usu ndilo linakwenda kupambana na wananchi kwa sababu wao kazi yao ni kulinda kile walichoambiwa, mwananchi yeye hakuelewi. Mwananchi yeye ana ng'ombe, anataka kufuga, anataka kulima na anaona ardhi yenyewe haitoshi, kule *population* inaongezeka, mahitaji ni makubwa, ardhi ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutarajie pia kwamba haya ambayo yamepimwa na kutambulika kama maeneo ya hifadhi na misitu ibaki kama ilivyo ili ardhi nyingine iendelee kupimwa, wananchi waendelee kutumia ardhi, lakini kuwepo na matumizi bora ya ardhi kwa maana ya kwamba kuwe na kukishirikiana kati ya Wizara hii na Wizara nyingine ya Adhi ili kuhakikisha kuwa ardhi ya Watanzania inawanufaisha watu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti jambo lingine, mimi ninatoka Wilaya ya Karatu, pale Karatu tupo jirani na Ngorongoro. Karatu ndicho kitovu cha utalii, kwa maana ya kwamba watalii wote wanaokwenda kutembea Ngorongoro atatoka alikotoka anakuja kulala Karatu na Karatu tuna hoteli nzuri za kitalii *(five stars hotel)* karibia 68, ni nzuri kabisa. Huko nyuma nimechangia mara nyingi sana; tunaomba Karatu muufanye uwe mji kweli kweli wa kitalii. Tunaomba tuwe na *culture tourism*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na programu inatwa *Karatu Culture Tourism Center*. Kuna timu iliundwa baina ya halmashauri na watu wa Ngorongoro, kuna kusuasua katika jambo hili. Tunaomba jambo hili lilifuke upya ili watalii wanapoenda Ngorongoro kutalii wapitie na Karatu, kuwepo na hiyo *center* ya *culture tourism* waangalie. Tuhakikishe kwamba tunaufanya Mji Karatu kuwa ni mji wa kitalii, tunauendeleza, tunauwekea miundombinu kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara zingine ili kuhakikisha kwamba na sisi Karatu pale tunafaidika na watu wanaokwenda kutalii, kwa sababu ndiyo barabara ya kwenda Ngorongoro, ndipo ambapo watu wote wanapita pale kwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili liende sambamba, kwenye Taarifa ya Kamati tumeonesha kabisa kwamba kuna uhaba wa vyumba vya kulala wageni, pamoja na hoteli tulizonazo lakini bado hoteli hazitoshelezi.

Kwa hiyo, tunaomba kuwepo na mikakati kati ya Wizara hii; pamoja na kwamba Kamati tumependekeza zile hoteli ambazo zilikuwa za Serikali zichukuliwe na kufufuliwa, lakini wako wadau ambao ni *private sector,* wako wadau ambao wana *interest* kuwepo na mazingira ya kuwawezesha. Wizara ije na mkakati wa kukaa na wadau, benki na watu mbalimbali kwa pamoja. Watu wenye *interest* wawezeshwe, lakini tuandae maeneo, kama pale ni Karatu ni Mto wa Mbu, maeneo jirani yote yapangwe, maeneo yatambuliwe kabisa kwamba maeneo haya ni kwa hoteli, maeneo haya ni kwa ajili ya uwekezaji wa wadau mbalimbali ili tuweze kufanikiwa na kuhakikisha ule upungufu wa vyumba tuliokuwa tuweze kuutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nakushukuru. Nimwite sasa Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Dkt. Amsabi Mrimi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mungu kwa afya na uzima wetu. Pia ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ile *Royal Tour* na nitasema kwa nini pongezi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu pamoja na pongezi nitazungumzia suala la misitu na umuhimu wa kuzingatia *local content* katika misitu. Nitazungumzia pia suala la bomu baridi hilo la kufukuza tembo, nitazungumzia utalii wa matukio na mwisho kama nafasi itatosha nitazungumzia sekta ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa ile *Royal Tour* na kwa bajeti hii pamoja na maandalizi yake napenda kupongeza Waziri Mheshimiwa Kairuki, kaka yangu Bwana Dunstan Kitandula, huyu ni mtu rahimu na mpole sana, lakini pia Katibu Mkuu Dkt. Abbas na Naibu Katibu Mkuu Kamishna Wakulyamba pamoja na watumishi, wafanyakazi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza kwanza kwenye sekta ya misitu. Kwa bahati nzuri na wewe unatoka kwenye misitu na unafahamu kwa namna gani sekta ya misitu ina mchango mkubwa katika uchumi wa watu wa Iringa na Mkoa wa Njombe mpaka maeneo ya Madaba. Sisi Mafinga tumejaliwa kuwa na msitu mkubwa ambao unakwenda katika Wilaya ya Mufindi mpaka maeneo ya Kilombero huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa na jambo moja kwa Mheshimiwa Waziri, timu yake na wenzetu wa *TFS*, tunapozungumzia *local content* wakati mwingine nadhani kwamba ile *local content* ni mambo tu ya Kimataifa na mambo ya kwetu hapa Kitaifa. Kumbe *local content* maana yake ni kwmaba hata wale wenyeji walioko kwenye yale maeneo kama ni ya utalii au ni ya misitu wawe *beneficiary* wa uwepo wa ile neema ambayo Mwenyezi Mungu amewajalia watu wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwangu hapa nasema nini, nimwombe Mheshimiwa Waziri na watu wa *TFS* wanapotoa ajira za muda mfupi, zile *temporary,* hakikisheni pia wanazingatia wenyeji wanaozunguka msitu wa *Sao Hili*. Wananchi wanaotoka kwenye vijiji vile nao wawe sehemu wa kupata vile vibarua. Wakati fulani tulikuwa tunatoa vibarua ikiwa inaeleweka kabisa kwamba msimu huu kijiji hiki kitapata vibarua labda watoto kumi au vijana kumi au akina mama kumi. Kwa hiyo, ninawaomba kuwepo na *clear information* ili wananchi wa Mufindi na Mafinga waweze kunufaika kama ambavyo wanasema siku zote kwamba ukiwa karibu na uaridi lazima unukie uaridi. Kwa hiyo, sisi watu wa Mafinga na Mufindi kunukia kwetu uaridi la kwanza na sisi kuwa sehemu ya washiriki katika ajira za muda mfupi zinazotokea

kwenye mashamba ya *Sao Hill*. Ninaomba hili tulizingatie sana kwa muktadha ule niliosema wa *local content*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili tuliwaomba Mheshimiwa Waziri na hii mimi tumewaomba Mkoa wa Iringa kwa nia njema. Tumewaomba kwamba jamani pale kwenye shamba la *Sao Hill* tutengeeni sehemu tujenge soko kubwa la mazao ya misitu la kimataifa, *this is good for both of us.* Nimewaambia, nimeongea na Mheshimiwa Waziri *personal*, nimeongea na Katibu Mkuu na pia nimeongea na Profesa Dos Santos. Sasa nikasema je, kweli jambo hili nina haja au sisi watu wa Mufindi tuna haja ya kumwandikia Waziri Mkuu kumuomba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kitu ambacho tumewaomba Mheshimiwa Waziri ni kwa manufaa yetu sisi sote, Wana-Mafinga, Wana-Mufindi, Wana-Iringa, Wana-Njombe, lakini pia wao ili tuikuze sekta. Tutakapokuwa na soko kubwa la mazao ya misitu tutakuwa pia tumeikuza hii sekta yetu. Tulisema, Profesa anajua, tumezungumza sana kuhusu *percentage recovery* kwenye mti, kwamba ule mti unakuta kwa jinsi ilivyo sasa hivi labda ni 40% tu ule mti ndio unatumika, 60% ni *waste*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiwa na eneo la namna hiyo maana yake ni kwamba katika mti tunaweza tukafanya ile *recovery percentage* ikawa hata 90%, kwamba huyu hapa atafanya mambo ambayo huyu hapa kama ana mambo ya *sawdust* atafanya. Kwa hiyo niwaombe, pamoja na kuwa Mheshimiwa Waziri alisema watalamu wamemweleza tofauti, mimi nawaombe, ninawaombeni kwa niaba ya wananchi wa Mafinga na Mufindi hebu mkalitafakari upya jambo hili, ni kwa manufaa ya sisi na sekta ya misitu, hili nimewasilisha kama ombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu katika misitu, tuliwaomba na mwaka jana nilisema pia kwamba makusanyo yale ya *cess*, zamani ilikuwa kwamba yule mtu anayepata kibali cha kuvuna analipa malipo yote kwa mkupuo mmoja, halafu baadaye mnatenganisha ile ambayo ni *cess* wanatupatia sisi halmashauri. Wakaja na utaratibu kwamba tujikusanyie wenyewe.

Ile pale kama nilivyosema, kama tuko karibu na uaridi na tunukie uaridi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba utaratibu ule tuufikirie upya. Mtu anapokwenda kulipia na sisi kama Serikali tumesema tunataka twende na utaratibu wa *one point* katika masuala ya malipo. Sasa kwa nini mtu asilipe, halafu baadaye mtugawie ile ambayo ni sehemu yetu ya *cess*. Watu wa *TFS* wanasema sijui kuna gharama za *bank charges* na kadhalika. Sisi tuko tayari ku-*share* hizo *costs,* lakini ilivyo sasa sisi kama tunategemea *cess* maana yake makusanyo sasa yanaendelea kushuka. Nawaomba wakae na *local government,* kwa maana ya TAMISEMI, tuone na tuje na huo mfumo ambao utatuwezesha sisi kukusanya *cess* pasipo kutumia mabavu wala nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo ninataka niliseme na nipongeze ni suala la bomu baridi kwa ajili ya kufukuza hao tembo na hapa ni lazima kama Serikali na kama Wabunge tuzipongeze Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ushirikiano na kitaasisi ambao umewezesha kuja na hili bomu baridi ambalo litasaidia sana maeneo ambayo wenzetu wanapata matatizo ya tembo kuingia kwenye makazi ya wananchi.

Kwa hiyo, napongeza vyombo, na nawapongeza nimeona wamekwishatoa *order*, wamenunua, na watu wengine tuunge mkono jitihada, vyombo vinapokuja na ugunduzi fulani fulani basi sisi kama Taifa, wale watu wa Mzinga wana mazao mbalimbali tuwaunge mkono, tununue mazao yale kwa ajili ya manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kuhusu *Royal Tour* kwamba utalii wetu uendane na kitu kinaitwa utalii wa matukio. Mtu akija kupanda Mlima Kilimanjaro, akija Serengeti, akija Ruaha mwakani aweze kupata hamu ya kuja ten ana ili aweze kupata hamu ya kuja tena maana yake ni kwamba tuwe na matukio ambayo yanasindikiza hivi vituo vyetu. Kwa mfano kuna maeneo wenzetu kama Brazil wana kitu kinaitwa *Rio Festival*. Hizi *festival* hata hapa Tanzania wenzetu Sauti za Busara Zanzibar watu wanakuja kwa

ajili ya utalii, lakini pia anakuja kwa ajili ya lile tukio. Kwa hiyo, tupanue wigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninaamini ndugu yangu Mafuru ni *brain,* atakuja kupitia *TTB* tukawa na utalii wa matukio. Leo hii tulikuwa na wageni hapa wa waratibu wa *The Great Ruaha Marathon*. Wamebuni kitu kizuri kwamba unakimbia *Marathon* ndani ya Mbuga za Ruaha. Kwa hiyo, tubuni, tuwe na matukio mbalimbali ambayo yataongoza vile vivutio vya utalii. Kuna kitu kinaitwa *Nyama Choma Festival,* yule mtu kama alikuja mwaka jana apate hamu tena ya kuja mwakani kwa ajili ya lile jambo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele imelia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huo utalii wa matukio kuna huu utalii wa michezo. Nilitoa mfano ile Simba ilivyoshiriki *African League,* yale ndiyo matukio ambayo pia yanaleta utalii. Tunavyokuja kufanya *AFCON* tunaleta utalii. Kwa hiyo, tupanue wigo pamoja na hii *traditional* utalii lakini tuongozane na utalii wa matukio…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nawapongeza tena Mzinga kwa kuja na bomu la baridi kwa ajili ya tembo na Wizara kwa kushirikiana na Mzinga kwenye jambo hilo muhimu Mungu atubariki sote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Dkt. Amsabi Mrimi, atafutiwa na mchangiaji wetu wa mwisho Profesa Manya. Kwenye *list* na MheshimiwaAnastazia Wambura, simuoni kwa hiyo tuendelee, Dkt. Amsabi. *(Kicheko)*

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia kwa mikakati yake mikubwa ya kukuza utalii nchini. Sisi tunaokaa huko maeneo ambayo watalii wanakuja, tumeona matokeo makubwa sana na kipekee sana Serengeti tunazo shukurani kubwa kwa sababu ujio wa watalii wengi umebadilisha hali ya uchumi wa maeneo yetu, kwa hiyo, tunamshukuru sana sana Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana nimshukuru Waziri wa Wizara hii, Dada yetu Angellah Kairuki pamoja na Naibu wake Waziri wanaendelea kufanya kazi na nzuri. Mara nyingi kiongozi mzuri utamwona wakati wa changamoto. Tunakumbuka wakati ule kulipokuwa na hali ya mvua ikinyesha kwa wingi sana maeneo mengi ya Hifadhi ya Serengeti yalikuwa hayapitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naona waliweka jitihada kubwa sana na ndani ya muda mfupi barabara zilianza kupitika. Kwa hiyo, tunawashuru na kuwapongeza pamoja na menejimenti nzima ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii pamoja na taasisi zake ikiwepo *TANAPA,* wanafanyakazi nzuri, tunawashukuru. Tunawaomba waendelee kuongeza kasi kubwa na uboreshaji uwe ni jambo lao na malengo yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuja na kununua mabomu ambayo yametengenezwa hivi karibuni kwa ajili ya kupambana na tembo. Jambo hili ni jema, lakini mimi nashauri kwamba imefikia wakati sasa jambo hili tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili kila wakati tembo wanapongia vijijini wanalaumiwa wao, lakini ni kwa nini? Tembo hao wakishaingia vijijini hawaangaliwi kwa maana ya kurudishwa, hawasimamiwi na watu wa *TANAPA,* wanaoshuhulika nao ni maafisa wanyamapori wa wilaya ambao wako chini ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kila taasisi kwa maana ya Wizara, inapoanzishwa inakuwa na *core functions* zake. Sasa

ukiangalia madhumuni ya Wizara, kazi yake mahususi Wizara ya Maliasili ni kuendeleza utalii na kuhifadhi wanyama wetu, lakini TAMISEMI wao kazi yao kubwa ni kutoa huduma kwa wananchi, kama vile barabara, elimu, maji na kadhalika. Sasa wao si rahisi sana waka-*allocate resources* katika kupambana na wanyama hao warudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kule Serengeti kila wakati wanyama wanapoingia kwenye vijiji ukimpigia *DGO* mafuta hana, imeenda imerudi, huku wanyama wanashambulia mashamba na kadhalika. Sasa kazi hii, ninakumbuka katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri pale Morogoro tukipokea mabomu baridi alisema halmashauri zinunue mabomu haya. Sasa nikiangalia zilitajwa pesa nyingi sana ambazo zinanunua mabomu. Kama wanashindwa kutoa mafuta lita 30 wanawezaje kununua mabomu? Kwa hiyo, jambo hili si rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe Wizara irudi, ichukue kazi hii ya kudhibiti wanyamapori iwe ni kazi yake. Watu wa TAMISEMI waachwe washughulike na mambo mengine haya ya kuhudumia watu, vinginevyo basi huyu *District Game Officer (DGO)* basi arudi kwa watu wa Wizara ya Maliasili na wawezeshwe fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanyama hawa wanapoingia katika maeneo ya wananchi waweze kudhibitiwa haraka na nguvu kubwa iwekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Serengeti tumepata madhara makubwa sana kwa hawa tembo pamoja na wanyama waharibifu. Tuombe sana Wizara sasa ichukue hatua za kudhibiti. Sawa kuna wakati mwingine tunauliza juu ya kifuta jasho, kifuta machozi na kadhalika, lakini hivi havisadii. Sisi tunahitaji wananchi wetu wabaki salama, tunahitaji mazao yetu yabaki salama, tuvune na kuendelea na shughuli zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo la pili ambalo ningependa kuishauri Wizara hii, tunahitaji kuona utalii unakua nchini na watalii wanaongezeka. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa ya kuitangaza nchi katika utalii, lakini ukirudi na ukiangalia miundombinu katika kufikia hifadhi zetu bado ni changamoto

kubwa na wakati mwingine gharama inakuwa kubwa. Leo gharama ya kuifikia Hifadhi ya Serengeti ni kubwa sana. Utoke *KIA* uende Arusha utoke Arusha mpaka Ngorongoro, Ngorongoro mpaka Serengeti ulipe geti ya Ngorongoro, uende Serengeti gharama inakuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuombe ule Uwanja wa Serengeti ujengwe. Uwanja huu umekuwa ni wa miaka mingi ambapo tumekuwa tunazungumza utajengwa, utajengwa. Wakati mwingine wanapatikana mpaka wafadhili, wanapatikana watu wa kuwekeza kutoka *private sector,* lakini bado tunachelewa kufanya maamuzi. Niombe sana Wizara ya Maliasili na Utalii ichukue hii ajenda hii na ishughulike nayo kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba bado barabara zinazoingia Serengeti ni changamoto, kwa maana ya barabara ya lami, kutokea kule Tarime pamoja na ile ya Sanzate – Nata, tunaomba Wizara iangalie barabara hizi ni za kimkakati kwa ajili ya kukuza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni kuhusu *WMA,* hizi Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori ambazo zinamilikiwa na vijiji leo wameanza kukata tamaa na wengine wanatamani sasa zingerudi maeneo yao yale wafanya shughuli zingine kwa sababu pesa zao zimekataliwa huko Hazina. Tunaomba sana Wizara msaidie, tuko pale Serengeti na *Ikona WMA,* tunaomba pesa zao zije, zimesaidia kiasi kikubwa sana maisha ya wananchi kukuza utalii, *I mean conservation* iliweza kuwa *improved* sana kwa sababu ya fedha ile pamoja na kujenga miundombinu mbalimbali katika afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe pia liko jambo lingine tunaiomba sana *TANAPA* iangalie vizuri, pamoja na Wizara hii kwa ujumla. Tunapotoa vibali vya ujenzi wa *camps* pamoja na *lodges* ndani ya hizi hifadhi zetu, naona kama ubora wa ujenzi wake si mzuri. Ninashauri Wizara iangalie sasa uwezokano wa kusomesha watu maalumu ambao watasimamia viwango vya ubora wa ujenzi wa hizi *camps.* Mtalii anakuja anaoneshwa picha

imetengezwa kwa namna fulani anaona kwamba *it is beautiful* ni sehemu nzuri, lakini akifika malazi yale yanakuwa siyo mazuri mno. Sasa sisi tunampa tu mtu eneo jenga *camp*, jenga *lodge,* lakini ni la viwango gani vya ubora wake? Bado hatujawa na watu wa kusimamia viwango vya ujenzi wa hizi *camps* pamoja na *lodges.* Kwa hiyo matokeo yake mtalii anakuja analala sehemu ambayo ni *sub-standard* kwa hiyo tunaomba sana Wizara iende kuwekeza katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana maeneo ambayo yanapakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti vijiji vile hasa upande wa *Western Serengeti* ambapo hakuna *buffer zone* tunaomba tujengewe malambo ya kutosha kwa ajili ya mifugo yetu. Tunaishukuru sana Wizara, mpaka sasa hivi yako ambayo yanajengwa lakini tunaomba yaongezeke kwa wingi zaidi ili ng'ombe wale wasiweze kupata shida ambayo wanapata sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna malambo na hata wakati Wizara ikiwasilisha, kwa maana ya Kamati, imesema lazima hivi vijiji pamoja na jamii zinazozunguka hifadhi tuweze kuziangalia, kwa maana ya kuzisaidia. Wame-*sacrifice land* na kwamba wanapata shida nyingi kwa kuishi pamoja na wanyama, kwa maana ya kupakana. Tuhakikishe kwamba watu hao wanajengewa malambo pamoja na huduma zingine za kijamii ili nao waweze kufaidika moja kwa moja na hifadhi hizi ambazo wanaishi pembeni nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niombe sana sasa Wizara hii kwa kushirikiana na *TANAPA,* waangalie namna bora ya kuongeza ajira kwa watu ambao wanapakana na hifadhi zetu hasa kwa upande ule wa Serengeti, wananchi wetu pamoja na kuwa na elimu nzuri bado ajira nyingi hazijapatikana kwa vijana wetu hata zile ambazo ni *seasonal.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, namuita sasa mchangiaji wetu wa mwisho Profesa Shukrani Elisha Manya.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na nikiwa mchangiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze kwa kazi kubwa za kuendeleza jitihada za kuongeza watalii na kuboresha miundombinu ya vivutio vya utalii hapa nchini, ili sekta hii iendelee kuchangia pato la Taifa kwa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kusema kwamba naunga mkono hoja pia naunga mapendekezo yote ya Bunge yaliyotolewa kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Wizara katika mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jioni ya leo nijitanue katika jambo ambalo nimewahi kuongea hapa Bungeni, lakini leo nataka niliweke wigo fulani hivi na jambo hili linagusa Wizara ya Maliasili na Utalii pia na Ofisi ya Makamu wa Rais. Ni maeneo haya ambayo yanaitwa *geoparks,* ambayo malengo yake ya kuyaanzisha ni kukuza utalii pia na mafunzo na kuifanya jumuiya ambayo ipo jirani kuendelea kufaidika na kuanzishwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwamba jambo hili lina fursa ambazo ni kama sisi kama nchi tunachelea kidogo na sababu ya kusema hivyo ni kwamba, wazo hili la kuhifadhi haya maeneo yenye urithi wa kijiolojia lilianza nchini Ufaransa mwaka 1991. *UNESCO* ikalibeba mwaka 1997 na kufikia mwaka 2004 *UNESCO* ikawa imeunda Mtandao wa *Geopark* wa kidunia unaoitwa *UNESCO Global Geopark Network.* Sasa hiyo ni 2004 na mabara mengine yakachangamkia fursa hiyo na yamekuwa yakipata fedha kutoka *UNESCO* kwa sababu ya kuanzisha *geoparks* katika

nchi zao. Hadi sasa nakwenda haraka kwa sababu utanza kugusa gusa *microphone* yako hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa *UNESCO* duniani ina *geoparks* zenye hadhi ya kidunia, maana unaweza ukawa na *geopark,* lakini hiyo ambayo inatambulika kama *UNESCO Global Geopark* zipo 243, lakini katika mataifa 48 tu. Afrika tunazo mbili tu, M'Goun *Geopark* ya Morocco, lakini bahati na habari njema ni kwamba mojawapo ni *Ngorongoro Lengai Geopark* ya nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii *geopark* yetu ya hapa Ngorongoo Lengai ambayo ina hadhi inayotambuliwa na *UNESCO globally* ilipata hadhi hiyo mwaka 2018 na walijumuisha maeneo mazuri ya *Crater* ya Ngorongoro, Mlima wa Oldonyo Lengai, Nyayo za Binadamu wa Kale za Laetoli pamoja na Tambarare za Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya faida ya kuwa na mfumo huo wa mtindo ambapo *geopark* yako inatambuliwa na *UNESCO* kwa ngazi ya kidunia. Fursa zitokanazo na kuwepo kwa hiyo *geopark,* lile jengo ambalo tunaliona pale Olduvai Gorge lilipata msaada wa fedha kutoka Umoja wa Ulaya bilioni tatu ndipo jengo lile likajengwa, lakini pia utagundua kwamba hata katika utalii wetu ndilo eneo ambalo pia linavuta watalii wengi sana kwa sababu limeanza kueleweka na kutambulika na *UNESCO geopark. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kwamba kuna fursa hapa ambayo kama nchi tunachelea kuitumia kwa sababu maeneo kama hayo ni mengi mno, yaani kwamba Mlima Kilimanjaro sasa hivi hifadhi yake bado haijatambuliwa kama *UNESCO Geopark* wakati ni kitu kikubwa sana kidunia na kinaeleweka hivyo kwamba sasa hivi ndipo ambapo Hifadhi ya Kilimanjaro imeomba *UNESCO* waje kufanya tathmini, ili hatimaye na yenyewe ipendekezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna maeneo mengi ya jinsi hiyo Tanzania, Mheshimiwa Mama Lulida anapenda sana

kuongea habari ya Tendaguru *Site* ya *dinosaurs* ni kitu kikubwa kijiolojia duniani lakini hapa ndani huwa tunakionaona tu tunasema pale alipotoka mjusi na tunamuita mjusi tunapadogosha. Yule *dinosaur* aliyeko Ujerumani hivi unajua anakaa kwenye hili jengo letu lote hapa, sisi tunaita tu Tendaguru mjusi sio mjusi yule ni *dinosauria* mkubwa kabisa. Kwa hiyo, haipaswi kitu kama Tendaguru kuendelea kuchukuliwa katika hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale Mapango ya Amboni Tanga na yenyewe yametokea, ukienda pale utakutana na mwongozaji ambaye hata hawezi kueleza yametokanaje, tunayaacha tu. Nilishatoa hoja pia ya *Mautia Hills* na mambo kama hayo, tuna maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pendekezo langu ni kwamba fursa hii ipo ila sisi kama nchi hatujaichukulia maanani. Mamlaka ya Ngorongoro mpaka ikapata, ilifanya jitihada binafsi kuunda Kamati ya Kitaifa ya *Geopark,* ili iweze kukidhi vigezo na kwa jinsi hiyo imekuwa inaifadhili kufanya shughuli zake, lakini kamati hii kama ingetambuliwa kitaifa maana yake ni kwamba tungeweza kupata faida nyingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sasa hivi kamati hii yaani inafanya shughuli zake ikifadhiliwa na Mamlaka ya Eneo la Ngorongoro, basi, lakini haitambuliki kisheria na kwa msingi huo nilikuwa napendekeza Serikali ilichukue kama ni Maliasili au Ofisi ya Makamu wa Rais ilibebe, ili liweze kuwa na ngazi ya kitaifa yaani lifanye mambo yake liliwa na mamlaka kamili ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifanya kazi hiyo itaweza kupendekeza maeneo mengi zaidi ili hatimaye Tanzania sasa kama Bara la Afrika tunazo mbili tu. Hebu tufanye fursa sisi tuendelee kuwa wa kwanza katika kupata hizo *geoparks* ambazo zina *level* ya *UNESCO* kutambuliwa kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kamati hii kwa sasa haina bajeti ya kufanya kzai zake kwa sababu ni Ngorongoro iliyoianzisha basi

inatoa fedha tu kwa ajili ya kuendelea kukidhi kuwa kama hiyo *UNESCO Global Geopark*. Kwa hiyo, ipewe bajeti na wazo hili…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kaka yangu Profesa pale, tunashukuru umetaja Mapango ya Amboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapango ya Amboni ni miongoni mwa *geopark* ambayo ninaamini kabisa kwenye ile *rock weathering* kama somo ambapo katika vyuo vyetu, inaweza ikatumika wanafunzi kwenda kujifunza pale. Mapango ya Amboni unapita chini kwa chini mpaka unatokea baharini. Ni miongoni mwa *geopark* ambayo haijafanyiwa tafiti ya kutosha namna gani tunaweza tukanufaika. Kule Japan nilishawahi kwenda sehemu kama Mapango ya Amboni na namna gani kama Taifa lao linanufaika, tuyatumie Mapango ya Amboni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Profesa Manya unaipokea Taarifa kutoka kwa *Engineer?*

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchango wangu naelekeza kwamba, hebu Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais waweze kurasimisha kamati hii iweze kuwa ni Kamati ya Kitaifa ya *Geopark*. Kwanza tupate hilo jambo, tukishalipata hilo jambo, itengewe bajeti ifanye kazi, ikishafanya kazi, vile vivutio vyote vilivyopo hapa ndani ikiwa ni Mapango ya Amboni na mambo mengi ambayo yanayoeleweka katika nchi hii maana yake yakishapata hadhi ya kidunia *UNECSO Global Geopark,* kwanza tutapata fedha kutoka *UNESCO* ambazo

tunazikosa kwa sasa, maana yake tutakuwa tunaongeza pato letu la utalii kutoka Fedha za Mfuko wa *UNESCO*, pili, tutaongeza watalii na hivyo kuongeza fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchango wangu hasa nataka kusisitiza kwamba hii Kamati ya Kitaifa ya *Geopark* isiendelee kubaki kama mtoto wa Mamlaka ya Ngorongoro, ili kufanya mambo yao ya kuendelea kuwa *geopark* ya kidunia yafae, badala yake ije hapa juu ipate hadhi ya kuwa Kamati ya Kitaifa ipewe bajeti, ili iweze kufanya kazi tuweze kupata *UNESCO Global Geopark Tanzania* za kutosha na tutagundua kwamba tutakuza mafunzo kwa watu wetu, tutakuza utalii, lakini pia tutapata fedha kutoka katika Mfuko wa Taifa wa *UNESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Manya. Huo ndio unaitwa mchango wa kiprofesa.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho, lakini nina tangazo moja, ni kuwakumbusha tu kwamba mnakumbushwa kesho tarehe 1 Juni, 2024 kutakuwa na semina kuhusu Matumizi ya Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi, itakayotolewa na Wizara ya Fedha, semina hii itaanza saa 4.00 asubuhi katika Ukumbi wetu wa Pius Msekwa.

Baada ya tangazo hilo, naahirisha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, tarehe 3 Juni, 2024 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.30 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu Tarehe 3 Juni, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*